

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 30 Juni, 2006

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA:- Waheshimiwa Wabunge kwenye Jukwaa la Spika naomba nimtambulisse Mzee wetu Mzee Rajani kwa mikoa mingi sana hapa Tanzania amefanya kazi nyingi sana za biashara lakini pia za huduma ya jamii. Ninavyofahamu huko Wilaya ya Kahama alijenga sekondari wa fedha yake mwenyewe na watoto wanapata elimu, namshukuru sana. Karibu sana Mzee Rajani.

Na. 117

Ujenzi wa Daraja la Munguri

MHE. PASCHAL C. DEGERA aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iliahidi kuchangia gharama za ujenzi wa Daraja la Munguri Wilayani Kondoa lakini hadi sasa haijatekeleza ahadi yake:-

- (a) Je, kwa nini Serikali haitekelezi ahadi yake hiyo?
- (b) Je, ni lini sasa Serikali itaitekeleza ahadi hiyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu Swalii la Mheshimiwa Paschal Constantine Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliahidi kuchangia gharama za ujenzi wa daraja la Munguri Wilaya ya Kondoa kwa kiasi cha Shilingi 122,000,000/. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imetimiza ahadi yake kwa kutoa jumla ya shilingi milioni 122 kama ilivyoahidi. Kwa mwaka 2004/2005 shilingi milioni 60 zilitolewa na kwa mwaka 2005/2006 Serikali imetoea fedha zilizobakia ambazo ni shilingi milioni 62 zilizobaki.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali (a), Serikali imekwishatimiza ahadi yake ya kuchangia ujenzi wa daraja la Munguri. Ujenzi wa daraja hilo ulikamilika mwezi Oktoba 2005 na lilifunguliwa rasmi na Makamu wa Rais Mheshimiwa Ali Mohamed Shein tarehe 24 Aprili, 2006.

MHE. PASCHAL C. DEGERA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwanza naomba niitumie nafasi hii kuishukuru sana Ofisi ya Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa msaada huu ambao wametupa. Tunashukuru sana.

Kwa kuwa, wakati Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa iliposaini kujenga daraja hili la Munguri ilikuwa na vyanzo vyake vyapato na ndiyo maana iliamini kwamba ingeweza kumudu kugharamia mradi huo.

Kwa kuwa, vyanzo hivyo vimefutwa na Serikali Kuu na hivi sasa Halmashauri haina vyanzo vyapato vyapato vyakwe, Je Serikali haioni kwamba ina wajibu wa kumalizia deni lililobaki la shilingi milioni 96? (*Makofii*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOAA NA SERIKALI ZA MITAA:- Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Paschal Degera kama ifuatavvyo:-

Mara nyingi suala hili la Serikali kutotimiza wajibu wake kwa kulipa fidia baada ya kuondoa ruzuku limekuwa likijitokeza sana, lakini kama tutakavyojaribu kutoa ufanuzi leo ukweli ni kwamba Serikali imekuwa ikitimiza wajibu wake kikamilifu kabisa kwa kulipa fedha kufidia kiwango cha fedha zote ambazo halmashauri ilifuta vyanzo vyake.

Tatizo ambalo tumelibaini Halmashauri nyingi sasa baada ya kuona fedha hii ya Serikali ni ya uhakika wamebweteka na hawajali sasa kutoa msukumo zaidi kukusanya mapato kwa sehemu iliyobaki, wengi hawafikii asilimia hata 70 kwa kuwa wamezembea katika eneo hilo. Kwa hiyo, kwa upande huo naweza nikasema kama ni suala la kuomba msaada mwingine katika ofisi yetu linaweza likaombwa lakini si kwa sababu waliyooitoa.

Ubovu wa Barabara ya Jimbo la Ubungo

MHE. ABBAS Z. MTEMVU (k.n.y. MHE. CHARLES N. KEENJA)
aliuliza:-

Kwa kuwa, Jimbo la Ubungo linakabiliwa na tatizo la ubovu wa barabara.

Je, Serikali itachukua hatua gani za makusudi ili kuimarisha barabara za Jimbo hilo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge wa Ubungo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Ubungo kuna mtandao wa barabara unaokadirwa kuwa na urefu wa Km 246. Kati ya hizo Km. 207 ni za changarawe na Km. 39 ni za lami. Km 126 zipo chini ya *TANROADS* na Km 120 zipo chini ya usimamizi wa Manispaa ya Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, katika hatua ya kuboresha barabara za Jimbo la Ubungo, Serikali imetekeleza yafuatayo:-

(i) Kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara, Ofisi ya Waziri Mkkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imeshatoa shilingi milioni 760 na kutenga shilingi milioni 900 kwa mwaka wa fedha 2006/2007 kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Shekilango yenye urefu wa Km. 3.8 ambayo imekadirwa kugharimu jumla ya shilingi bilioni 2.8.

(ii) Kati ya mwaka 2005/2006 Ofisi ya Waziri Mkkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilitenga jumla ya shilingi 100,000,000/= kwa ajili ya kutengeneza barabara ya Igese kwa kiwango cha lami, barabara hiyo ina urefu wa mita 700. Utekelezaji wa miradi yote miwili umeshaanza na kazi inaendelea.

(iii) Katika mwaka 2006/2007 Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 210 kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Manispaa ya Kinondoni, kati ya hizo Shilingi milioni 29 ni kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo ya kawaida barabara za Sam Nujoma, Africasana, Mori, *Old Kigogo* na Mabibo na *NIT*.

(iv) Aidha, Serikali kwa kupitia wakala wa barabara nchini *TANROADS* imekusudia kuikarabati barabara ya Sam Nujoma yenye urefu wa Km. 3.9. Utekelezaji wa barabara hiyo upo kwenye usanifu.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia Bunge lako tukufu naomba kuwapongeza Mfuko wa *Japan Food Aid Counterpart Fund* na Manispaa ya Kinondoni kwa kuchangia ujenzi wa *Box Culverts* Kigogo mwisho, Mavurunza na Kilungule. Pia natoa wito kwa Manispaa zote kufanya hivyo, kwani ushiriki wa Manispaa ni muhimu katika kukidhi mahitaji ya matengeneo ya barabara na hivyo kumaliza kero za usafiri kwa wananchi.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea na kipindi chetu cha maswali nilikuwa nimeletewa taarifa hapa kwamba kwenye *Gallery* upande wa kulia *Public Gallery* tunao wanafunzi 40 kutoka Shule ya Sekonari ya Menonite haisemi ni wapi labda Dodoma au vyovoyote vile na wanafunzi watano kutoka shule ya Sekondari ya Dodoma, naomba wasimame. Ahsante sana vijana na ahsante sana Walimu kwa kuwapa fursa watoto wetu wajifunze Demokrasi inavyoendelea katika Bunge hili. Ahsate sana. (*Makofi*)

MHE. ABBAS Z. MTEMVU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Dar es Salaam ndiyo sura ya nchi yaani Rais yupo pale, Waziri Mkuu, Mawaziri wote, Mabalozi kadhalika hali ya barabara za Dar es Salaam kwa ujumla Kinondoni, Ilala na Temeke siyo nzuri.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza pesa kwenye Mfuko wa Barabara wa Mkoa na wa Manispaa hizi tatu?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, napenda nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abbas Mtemvu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Dar es Salaam barabara zake siyo nzuri na Serikali imekuwa ikiliona hilo lakini suala la kuongeza Mfuko wa Barabara fedha zaidi ni suala la kisheria na vilevile inategemea kwa kweli fungu ambalo Serikali inalo.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo Serikali imekuwa ikijaribu kuchukua hatua mbalimbali kwa mfano hivi karibuni imeundwa Tume ya Kuangalia Matatizo ya Barabara katika Jiji la Dar es Salaam na Kamati ile imekuja na gharama za kutengeneza baadhi ya barabara ambazo zitaondo tu siyo tatizo la usafiri kwa ujumla lakini msongamano katika Jiji la Dar es Salaam.

Kwa sasa Serikali inajaribu kuangalia itapata wapi fedha hizo ambazo ni karibu bilioni 8.5 ili kuweza kukarabati baadhi ya barabara hizo, nina hakika hatua hizi zikichukuliwa hali ya barabara katika Jiji la Dar es Salaam itakuwa nzuri ukilinganisha na ilivyo sasa. (*Makofi*)

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba na mimi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, Kibaha ina hadhi ya Mji hivi sasa haina barabara hata moja ya

lami, je Serikali ina mpango gani wa kuzipa barabara za Kibaha zipate lami ili na yenye we iweze kuwa kioo katika Mkoa wa Pwani?

SPIKA: Mheshimiwa Zaynab Vullu swali hili labda ili lipate faida ya majibu kikamilifu kwa kuwa imeruka imekwenda Mkoa mwingine kabisa pengine liulizwe nalo kwa maandishi litapata majibu kikamilifu. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nilikuwa naomba kuuliza kuhusiana na utunzaji wa barabara ambazo tayari zinakuwa zimeshatengenezwa kwa hizo pesa kidogo tulizonazo.

Je, Serikali haioni sasa ni msingi na muafaka kuweza ku – *maintain* barabara zetu zile chache ambazo zinakuwa zimeshatengenezwa kwa sababu barabara nyingi baada ya kufanyiwa ukarabati zinaachwa pamoja na kwamba kuna Makandarasi lakini wako kwenye barabara chache tu Kwa hiyo, kwenye mifereji kunakuwa na michanga, maji yanatuama kiasi kwamba zile barabara zinaharibika tena mapema sana hazipati utunzaji wa kuendelezwa. Naomba nijibiwe.

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, napenda nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, kama ifuatavyo:-

Kweli suala la *maintanance* ni suala ambalo ni la msingi Serikali imeliona hilo na kwa kweli kuanzia sasa mkakati wa Serikali ni kuendelea kutenga fedha nyingi zaidi kwenye matengenezo au *maintenance*, pamoja na kutenga fedha kwa ajili ya kujenga barabara mpya lakini kipaumbele kwa kweli kitatolewa katika *maintenance*. Kwa kweli hata wafadhili amba wanatupatia fedha au wanatusaidia katika matengenezo ya barabara wamekuwa wakisitisiza kwamba tuwekeze zaidi kwenye suala la *maintenance* na ndiyo maana kuna fungu la *TANROADS* kwa upande wa barabara ambazo zinakuwa chini ya *TANROADS* kwa ajili tu ya ku – *maintain* barabara zetu hazitoshi na tutaendelea kuongeza kiasi kile mwaka hadi mwaka. (*Makofi*)

Na. 119

Majengo kwa Ajili ya Shule

MHE. MICHAEL L. LAIZER aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wamejenga Madarasa na Nyumba za Walimu katika maeneo ya shule nyingi za Sekondari na kwa kuwa Serikali kuititia mpango wa MMES iliahidi kuwa itajenga Maabara, Maktaba na Majengo ya Utawala.

Je, ujenzi huo utaanza lini, kwani katika shule nyingi majengo hayo yanahitajika kwa haraka?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Wizara yangu kuptitia MMES, iliahidi kujenga maabara, maktaba na majengo ya Utawala katika shule za sekondari hapa nchini. Pamoja na nia hiyo nzuri, ahadi haikutekelezwa kutokana na ufinyu wa Bajeti.

Hata hivyo katika Bajeti ya mwaka 2006/2007 Wizara yangu imepanga kujenga Maabara 40 na Maktaba 30. Aidha, Serikali itaendelea kujenga majengo hayo kadri fedha zitakavyokuwa zikipatikana.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, wanafunzi wengi wamemaliza sekondari bila kuwa na maabara Serikali haioni kwamba kutokuwa na maabara kumeshusha kiwango cha elimu na watoto wengi wamefeli kutokana na kutokuwa na maabara?

Kwa kuwa, wananchi wamejenga shule nyingi sana za Sekondari na nadhani ni zaidi ya hizo shule 40 alizosema. Je ni lini Serikali itajenga maabara katika shule zote zilizojengwa na wananchi?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU BAKARI MAHIZA):-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Michael Laizer, kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba zipo baadhi ya shule ambazo wanafunzi wake wamemaliza kidato cha nne bila kuwa na maabara lakini naomba kumwarifu rasmi Mheshimiwa Mbunge kwamba zile shule ambazo zilikuwa hazina maabara zilielekezwa kwenye mchepuo mwingine kutegemea na mahitaji na vifaa vilivyokuwepo. Aidha, upungufu huo unafanyiwa kazi.

(b) Shule nyingi zimejengwa tunawapongeza sana wananchi kwa juhudini zao kubwa kama nilivyoleza kwenye jibu la msingi kadri uwemo wa Serikali utakavyopatikana ndiyo tutakavyojenga maabara hizo kwa awamu hadi hapo tutakapo hakikisha kwamba shule zetu zote zimepata maabara. Naomba tuongeze juhudini na tushirikiane na kwa hakika kwa pamoja tutafanikiwa.

MHE. DR. WILBROD P. SLAA:- Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, Waziri ametuomba tuongeze juhudhi na kwa kuwa juhudhi hizo zilifanyika hata mwaka jana na wananchi wamejenga shule nyingi na hela zilizoahidiwa kwa mwaka 2005/2006 hata sasa hazijatoka.

Je, ni nini tatizo la msingi na lini sasa fedha kwa mwaka jana zitatoka? (*Makofi*)

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:- Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niongeze taarifa fupi zaidi ya yale majibu mazuri aliyotoa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuhusiana na swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba nguvu za wananchi zimejenga shule nyingi na kwa bahati mbaya kutokana na ufinyu wa fedha kama alivyoeleza kwenye jibu la msingi kwamba uwezo wa Serikali umekuwa si mkubwa sana kufuatana na nguvu za wananchi.

Lakini mimi ningependa kutoa wito kwa waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kwamba gharama ya maabara moja ni milioni 40 ili ikamilike ni kiasi kikubwa cha fedha lakini ukiangalia sehemu kubwa ni vile vifaa vya ndani na hasa vifaa vya maabara vyenyewe. Boma kama boma si gharama kubwa sana ukilinganisha na vifaa vilivyomo ndani. (*Makofi*)

Mimi ningewaomba Wananchi na Waheshimiwa Wabunge tuendelee kujenga yale maboma, vifaa vya ndani ziko njia nyingi ambazo zinaweza kusaidia, kwa mfano hii Mamlaka ya Elimu wanatoa vifaa halifu hata nakumbuka mimi kwa msaada wa *TASAF* pia tunaweza kupata vifaa.

Kwa hiyo, mimi nawaomba kwamba tuisubiri tu hii nguvu ya Serikali kama tunavyosema lakin tuongeze kwa kutumia hizo njia nyingine kama msaada wa *TASAF* na Mamlaka ya Elimu ambayo inasaidia sana kwa sehemu nyingi.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kabisa kwamba Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Shinyanga naamini kabisa kwamba wanaweza kusaidia uzoefu wao wa jinsi ambavyo walitumia wakapata msaada kutoka Mamlaka ya Elimu kwa haraka sana.

Naomba tuendelee kujenga tu tusikate tamaa. Ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 120

Kufungwa kwa Sekondari za Magamba

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO (k.n.y. MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA) aliuliza:-

Kwa kuwa, Sekondari ya Magamba, iliyokuwa Sekondari pekee ya Kidato cha sita, iliyokuwa inamilikiwa na Serikali sasa imefungwa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Sekondari za Kidato cha tano na sita angalau kwa kuanzia na shule tatu Wilayani Lushoto?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE: LUDOVICK J. MWANANZILA) ali jibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shule ya Sekondari ya Magamba ilifungwa ili kutoa nafasi ya kufungua Chuo Kikuu katika majengo ya shule hiyo. Serikali iliridhia mpango huo kwa lengo la kuongeza nafasi za Vyuo Vikuu katika nchi yetu. Kwa sasa Serikali haina mpango wa kujenga shule mpya ya sekondari ya Kidato cha 5 na 6 katika eneo alillitaja Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, shule za sekondari za Kidato cha 5 na 6 ni za Kitaifa, hupokea wanafunzi kutoka Mikoa yote.

Kwa hiyo, shule ya Sekondari ya Magamba kubadilishwa kuwa Chuo Kikuu, hakuathiri wanafunzi kutoka wilaya ya Lushoto kupata nafasi za Sekondari za kidato cha 5 na 6 katika shule nyingine zilizopo nchini. Hata hivyo, Wizara iko tayari kushirikiana na Wananchi wa wilaya ya Lushoto kupandisha daraja mojawapo ya shule za sekondari zilizopo kuwa sekondari ya kidato cha 5 na 6.

Na. 121

Wavuvi Kupatiwa Ulinzi

MHE. PETER J. SERUKAMBA aliuliza:-

Kwa kuwa, uvuvi ni njia mojawapo ya kuondoa umasikini kwa watu wa Kigoma; na kwa kuwa, uvuvi ndani ya Ziwa Tanganyika umekuwa sio salama, kwani wavuvi wengi wanavamiwa wakiwa Ziwani na kunyang'anywa mali zao na kuhatarisha uhai wao:-

(a) Je, ni lini Serikali itafanya mpango madhubuti wa kulinda raia wake wakiwa Ziwani?

(b) Je, kuna utaratibu wowote wa kuwafidia watu wanaonyang'anywa mali zao na kuhatarisha uhai wao?

NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA ali jibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama na Raia, napenda kumjibu Mheshimiwa Peter Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Serukamba kwamba yamekuwepo matukio ya wavuvi kunyang'anywa mali zao. Serikali inalitambua tatizo hilo na inachukua jitihada ili kuimarisha ulinzi kwa kuongeza nguvu katika Vituo vidogo vya Polisi vya Kibirizi, Kagunga, Sigunga, Mgambo na Kalya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuongeza nguvu za Jeshi la Polisi hivi sasa linaendelea kukamilisha matengenezo ya boti za doria, ambapo mara baada ya matengenezo kukamilika itasaidia kuimarisha ulinzi katika eneo hilo. Aidha, Jeshi la Polisi lina mpango wa kununua boti mpya za doria kwa ajili ya ulinzi katika Maziwa Makuu na Baharini.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia inaendelea na mazungumzo ya pamoja na nchi jirani ili kuona namna ambavyo wahamiaji na wageni haramu watakavyoweza kudhibitiwa na kurejeshwa makwao.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haina sheria ya kuwalipa fidia wananchi waliojajiri wenyewe. Hata hivyo, wavuvi hao wanayo fursa ya kujiwekea Bima za maisha na mali zao.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza swali mawili madogo ya nyongeza. Jibu lake la msingi amesema boti inafanyiwa ukarabati, lakini kipindi sasa kimepita wananchi wanauawa na wananyang'anywa mali zao. Tutakuwa na haraka ipi sasa ili hiyo boti iweze kuokoa maisha ya watu?

Swali la pili, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema mpango wa muda mrefu ni kununua boti za mashua kwa ajili ya kufanya *patrol* katika Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, watanzania wenzetu wanauawa na wananyang'anywa mali zao hatuoni umefika wakati wa kuwa na mpango wa muda mfupi kuliko kuwa na mpango wa muda mrefu? (*Makofit*)

NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAI: Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Peter Serukamba kwamba boti ile ambayo ipo kule Kigoma imeshafikia hatua za mwisho na sasa lina tatizo la *radar*, lakini tunalishughulikia tatizo hilo na mara tukimaliza tatizo hilo, hiyo boti itaanza kufanya shughuli za kuendelea kupambana na wahalifu katika eneo lile.

Mheshimiwa Spika, lakini ningependa Mheshimiwa Peter Serukamba aelewe kwamba Serikali inachukua hatua mbalimbali za kupambana na uhalifu na ndiyo maana

tukapanga mipango ya muda wa dharura, muda wa kati na muda mrefu. Tunajua tatizo lililopo katika maeneo hayo na ndiyo maana Mheshimiwa Waziri Mkuu alilingilia kati tatizo hilo kwa kuongeza *operation* maalum za kupambana na wahalifu katika maeneo ya mipaka kwa kushirikisha vyombo vyote nya dola.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Peter Serukamba na wananchi wote wa eneo lile kwamba sasa *operation* zimeanza rasmi na usalama wa watu wetu katika maeneo yale inachukuliwa kila hatua ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu na mali zao wako salama. (*Makofî*)

MHE. AHMED ALLY SALUM: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Tarafa ya Nindo Kata ya Sarawe kuna tatizo kubwa sana la matukio ya ujambazi. Na ninamshukuru sana *RPC* wa Mkoa wa Shinyanga alipeleka Polisi katika Kata ya Sarawe, lakini hawana ofisi wala sehemu ya kulala. Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia Polisi ili kujenga ofisi.

SPIKA:Hilo ni swali jipya kabisa. Kinachozungumziwa sasa ni ujambazi katika Ziwa Tanganyika. Sasa inaweza kuwa pia ujambazi au unyang'anyi katika maziwa yoyote mengine. Lakini Askari wa nchi kavu na ujambazi huo mwingine kwa sasa hauhusiani.

MHE. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa inafahamika kabisa kwamba wizi na unyang'anyi unaotumika katika *Lake Tanganyika* umekwisha kuwa sugu na kutokana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba inafanyika *operation*. Anaweza akatuthibitishia ni *operation* gani iliyofanyika katika Ziwa Tanganyika wakati boti ni mbovu? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA: Mheshimiwa Spika, kama alivyonisikia wakati nikijibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Peter Serukamba nimesema tunafanya *operation* ya vyombo vyote nya dola si boti zote ambazo ni mbovu. Vipo vyombo vingine nya ulinzi ambavyo tunasaidiana navyo katika kufanya *operation* hiyo. Ninachoomba wananchi wavute subira waone matokeo hayo. Hata hivi sasa ukiangalia matukio ya uhalifu yameanza kupungua katika Ziwa Tanganyika.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swalii moja la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Kwanza katika miaka ya 1980 ilitambua umuhimu wa kulinda Maziwa yetu na ikaagiza boti saba kutoka Yugoslavia ili zifanye kazi hiyo. Boti hizo zilipelekwa Musoma, Mwanza, Bukoba na boti moja ikapelekwa kule kwetu Kigoma – *Lake Tanganyika* ili isaidie. Lakini je, kwa nini Mheshimiwa Naibu Waziri kama anaona kuna matatizo ya kutumia boti hizo ambazo mimi mwenyewe ninazifahamu na niliwahi kuzitumia ni nzuri sana kama zina matatizo kwa nini wasiziuze ili wakapata fedha za kununua boti nyingine?

NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA: Mheshimiwa Spika, licha ya kufanya ukarabati wa boti ambazo tunazo, lakini katika jibu langu la msingi nimeeleza kwamba nia ya Serikali ni kununua boti mpya. Hivi Serikali ina mpango gani wa kununua boti tano mpya wakati mahitaji hasa ni kuwa na boti tisa. Hivi sasa tunazo boti mbili ambazo ziko katika bahari na ni nia yetu katika kipindi si cha muda mrefu sana kuweza kununua boti zingine. Lakini hasa tunataka tuhakikishe tunakuwa na boti tano za ziada kwa nia ya kufanya kazi hiyo.

Na. 122

Gari la Doria Tarafa ya Kigamboni

MHE. MWINCHOUM A. MSOMI aliuliza:-

Kwa kuwa, kwa muda mrefu sasa Tarafa ya Kigamboni imekuwa haina gari la uhakika kwa Polisi kufanya kazi ya Doria; na kwa kuwa, Tarafa hiyo inapanuka kwa kasi sana:-

- (a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua tatizo hilo, badala ya kutegemea doria ya Kongowe?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha huduma za ulinzi na usalama wa raia katika Tarafa hiyo?

NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia , napenda kumjibu Mheshimiwa Mwinchuom Msomi, Mbunge wa Kigamboni, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kufahamu tatizo la ukosefu wa gari la doria linaloikabili Tarafa ya Kigombani kwa muda mrefu na kwa kufahamu kuwa Tarafa hiyo inapanuka kwa kasi kubwa, mnamo tarehe 3 Februari, 2006, Serikali ilikipatia Kituo cha Polisi, Kigamboni gari jipya ainaya *Landrover Defender 110/UP* lenye namba za Usajili PT.0967. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa ushirikiano mkubwa na Jeshi la Polisi.

(b) Mheshimiwa Spika mpango ilionao Serikali katika kuimarisha huduma za ulinzi na usalama katika Tarafa hiyo ni pamoja na kuimarisha doria za askari wa miguu na kwa kutumia gari hilo jipya. Vilevile Serikali kupitia Jeshi la Polisi ina mikakati ya kuimarisha doria katika maeneo mbalimbali yasiyopitika kwa gari kwa kutumia pikipiki ili Askari wetu waweze kuzifikia Kata zote mara kwa mara na pia kupata taarifa za uhalifu kwa njia ya ulinzi shirikishi jamii. Mpango huu umeanzishwa na unatekelezwa nchi nzima.

MHE. MWINCHOUM A. MSOMI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa katika Kata za Kibada, Somangira, Kipiji, Pembamnazi hadi Kisarawe II, Kata hizo mpaka sasa hazina huduma za Polisi. Tunategemea Kituo kimoja tu cha Kigamboni. Je, Serikali haioni kwamba kwa sasa kuna umuhimu wa kujenga Kituo kikubwa cha Polisi cha kuweza kukidhi maeneo hayo?

NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA: Serikali inatambua tatizo la upungufu wa Vituo vya Polisi katika Kata hizo. Lakini Serikali ina sera kwa wale wananchi wanaojitokeza wenyewe kuanzisha ujenzi wa Vituo vya Polisi na Serikali inaongeza nguvu zake. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na wananchi wa Kata hizo kuanzisha mpango wa kujenga wa Vituo vya Polisi katika maeneo hayo na Serikali itaongeza nguvu katika utekelezaji huo. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. CHACHA Z. WANGWE: Ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali inafanya juhudzi za kumaliza ujambazi na pia ina mpango wa kuwashirikisha wananchi kikamilifu ili kuweza kuimarisha ulinzi katika kila sehemu ya nchi yetu. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kulegeza masharti ya kupata silaha ili kila mwananchi aweze kuwa na silaha na ulinzi utaimarika zaidi?

NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA: Mheshimiwa Spika, Serikali ina utaratibu wake katika kuhakikisha kwamba wananchi wanamiliki silaha hizo. Lakini ningependa nimwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa taaarifa tulizonazo mara nyingi wale wananchi ambao wanamiliki silaha wanapovamiwa na majambazi ndiyo hao wanaathirika na kusababisha matatizo makubwa. Na wananchi wengi sasa wenyе silaha wananyang'anywa silaha zao na silaha hizo zinatumika kwenye ujambazi. Kwa hiyo, tuna utaratibu maalum wa kuhakikisha kwamba tunatoa silaha kwa utaratibu maalum ambao hautasababisha matatizo hayo yaliyojitokeza.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali ndogo la nyongeza. Kwanza, nalipongeza sana Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri ya kudhibiti hali ya ujambazi nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na swali la msingi alilouliza Mheshimiwa Mwinchuom Msomi kuhusiana na suala la doria. Ujambazi ni ujambazi. Sisi kule kwetu pamoja na ujambazi huu kwa kutumia silaha kuiba katika maduka ya watu. Lakini upo wizi wa ng'ombe na huu wizi wa mifugo umeenea sana. Lakini tuna matatizo ya magari kwa ajili ya kufanya doria. Je, Wizara sasa iko tayari kutoa magari ya doria kwa maeneo ya wafugaji ili kuweza kudhibiti wizi wa ng'ombe? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA: Mheshimiwa Spika, kwanza tunapenda tupokee pongezi za Mheshimiwa Juma Kilimbah na tunamshukuru sana kwa pongezi hizo.

Mheshimiwa Spika, tatizo letu si kwamba tunaona tabu kugawa magari kwa kila eneo kwa ajili ya kufanya shughuli za kupambana na uhalifu. Tatizo letu ni hali halisi ya uchumi wa nchi yetu. Kwa hiyo, tunagawa magari kutokana na mahitaji halisi ya eneo hilo. Lakini tutafanya kila jitihada kuongeza idadi ya magari kwa nia ya kusaidia Vituo vya Polisi mbalimbali kupambana na uhalifu. Katika mwaka huu wa Fedha tunatarajia kununua magari mpya mengine 70. Tunachowaomba Waheshimiwa Wabunge waipitishe kwa kishindo bajeti yetu ili tujenge uwezo wa kushughulikia Vituo vyote vya Polisi hapa nchini. (*Makofi*)

Na. 123

Ziwa Nyasa kuwa Ramsar Site

MHE. JACKSON M. MAKWETTA (k.n.y. MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI) aliuliza:-

Kwa kuwa, ni muda mrefu sasa tangu kuwepo na mpango wa kulifanya Ziwa Nyasa kuwa *Ramsar Site* kwa ushirikiano na nchi za Malawi na Msumbiji:-

Je, mchakato huo umefikia hatua gani mpaka hivi sasa?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la Kuhifadhi Maliasilli Duniani yaani *The World Wide Fund for Nature (WWF) – Living Waters Programme*, mwezi April, 2003 ulianza mchakato wa kutambua Ziwa Nyasa kwa upande wa sehemu ya Tanzania kuwa linakidhi vigezo vya kuliwezesha kutambuliwa kuwa ardhioevu yenyе umuhimu wa Kimataifa (*The wetland of International Importance (Ramsar Site)*). Taarifa za Kitaalamu zilikusanywa na kuonekana kuwa Ziwa hili lilikuwa linakidhi kuwa ardhioevu yenyе umuhimu wa Kimataifa. Wizara ilituma taarifa ya kuwa eneo la Ziwa Nyasa linafaa kuwa eneo la *Ramsar* kwa Sekretarieti ya Mkataba na nakala *WWF – Living Water Programme* mwezi Januari, 2004.

Mheshimiwa Spika, kutangaza eneo la ardhioevu kuwa lenye umuhimu wa Kimataifa ni utekelezaji wa nguzo ya pili ya Mkataba wa Ardhioevu (*Article 2 of the Convention on Wetlands*). Kutangazwa kwa ardhioevu yenyе umuhimu wa Kimataifa kunafanywa na nchi mwanachama wa Mkataba peke yake na siyo kwa pamoja kama swali liliyoulizwa, japokuwa nchi jirani zinaweza kushirikiana katika kusimamia na kuhifadhi ardhioevu ambayo wanachangia kwa vile inavuka mipaka ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo Serikali yetu kwa kushirikiana na Serikali ya Malawi iko katika mchakato wa kutekeleza programu ya Bonde la Mto Songwe, ili kudhibiti kuhamahama kwa mto. Hivyo kusababisha mpaka wa Kimataifa kati ya nchi yetu na Malawi, pia kuhama. Kutokana na hayo Wizara yangu ilibidi isitishe kwanza zoezi la kulifanya Ziwa Nyasa kuwa *Ramsar Site* hadi hapo suala la mpaka wa Kimataifa kati ya nchi yetu na Malawi litakapopatiwa ufumbuzi.

MHE. ANIA S. CHAUREMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kuwepo kwa mpango wa Ziwa Nyasa kuwa *Ramsar Site* kwa pamoja na ushirikiano wa nchi ya Msumbiji na Malawi. Ningependa kujua ni kwa nini maeneo haya yamepewa jina la *Ramsar Site*? Maana ya *Ramsar Site*.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, labda kwanza ningeeleza *Ramsar* ni mji mdogo uliopo nchini Iran. Mwaka 1971 nchi 18 zilikutana katika Mji huo ili kutia saini Mkataba wa Kimataifa wa Kuhifadhi Ardhioevu. Hivyo basi, jina hilo nalo likawa limechukuliwa kuwa na maana ya ardhioevu ambayo inatambuliwa umuhimu wake Kimataifa. (*Makofi*)

SPIKA: Ninamshukuru sana Mheshimiwa Ania Chaurembo kwa swali lake hili ambalo hata Spika, ameelewesha. Mnajua mimi siwezi kuuliza maswali. Nilikuwa sijui kabisa hiyo *Ramsar Site*. Ahsante sana.

Na. 124

Uharibifu wa Miundombinu ya TTCL

MHE. RAYNALD A. MROPE aliuliza:-

Kwa kuwa, Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*) imetangaza zawadi nono kwa watakaofanikisha kukamatwa kwa wanaoharibu miundombinu yake; na kwa kuwa, uharibifu huo umefanyika nchi nzima:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupambana na tatizo hilo?
- (b) Je, Serikali haioni kwamba, sasa umefika wakati muafaka wa kuondokana na teknolojia ya *fixed terrestrial and line* na *Digital Satellite Communication* ili kuondokana na hasara kubwa ya uharibifu wa miundombinu ya waya?
- (c) Je, Serikali ina mpango gani katika kuiwezesha *TTCL* kutoa huduma ya simu za mkononi mapema iwezekanavyo badala ya kuiacha kutoa huduma hiyo ya *Fixed Land and Release*?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-(a) Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*) ikishirikiana na Jeshi la Polisi imepambana na wezi na waharibifu wa miundombinu ya simu, kwa kutoa kikosi maalumu cha Askari Polisi tangu mwaka 2001 kwa ajili ya kupambana na wahalifu hawa. Hadi sasa wahalifu wapatao 620 wametiwa mbaroni kwa tuhuma za kuhujumu miundombinu ya *TTCL* ambapo kesi zipatazo 338 zimesajiliwa katika Mahakama mbalimbali kwa nchi nzima, kati ya hizo kesi 285 ziko Mahakama ya Kisutu Dar es Salaam, hali inayoonyesha kwamba wimbi kubwa la uhalifu liko Dar es Salaam. Aidha, mafanikio haya pia ni matokeo ya mkakati wa kutangaza motisha wa zawadi nono zinazotolewa na *TTCL* kwa siri.

(b) Mheshimiwa Spika, teknolojia ya *Digital Satellite Communication* inahitaji mtaji mkubwa ili kuweza kujenga mtandao wa *Satellite*. Maeneo mengi hapa Tanzania haya idadi kubwa ya watumiaji wa huduma hii ya *Satellite*, hivyo kujenga *Earth station* kwenye maeneo yenye wateja wachache itakuwa ni gharama kubwa isiyolipa kibiashara. Teknolojia hii ni nzuri na hutumika sana sehemu zenye mawasiliano magumu ya barabara kwa mfano Kongo (*DRC*), Amerika ya Kusini (Amazon) na hata Msumbiji hadi miaka ya karibuni.

Katika Bara letu la Afrika upo mradi wa *RASCOM*" unaolenga kuanzisha huduma hii ya *Satellite* ambapo pia Tanzania kupitia *TTCL* ni mwanachama. Napenda kuwalishwa Waheshimiwa Wabunge kwamba, kwa hivi sasa huduma ya *Digital Satellite Communication* tayari inatolewa hapa nichini kupitia wakala binafsi kutoka mtandao wa *satellite* wa Inmarsat na Thuraya lakini ukweli ni kwamba ni wale wachache wenye uwezo kifedha ndio wanaofaidika na huduma hii.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia Kampuni ya Simu Tanzania ipo mbioni kuanzisha simu za mkononi kwa kutumia teknolojia ya *Code Division Multiple Access (CDMA)* Huduma hii tayari imeanza kutolewa tangu mwanzoni mwa mwezi Aprili, mwaka huu katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Mwanza. Juhudi hizi zinaendelea hasa baada ya kupata leseni kutoka Mamlaka ya Udhiliti wa Mawasiliano Tanzania -*TCRA* ya kutoa huduma hiyo.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa simu za mkononi sasa hivi ndiyo zinazotegemewa zaidi huko Vijijini hasa katika Mikoa ya Lindi na Mtwara kutokana na uharibifu mkubwa wa hizi nyaya za simu. Serikali inafikiria mpango wowote wa kupunguza gharama za simu za mkononi baada ya kupitisha bajeti yetu mpya hiyo ambayo makali yake yataanza kuonekana kesho. Je, Serikali haiwezi kufikiria namna ya kuwasaidia wananchi hawa wa Vijijini?

La pili, bei ya mawasiliano ya simu Tanzania ni aghali sana. Nitatoa mfano, Marekani kwa *dollar* tano unaweza kuzungumza kwa muda wa nusu saa. Ukipiga simu kutoka Tanzania wakati huo huo itakugharimu kama shilingi 200,000.

Sasa kwa mtaji huu Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba simu za mkononi au simu za kawaida Tanzania ni za ku-beep tu au kutuma *message* badala ya kuwa za biashara ya sawasawa? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI): Mheshimiwa Spika, ninakubaliana naye kwamba gharama za simu kwa Tanzania ziko juu kidogo ukilinganisha na Marekani kama alivyosema yeche.

Mheshimiwa Spika, lakini napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inao mpango wa kuweka *Sub-Marine Cable* na vilevile kuweka *landline* kutoka kwenye *junction* ya Dar es Salaam kwenda juu.

Mheshimiwa Spika, mtandao huo utakapowekwa tunaamini utapunguza bei ya gharama za simu kwa kiasi kikubwa sana. Tunamwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira.

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika huu mradi ambao nimeuzungumzia wa *CDMA* ambapo tunategemea Mkoa wa Mtwara, Liwale Nachingwea, Rwanwa, Kipele na kwa Mtwara ni Ndanda, Lilungu, *Mnazibay* na Mahuta watafaidika na mradi huu na tuna hakika mawasiliano kwa kutumia mtandao huu yatakuwa ni ya nafuu zaidi. (*Makofi*)

Na. 125

Barabara zote Nchini kuwa chini ya Wizara ya Miundombinu

MHE. MGENI JADI KADIKA aliuliza:-

Kwa kuwa, kuna wazo kwamba, barabara zote nchini ziwe chini ya Wizara ya Miundombinu:-

(a) Je, Serikali inalichukuliaje wazo hilo?

(b) Je, ni lini Serikali italifanyia kazi wazo hilo ili kuzipunguzia majukumu Serikali za Mitaa ambazo hazina uwezo kifedha?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA) aliuliza:-

Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Barabara (*Highway Ordinance Cap. 167 of 1969*) imeugawanya mtandao wa barabara zote nchini katika makundi ama madaraja yafuatavyo:-

- (i) Barabara Kuu (*Trunk Roads*)
- (ii) Barabara za Mikoa (*Regional Roads*)
- (iii) Barabara za Wilaya (*District Roads*)
- (iv) Barabara za Vijiji (*Feeder Roads*)

Katika mgawanyo huo, vimeainishwa vigezo vinavyotumika katika kuiweka kila barabara katika Kundu husika. Aidha, umiliki wa barabara kuu na zile za Mikoa zenye jumla ya kilometra zipatazo 35,000 upo chini ya Wizara ya Miundombinu. Barabara za Wilaya, Majiji na Miji zenye jumla ya kilometra zipatazo 50,000 zinamiliwi na Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji, chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Zipo pia barabara zinazomiliwi moja kwa moja na watumiaji wake, mfano zile zilizomo ndani ya hifadhi za wanyamapori, maeneo ya machimbo ya madini, mashamba makubwa ya kilimo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wazo la kuziweka barabara zote nchini kuwa chini ya Wizara ya Miundombinu halijafikishwa rasmi Serikalini na chombo chochote, bali limekuwa likiibuliwa na baadhi ya Wabunge kama muuliza swali, kwa sababu zinazolewaka kwa kweli.

Mheshimiwa Spika, tatizo hasa ni kwamba ngazi ya Wilaya na Vijijini hakuna utaalamu wa kusanifu na kujenga barabara nzuri hata katika baadhi ya Halmashauri.

Aidha, hakuna fedha za kutosha, na moyo wa kujitolea uliokuwa vijijini nao umefilia au kutokuwepo. Kitaifa upo ukweli pia kuwa kama barabara zote zingekabidhiwa Wizara yangu fedha nazo hazingetosheleza, na utaalamu nao ungekuwa pungufu kuliko kazi yenyewe. Kwa hiyo, Wizara yangu kwa sasa inachukua hatua zifuatazo kulikabili tatizo hili:-

(a) Itaweka mfumo mpya wa kutumia watalamu waliopo Wizarani, Sekretarieti za Mkoa na *TANROADS* Mkoa kuimarisha utaalamu uliopo Wilayani na Vijijini ili waweze kutengeneza barabara nzuri zaidi.

(b) Itafundisha mafundi wa vijijini chini ya mpango wa *Labour Based Road Construction* wa kutengeneza barabara vijijini kwa teknolojia sahihi.

(c) Itabadili sheria husika kwa lengo la kuwawezesha makandarasi na mafundi wadogo kufanya kazi vijijini.

(d) Mwisho, itaandaa makandarasi wazalendo katika kila Mkao ili wafanye kazi zinazohitaji utaalamu na bora zaidi wa kazi kwa kulipwa na Halmashauri, Mfuko wa Barabara na vyanzo vinginevyo na hivyo kuwezesha uwepo wa barabara zinazodumu zaidi kuliko ilivyo sasa. (*Makofî*)

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ningependa kuuliza suala moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba barabara zilizoko chini ya Halmashauri zinatengenezwa kwa kiwango ambacho sio kizuri kwa sababu ya ukosefu wa utaalalm na ukosefu wa fedha. Kwa sababu amesema sheria inarekebishwa. Swali langu ni kwamba je kwa sasa Serikali iko tayari wakati inafanya mpango wa kurekebisha sheria iko tayari kurekebisha asilimia inayokwenda Halmashauri katika Mfuko wa *TANROAD* walau ifike asilimia 50 kwa 50 ili kuwezesha Halmashauri zetu kuweza kupata fedha za kutosha kwa ajili ya kutengeneza barabara zilizo chini yake?

SPIKA: Majibu Mheshimiwa Waziri, ingawa muda wa maswali umetimia yaani mwisho lakini nafidia ule muda ambao nilikuwa natoa matangazo kuhusu wageni. Kwa hiyo, tunaendelea.

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA): Mheshimiwa Spika, ni kweli sheria inafanywa marekebiso na nia ya Serikali ni kwamba sheria hii ije hapa Bungeni kabla ya mwisho wa mwaka huu. Tunachosubiri sasa hivi ni kuandaa zile *schedules* ambazo zitaonyesha ni barabara zipi zitakuwa bado chini ya Wizara ya Miundombinu na zipi zitakuwa kwenye Halmashauri. Kazi hii imekamilika katika ngazi ya Wizara lakini katika ngazi ya Halmashauri wamemchukua *consultant* wa Benki ya Dunia na ameahidi kukamilisha kazi hii kufikia mwezi Agosti. Kwa hiyo, tunadhani mwezi Novembra sheria hii inaweza ikaja Bungeni.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa muda huu kwa sababu sheria itakuja mwaka huu suala la kubadilisha viwango vya kugawa katika Halmashauri na za kubaki katika Wizara lingesubiri kwa sababu sio muda mrefu na ni mwaka huu. Lakini hata hivyo ningependa kueleza kwamba kwa vyovytote vile itakavyokuwa kwa sababu pamoja na kwamba asilimia kubwa inakwenda Wizarani lakini Wizara inashughulikia barabara ambazo ni *Trunk Roads* na *Regional Roads* na hizi zinahitaji matengenezo makubwa na gharama zake ni kubwa. Lakini tungojee tumalize sheria hizo na Wizara ya Fedha inashughulikia kuangalia mgawanyiko huu na pindi itakapokuwa tayari mtajulishwa rasmi.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge ni vyema tumalize swali la mwisho, swali la Wizara ya Maji.

Na. 126

Uhaba wa Maji Mji wa Mombo

MHE. LAUS O. MHINA aliuliza:-

Kwa kuwa, Mji wa Mombo una hadhi ya Mamlaka ya Mji Mdogo; na kwa kuwa, Mji huo mbali na kuwa na zaidi ya wakazi 3800 pia ni kituo maarufu cha wasafiri wanaotumia barabara ya Arusha – Dar es Salaam na wale wanaokwenda Lushoto; na kwa kuwa, Mji huu una uhaba mkubwa wa Maji tatizo ambalo hata Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne aliliona wakati wa Kampeni zake na kuwahidi wananchi kuwa tatizo la Mji litashughulikiwa haraka iwezekanavyo:-

- (a) Je, ni hatua gani zimeshachukuliwa na Serikali hadi sasa kuondoa tatizo hilo;
- (b) Je, ni lini tatizo la Maji katika Mji huo litakwisha kabisa?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Laus Omar Mhina, Mbunge wa Jimbo la Korogwe Vijijini, lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa kuwa na maji ya kutosha eneo la mji mdogo wa Mombo, Wizara yangu ikishirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe imeweka mpango wa kuondoa tatizo la maji kwenye eneo hilo. Mpango huo ni kufanya uchunguzi wa kupata vyanzo vya maji kwa mji huo, kufanya usanifu wa mradi wa maji wa mji wa Mombo na kujenga mradi.

Mheshimiwa Spika, Mpango huo utatekelezwa katika Programu ya Taifa ya Maji na Usafi wa Mazingira itakayoanza kutekelezwa kwenye mwaka wa fedha 2006/2007. Katika programu hiyo upembuzi yakinifu utafanywa ili vipatikane vyanzo vya maji vya kutosheleza mahitaji katika Mji wa Mombo. Aidha, baada ya usanifu wa kina kufanyika, utekelezaji wa mradi utafanyika kwa kutumia fedha za programu.

Mheshimiwa Spika, wakati tukisubiri utekelezaji wa mpango nilioutaja hapo, Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe imetenga jumla ya shilingi milioni 12.5 katika mwaka 2005/2006 kwa ajili ya ukarabati wa mradi wa maji katika mji wa Mombo. Ukarabati unaendelea na mara utakapokamilika upatikanaji wa maji utakuwa umeongezeka kutoka mita za ujazo 261 kwa siku hadi kufikia mita za ujazo 340 kwa siku.

MHE. LAUS O. MHINA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swalii la ziada.

Kwa kuwa vitongoji vya mji wa Mombo na vijiji vingi katika jimbo la Korogwe vijijini ni kuwa kulikuwa na visima vifupi vinavyotumia pampu za mkono. Asilimia 50 ya pampu hizi zimekufa. Nataka kuuliza je, Serikali ina mpango gani kufufua pampu hizi

ili kuondoa adha inayowapata akinamama, dada zetu na wake zetu kufuata maji kwa umbali zaidi?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, Wizara yangu katika kutekeleza huduma za maji kwa upande wa Jimbo la Korogwe na Wilaya ya Korogwe nzima kuna miradi ya maji ambayo kwa sasa inafufuliwa na Halmashauri imeshaleta maombi ya fedha. Miradi hiyo ikiwemo visima vifupi 8 pamoja na *Water Supply* mbili ikiwemo ya Hale na ya Kwamsisi na hivyo visima nilivyotaja.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali sasa umekwisha na maswali yenye we yamekwisha pia.

Matangazo. Tangazo kutoka kwa Dr. Slaa, Katibu Mkuu wa *APNAC*. Wajumbe wote wa Kamati ya Utendaji ya *APNAC* mnaombwa kukutana leo tarehe 30 Juni, 2006 saa tano asubuhi ukumbi namba 219 ghorofa ya pili.

Mheshimiwa Susan Lyimo, Mwenyekiti wa Kamati ya *Strategic Plan* ya *Tanzania Women Parliamentary Group* anawatangazia Wajumbe wote wa Kamati ya Kutengeneza *Strategic Plan* wakutane yeze anasema nje ya ukumbi, nadhani nimsaidie. Nje ya ukumbi eneo karibu la Kantini. Kwa sababu eneo ni kubwa mno ikiwa nje ya ukumbi watatangatanga tu. Kwa hiyo nadhani waelekee karibu ya Kantini halafu watasikilizana kama hapo hapawafai mara baada ya kipindi cha maswali na majibu. Ni muhimu sana anasisitiza Mwenyekiti huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo na Ardhi, Mheshimiwa Gideon Asumulike Cheyo anawaomba Wajumbe wote wa Kamati hiyo ya Kilimo na Ardhi kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo leo tarehe 30 Juni, 2006 saa saba mchana ukumbi namba 219. Nadhani huu mkutano mwagine wa Dr. Slaa utakuwa umekamilika kwa sababu ni ukumbi huo huo wa tangazo la awali. Kwa hiyo Kamati ya Kilimo na Ardhi wao ni saa saba mchana wakati *APNAC* ni saa tano asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge ninao wachangiaji wanne amba ni sawa sawa kabisa na kutimiza muda wetu ukiacha dakika chache tu. Ninayo taarifa Mheshimiwa Savelina Mwijage hayupo amesafiri tangu jana aliniomba Mheshimiwa Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi achukue nafasi hiyo. Kwa hiyo, namwita yeze sasa atafuatiwa na Mheshimiwa John Shibuda CCM Maswa, Mheshimiwa Laus Mhina CCM Korogwe Vijijini na atakayefunga dimba ni Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Mbunge wa Chalinze, CCM.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali Kwa Mwaka 2006/2007 Ofisi ya Waziri Mkuu

(Majadiliano yanaendelea)

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nichangie hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, mimi ningeungana na wenzangu pia kumpongeza Waziri Mkuu na Ofisi yake kwa jumla kwa kuwasilisha hotuba nzuri ambayo imetupa mwelekeo. Pia nitachukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kasoro moja tu kuwa Mwenyekiti wetu.

Mheshimiwa Spika, tunesikia kwenye Bunge hili kwamba labda tutapoteza muda mwingi kupongeza lakini sasa tutafanya nini kama mtu amefanya kazi nzuri. Ni ada hiyo kwamba mtu anapofanya kazi nzuri anapongezwa. Kama mnavyofahamu ndani humu kuna *tension* sasa ni lazima kuwe na *element* ya *relaxation* sasa tunapongeza basi mjue hivyo tunatiana moyo.

Mheshimiwa Spika, mimi nimpongeze sana Waziri Mkuu kwa kuwasilisha bajeti nzuri yenyewe mwelekeo. Niungane na ndugu yangu Missanga aliyezungumza kuipongeza Serikali kwa kutuletea Mkuu wa Mkoa mpya. Namshukuru sana tunayo Mheshimiwa Kone ni mtu anayehimiza maendeleo, mtu anayeshawishi maendeleo katika muda wa kipindi kifupi tumeona kwamba tunaweza tukasonga mbele. Kwa bahati mbaya sana na mwenzake aliyeondoka tulimzoea Kanali Tarimo alitusukumia sana maendeleo na basi kama ilivyo taratibu imebidi ahamie kituo kingine. Kwa hayo kwa kweli tumenufaika na nadhani mchango wa Mheshimiwa Kone utatusaidia sana kuhimiza maendeleo ya Mkoa wetu. Singida kwa muda mrefu ilikuwa imekuwa kama *military outpost*. Tumekuwa na watu hawa tulikotokea Brigadia Moses Mhauye, huyu alitusaidia sana kwenye masuala ya utamaduni tulicheza sana ngoma alihimiza sana upande huo basi hatukukaa sawa sawa akaja Meja Jenerali Silas Mayunga kutoka hapo akaja Luteni Peter Kafanabo hatukukaa akaja Meja Jenerali Mwita Marwa upande wa Serikali. Upande wa chama tukawa na Brigadia Mwakanjuki basi ni *salute* tu maofisini humo mpaka tukawa na wasi wasi kuwa huu mkoa ni wa jeshi au nini, mara nyingine tulifikiri labda tuko Nigeria au wapi. Lakini nadhani ilikuwa ni katika kuhimizana na nadhani safari hii tutakuwa *serious* katika kuleta maendeleo katika mkoa wetu.

Mheshimiwa Spika, tunaposimama kuchangia labda kuna umri wa kufanya hivyo lakini utailaumu nini Serikali ya sasa hivi kwa sababu ndiyo kwanza inaanza. Lakini tunachosema ni kwamba tunahimiza isiangukie katika *past mistakes*. Makosa ya nyuma ndicho hasa tunachozungumzia. Kwa sababu mimi sidhani nitalaumu nini hapa kwa sababu hawa watu ndio kwanza wametupanga, ndiyo kwanza bajeti ya kwanza mimi nadhani mwakani hasa tutakapokuwa tunagomba tunakuwa *justified* kwa nini tunagomba. Lakini safari hii ni lazima tugombe tuna-*quotation* kwamba jamani *past performance* kumekuwa na *mistakes* hizi na hizi sasa tusije tukarudia hizo *past mistakes*.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba kuchangia katika maeneo machache lakini nimeona tatizo kubwa kwa upande wa Serikali kuwa ni tatizo la takwimu. Kuna Mheshimiwa mmoja aligusia hilo juzi lakini kwa kweli takwimu zetu zimekuwa si sahihi mara nyingi. Sasa bila ya kuwa na takwimu sahihi huwezi ukapanga vizuri maendeleo. Hata juzi juzi katika jimbo langu unasema mtu unapeleka chakula lakini hujui idadi

kamili ya watu wa eneo hilo. Mimi katika kikao cha tatu nilishangaa sana nilipokuwa najibiwu swali langu la nyongeza. Katika swali langu la msingi nilitaka kujua uwezekano wa kugawa Wilaya yetu ya Manyoni kutokana na ukubwa wake na kwa muda mrefu Wilaya hiyo toka wakati wa ukoloni imekuwa nyuma tukafikiri labda tungeweza kuhimiza maendeleo kwa njia hii. Lakini nilikuja kushangaa nikaambiwa kwamba ninyi bado kwa sababu kwanza *scarcely populated* maeneo yenu hayana watu yakaainishwa vigezo vikawekwa kwamba mnatakiwa mtimize vigezo hivi na hivi. Sasa nikaambiwa kwamba mimi eneo langu lina watu 67,000, lina vijiji 17, lina Kata 5 sasa mimi kama Mbunge wa CCM siku ile niliamua kunyamaza tu maana nikianza kugombana na Mheshimiwa Waziri kwamba si hivyo. Basi niliona afadhali ninyamaze nikajaribu kuangalia mara mbili nilipomwuliza Mkurugenzi wangu akasema bwana takwimu hizo si sahihi. Nikawaambia sasa nani alimpelekea Waziri? Akasema hajui.

Mheshimiwa Spika, mimi nimechaguliwa na watu wa Kata 7 vijiji 25 na vitongoji 13. Nimeshiriki katika chaguzi toka mwaka 2000 nimeyajua maeneo yangu yote sasa nakuja kuambiwa kwamba wewe bwana una Kata 7. Mimi nina Kata ya Idoduyandole ambako kuna Idoduyandole, Kashangu, Mbugani hivyo ni vijiji halafu na vitongoji vya Mirumbi, Ipangamasasi, Madibila, Jeje A na Jeje B, hiyo ni Kata moja. Nina Kata ya Ipande ambayo ina vijiji vya Ipande, Muhamanga, Jilimuli na Damweru. Tatu nina Kata ya Aghondi, ambaye kuna Kata ya Aghondi, Kamenyanga, Njirii na kitongoji cha Mabondeni. Nne, kuna Kata ya Sanjaranda ambaye ina Kata ya Sanjaranda, Gurungu, Kitopeni. Nina Kata ya Itigi ambako kuna Majengo, Mlowa, Itigi Mjini, Doroto na Kitaraka na vitongoji vya Genge Namba 48 halafu Kahomwe na Bangayega.

Mheshimiwa Spika, nina Mgandi ambapo kuna Itagata A na Itagata B, Kayui, Makale Mtakuja, Mitundu Kalangali. Vitongoji viko vya Ipalalyu na Uswesanoni. Kata ya 7 ni Rungwa ambaye ina vijiji vya Mamagembe, Kintanula na Rungwa yenyewe. Sasa inabidi nitoe takwimu sahihi ielewewe labda pengine hizi ofisi hazina hizi takwimu. Mimi ningombaa sana tunapokuwa tunapanga mambo tuwe na takwimu sahihi tunaelewa ni nini tunashughulika nacho. Hata juzi nilishangaa katika jibu la msingi kuhusu walemvu Serikali imekiri kabisa inasema kabisa kwamba Serikali haina idadi kamili ya watu wenye ulemavu wenye shahada au stashahada walipo ndani na nje ya nchi. Ikaendelea pia ikasema pia Serikali haina idadi kamili ya watu wenye ulemavu Mameneja, Wakurugenzi, Wawakilishi sasa kama hawa watu amba wana vyeo vya namna hii hawajulikani haina idadi je sembuse mlemavu ambaye yuko vijijini.

Mheshimiwa Spika, ningeliomba sana kwamba Serikali iwe na takwimu sahihi kundi hili linalalamika sasa hivi kwa sababu linaonekana kama Serikali haiwajali. Mimi nadhani wangeainishwa hao walemvu wote, kuna wenye uwezo pengine lakini wengi wao hawana uwezo basi liwekwe katika kundi la kuweza kupewa kipaumbele katika shughuli za elimu. Waweze kupewa elimu, wengi wana vipaji vizuri sana. Miaka michache tulishuhudia jinsi Tony Blair alimteua Waziri wa Mambo ya Ndani asiyeona alifanya maajabu sana na ndiye alikuwa anamtegemea. Alikuwa akisoma Bajeti yake kwa njia ya kutumia *braille* na kwa kawaida watu wa aina hiyo hawana gharama kubwa wao ni ofisini na nyumbani. Matumizi ya ajabu ajabu hawana. Mimi ningeliomba sana

kwamba ninakazia sana suala la takwimu ili tunapofanya mambo tufanye kazi kwa makini na tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho ningeweza kuchangia hapa ni suala la mipaka. Katika hotuba ya Waziri Mkuu amesema atashughulikia suala la mipaka. Sisi sensa ya mwaka 2002 hatukujua kabisa kwamba baadhi ya vijiji havikuhesabiwa upande wetu vilihesabiwa upande wa Sikonge. Sasa watu wa namna hiyo wanaumbuliwa. Hii barabara ya kutoka Itigi kwenda mpaka Mbeya kuna vijiji hivi ambavyo nilivitaja. Lakini unapofika Kalangali unafika Kiyombo ndio sasa unaingia Sikonge. Kirumbi, Sikonge, halafu ndio unatoka unakwenda Mwamagembe Manyoni, Kintanula - Manyoni, Rungwa - Manyoni, hivi hawa hata watu wa Kiyombo maana watu wa Kalangali wanaambiwa waende Sikonge ni nani atakubali kwa sababu wanachotaka ni huduma.

Mheshimiwa Spika, mimi ningeliomba kwamba sisi kwa mfano Kalangali pale ninayoigombania iende upande wa Sikonge ni kwa misingi ipi ni ukabila au nini? Kwa sababu watu tumejenga shule pale, tumejenga hospitali na watu wanapata huduma kilomita 50 kutoka Kalangali kuja Itigi kiasi cha namna hiyo. Lakini mtu anayetoka huku ambaye yupo Kiyombo ambaye wanasema yupo Sikonge anaposafiri Mwalimu pale kufuata mshahara anatumia shilingi 15,000/= . Anatoka pale anakuja Itigi kuja kupanda treni halafu anakwenda Tabora analala aondoke kufunga safari ya kwenda Sikonge Makao ya Wilaya, halafu kesho alale pale hiyo ni gharama ya kulala na chakula ni nyngine halafu kesho yake ageuze sijui siku ngapi halafu kesho tena arudi kwa *route* ile ile. Akitaka aende kwa upande mwingine inabidi aende mpaka Rungwa, halafu Kihwele, apande magari ya Makongolosi kule. Kihwele aende tena Makao Makuu ya Wilaya. Sasa hivi kweli huo ni uungwana kweli? Sidhani kama ni uungwana kwa sababu unamtendea vipi huyu Mwalimu kweli atatulia. Wacha Walimu tu lakini hata mwananchi awe na shida. Kwa hiyo, mimi nilifikiri mipaka yetu iangalie ni huduma gani zilizoko pale.

Mheshimiwa Spika, mimi ningeliomba sana suala hili lingeshughulikiwa haraka ili watu wetu wa Kalangali waweze kufanya maendeleo kwa utulivu sio kwa ajili ya misingi ya ukabila ili kusema kwamba ninyi ni watu wa huku au Chifu nani alikuwa huku. Sasa hizi ni nyakati nyngine. Kama tunadai uchifu hata sisi wengine tulikuwa machifu tunaweza tukadai. Lakini mambo haya yalishapitwa na wakati tunasonga mbele. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho ningependa kuchangia nampongeza Waziri wa Miundombinu. Nimeona katika Ilani barabara ya kutoka Rungwa mpaka Itigi ambayo imeainishwa kwamba nafikiri mwakani itawekwa katika mpango wa kujengwa kwa lami.

Kwa sasa hivi inaimarishwa. Lakini inapokuja Itigi amesema kwamba inakwenda mpaka Isuna. Hapana inakwenda mpaka Mukwa wasahihishe hapo. Huu ukurasa wa 24 wa kitabu cha Ilani hapa ni kutoka Rungwa/Itigi/Mukwa. Sasa wamesema kwamba imewekwa katika ilani kwamba itaimarishwa. Lakini kwenye maagizo tungependa kweli iimarishe.

Mheshimiwa Spika, tulioona barabara.....

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge, kengele ya pili hiyo.

MHE. JOHN P. LWANJI: Ahhaa!!!! Naunga mkono hoja Mheshimiwa Spika, Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. JOHN M. SHIBUDA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipatia fursa hii ili na mimi niweze kuchangia katika mjadala wa hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu na kuhusu Mapitio ya Mwelekeo wa Kazi za Serikali na Makadirio na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kwamba hii ndiyo mara yangu kwanza naomba kunena kwa heshima na taadhima na nampongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kuwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Vile vile naomba kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Shein kwa kuwa Makamu wa Rais na vile vile napenda kumpongeza Mheshimiwa Aman Abeid Karume kuwa Rais wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar na vile vile napenda kutambua kwamba hivi sasa tuna Mheshimiwa Makamba, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi naye nampongeza na nawapongeza Wabunge wote kwa teuzi walizopata katika Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wahenga husema aliyepewa na Mola hapokonyeki. Naomba kumtambua Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwamba ni nyota ya jaha kwa awamu yetu ya nne na naomba Mwenyezi Mungu amjalie hekima na baraka zake katika shughuli zake zote.

Vile vile napenda kumtambua na kumpongeza Mheshimiwa Lowassa kwa ushindi wake wa kishindo wa kuwa Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Monduli na hatimaye kuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Tanzania. Vile vile napenda kutambua ushindi wako Mheshimiwa Spika wa Jimbo la Urambo Mashariki kwamba ni ushindi wa kishindo na vile vile naomba nitambue ushindi wako wa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nakupongeza kwa vipaji na bashasha ulizonazo ambazo hazimtoshi mtu kupata maongozo yako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi wa shukrani sasa naomba nirejee katika kuchangia hotuba na ajira ya Serikali. Waungwana husema usione chaelea kimeundwa.

Awali ya yote leo tumempata Mheshimiwa Makamba mtani wetu, lakini napenda kumwambia mtani wangu ya kwamba ukitaka kuingia katika nyumba sharti ufute vumbi la sivyo utakuta nguo zako zimeliwa na mende. Vile vile napenda kumhasa Mheshimiwa Makamba ya kwamba ukitaka kitowe lazima umchinje kuku. Kwa hiyo, nakushauri maradhi ya kichwa ni maumivu ya mwili wote, kazi kwako. (*Makofi*)

Baada ya hayo naomba kumpongeza Mheshimiwa Dr. Ngasongwa pamoja na Mheshimiwa Zakia Meghji kwa kazi nzuri waliyofanya ya kuibua Bajeti ya Taifa ambayo ndiyo kipandio cha awamu ya nne katika kuondokana na maradhi, ujinga na matatizo mbalimbali ambayo yanaikabili nchi yetu. Vile vile napenda kuwatambua Wabunge wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa kazi nzuri waliyochangia hatimaye ikatokea hiyo Bajeti.

Mheshimiwa Spika, sisi sote tuko hapa kushiriki kuchangia ufanisi wa Serikali. Napongeza misingi mipana ya Serikali kwa juhudi mbalimbali ambazo zina lengo la kutupa nyenzo ya kurutubisha kuchochea ustawi na maendeleo na wananchi katika mikoa yetu, Wilaya zetu na majimbo yetu. Tanzania ni pana sana lakini mtu akiambiwa leo kwamba kuna maeneo ambapo wananchi wanachangia maji pamoja na mifugo hususan mtoto aliyeleleka katika miji na kukulia katika miji ataona jambo la ajabu sana.

Naiomba Serikali iandae juhudi kuititia Wizara zake za kutukwamua katika adha mbalimbali katika jimbo la Maswa hususan katika maeneo ya tatizo la maji, miundombinu. Vile vile napenda kuitaarifu Serikali kwamba jimbo la Maswa tuna miundombinu ambayo hivi sasa ni chakavu takriban miaka 45 toka ijengwe. Vituo vya afya vilijengwa wakati tunapata uhuru mwaka 1961. Vituo vya afya vilivyopo ni vile vilivyokuwepo wakati wananchi wa kiasi cha takriban laki moja na nusu kabla ya Wilaya Bariadi haijazaliwa na Wilaya ya Meatu haijazaliwa.

Lakini hivi sasa ukifika miundombinu hiyo imechakaa, mabomba yamechakaa, barabara vijijini sasa ni chache kwa sababu tulikuwa na vijiji vichache. Wigo wa vijiji kutoka kituo cha hospitali kimoja ni mbali sana. Hivi sasa tuna vijiji 104. Tuna shida tunasutwa na kwamba bado tuna mauaji ya wakongwe, tuna imani za kichawi lakini ukweli miundombinu ya kutupa ustaarabu wa kisasa bado hatuna.

Vijijini tuna matatizo, tuna maisha ya ujima. Ninaomba Serikali itupatie kipaumbele katika kututatulia matatizo. Vituo vya Afya Wizara ya Afya naiomba isaidie katuondolea dhahama tuliyonayo kwa sababu ukienda kituo cha afya hakuna darubini ya kupimia malaria, dawa hakuna, waganga shida tupu na wakati wa masika watoto wanapoteza maisha kwa sababu usafiri unakuwa wa mikokoteni ya ng'ombe.

Sasa naiomba Wizara ya Miundombinu itupatie upendeleo, Udugu ni kusaidiana. Naiomba Serikali itupie macho kwa kina kabisa kujua kwamba kule tuko nyuma. Ni aibu sana kusikika kwamba bado kuna mauaji ya imani za kichawi. Lakini hao ndugu zetu wanategemea sana wapiga ramli. Sasa haya kwa kweli si mambo mazuri lakini tufanye nini? Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa juhudi zake njema alizofanya hivi karibu za kuja katika Mkoa wa Shinyanga akaibua nguvu na umoja na mshikamano na hatimaye pakajengwa sekondari ambazo hivi sasa zinahitaji kukinaishwa kwa kapatika kwa walimu.(Makofi)

Mheshimiwa Spika, wahenga husema mbuzi hula kwa urefu wa kamba yake. Lakini ukweli pana jangwa nyemelezi huko kwetu. Tuna tatizo la maji ya mifugo. Tarehe 29 Januari ilikuwa ni aibu. Najisi aliingia katika lambo ambalo binadamu

huchangia na mifugo kunywa maji, aliingia mbwa. Lakini utafanya nini. Basi unasema *inshallah* Mwenyezi Mungu atakuepushe, unachota maji hayo, unachemsha, unapata maradhi, maradhi yenyewe kama tiba hakuna kwa sababu ya uduni wa elimu. Watu wanapoteza maisha yao, kesho wanakwenda kwa waganga wa jadi. Kwa hiyo, naomba Serikali ituunge mkono kupiga vita maisha ya ujima.(*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile, kutoa taarifa kwamba wafugaji wa Jimbo la Maswa wapo tayari kushirikiana na Serikali katika kuimarisha mazingira. Wafugaji wa Jimbo la Maswa wanaomba mbegu za nyasi ili waweze kwenda kulima kama wanavyolima pamba, wafugaji wanaomba maji kwa ajili wa mifugo, wafugaji wakishapata maji, wakipata mbegu za nyasi kwa malisho, kwa ajili ya mifugo napenda kukuhakikishieni kwamba watapunguza kuhamahama na hawatoonekana katika maeneo ya ajabu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ipate fursa ya kukaa na Wabunge wanaotoka katika maeneo ya wafugaji ili tuweze kujadiliana kwa kina na kusaidiana mawazo. Tusipende kuwatuhumu wafugaji wa ng'ombe kwamba ni wavamizi. Kwa kweli neno uvamamizi lina mtafaruku wa mshikamano, na ninasikitika neno mvamizi likishikwa na wanasiasia uchwara litaleta tafrani katika hali zetu za mshikamano. Kwa hiyo, naomba neno mbadala litafutwe ili kudhibiti kuwaita wafugaji ni wavamizi. Nasema hivyo kwa sababu Tanzania hivi sasa kila mmoja anaafuata na kusaka neema ya biashara anazunguka kutoka Mkoa hadi Mkoa na hivyo hivyo wafugaji ninaomba wafugaji tuwaonee huruma tusiwapachike maneno mazito ambayo si ya umoja na mshikamano wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudini njema za Mheshimiwa Waziri Mkuu kuja kuibua maswala ya elimu ya sekondari. Naomba kuleta kilio cha ombi la kupatiwa walimu wa shule ya msingi. Kwa sababu elimu ya msingi ndiyo msingi wa mavuno ya elimu ya juu ambayo inakuwa ni makini. Maswa peke yake tunamatatizo ya upungufu wa walimu katika shule zetu 106.

Mheshimiwa Spika naomba vilevile nichangie suala la ufanisi kwa Serikali, dhamira ya Serikali ni kuwa na ufanisi. Lakini wakati umekuwa ni mwema huu sasa tubadilishe kanuni na sheria ambazo ni vikwazo kwa watumishi. Sisi tuna Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya, tuna *Speed and Standards*, je watumishi wetu vile vikwazo ambavyo vilikuwa vya wakati ya kuhodhi madarakka, leo tuna fikra endelevu, tuna fikra mapinduzi, fikra chochozi.

Kwa hiyo, naomba kwamba wafanye sasa utafiti wa kujua kanuni ambazo zina rejesha *speed and standards* na zinarejesha Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya kwa watumishi. Kuwaongeza marupurupu si kuinua *standard* tunahitaji viwango vya utumishi viendane na kanuni mpya kwa sababu Agano la Kale haliongozi Agano Jipyä.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuchangia kwa upande wa bajeti kuipongeza Serikali kwa kufanikisha majengo, lakini Waheshimiwa Wabunge ni sawasawa na Hamila katika Majimbo yetu. Tunahitaji kusaidia uchangiaji wa ujenzi wa shule, vituo

vyo afya, ujenzi wa miskiti, yatima na kila aina ya watu wanakuja na shida zao; na kwa sababu Mbunge ndiyo hamila ndiye anayeombwa, ninaomba boresho la wajibu kwa Wabunge ili tuweze kuchangia maendeleo. Wananchi hawajui kama hatuna pesa za kuboresha maombi mbalimbali kuchochera ustawi wa jamii. Vilevile naomba Serikali ijaribu kutizama maslahi ya Mawakili na Mahakimu ili hawa nao wapate boresho la wajibu wasiwe na fikra ambazo kila wakati zinavishawishi kama tulivyoboresha wajibu wa TRA, ili na wao waweze kutulia kutoa haki kwa mstakabali wa haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kumalizia kwa kuwashukuru na kuwatambua Mawaziri mbalimbali ambao wameonyesha nia ya kulisaidia Jimbo langu la Maswa. Naomba kutambua shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, alivyofika Maswa na kuahidi kusaidia wananchi wa Lalago. Vilevile napenda kutambua ujio wa Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, Waziri wa Kilimo, Waziri Dr. Siyame aliyesughulikia maswala ya njaa. Naishukuru sana Serikali kwa kutujali. Nashukuru vilevile azma ya Mheshimiwa Mramba, Waziri wa Miundombinu, kwa kutatua matatizo ya vijijini vya Maswa, namshukuru vilevile Waziri wa Usalama wa Raia kwa jinsi anavyofuutilia matatizo ya Maswa. Namshukuru Mwanasheria Mkuu kwa kutambua dhuluma zinazofanyika kule na akachukua hatua za kukemea nashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia napenda kusema kwamba Maswa tunahitaji msako wa Ustawi na Maendeleo ya Jamii. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu upatapo fursa ujaribu kuja kule aidha uliona hali ya dhuluma iliyokuwa ikifanyika katika baadhi ya watendaji wa vyombo vya dola udhoofu wa *Sheikh* sio udhoofu wa Msaaful. Aidha udhoofu wa Askofu si udhoofu wa Biblia. Lakini tunapopakwa matope inakuwa inatupa mtihani wa kisasa. Ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu ujaribu kuhimiza kuhakikisha *IGP* sasa anakuja kukutana na wananchi ana kwa ana kama jeshi la wananchi linapendwa sana na wananchi tuwe na ibuo jipya la hivi sasa jeshi la wananchi kuwa na unganisho na fungamano la wananchi kwa ridhaa ya kwamba askari si mnada wa haki za wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema nashukuru sana na naunga mkono hoja ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nimepata malalamiko hapa kuwa: "Mheshimiwa Spika tunaomba viyoyozi virekebishwe, baridi imezidi humo ndani na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wakinamama wanatetemeka ila wanaogopa kusema." Sasa ni hivi viyoyozi humu ndani vimewekwa ili kukidhi hali ya Waheshimiwa Wabunge wakiwa wametimia 320 humu ndani. Tunapopungua basi sisi wachache tunaobaki humu inabidi tuibebi hiyo baridi ya wale wenzetu wa waliotoka. Sasa itakuwa vigumu sana Waheshimiwa Wabunge kwamba kila wakati mafundi wawe wanakwenda kurekebisha kulingana na idadi, maana baadaye tena watarejea utaonekana tena ni joto.

Kwa hiyo, kwanza mtu ujitzame kama sasa hivi unatetemeka pengine unahitaji kumwona Daktari, sio suala la baridi. Kwa hiyo tunaendelea anayefuata ni Mheshimiwa Laus Mhina, Korogwe Vijijini CCM. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. LAUS O. MHINA: Mheshimiwa Spika ahsante. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa hapa na kuipata nafasi hii adimu. Napenda nimpongeze Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa ushindi aliouputa katika uchaguzi wa Rais na pia ushindi wa kishindo tuliompa sisi wanaccm kwa kuchukua jukuma la kuwa Mwenyekiti wa Chama chetu cha Mapinduzi (CCM).(*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nitakosa fadhila bila ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri ambayo ameiandaa na kutuwezesha kutuongoza katika Bunge lako hili Tukufu. Napenda pia nikupongeze wewe mwenyewe na Naibu wako kwa kuchaguliwa kuwa Spika kwa ushindi wa kishindo, tuliokupa sisi. Pia napenda niwapongeze Wabunge wenzangu kwa kushinda na kuwapo hapa leo, nawapongezeni sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nikiingia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni hotuba ambayo kwa kweli imemfurahisha kila mwananchi. Hotuba hii inayosisitiza utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi wa Chama changu cha Mapinduzi. Isitoshe pia nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hoja ambayo imemsisitiza kila mtu, ni hotuba ambayo imezingatia kikamilifu mpango wa bajeti iliyowasilishwa hapa kwetu Bungeni.

Mheshimiwa Spika, hotuba ile imezingati dhana ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Si hayo tu imezingatia uwezeshaji wa Watanzania, ajira kwa vijana na pia vilevile maisha bora kwa kila Mtanzania. Kabla sijaanza mchango wangu ningependa kwa dhati kabisa niwashukuru wananchi wa Korogwe Vijijini kwa kuniwezesha leo hii kuwa hapa. Kwa kweli si wanaccm ni wananchi wote wa Korogwe Vijijini kwani kura nilizopata nilizipata pengine hata kwa wapinzani na wale ambao hawafungamani na chama chochote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ningependa nianzie na sekta ya kilimo. katika sekta ya kilimo nimejaribu kuigawa katika mafungu mawili. Kilimo cha mazao ya chakula na kilimo cha mazao ya biashara. Nikianzia na kilimo cha mazao ya chakula, sisi ambao tunatokea kwenye Majimbo ya vijijini tegemeo letu kubwa na kilimo. Kilimo ndicho ambacho tunachotegemea kabisa kwamba kitatuondolea umaskini upande wa vijijini. Kilimo ndiyo tegemeo letu ambalo linatupa ajira kwa upande wa vijijini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ili tukiwezeshe kilimo hiki kwa uhakikaka tunatakiwa tufanye baadhi ya mambo. La kwanza kabisa ni kuwatumbia vizuri wataalam wetu ambao tunao isitoshe wataalam tunawaomba wafike vijijini, wafike wapate kutoa elimu kwa wale wakulima sio maofisa wa kukaa maofisini tu. Pia ningependa kusisitiza kuanzisha benki za maendeleo. Kwa kweli huyo atakuwa mkombozi mkubwa kwa wakulima. Benki tulizonazo ni za biashara ni benki ambazo kwa kweli zinaendeshwa kibiashara hatakubali kutoa mkopo kwa kutegemea kupata hasara ua kupata faida ambayo hataikubali yeye; na ndiyo maana nasisitiza kwamba tunaiomba Serikali ituanzishie benki za maendeleo ambazo riba yake kwanza itakuwa ni nafuu. Halafu marejesho yake yatakuwa ya muda mrefu huyo atakuwa kwa kweli mkombozi kwa wakulima wadogo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, isitoshe pia kubwa ambalo limeongelewa hapa ni kilimo cha umwagiliaji nashukuru kwamba katika Jimbo langu la Korogwe Vijijini tunayo maeneo ambayo yanakidhi dhana hii ya kilimo cha umwagiliaji. Kinachotakiwa kwa kweli ni kujaribu kujenga skimu za umwagiliaji. Ninayo mabonde kwa mfano katika tarafa ya Mombo ambayo ni Mkomazi, Mazinde inakuja mpaka Mombo.

Hili ni bonde zuri kabisa kama tutaweza kulitumia kikamilifu nina imani tutazalisha chakula ambacho kinaweza kikatosheleza achilia mbali kwa Wilaya ya Korogwe kwa Mkoa mzima wa Tanga na pia hata kwenda nje ya Mkoa wa Tanga. Tunalo bonde la Binde jingine katika tarafa ya Magoma ambalo linaanza Mashewa linakuja hadi Magoma, Kerenge hadi kufikia sehemu inaitwa Mahenge. Ni bonde ambalo linarutuba halihitaji mbolea, linachohitaji ni kujengewa nyezo za kuweza kumwagilia ili wananchi wapate katika kipindi kizima cha mwaka mzima. Bonde hili linatumika kwa kilimo cha mahindi na kilimo cha mpunga. Kwa hiyo, nina hakika kabisa kama tutyalitumia kikamilifu Korogwe haiwezi ikawa na njaa hata siku moja.(*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niingie sasa kwenye kilimo cha mazao ya biashara. Bahati nzuri Korogwe Vijijini tunayo mazao ya biashara ya aina mbalimbali. Tunazo korosho, pamba, chai, kahawa na tuna mkonge. Ningependa leo niongelee kuhusu zao la mkonge tu. Awali zao hili la mkonge wengi walikuwa wanalichukulia kwamba ni zao la wakulima mabepari, wakulima wakubwa, wakulima wenye nyenzo za hali ya juu. Lakini ninamshukuru Mungu kwamba dhana hii kwa sisi wananchi wa Korogwe tumeiondoa. Zao la mkonge siku hizi kwa Wilaya ya Korogwe hususan katika Jimbo la Korogwe Vijijini, zao hili linalimwa na wakulima wadogo. Zao la mkonge limefikia mahali sasa hata mtu katika shamba lake binafsi analima hata kama ni ekari moja.

Mheshimiwa Spika, zao hili kwa bahati nzuri halihitaji mvua. Ni zao ambalo linastahimili ukame. Isitoshe pia ni zao ambalo unaweza ukachanganya na mazao mengine, unaweza ukapanda mahindi katika miraba ile, unaweza ukapanda maharage, unaweza ukapanda kunde au kitu chochote kila katika kipindi cha mwanzo. Isitoshe pia zao hili ni zao ambalo kwa kweli linaweza likautoa umaskini wa watu wa vijijini.

Kwa mtu wa kijiji anapolima hekta moja ya mkonge inamwezesha kupata wastani wa shilingi 100,000/- kwa kila mwezi wakati atakapoanza uvunaji wa majani. Kwa mkulima wa kijiji kuwa na kipato cha shilingi 100,000/- kwa kila mwezi ni kipato kizuri sana. Maana yake kwanza atakuwa na uhakika wa kupanda chakula kwenye miraba ile na bado anakipato cha shilingi 100,000/- kwa kila mwezi. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali iweke mkazo kwenye hili zao la mkonge iwawezeshe wakulima hawa wa mkonge walime katika njia ya utaalam zaidi na ya ufasaha zaidi ili mazao yao yapate kutoa uzalishaji bora.(*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, isitoshe pia zao la mkonge ni zao ambalo limeongeza sana ajira katika Wilaya ya Korogwe. Hivi sasa kuna wananchi karibu laki moja ambao wameajiriwa katika mashamba ya mbalimbali ya mkonge. Hii ni ajira nzuri sana kuweza kuwaajiri watu zaidi ya laki moja, kwa kweli ninashukuru sana kwa hilo

Mheshimiwa Spika, zao la mkonge halimkomboi mwananchi wa Korogwe peke yake. Zao la mkonge hivi sasa ni zao ambalo linatakiwa karibu dunia nzima. Zao la mkonge linaweza likaliongezea taifa letu fedha nyingi za kigeni. Katika mkonge tunapata karibu kila kitu. Kwenye mkonge tunapata mazao mbalimbali, tunapata kamba, mifuko, mazulia, gesi, mbolea na mkonge tunapata hata umeme.

Nadhani wengi watakuwa mashahidi kwamba kuna mradi ambao uko sehemu moja inaitwa Hale wa kuzalisha umeme. Mradi ule unaweza ukatoa kiasi hata cha *Megawatts* mbili. *Megawatts* mbili za umeme kwa kweli ni kiasi ambacho kinaweza kikatosheleza kabisa mahitaji ya wakazi wa sehemu yote ile ya Hale na pia bado ukauzwa kwa *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, ninachojaribu kuomba ni kwamba, Serikali ijaribu kuwaunga mkono wakulima hawa wadogo kwa kuwapatia mikopo midogo midogo. Mikopo hiyo itapatikananaje?

Mikopo hiyo inaweza ikapatikana tu kama Serikali itapima ardhi na kutoa hati katika mashamba ya wakulima wadogo.

Mheshimiwa Spika, naomba niingie kwenye sekta ya miundombinu. Tunapoongea uchumi, tunapoongea kumuondolea umaskini mwananchi hasa sisi wa vijijini ni kumboreshea njia zake. Kwa sababu haina maana mkulima anapolima halafu akakosa barabara ya kupeleka mazao yake sokoni siku zote inamaana atategemea mlanguzi aje ampangie yeye bei. Kwa sababu yeye atakuwa hana uwezo wa kupeleka mazao yake sokoni, itakuwa kwa kweli hatujaongeza tija kwa mkulima hapa badala yake tunaendelea kumuumiza tu. Isitoshe ninaomba Serikali yetu ijaribu kuwafikiria wakulima kwa kuwapatia pembejeo mbalimbali, kuwapatia tena mikopo nafuu, mikopo ambayo marejesho yake ni ya muda mrefu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo awali, tusizitegemee benki za biashara ni vizuri tuanzishe benki za maendeleo ambazo kwa kweli nina hakika kabisa ndizo zitakuwa mkombozi wa mkulima huyu mdogo ninayemzungumzia. Katika Jimbo langu tuna barabara ambazo zinahudumiwa na Halmashauri zipatazo karibu kilomita 600. Kidogo imenisikitisha kuona katika Bajeti ya mwaka jana Jimbo langu limepangiwa shilingi 130 milioni tu. Ukichukulia shilingi 130 milioni kwa kilomita 600 kwa kweli hiki ni kisi kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofî*)

MHE. RAMADHANI A. MANENO: Mheshimiwa Spika kwanza nishukuru kwa kupata nafasi na kuwa kitinda mimba katika kuchangia hoja ya hotuba ya Waziri Mkuu. Lakini nishukuru kuwa wa mwisho katika kuchangia hoja kwangu mimi ni faraja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na wananchi wa Jimbo la Chalinze kwa kunichagua kwa kura nyingi sana ili niweze kuwa Mbunge wa Jimbo la Chalinze.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chalinze, tunampongeza mpigakura mwenzatu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kushika nafasi ya Uwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi taifa. Lakini wananchi wa Jimbo la Chalinze pia wanawapongeza wale wote waliopata uteulizi kushika nafasi mbalimbali katika Chama cha Mapinduzi. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri katika ofisi yake kwa kuandaa hoja nzito, yenye mafanikio, yenye matarajio kwa mwananchi 2006/2007. Nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala pamoja na wajumbe wa Kamati hiyo nikiwemo mimi mwenyewe kwa ushirikiano mkubwa na Ofisi ya Waziri Mkuu tulipoijadili hoja hii ya Matumizi na Makadirio ya ofisi yake kwa kipindi cha mwaka 2006/2007 na sisi tulimwambia Mheshimiwa Mizengo Pinda kwamba hii hoja itapita bila matatizo na kweli Wabunge wamechangia kwa nguvu na ari mpya. Nimshukuru sana Mwenyekiti wangu Mheshimiwa George Lubeleje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la kilimo. Kwa kweli tunapohitaji kilimo cha kisasa kutoka kwenye kilimo ambacho tunacho sasa hivi. Basi watalaan wetu nao wapelekwe mashulenii ama wapelekwe vyuoni kwenda kupata elimu ya kutosha kwa ajili ya kilimo cha kisasa. Lakini ikiwa watalaan wetu ni walewale huku tunasisitiza kilimo cha kisasa itakuwa ni kazi bure siku hadi siku. Naomba nizungumzie suala la vituo vya afya. Vituo vya afya vingi hususan vilivypopo Jimboni kwangu kama pale Lugoba na Chalinze. Wakati vinajengwa vilikuwa vinabeba mzigo wa vijiji vitatu hadi vinne. Lakini sasa vinabeba mzigo takriban vijiji kumi au zaidi ya kumi. Wananchi wameshakuwa wengi, lakini huduma ya dawa pale, dawa zinafunguliwa tarehe moja ikifika tarehe kuni dawa zimekwisha. Vituo hivyo vya afya vinasaidia hata kata za jirani kwa maana ya Majimbo ya jirani kama kwa ndugu yangu Mheshimiwa Abdallah Kigoda. Kwa hiyo, jitihada za msingi zielekezwe katika kuongeza ufanisi wa dawa kwenye vituo vyetu vya afya. Lakini pia uhaba au uchache wa watumishi kwenye mashule na kwenye vituo vya afya nalo pia litiliwe mkazo. Nije kwenye suala la utalii, kwenye Jimbo langu kuna mbuga ya hifadhi kule ya Saadan, ni mbuga nzuri sana ina vivutio vizuri sana. Ni mbuga ambayo ipo kandokando ya bahari kwa Afrika Mashariki na Kati hakuna mbunga nyingine yoyote kuwa kandokando ya bahari. Lakini mbuga ambayo inasamaki wa aina ya kasa wa ajabu sana wanatagia nchi kavu. Tena ningeomba Kamati ya Maliasili na Mazingira kama itapata nafasi itembelee mbuga ile hatimaye wanisaidie kuitangaza na kuongeza pato la taifa na wananchi wa Jimbo langu kwa maana ya ajira. (*Makofi*)

Nizungumzie suala la watumishi nao kukaa muda mrefu kwenye vituo. Utakuta watumishi wanakaa muda mrefu, miaka kumi, kumi na tano, hatimaye wanakuwa hafanyi kazi ipasavyo. Anakuwa hana kasi hana ari wala hana nguvu kilichobaki pale ni yeze tu kuamua nini cha kufanya lakini haelewi kwamba yeze yupo pale kwa ajili ya kuwatumikia wananchi. Hilo litazamwe, vinginevyo kasi hiyo itawashinda. Lakini lingine ni kuhusu watendaji wetu wa vijiji na kata. Ningemwomba Waziri wa TAMISEMI

ashauriane na wakurugenzi kuona jinsi gani sasa kwa watendaji wetu wa kata na vijiji either kuwabadilisha vituo au wale ambao tunawaona hawaendani na kasi hii basi watupishe. Kwani yapo maeneo baadhi ya watendaji ni kero mno kwa wananchi. Wananchi wanahitaji maendeleo wanachohitaji ni kushirikishwa wakishashirikishwa wao hawana matatizo.

Lakini watendaji walio wengi hawawashirikishi wananchi wao wanajiamulia kivyao kwa kuona kwamba wameshika mpini. Lakini pale Mbunge anapoitwa na wananchi hao kutaka kusikilizwa shida zao, wanamhitaji Mbunge wao kwani Mbunge katika majukumu yake makubwa pia ni kusikiliza kero za wananchi. Mbunge unapokwenda kuwasikiliza wale wananchi kujua tatizo ni nini. Hapa tunatatizo na watendaji wetu. Unapotaka kuweka suluhu juu ya jambo hilo basi umeanzisha kero na vurugu kubwa kati yako wewe Mbunge na watendaji kuona kwamba unawapendelea wananchi. Lakini wananchi ndiyo walionichagua nitafanyaje. Kwa hiyo, hilo nalo litiliwe msisitizo sana kwa wakurugenzi wetu wawaonye baadhi ya watendaji wetu jinsi ya utendaji wao wa kazi. Kwani wengine wanafikia hatua hata ya kukuwekea vikao kukujadili Mbunge kwanini umekuja pale kuwasikiliza wananchi. Hilo nalo litiliwe mkazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la ujenzi wa mashule. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kweli tunampongeza sana. Hasa pale alipoagiza ujenzi wa shule wa shule kwa maana kupunguza idadi kubwa ya wanafunzi iliyokuwa imejitokeza ya wanafunzi waliokosa nafasi. Kwa kweli wananchi wamejitleea Serikali imejitolea kuitia Waziri Mkuu kuitia Wizara ya Elimu. Tunampongeza sana Mheshimiwa Mwantumu Bakari Mahiza kwa jitihada zake za ufuatiliaji wake wa kina kuhakikisha shule zinajengwa na kweli shule nyingi zimejengwa. Lakini pia kwenye suala hili la usambazaji wa chakula. Ofisi ya Waziri Mkuu ilifanyakazi ya ziada kwelikweli kuhakikisha chakula cha msaada kinawafikia wananchi. Pongezi sana Waziri Mkuu niwapongeze na Mawaziri waliochini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi nzuri sana. (*Makofi*)

Pia nzungumzie suala la Madiwani wetu ni nguvu kazi, Madiwani wetu tunawategemea na hawa nao wafikiriwe hata kukopeshwa pikipiki ili mradi ziwasaidie kwenye ufanisi wao wa kila siku kwenye Kata. Kwani, kuna Kata tatu za Jimbo langu, ukubwa wa Kata moja, hata Jimbo la Kibaha ni dogo. Fikiria Diwani huyo atafanyeje ufanisi huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini, pia magari ya Ma-DC yamechoka. Yana nguvu, kasi hayana. Yalijitahidi sana kushughulika na jambo kubwa la uchaguzi. Magari yameishachoka, hivi sasa na wao wapatiwe magari ili waendane na kasi mpya hii tunayokwenda nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu la Chalinze, nasema nalo ni kubwa. Basi pale itakapobidi, Serikali iangalie kwa jicho la huruma pale itakapoona sasa kuna mgawo wa Wilaya, basi Jimbo langu nalo si vibaya likatizamwa kwa jicho la huruma lipate Wilaya. Kama suala la kuona ni jinsi gani vigezo vya Jimbo la Chalinze kuwa Wilaya, nina imani vigezo vingine vilishakamilika. Lakini kama ni idadi ya watu, basi nitaenda kukaa na

wananchi wangu wale nione jinsi gani kuongeza idadi ya watu ili iweze kuwa Wilaya. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, nimalizie suala la kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu kwa jinsi tunavyoshirikiana nao na nawaomba sana wanizidishie kunipa ushirikiano ili niweze kuwatumikia na nawahakikishia sitowaangusha, Mbunge sasa wamepata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja ya hotuba ya Waziri Mkuu kwa zaidi ya asilimia 100. Ahsante sana. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. RICHARD S. NYAULAWA: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri Mkuu kwa matayarisho makini na hotuba nzuri aliyoitao Bungeni. Hotuba hii imeainishwa barabara na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ambayo ni maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Serikali kutenga fedha za kutosha kwa programu mbalimbali kwa ajili ya kuleta maendeleo na kuinua maisha ya wananchi wanaoishi vijijini. Ili kuleta mageuzi ya kilimo ni lazima kuendesha viwanda vidogo, vya kati na vikubwa kwa kuwashirikisha wananchi wenyewe kumiliki viwanda hivyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nawasilisha.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ninawapongeza Waziri Mkuu na Waziri wa Nchi, TAMISEMI, kwa kazi nzito wanazofanya, wanadhihirisha umahiri na umakini.

Mheshimiwa Spika, naomba mambo yafuatayo: -

(i) Suala la kupata hadhi ya Mji Mdogo wa Nzega ili iwe Halmashauri ya Mji wa Nzega lipewe uzito unaostahili na hasa katika bajeti.

(ii) Halmashauri mfano ya Nzega kupewa adhabu ya kunyimwa fedha za maendeleo kwa ajili ya hati chafu, kosa ni la watendaji siyo la wananchi, hivyo fedha zilipwe na waliosababisha hati chafu waadhibiwe.

(iii) Napongeza hatua za kulazimisha wachimbaji wa madini (dhahabu) kulipa Halmashauri kodi. Mkazo uongezwe kwa makampuni wabishi, mfano *Resolute* ya Nzega kuchelewa kuilipa Halmashauri.

(iv) Mradi wa maji toka Ziwa Victoria, Awamu ya Pili uzingatie katika tatizo la maji Wilaya ya Nzega (mkazo uelekezwe vijijini).

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, hapo ndio mwisho wa uchangiaji kutoka kwenye *floor*. Sasa watakaozungumza ili kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kutoka hii Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kwa mpangilio ufuatao, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, atazungumza kwa nusu saa yaani dakika 30. Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Celina Kombani, atazungumza kwa dakika 15. Hii, sikupanga mimi, hivi ndivyo walivyojipanga. Natangaza tu ili Wabunge waelewewe na wasishangae pale inapokuwa kuna tofauti. Ni namna wlivyopanga kulingana na uzito wa hoja zilivyokwenda katika eneo mhusika, Naibu analisimamia au Waziri wa Nchi analisimamia. Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Juma Akukweti atafuatia, ataongea kwa dakika 30 na hatimaye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mheshimiwa Mizengo Pinda, ataongea kwa dakika 45. Hapo tutakuwa tumefika saa 7.00. Sasa namwita Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. LUKA J. SIYAME): Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nichukue fursa hii nami niungane na wenzangu ambao wamekwisha kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Pia, napenda nichukue fursa hii kuwapongeza wale wote ambao wameteuliwa na kuchaguliwa kwa nafasi mbali mbali za Chama chetu cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitakuwa ni mdogo wa fadhila kama wakati huu sitachukua fursa hii kuweza kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye kwa miezi hii sita niliyofanya kazi katika Ofisi yake nimejifunza mengi kwake, nimepata ujasiri kutoka kwake na ninaamini nitajitahidi kwa uwezo wangu ili niweze kulitumikia hili Taifa vilivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja zilizotolewa na ambazo inabidi nianze kuzijadili, ziko katika makundi matano, hoja ya kwanza ni kuhusu chakula cha njaa, hoja ya pili ni dawa za kulevyo, hoja ya tatu ni Tume ya UKIMWI na UKIMWI wenyewe, hoja ya nne inahusu walemavu na hoja ya tano Programu ya Uendelezaji wa Mfumo wa Masoko ya Mazao ya Kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuanza, Mheshimiwa John Malecela Mbunge wa Mtera alitaka Serikali iongeze akiba ya chakula, *SGR*, kwani kiwango cha sasa cha tani 150,000 kimepitwa na wakati kufuatana na ongezeko la idadi ya watu. Serikali ingependa kumjibu kwamba kama ilivyokwisha kutamkwa kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, Serikali itaimarisha Hifadhi ya Chakula cha Taifa ili kuwezesha kuwepo kwa chakula cha kutosha kwa angalau miezi mitatu wakati wa njaa. Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika itaandaa utaratibu wa kutekeleza maelekezo hayo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa alitoa taarifa kwamba Wilaya ya Kongwa bado inakabiliwa na njaa na inahitaji chakula cha msaada na mbegu za mtama kwa ajili ya kuijandaa kwa kilimo cha msimu ujao. Hoja hii ilifanana na

hoja ya Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mbunge wa Singida Kusini na pia Mheshimiwa Felister Bura, Mbunge wa Viti Maalum.

Jibu la Serikali ni kwamba tunakubaliana kwamba bado kuna maeneo nchini ambayo hali yake ya chakula siyo nzuri. Serikali inafanya tathmini ya hali ya chakula ilivyo sasa na hatua zitachukuliwa. Kwa Mikoa ambayo kutakuwa na mavuno mazuri ya chakula, viongozi wahimize utaratibu mzuri wa kila kaya kujiwekea chakula cha kutosha kama hifadhi. Tuchukue fursa hii kuwakumbusaha viongozi kuwahimiza wananchi kupanda mazao ambayo yanaendana na hali ya eneo husika. Pia, Mheshimiwa Felister Bura, alitaka *SGR* isibague mazao ya kununua hasa kwenye maeneo ambayo Mtama na Uwele unalimwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sera ya Serikali na utaratibu ni kwamba sisi tunanunua nafaka zote bila ubaguzi, ila mwaka 2005/2006 Serikali ilipanga kununua tani 10,000 za Mtama lakini haukupatikana. Hivyo wananchi wanahimizwa kulima Mtama na Serikali itanunua. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, naye aliuliza swalî linalofanana na lile la Mheshimiwa Job Ndugai, alitaka Serikali iendelee kuzipa chakula Tarafa za Kwamtoro na Farkwa kwani zina njaa. Jibu ni lile lile kwamba Serikali itafanya tathmini na hatua zitachukuliwa kama hali hiyo ndivyo ilivyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mbunge wa Kilombero, alitaka Serikali iuwezeshe Mkoa wa Morogoro kuzalisha chakula cha kutosha kwa Tanzania nzima. Kwa hakika Serikali itaendelea kutoa utaalâm, pembejeo, kutafuta masoko na uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji na barabara ili kuendeleza kilimo. Aidha, viongozi wote wanatakiwa kuhamasisha wananchi kwenye maeneo yao katika uzalishaji wa chakula. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mbunge wa Temeke, alitaka Serikali iupatie Mkoa wa Dar es Salaam, msaada wa chakula cha njaa kama ilivyo katika Mikoa mingine. Ningependa kumjibu Mheshimiwa Abbas Mtemvu, kwamba kiutaratibu chakula cha njaa hutolewa kwa wananchi ambaao shughuli zao za kilimo zimeathiriwa na janga kama ukame na mafuriko na vile vile mwananchi huyu anakuwa hana mbînu nyingine ya kupata chakula. Kwa kawaida, wananchi wengi wa Dar es Salaam si wakulima, hivyo hawawezi kuhusika katika utaratibu wa kupatiwa chakula cha njaa na utaratibu huu unaihusu pia miji mingine yote nchini, si Dar es Salaam peke yake.

Mheshimiwa Spika, fungu la pili la hoja zangu kama nilivyokwisha kusema ni kuhusu dawa za kulevyâ. Katika kundi hili nina hoja tano, kwanza kabisa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ilitaka Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevyâ iwafuatilie walioathirika na dawa hizo na iendelete mikakati ya kupambana na janga hilo. Jibu letu ni kwamba Tume imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali katika kudhibiti dawa za kulevyâ. Hata hivyo Tume inakusudia kuboresha ushirikiano na wadau hao katika

kuweka utaratibu wa kufuabilia walioathirika na kupambana na janga hili kwa nguvu zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, alitaka Serikali ifanye juhudhi za kusaka wanaojihusisha na madawa ya kulevyaa na iandae mkakati wa kusaidia waathirika.

Ningependa kwanza kuelezea hoja hii katika makundi mawili, kwanza, ni kuzagaa kwa dawa za kulevyaa. Serikali imekuwa ikifanya jitihada za kupambana na tatizo la biashara ya dawa za kulevyaa kwa kuwakamata wahusika. Kwa mfano, mwaka jana watuhumiwa 4,532 walikamatwa na kesi 3,368 zilifunguliwa Mahakamani. Tatizo hili linahitaji ushirikiano wa wananchi kutoa taarifa kwa vyombo vinavyohusika kuwafichua wahusika.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ni kuhusu tiba ya waathirika wa dawa za kulevyaa. Ningependa kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba waathirika wa dawa za kulevyaa wanaojitokeza wanapata tiba katika hospitali mbalimbali. Hata hivyo kuna tatizo la wazazi na ndugu wa waathirika kutokuwapeleka waathirika hospitalini kupata tiba. Wazazi ama walezi wanahimizwa kuwapeleka waathirika hospitalini. Aidha, Serikali itaangalia upya sheria inayohusika, ili suala la tiba kwa waathirika isiwe hiari kama ilivyo sasa. Serikali imeandaa rasimu ya mwongozo kwa waathirika ambaa utasambazwa katika hospitali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mbunge wa Viti Maalum alitaka Serikali iweke mkakati utakaodhibiti kilimo cha bangi. Mheshimiwa Spika na Bunge lako Tukufu, Serikali imeweka mkakati wa kutokomeza kilimo cha bangi kuititia mpango kabambe wa Taifa wa kudhubiti dawa za kulevyaa unaojumuisha mikakati ifuatayo, kwanza, kutilia mkazo kilimo cha mazao mbadala yatakayowaingizia kipato wakulima. Pili, kuendesha operesheni maalum, kugundua, kukamata na kuteketeza bangi popote inapolimwa nchini na tatu, kuelimisha wakulima madhara yatokanayo na kilimo cha bangi pamoja na athari za utumiaji wake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mbunge wa Fuoni, alitaka Serikali iweke mkakati wa kuvunja mtandao haramu wa madawa ya kulevyaa zinazohatarisha maisha ya vijana. Kama nilivyokisha kueleza, Serikali itaendelea kufanya operesheni maalum kupambana na wote wanaojihusisha na dawa za kulevyaa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, katika fungu hili, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mbunge wa Fuoni alitaka vyombo vyaya dola vinavyoshughulikia madawa ya kulevyaa vitekeleze majukumu yao ipasavyo. Ningependa kumhakikishia kwamba vyombo vyaya dola kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wanafanya hiyo kazi vizuri sana kama ipasavyo, kama nilivyokwisha kueleza kwenye taarifa kuhusu waliokamatwa na wale waliopelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, fungu la tatu katika hoja ninazojadili sasa hivi ni kuhusu Tume ya Kudhibiti Ukimwi na Huduma za Ukimwi. Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilitaka Tume ya Kudhibiti Ukimwi iendelee kupanua shughuli zake zaidi ili

ziwafikie wananchi wengi vijijini na iweke mikakati ya kufikia wananchi walioathirika na Virusi vya Ukimwi pamoja na yatima.

Mheshimiwa Spika, ningependa kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba Tume ya kudhibiti UKIMWI ina utaratibu wa kufikia jamii kwa kutumia wakala wao ambao wameingia mkatuba wa kuzijengea uwezo Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Wakala hawa ndiyo wanaosaidia wanaoishi na virusi vya UKIMWI pamoja na yatima. Wakala hawa wanapatikana kwa mchakato wa uwazi kwa kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Serikali ya mwaka 2004 na kwa kushirikisha Halmashauri na wadau wengine. Pamoja na hilo, Tume itaendelea kuboresha na kupanua shughuli zake kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati na wadau mbali mbali. Katika uboreshaji huo, Halmashauri na Asasi zinazohusika, wanashauriwa kutoa ushirikiano wa dharti katika kuwatambua na kuwafikishia misaada walengwa wa virusi vya UKIMWI na yatima. Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala pia ilitaka Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania ishirikiane na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Zanzibar kupambana na janga la UKIMWI kila inapowezekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba Tume zote mbili za Tanzania Bara na Zanzibar zimekuwa zikishirikiana katika masuala mbalimbali ya kudhibiti UKIMWI. Hata hivyo, ushauri wa kuimarisha ushirikiano, umezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, wakati akiongea kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, alitaka Serikali iangalie upya mfumo mzima wa uendeshaji wa shuguli ndani ya *TACAIDS*, utumiaji wa mawakala kushughulikia suala la UKIMWI nao uangaliwe upya. Ni kweli Serikali inatumia mpango wa mawakala ili kuongeza nguvu za Kamati za Halmashauri na asasi zisizo za Kiserikali. Wakala hawa wamepangiwa kufanya kazi katika Halmashauri zote nchini. Tunawaomba Waheshimiwa Wabunge washirikiane na Halmashauri pamoja na wakala ili kuongeza nguvu katika kupambana na UKIMWI nchini. Hata hivyo, kasoro zinazojitokeza katika utaratibu huo, zinafuatiliwa na kushughulikiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum alitaka wananchi wahamasishwe juu ya kujikinga na UKIMWI ili wachukue tahadhari. Aidha, Serikali isadie kuwapatia dawa za kupunguza makali ya UKIMWI waathirika. Ningependa kumjibu Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah kama ifuatavyo: Serikali imekuwa ikielimisha wananchi kwa kutumia njia mbalimbali za utoaji elimu ya kujikinga UKIMWI kwa kutumia vyombo vya habari, vijarida, elimu kwa njia ya semina, warsha na nyenzo mbalimbali. Serikali ilianzisha mpango wa tiba ya bure kwa waathirika tangi mwaka 2004. Sasa hivi, waathirika 27,000 wanapata dawa hizo bure.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi watakuwa wanafadhaika kwamba mbona tunaambiwa kuna waathirika 2,500,000. Taratibu za utoaji tiba zina kanuni maalum kwamba mwathirika wa UKIMWI awe ametimiza vigezo kadhaa ikiwa ni pamoja na kuwa na *CD4* chini ya 200. Aidha, Serikali itaendelea kuongeza juhudzi za kuwahudumia wale ambao watapimwa na kuonekana wameathirika na kuwa na *CD4* chini ya kiwango hicho.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mbunge wa Viti Maalum, naye pia alitaka mashirika yasiyokuwa ya Serikali (*NGOs*) yanayojinufaisha na fedha za kampeni dhidi ya UKIMWI yaangaliwe na kuchukuliwa hatua. Ningependa kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba *NGOs* zinazoshughulika na Kampeni dhidi ya UKIMWI zinatakiwa kutumia fedha zilizotolewa kwa manufaa ya wananchi. *NGOs* zinapata fedha kwa njia mbali mbali. Kuna zile zinazopata fedha moja kwa moja kutoka kwa wafadhili na zile ambazo fedha zake zinapatikana kutoka Serikalini.

Hata hivyo, mamlaka za Serikali za Mitaa zinawajibu wa kujua bajeti ya *NGOs* zilizo katika maeneo yao pamoja na kufuutilia utekelezaji wa shughuli zote za kupambana na UKIMWI katika maeneo husika. Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuchukua hatua endapo inaonekana *NGOs* hizo hazitekelezi mipango kama ilivyopangwa. Katika hili, samahani naomba hapa nipitilize kwa sababu Mheshimiwa aliyekuwa ametayarisha suala hilo lilikuwa linafanana na yale ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum alitaka semina kwa ajili ya kampeni dhidi ya UKIMWI zipunguzwe na badala yake huduma za dawa na lishe zitolewe hasa vijijiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, napenda kurudia tena kwamba semina kuhusu vita dhidi ya UKIMWI, hutolewa kwa kuangalia masuala mapya yanayojitokeza kama vile mahitaji ya dawa za kupunguza makali ya UKIMWI, ongezeko la maambukizi kwa makundi mbalimbali katika jamii na suala la lishe. Kwa jumla ningependa kusema kwamba semina zitafanyika pale zinapohitajika ili kuweza kupata taarifa mpya, kuweza kupata maendeleo katika uvumbuzi wa kinga na baadae tiba ya UKIMWI. Hivyo basi ushauri wa kupunguza semina, utazingatia uwiano kati ya mahitaji ya elimu na upelekaji huduma kwa walengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mbunge wa Makete alitaka Serikali iande mkakati wa kutoa elimu ya kupambana na UKIMWI kwa wakazi wa Wilaya ya Makete, kwani sababu za kueneo kwa UKIMWI Makete ni pamoja na ujinga na umaskini.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imeunda Kamati za kudhibiti UKIMWI katika mamlaka ya Serikali za Mitaa nchini ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Makete. Kamati hizi huandaa na kusimamia utekelezaji wa mipango ya kudhibiti UKIMWI. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, tayari imeandaa mpango wa kutoa elimu ya UKIMWI katika shule zote nchini. Elimu hii ikitolewa shulenii, itaifikia jamii kwa haraka na kwa upana mkubwa. Serikali inatambua tatizo la UKIMWI Wilaya ya Makete na itaendelea kushauriana na viongozi wa Makete wakiwemo Waheshimiwa Wabunge ili kutatua tatizo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, alitaka Serikali isisitize zaidi katika malezi ya vijana kama njia mbadala ya kupambana na UKIWMI badala ya kusositiza matumizi ya kondomu kama kinga. Suala hili

lilichangiwa pia na Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka. Ushauri umekubaliwa na utazingatiwa kwani hatua zote ni muhimu na zinasaidia katika kupunguza ongezeko la UKIMWI nchini. (*Makofi*)

Hoja inayofuatia ambayo ni moja tu, ilitolewa na Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge wa Viti Maluum aliyetaka Serikali iandae mkakati wa kuwasaidia walemaru badala ya kuacha jukumu hilo kwa watu binafsi. Kama ilivyo katika hotuba ya Waziri Mkuu, Serikali ina Sera ya Taifa ya Watu wenye Ulemavu na itaendelea kuitekeleza ili wapate fursa za kiuchumi, kisiasa, ajira, elimu, afya na mikopo kama watu wengine katika jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya mwisho ni kuhusu mawakala wa programu ya uendelezaji wa Mfuko wa Masoko ya Mazao ya Kilimo (*AMSDP*). Hii ilitoka kwa Mheshimiwa Devota Likokola, Mbunge Viti Maalum. Yeye alitaka mawakala wa programu hii wawajibike kwenye Halmashauri za Mikoa ili wananchi waelewe vizuri mradi huo. Ili kuipa Wilaya husika mamlaka ya usimamizi wa utakelezaji wa programu ya *AMSDP*, kamati ya ushauri imeundwa na Wilaya. Kamati hii inayojulikana kama *Folk Area Advisory Group*, ndiyo yenye mamlaka ya kushauri, kusimamia na kukubali mipango yote ya wakala mwezeshaji. Kamati hii ndiyo inayopitia malipo, mpangokazi na bajeti ya wakala mwezeshaji. Kazi ya programu hii ni kulipa kile kinachokubaliwa na kamati hii na kutoa ushauri wa kitaalam ikibidi. Ushirikiano huu uko ndani ya mkataba maalum ambao unaainisha wajibu wa kila mdau kati ya Halmashauri ya Wilaya, wakala maalum ambao unaainisha wajibu wa kila mdau. Waheshimiwa Wabunge wanaweza kuuona mkataba huu kwa Mkurugenzi Mtendaji wa kila Wilaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongea haya naomba nitoe shukrani zangu maalum kwa wananchi wangu wa Wilaya ya Mbozi hususan wale wa Wilaya ya Mbozi Magharibi ambao waliniwezesha kufika katika Bunge hili Tukufu na baadae kuweza kuteuliwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu. Hivyo basi naomba shukrani zangu ziwafikie kwa dhati. Nitaendelea kulitumikia Taifa hili kama ambavyo nitaendelea kuwatumikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote kama ilivyo ada, kwanza naomba kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingui na wananchi wa Tanzania. Wakati huo huo namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri.

Tatizo la mitaji ya kuanzisha viwanda litaendelea kuwepo na kutegemea wawekezaji kutoka nje ingawa kuna fedha nyingi nchini ambazo ziko mikononi mwa wananchi. Kuendelea kukua kwa uchumi (*GDP*) wa Taifa ina maana kuwa uwezo wa wananchi unaongezeka.

Mheshimiwa Spika, uwezo huu wa kifedha wa wananchi imedhihirishwa na *NICO* kukusanya takriban shilingi bilioni 16 na *Unit Trust Fund* iliweza kukusanya karibu shilingi bilioni 95 mwaka 2004 kwa ajili ya kuwekeza katika viwanda au makampuni mbalimbali. Fedha zilizokusanywa na zingeweza kujenga viwanda vitatu au vinne vyat kati vinavyomilikiwa na wananchi.

Ufumbuzi wa tatizo la mitaji ni kwa Serikali kuunda *Promotional Team* ya Serikali na wafanyabiashara kama *NICO* na *UTF* itakayofanya kazi ya kuhamasisha ukusanyaji wa fedha kutoka kwa wananchi ambazo zinaweza kuwekezwa kwenye:-

(a) Viwanda mbalimbali kama mbolea, kusindika mazao ya kilimo, maziwa, kusaga nafaka, viwanda vyat kuhudumia migodi na kadhalika.

(b) Migodi ya kati na mikubwa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kufanya hivi Serikali itakuwa inawashirikisha au inawahamasisha wananchi kumiliki viwanda. Viwanda hivi vitakuwa ni soko kwa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuijali elimu kwa kuwa na msingi wa maendeleo na kiasi cha zaidi ya shilingi bilioni 891 kwa ajili ya maendeleo ya elimu.

Pamoja na mpango wa vijana 3,500 waliomaliza kidato cha sita kupatiwa mafunzo ya mwezi mmoja ili wakihitimu wafundishe shule za sekondari ambako kuna uhaba mkubwa wa walimu. Kwa kuwa mafunzo hayo ni mafupi na hayatatosheleza, nashauri kuwa Serikali iwe na programu maalum ya kuwaendeleza kielimu ili waweze kujenga uwezo wao wakiwa kazini.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wa Dar es Salaam wanapata matatizo makubwa sana ya usafiri. Nashauri shirika la UDA lingemarishwa ili pamoja na majukumu mengine lingepewa jukumu la kuwahudumia wanafunzi kwa ushirika wa Serikali na wazazi. Wazazi watashiriki kwa kulipa nauli itakayopangwa na Serikali wakati wanafunzi wakiwa darasani magari hayo yangeweza kusafirisha wananchi wengine ili wachangie gharama ya kuendesha mradi huu. Kuwabana na kupanga bei za usafiri kwa wafanyabishara wa usafirishaji abiria hailingani na sera ya soko huria. Serikali mpaka sasa haipangi bei ya mafuta wala vipuri vyat magari, kutokana na hali hiyo upangaji wa bei ya usafiri imeshindikana kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa fedha mwaka 2004 kwa ajili ya kuwalipa wakulima wa pareto wa Mbeya, Makete, Njombe na Mufindi kwa mavuno ya mwaka 2001/2002. Baada ya kufuutilia tatizo hili wakulima wengi wamelipwa mwezi Februari na Machi, 2006. Wakulima wa kata ya Tembeli, Ijombe na Iyunga Mapinduzi hawajalipwa hadi sasa. Hakuna hatua zozote zilizochukuliwa kwa wanunuzi wa pareto amba walipewa fedha za kuwalipa wakulima lakini hawakufanya hivyo.

Bodi ya pareto imepitwa na wakati kwa kuwa soko huria ndilo linalofanya kazi. Uhusiano wa kiwanda na wakulima ndio utakaofanya wakulima waongeze mazao, ubora na kupata bei nzuri mbali na hilo Bodi hii iko Dar es Salaam ambako pareto hailimwi. Bodi ya Pareto inapunguza kipato cha wananchi na mwananchi hapati manufaa kutoka Bodi.

Mheshimiwa Spika, naomba kasoro zilizopo zisahihishwe ili kuwawezesha wakulima wa pareto ambalo ndilo zao kuu la biashara katika maeneo ya Mbeya kuongeza juhudzi za kulima zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza tena Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri. Nami naomba kuunga mkono hotuba hii.

MHE. USSI AME PANDU: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nydingi za Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi kuwa Mwenyekiti wetu mpya wa Chama, kuchaguliwa kwake huko kwa kura nydingi ni ishara tosha ya uwezo aliokuwa nao wa kuliongoza Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Yusuf Makamba, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Katibu Mkuu wa Chama chetu cha Mapinduzi, pamoa na Wabunge wote ambao wamepata uteuzi mpya wa chama.

Mheshimiwa Spika, pia nataka nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Mtoni ambao wamenichagua kwa kura nydingi na mimi nawaahidi kuwatumikia kwa nguvu zangu zote.

Mheshimiwa Spika, moja, katika kuchangia bajeti ya Waziri Mkuu naomba nianze na ukurasa wa 40 ambao ukurasa huu unazungumzia ahadi za CCM wakati wa kampeni za uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, hapa naomba nikipongeze sana Chama chetu cha Mapinduzi kwa kukumbuka ahadi hizi, kwani vijana wa kike na kiume walituunga mkono sana katika kufanikisha ushindi ule, hivyo ila kujiandaa kwa uchaguzi wa mwaka 2010 naiomba Wizara yako Mheshimiwa Waziri Mkuu ichukue kila juhudzi kuona kwamba shilingi milioni 500 ambazo zitatolewa kwa kila Mkoa kuitia benki kwa ajili ya kuwakopesha vijana hao zinapatikana na kama alivyosema Waziri Mkuu wakati wa fedha hizo kuingizwa benki Waheshimiwa Wabunge kuitia Majimbo yao washirikishwe kikamilifu kwani wao ndio zaidi wanapata malalamiko hayo ya ajira kutoka kwa vijana hao.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo wakati Rais wetu mstaafu Mheshimiwa Benjmini Mkapa alipokuwa anafungua barabara ya Amani - Mtoni ambayo barabara hiyo imepita ndani ya Jimbo langu kwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa barabara hiyo aliahidi kwamba awamu ya pili ya ujenzi wa barabara hiyo ingemalizika kabla ya kuondoka madarakani, hivyo ili kutimiza ahadi ile ambayo aliitoa wakati wa kampeni za uchaguzi 2005 naomba imalizwe ili tutimize ahadi za viongozi wetu na za chama chetu.

Mheshimiwa Spika, ukienda ukurasa wa 24 wa bajeti hii ambao unazungumzia Shughuli za Bunge, hapa naomba nipongeze sana ofisi ya Waziri Mkuu kwa juhudzi zilizofanywa kwa kumalizika ofisi ndogo ya Bunge ilioko Zanzibar lakini pamoja na kumalizika ofisi ile kwa kweli vitendea kazi bado havijawekwa wala haina wafanyakazi wa kutosha, hivyo naiomba kupitia bajeti hii vitendea kazi viwekwe na wafanyakazi pia waajiriwe wa kutosha ili Wabunge kutoka Zanzibar wawe na Ofisi yao iliyokamilika. Sambamba na hilo pia naipongeza Ofisi ya Bunge kwa nia yake nzuri ya kutaka kuwajengea Waheshimiwa Wabunge ofisi za kileo Majimboni mwao zinazofanana na mazingira ya kileo.

Mheshimiwa Spika, nikienda kuchangia ukurasa wa 20 wa kitabu hiki cha bajeti nataka nichukue fursa hii kwa mara nyingine tena kukipongeza Chama cha Mapinduzi kwa kushinda uchaguzi ule wa mwaka 2005 kwa kishindo na kupata asilimia 80.28 kwa uchaguzi wa Rais.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na kufanikiwa vizuri kwa uchaguzi ule kuna matatizo ambayo yalijitokeza hasa pale wakati uchaguzi ule ulipoahirishwa baada ya kifo cha mgombea mwenza wa Urais wa CHADEMA bwana Jumbe Rajab na baada ya tarehe 30/10/1005 uchaguzi ule ukafanyika tarehe 14/12/2005.

Mheshimiwa Spika, hapa mimi nataka kutoa ushauri ili kuepuka matatizo kama yale ya kurefusha muda wa uchaguzi na Serikali kulazimika kutumia fedha zaidi, naomba sheria ile ikafanyiwe marekebisho ili mambo kama yale yasitokee tena.

Mheshimiwa Spika, mwisho nikushukuru na naipongeza hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na naunga mkono kwa asilimia mia moja.

MHE. MARGRETH A. MKANGA: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Rais na Mwenyekiti wa CCM. Pia nawapongeza Mawaziri na Manaibu Mawaziri wote bila kumwacha msaidizi mkuu kabisa Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri Mkuu wote kwa kuanza kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, pongezi nyingi ziwaendee Mheshimiwa Spika, Naibu Spika kwa ushindi walioupata kwa kura nyingi humu Bungeni hivyo kupewa ridhaa na imani ya kuongoza na Waheshimiwa Wabunge wote. Hongera zaidi ziwaendee Waheshimiwa Wenyeviti ambao nao wameanza kuonyesha uwezo mkubwa wa kuongoza shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huu naomba nijielekeze katika masuala kadhaa yaliyomo ndani ya hotuba hii. Nimefarijika sana katika ukurasa 9 Serikali imedhamiria kujali maslahi na mahitaji ya makundi maalum hasa wanawake, watoto, vijana, yatima, wazee na walemovu. Katika hili nitajikita zaidi kwa jamii ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, jamii ya watu wenyewe ulemavu wana matatizo mengi lakini naomba Serikali izingatie masuala kadhaa kwa mfano umuhimu wa kutoa ruzuku kwa vifaa (nyenzo) za kujimudu. Pamoja na kwamba Serikali haitozi kodi ya kutolea mizigo bandarini lakini vifaa hivyo bado hubaki kuwa ghali kwa ajili ya gharama za matengenezo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu upatikanaji wa mikopo kwa walemovu waliojiunga kwenye vikundi bado ni matatizo kwa vile katika Halmashauri zilizo nyingi vikundi hivi hawavitili maanani. Hivyo wanashindwa kuongeza mitaji yao kwa minajili ya kukuza shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala UKIMWI na elimu ya UKIMWI. Nimejaribu sana katika miaka minne iliyopita nikiwa Mbunge kuishauri Serikali umuhimu wa kuwa na meza (*desk*) maalum ndani ya *TACAIDS* ili pawe na mchanganuo na uratibu kamili wa jambo hili kwa jamii ya watu wenyewe ulemavu.

Mheshimiwa Spika, walemovu wa aina tofauti ya ulemavu wana tofautiana pia kutegemea aina ya ulemavu kwa mfano wasioona, viziwi, walemovu viungo, viziwi wasioona, walemovu wa akili na kadhalika. Hivyo kutokana na tofauti hizo za ulemavu, uelewa na jinsi ya kuwaelimisha jamii hii huhitaji mbinu tofauti.

Mheshimiwa Spika, ifahamike kuwa walemovu nao wako kwenye hatari ya kuambukizwa virusi vya UKIMWI kwa sababu wanaweza wakabakwa wakashindwa hata kujitetea kwa kushindwa kuona aliyembaka, akashindwa kusema bubu akashindwa hata kukimbia na kadhalika. Kwa msingi huo nashauri tena pawe na *desk* maalum ndani ya *TACAIDS* litakaloshughulikia masuala haya kwa undani zaidi kwa manufaa ya Taifa na walemovu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu naunga mkono hoja hii.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ya bajeti kwa mwaka 2006/2007. Aidha, nawapongeza watumishi wote wa Ofisi yake (Mawaziri na wataalam) kwa kazi nzuri sana. Pamoja na hayo napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Moja, shughuli za Ubunge ukurasa wa 23 wa hotuba. Kwa kuwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kupitia bajeti imeonesha kuwajali Wabunge kwa kuamua kwa dhati kabisa kuboresha ofisi za Wabunge Majimboni ili zifanane na wajibu wao. Naamini Serikali ya CCM chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu itatekeleza ahadi yake kwa uaminifu kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inawapa Wabunge magari ili waweze kutimiza wajibu wao Majimboni na kwa kuwa Serikali inawapa Wabunge bendera za kupeperusha kwenye magari na kwa kuwa Mbunge hawezikuendesha gari mwenyewe huku bendera ikiipepea, basi nashauri Serikali imlipie Mbunge mshahara wa dereva kama

inavyofanya kwa wasaidizi wa ofisi, vinginevyo Mbunge atalazimika kuajiri dereva na kumlipa kutoka kwenye mshahara wake. Hii nadhani si sahihi naomba hili Mheshimiwa Waziri Mkuu alitolea maelezo.

Pili, Serikali za Mitaa ukurasa 31 wa bajeti. Naomba kurejea sehemu ya hotuba ya hiyo inasema: "Mkakati ambao Serikali inatumia katika kuboresha mfumo wa Serikali za Mitaa ni kupeleka madaraka, majukumu na rasilimali zaidi kutoka Serikali Kuu hadi kwa wananchi kupitia Serikali zao za Mitaa." Ukurasa 31 wa hotuba.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kuzungumza hapa ni kwamba pamoja na kupeleka madaraka zaidi kwenye Serikali za Mitaa, lakini bado maeneo ya utawala hasa katika Jimbo langu la Mbozi Mashariki ni makubwa sana na hivyo hayataliki kwa urahisi na rasilimali haziwafikii wananchi kwa urahisi. Wilaya yenyewe ya Mbozi ambayo ina Majimbo mawili ya uchaguzi na ni kubwa sana ina idadi ya watu wanaokadirwa kufikia 600,000. Kata ya Itaka ina vijiji 13 na Idadi ya watu karibu 60,000 Kata ya Isansa ina vijiji 12 na idadi ya watu wapatao 35,000, Kata ya Igumba ina watu 30,000 vijiji 8. Kata ya Ihanda vijiji 12 na ina idadi ya watu wapatao 32. Katika hali kama hii itakuwa vigumu sana kwa maeneo hayo kutawalika na kuyafikishia huduma.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wilaya ya Mbozi igawanywe kuwa Wilaya mbili na Kata za Itaka, Isansa na Ihanda zigawanywe katika Kata mbili yaani kila Kata izae Kata nyingine. Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi ulishakaa na kuleta mapendekezo yake Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, tatu, kilimo cha umwagiliaji. Mbozi ni Wilaya ya Kilimo hivyo naomba Serikali iendelee kuwapa wananchi uwezo ili waweze kuzalisha zaidi. Mbozi pia kuna kilimo cha umwagiliaji katika maeneo ya Nami - Ng'ongo Kata ya Chitete-Mbozi Magharibi na Kijiji cha Songwe-Kata ya Ruanda-Mbozi Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa nia nzuri kabisa iliamua kujenga mifereji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji huko Nami - Ng'ongo, mradi huo umegharimu kiasi cha shilingi milioni 900 cha ajabu sana ni mradi ambao umetumia kiasi kikubwa cha pesa na hata kabla ya miezi sita haijaisha tangu kukamilika kwa ujenzi wake *intake* yake imeshaharibika. Mimi nina wasiwasi na ubora wa kazi yenyewe pamoja na mkandarasi aliyefanya kazi hiyo. Naomba Waziri Mkuu ikiwezekana na naomba iwezekane utume ujumbe ukakague mradi huo ulivyojengwa ukilinganisha na pesa nyingi zilizotumika.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kijiji cha Songwe ambacho tayari kina mfereji ambao haujajengwa kisasa na una maji kipindi chote cha mwaka sasa ujengwe kisasa ili kuwawezesha wananchi wa Songwe waweze kuzalisha kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, nne, kuhusu elimu. Moja, Wilaya ina upungufu mkubwa sana wa walimu kwa shule zote za msingi na sekondari. Serikali iikumbuke Wilaya ya Mbozi katika hili. Pili, Serikali iziagize Halmashauri ili walimu wapangwe hata shule

za vijijini na liwe agizo kwa maandishi. Tatu, kwa kuwa baadhi ya walimu wakipangwa shule za vijijini hukimbia baada ya kuona hakuna nyumba za kuridhisha katika shule nyingi vijijini, basi naishauri Serikali ione umuhimu wa kuwa na mpango kabambe wa kujenga nyumba za walimu vijijini.

Mheshimiwa Spika, tano, kuhusu miundombinu. Naomba Serikali ifikirie daraja katika mto Momba. Mto Momba ndio hutenganisha Wilaya ya Mbozi-Kata ya Kamsamba na Kata ya Kiliamatundu katika Wilaya ya Sumbawanga Vijijini. Barabara yenewe huanzia Mlowo hadi Kamsamba, kujengwa kwa daraja hilo ambalo sasa wananchi huvuka kwa kamba na kuhatarisha maisha yao, kutafungua maeneo ya Jimbo la Mbozi Magharibi na Jimbo la Kwela - Sumbawanga Vijijini kiuchumi, huko kuna kilimo cha mpunga, uvuvi na mifugo.

Mheshimiwa Spika, sita, wakati wa kampeni mwaka jana tarehe 31/8/2005 Mgombea wa CCM kwa nafasi ya Urais Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ambaye sasa ndiye Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliahidi kutatua tatizo la maji kwa Miji ya Tunduma na Mlowo iliyio Wilayani Mbozi. Hata hivyo, nilipopitia kitabu cha ahadi azozitaja Mheshimiwa Rais ahadi ya maji kwa Miji hiyo miwili sikuona. Naomba kujua hatma ya ahadi hii ya Mheshimiwa Rais ni nini, imeachwa kwa makosa au haifahamiki? Kama haifahamiki, sasa naomba ifahamike kwa kuwa Mheshimiwa Rais aliahidi kwenye mkutano ya hadhara.

Mheshimiwa Spika, uharibifu wa mazingira ni mkubwa sana katika vyanzo vya maji katika Mito ya Nkana na Hahungu Wilayani Mbozi. Naomba Ofisi ya Waziri Mkuu mwenyewe isaidie Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi katika kukabiliana na hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, saba, Shamba na 208 *NAFCO* Magamba, Mbozi. Shamba hilo lilianzishwa na Serikali mnamo miaka ya 1970 na ilishindwa kuliendesha kwa sababu *NAFCO* ilishindwa kuliendesha kwa sababu ambazo *NAFCO* yenewe ilizijua. Shamba hilo lina ukubwa wa ekari 12051 sawa na hekta 4879. Baada ya *NAFCO* kushindwa kuliendesha shamba hilo wananchi walianza kulikodisha kwa kulipia kiasi cha shilingi 10,000 kwa ekari moja. Hivyo, wananchi karibu 10,000 wa vijiji vinavyozunguka shamba hilo hutegemea shamba hilo kwa kilimo cha mahindi na wote huzalisha ziada na kuwauzia watu wengine.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali wa kutaka kuyauza mashamba hayo itakuwa ni kuwanyima wananchi hao fursa ya kuzalisha chakula na kwamba hali hiyo inaweza kuwavunja moyo wananchi hao na kwa kuwa watakuwa hawana mahali pengine pa kulima.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Serikali ijali maslahi ya wananchi wake kuliko kuwajali wawekezaji wachache. Si vizuri Serikali ikawafanya wananchi wake wawe vibarua katika nchi yao. Ni vizuri pia Serikali ielete kwamba wananchi wa Jimbo langu ni wakulima hodari hasa ukizingatia kwamba mpaka sasa shamba lote hilo hulimwa na wananchi na bado wengi hukosa. Je, Serikali ikibinafsisha shamba hilo inatarajia

wananchi hao waende wapi? Ni vizuri pia Serikali ielewé kwamba wakati shamba hilo linaanzishwa kuna wananchi ambao kwa nia nzuri waliondoka katika eneo hilo na wakati huo idadi ya wananchi katika vijiji vinavyozunguka shamba hilo ilikuwa karibu 3000 hivi, leo vijiji hivyo vina idadi ya watu wanaokadiriwa kufikia 30,000. Tunataka hawa waende wapi?

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali itengue uamuzi wake wa kulibinafsisha shamba hilo kwa manufaa ya wananchi wa Wilaya ya Mbozi. Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi iko tayari kulinunua shamba hilo na baadaye kufanya utaratibu wa kuwauzia walengwa kwa utaratibu mzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kama iliwezekana kwa wananchi wa Peramiho kwa kuwapa shamba la Hanga, sioni kwa nini Serikali isikubali ombi la wananchi wa Mbozi. Naamini Serikali ni sikiu na itasikia kilio na ombi la wananchi wangu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HASNAIN G. DEWJI: Mheshimiwa Spika, ninayo furaha kupata nafasi hii ili kutoa maoni yangu kwa njia ya maandishi kuhusu hoja yako. Kwanza, kabla sijatoa maoni yangu, niseme tu naunga mkono hoja yako.

Pili, ninayo machache kuhusu hoja hii, nayo ni haya yafuatayo, ambayo ni maoni yangu kuwa yatafanyiwa kazi kwa njia moja au nyingine.

Moja, katika Wilaya yangu ya Kilwa inayo mapori mengi ambayo yako kando kando na *Selou Game Reserve* na kwa kuwa kuna *Open areas* ambazo hupewa kampuni za watalii lakini bado mchango wao ni mdogo katika Halmashauri yetu, tunaiomba Serikali iangalie suala hili na ikiwezekana itupe mgao mkubwa unaotokana na kipato kutoka kwa watalii hao.

Pili, kama inavyoilewaka, Wilaya ya Kilwa tunayo gesi ya Songsongo ambayo inaweza kabisa kutumika majumbani kwa ajili ya wananchi kupikia na kuinusuru nchi yetu katika kuharibu mazingira kwa kutumia kuni au mkaa. Mfano mzuri pia ni wenzetu wa India ambao hutumia gesi kama nishati mbadala ya petroli.

Mheshimiwa Spika, tatu, naiomba Serikali kuifikiria Wilaya ya Kilwa ipate ruzuku kutokana na mapato ya gesi ya Songsongo ili Halmashauri yetu ipate mgao maalum, ili kutokana na kipato hicho inawezekana kabisa ukapatikana mchango kwenye sekta za Afya, Elimu, Maji, Barabara na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nne, naomba pia Serikali iangalie uwezekano wa kujenga pia kiwanda cha Mbolea kwa kuwa inatengenezwa na *Gas-asilice* ambayo inapatikana Kilwa. Kwa miaka ya nyuma pia kulikuwa na mpango wa kupata Kiwanda kama *TPDC* naomba hiyo pia ifikiriwe kwa vile suala hili litakuwa ni kuendeleza yale yaliyokuwa yamefikiriwa kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, tano, Wilaya ya Kilwa ina Madini ya *gepson* ambayo yapo katika vijiji vya Mandawa na Kiranjeranje, ninaiomba Serikali iangalie namna ya kuyatafutia soko madini hayo ili vijiji hivyo viweze kunufaika na pia kumpata mwekezaji kwa ajili ya kiwanda cha sementi.

Mheshimiwa Spika, sita, Wilaya ya Kilwa ina matatizo makubwa ya Maji safi ya kunywa hasa katika kata za Pande na Limayao, ninamuomba Mheshimiwa Waziri wa Maji aweze kuwasaidia wananchi hao nao wapate maji safi na salama.

Saba, Kijiji cha Pande barabara zake ni mbovu sana yaani imekuwa kama kisiwa kwa maana kwamba barabara za kwenda huko hazipitiki kabisa na pande ni kijiji ambacho kinalima korosho kwa wingi, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri Muhusika aangalie namna atakavyotusaidia katika suala hilo.

Nane, tunaomba pia hasa wananchi waliopo kwenye mwambao wa bahari kuwana mipango maalum ya kuwakopesha wavuvi pembejeo na tupate viwanda vyakusindika samaki.

Tisa na mwisho, kama Mheshimiwa Waziri na Miundombinu alivyosema kuhusu wakandarasi wa barabara wasaidie jamii zilizoko kandokando ya barabara, kwenye sekta za Afya, Maji, Elimu ili kuweza kusaidia kuleta maendeleo katika vijiji hivyo.

Mwisho ni matumaini yangu kuwa mchango wangu utafanyiwa kazi kwa njia moja au nyingine.

MHE. ZUBEIR ALI MAULID: Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kwa mara nyingine tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka hai na wazima wa afya. Vile vile napenda kuchukua nafasi hii kuzingatia itifaki katika kuwapongeza wale wote waliopata uteuzi katika nafasi mbalimbali katika Chama cha Mapinduzi kutoka mionganoni mwa Wabunge wenzenetu.

Mheshimiwa Spika, katika hoja hii napenda tena kuendelea kuchangia sehemu inayohusu kuuimarisha Muungano kama inavyojitokeza katika ukurasa wa 22 na 23 katika kitabu. Kwenye hili nawapa pongezi Mheshimiwa Rais kwa nia yake thabiti ya kuuimarisha Muungano na pia Waziri Mkuu kwa kwanza kuonesha njia katika kuitekeleza ahadi hii ya Rais. Wasiwasi wangu pamoja na wananchi walio wengi ni kwamba kwenye hili, Mheshimiwa Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu huenda wakawa wanakwenda kasi ambayo baadhi ya Watendaji inaonekana kama hawaimudu. Suala la kuondoa kero halihitaji ahadi za majukwaani bali zinahitaji utekelezaji na utekelezaji wenyewe ni wa kuzimaliza na sio wa kuendelea kuziongeza.

Mheshimiwa Spika, ni hivi karibuni tu wakati wa kuchangia hoja ya Bajeti ya Serikali, tuliizungumzia sana Taasisi ya *TRA* kwamba inawanyanyasa wafanyabiashara na wananchi wa Zanzibar, lakini cha kusikitisha ni kwamba wakati wa kujibiwa hoja zetu, Naibu Waziri akatuambia kwamba na hili nalo litaingizwa katika orodha ya kero. Suala nilizozungumzia lilihusu gari zilizosajiliwa kwa namba za Zanzibar. Nilisema

kwamba kwa vile kodi za uingizaji gari Tanzania madhali zinakusanywa na Taasisi moja ya Muungano (*TRA*) suala la usajili lisitugawe na wala haileti haiba nzuri gari zenye usajili wa Bara kutokamatwa Zanzibar na zile za Zanzibar kukamatwa Bara.

Mheshimiwa Spika, suala hili halihitaji kusubiri vikao vya kuondoa kero, hili linahitaji kauli ya kiongozi mmoja madhubuti kulisimamisha na kulikemea lisitugawe. Kiongozi kama Waziri Mkuu hili halimshindi na wala halihitaji kauli ya Rais. Katika nchi za wenzetu, gari zinasajiliwa katika majimbo na wala hazipati usumbufu kwenye jimbo lingine. Mfano ni Marekani (*USA*), India au hata Afrika Kusini. Sisi Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Muungano ambao ni mfano duniani, hili mbona dogo.

Naomba nimalizie kwa kuligusa kidogo suala la michezo. Michezo ina mchango mkubwa katika kuitangaza nchi. Hivi sasa kuna Kombe la Dunia linaendelea. Tunaiomba Serikali ifanye kila iwezalo kuhakikisha kwamba mchezo wa mpira wa miguu inaimarishwa. Mchezo huu una mchango mkubwa sana katika kuwaunganisha watu. Tuangalie nchi zenye migogoro ya kisiasa na halafu timu zao zikajaaliwa kuingia katika Mashindano ya Kimataifa. Watu kwa muda husahau tofauti zao na wakaungana katika kuzishangilia timu zao. Nchi kama Cote'D'Ivoire, Congo mifano hii ilijitokeza. Vile vile Serbia na Montenegro zilizokuwa Yugoslavia. Tunaomba michezo ili ituletee pamoja Watanzania. Nia tunayo, utekelezaji wake kidogo matatizo.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kuiunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Spika, napenda nirudie shukrani na pongezi zangu kwa hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Pamoja na maeleo niliyokuwa nimetoa awali kwa kuchangia kwa kusema.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo ambayo ningemwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu ayawewe kwenye kipaumbele katika mipango yake ya mwaka ujao.

Kwanza, mipango ya kukabiliana na madawa ya kulevyaa yapewe kipaumbele kama ilio Kampeni za UKIMWI. Hali ya sasa mijini vijana wastani wa asilimia 74 wanatumia dawa hizi, ni hatari kwa usalama wa Taifa la sasa na la kesho. Kasi zaidi itumike maana hata makahaba zaidi ya asilimia 80 wanatumia madawa hayo ili kuondoa aibu.

Pili, lingine ni sera ya wazee na sera ya idadi ya watu bado zimechelewa sana tangu mwaka 2002 hadi leo. Ni vizuri mwongozo ukatolewa kwa Wizara husika kukamilisha haraka iwezekanavyo wengi wanauliza mbona sera hizi zimewekwa kapuni.

Mheshimiwa Spika, tatu, wazee wastaifu wa Afrika Mashariki (1977) wapo kila siku kwenye milango hii ya Bunge letu. Hivi kuna nini huko ambako bado wanalamika?

Nne, mahusiano ya kiutaalamu ya kila Wizara kwa Halmshauri yaangaliwe upya ili madaraka ya kuzishauri Halmashauri zetu kiutaalamu bila vikwazo vya kisheria.

Mheshimiwa Spika, naiomba Ofisi ya Waziri Mkuu itazame uwezekano wa kutenga fedha za kutosha ili kumalizia jengo la Ofisi ya Manispaa ya Sumbawanga ambayo inajengwa kwa gharama ya shilingi 700 milioni. Pamoja na shukrani kwa Hazina kutupatia fedha za kuendeleza jengo hilo, awamu kwa awamu, wasiiasi wetu ni juu ya gharama zinaweza kuwa kubwa sana kwa kutoa fedha kidogo kidogo, kila mwaka. Tunaomba tukamilishe kwa muda mfupi ili kuondoa hasara kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru pia kwa Serikali kutupatia shilingi 145 milioni kwa ajili ya kuchimba visima vya maji na kutandika mabomba. Pamoja na hilo, naomba Serikali iendelee kututafutia wafadhili wa ndani na nje. Tunashukuru pia kwa Serikali kututengea pia fedha katika bajeti hii kwa ajili ya kununulia gari la zimamoto kwa ajili ya Halmashauri yetu.

Mwisho tunaishukuru Serikali kupitia kwa Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kutupatia kipaumbele. Sisi wananchi wa Mkoa wa Rukwa kupewa umuhimu wa mipango ya maendeleo. Hivyo tunaomba sana watumishi wanaoletwa mkoani wawe na upendo kwa Mkoa wa Rukwa, au tutapoteza dira aliyonayo Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote waliopo katika Ofisi yake na watendaji walomsaidia kuboresha hotuba yake nzuri ya bajeti ya mmmwaka 2006/2007.

Lengo kuu la mchango wangu ni kupendekeza mtazamo wa ratiba shirikishi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa utakaosaidia kupanga bajeti ya Taifa, kwa kuamini kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ndio msimamizi mkuu wa shughuli za Serikali na kwamba Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Wizara ya Fedha ziko chini yake. Bajeti shirikishi ya Kitaifa lazima ihusishe Mpango wa Maendeleo ya wananchi kuanzia ngazi ya kitongoji/kijiji, kuelekea ngazi ya Kata, Wilaya na Mkoa. Ngazi ya Wizara maalum na hatimaye Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na hatimaye Wizara ya Fedha na Bajeti ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, ifuatavyo ni pendekeso la ratiba ya Mpango Shirikishi wa Kitaifa kwa mwaka:-

Mwezi Julai kikao cha Bajeti na mhusika ni Bunge, mwezi Agosti mwanzo wa utekelezaji wa Bajeti mpya na mhusika ni Hazina, mwezi Septemba ni kuandaa mpango wa maendeleo ngazi ya kitongoji na husika ni Serikali za Vitongoji, mwezi Oktoba ni mpango wa maendeleo ngazi ya Kijiji na mhusika Serikali ya Kijiji, mwezi Novemba ni Mpango wa Maendeleo ngazi ya Kata na mhusika ni *WDC* na mwezi Desemba, Mpango wa Maendeleo ya Wilaya na mhusika ni Halmashauri ya Wilaya (*Full Council*).

Mheshimiwa Spika, mwezi Januari ni Mpango wa Maendeleo ya Mkoa na mhusika ni *RCC*, mwezi Februari ni Mpango wa bajeti ngazi ya Wizara na mhusika ni Wizara, mwezi Machi ni majumuisho Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwekezaji na

mhusika ni Wizara ya Fedha, mwezi Aprili na Mei ni makisio ya Bajeti namhusika ni Wizara ya Fedha na mwezi Juni na Julai ni Mkutano wa Bajeti na mhusika ni Bunge.

Mheshimiwa Spika, ili mpango huu utekelezeke ni lazima wawepo viongozi wenye elimu nzuri ya kusimamia matayarisho na andiko la mpango ngazi ya Kitongoji, Kijiji na Kata. Tulipoazimia kuwepo kwa watendaji wa Vijiji kiwango cha chini cha Elimu kiliwekwa kuwa darasa la kumi na mbili. Hata hivyo Halmashauri nyingi zikalalamika kwamba watu hao hawapo vijijini ni hivyo kuajiri wazee na vijana wa darasa la saba. Huu ni udhaifu!! Chuo cha Mipango Dodoma kipewe jukumu maalum kuandaa Watendaji watakaomudu jukumu hilo vijijini na hao ndio pia wawe Watendaji wa Vijiji na Kata. Watendaji hao pia wafanyakazi pamoja kwa kuwashirikisha Maofisa wa Ustawi wa Jamii ngazi ya Kijiji na Kata wote wawe na Elimu nzuri ya juu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutambua haja ya ushauri wa Waheshimiwa Wabunge katika kutekeleza shughuli za Serikali za Mitaa na kutoa wito maalum kwa Waheshimiwa Wabunge kwa nafasi yao ya Udiwani wajihusise zaidi na shughuli za Serikali za Mitaa katika Wilaya zao.

Aidha, Mheshimiwa Waziri Mkuu akatoa wito kwamba ratiba za vikao vya Halmashauri zipangwe kwa namna itakayomwezesha Mbunge kushiriki (ukurasa wa 32/33 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, napendekeza wito huu muhimu wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ufuatiwe na maandishi maalum kwa Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri zote. Uzoefu umeonyesha Wakurugenzi kupuuza wito uliokwisha wahi kutokwa mara nyingi hapa Bungeni kuhusu suala hilo na wanapoulizwa wanajitetea kwamba hawana maagizo rasmi kutoka TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, leo hii tarehe 28/6/2006 Mheshimiwa Waziri Mkuu anaweza kupata Halmashauri vinavyoendelea huko Wilayani ikiwa ni pamoja na Mikutano ya Mabaraza ya Madiwani (*Full Council*) wakati Waheshimiwa Wabunge tukiwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yetu kwamba uimara wa uongozi wa Serikali hii iliyopo madarakani sasa utendaji katika Halmashauri zetu utabadilika kuwa makini na kutumia fedha za Serikali kwa uaminifu na uadilifu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikushukuru wewe binafsi kwa kuwasilisha hotuba yako ya bajeti kwa mwaka 2006/2007. Pia niwapongeze wasaidizi wako wote Waziri wa TAMISEMI, Naibu wake, Waziri wa Nchi, Bunge, Naibu Waziri wa Nchi Maafa na UKIMWI na Sekretarieti yote kwa maandalizi mazuri ya bajeti inayolingana kabisa na kauli mbiu ya CCM, ari mpya, nguvu mpyana kasi mpya.

Mheshimiwa Spika, pia niupongeze uongozi mpya wa CCM Mwenyekiti wa Taifa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Katibu Mkuu Yusuf Rajab Makamba, Katibu Mwenezi Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Katibu Mipango Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe na Katibu Mambo ya Nje, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro.

Mheshimiwa Spika, sasa nitumie fursa hii ili nichangie kwa maandishi hotuba yako.

Mheshimiwa Spika, ni sahihi kabisa kama ilivyo kwenye kauli mbiu yetu kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu, maneno haya ni sahihi kabisa kwani bila kilimo hakuna habari ya maisha bora kwa kila Mtanzania wala suala la udhibiti wa wananchi halipo kwani ni dhahiri kdhibiti watu wenyenjaa ni suala gumu.

Mheshimiwa Spika, hali hii sio ngeni kwani tumeshuhudia pilika pilika hasa za viongozi wa Chama na Serikali walivyotaabika kwa msimu wa njaa wa mwaka 2005, shughuli za maendeleo nyingi zilisimama kwa kazi hii ya kuwaokoa wananchi katika janga la njaa. Labda nikupongeze wewe mwenyewe kwa juhudzi zako za kuokoa wananchi katika janga lile baya la njaa lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na kazi yako nzuri na wasaidizi wako, napenda nitoe ushauri ili kuboresha suala hilo kwa dhamira ya kuepuka kazi za zimamoto.

Mheshimiwa Spika, nina mapendekezo yafuatayo, kwanza Naibu Waziri mwenye dhamana ya Maafa na UKIMWI kuwa na takwimu sahihi muda wote ili basi pale panapojitokeza mapungufu iwe rahsi kiutekelezaji. Hali iliyojitekeza mwaka 2005 haikuwa sahihi kuendelea kupata taarifa (takwimu) wakati watu wanataabika na njaa.

Pili, wataalamu wa hali ya hewa (*TMA*) watumike ipasavyo ili kutoa tathmini sahihi ya hali ya hewa, ili kufanya maandalizi ya kutosha na tatu, Hifadhi ya chakula (Maghala) kila Wilaya yawepo na yapewe kipaumbele kwa mazingira ya kutunza chakula, ubora wa maghala na madawa ya Hifadhi.

Nne, Mikoa yenyekuame kama ilivyo kwa Singida na Dodoma hasa kwa majimbo kama Iramba Magharibi zao la mtama, uwele na mazao yale ya mizizi mihogo na viazi yahimizwe na yawe mazao makuu. Mazao haya yasipewe kipaumbele nyakati za ukame tu bali liwe kwa muda wote. Kadhalika Serikali itambue zao hili kitaifa kama inavyolitambua mchele, ngano na mahindi.

Mheshimiwa Spika, suala la elimu, kwanza juhudzi za *MMES* ni nzuri sana lakini sifa za utoaji wa fedha za *MMES* hauko bayana ni kazi ya kiwango gani inastahili kuungwa mkono na Serikali (*MMES*) baada ya wananchi kujitolea.

Mheshimiwa Spika, mamlaka yanayobebwa na Wakuu wa Shule (*Head Masters*) ni makubwa mno ambayo hayatoi mamlaka kwa Bodi ya Shule au chombo kingine chochote bali mamlaka yote anayo huyo Mkuu wa Shul, kadhalika shule iliyo tayari kuilea ile inayoanzishwa hizi zote ni kasoro tunahitaji marekebisho na nne, nguvu ielekezwe kuhakikisha (Maboma) madarasa yote yanakamilika kwani kiwango cha

kufaulu sasa kimeongezeka na wananchi wamehamasika sana kuwapeleka watoto waliofaulu kuijunga na Sekondari.

Kuhusu hali ya kisiasa, naipongeza CCM kuhimili ushindani wa kisiasa na kuwa mwasisi wa mageuzi kwa umahiri mkubwa. Pia Sheria namba 5/1992 Usajili wa Vyama vya Siasa itazame vizuri inapovisajili hivi vyama lipo udanganyifu mkubwa kwa orodha ya wanachama bandia hasa kwa Mikoa ya Pemba, ushahidi unaonyesha mbali ya CCM na *CUF* hakuna chama chochote kilicho na wanachama zaidi ya mia mibili. Huko Pemba, tafiti zimeonyesha nyakati za chaguzi mbalimbali kimatokea.

Kuhusu vyama vinavyoikiuka maadili visionewe aibu, suala kama migogoro ya muda mrefu, ubadhirifu, uongo (*Fabrication*), lugha za matusi na kadhalika Sheria ichukue mkondo wake vifutwe mara moja.

Kuhusu utawala bora, bado Halmashauri nyingi zinanuka kwa rushwa na maadili ya utendaji hayazingatiwi. Maafisa wengi wame-over stay waondoshwe mara moja.

Kuhusu *PCB*, ifanye ngazi hadi ngazi za chini kuanzia Kata, Kijiji na kadhalika. Pia ifanye kazi yake kama ilivyoelekezwa ya kuzuia na sio kuweka mitego ili kukamata. Elimu itolewe kwa wananchi na vyombo vya kiutendaji vinavyolalamikiwa sana kama vile Mahakama, Polisi, Hospitali na kadhalika. Serikali isione aibu kuwajibisha watu wasio waaminifu hasa kwa shughuli za wananchi.

Kuhusu Tume ya Kudhibiti UKIMWI (*TACAIDS*) ifanye kazi kwa kushirikisha Wabunge. Muundo wa kupitia Wilayani (Halmashauri ni wa urasimu na unajenga mazingira ya rushwa, kwanza Halmashauri utekelezaji wa majukumu yake Kiwilaya bado unazo kasoro nyingi. Hivyo sio busara kuwabebesha mzigo mwingine.

Orodha ya *NGO's* zinazoshughulikia UKIMWI Kiwilaya ziorodheshwe na zifulikane wazi wazi ili kupewa kipaumbele zaidi katika utoaji wa elimu ili kuepuka zile za ubabaishaji toka Dar es Salaam. Tume iwe na wepesi wa kuwashirikisha Wabunge, iepuke kama ilivyokuwa kwa miaka ya nyuma pale ilipoonekana haionyeshi kujali au kuendesha masuala mengi kuficho.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hoja hii kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa naomba niitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungao wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Mwneyekiti wa CCM. Pia naomba niwapongeze viongozi wapya wote wa CCM akiwemo Mheshimiwa Yusuf Makamba kuwa Katibu Mkuu, Mheshimiwa Aggrey Mwanri kuwa Katibu Mwenezi, Mheshimiwa Rostam Azizi kuwa Mweka Hazina na Mheshimiwa Jaka Mwambi kuwa Katibu Mkuu Msaidizi.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hoja ya Bajeti yake ambayo ni nzuri na inaendana na utendaji wake japo naamini pia imehusisha na umaliziaji wa kazi zilizoanzwa na viongozi waliopita.

Mheshimiwa Spika, nina imani na utekelezaji wake pia kwa kuwa namfahamu vizuri Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mtu wa kutaka mambo yatokee, *action oriented person*. Mheshimiwa Edward Lowassa ana sifa zote za wajasiriamali, *pragmatist, activist, reflector* na *moderate theorist*. Ana kiu ya mafanikio, mshirikishaji, mvumilivu, anajiamini, anathubutu, kipenzi cha watu na mengine mengi. Kwa sababu hizo najikuta nashindwa kuvumilia kutokuchangia hoja yake, ndiyo maana imenibidi nichangie kwa maandishi ili mradi tu fursa hii iweze kuongeza japo mawazo machache.

Mheshimiwa Spika, katika suala la afya ni maeneo mengi ambayo Serikali yetu inajitahidi. Lakini kwa kweli ni jambo la msingi kuweza kutumia iwezekanavyo raslimali zote tulizonazo. Kwa hali ya sasa Serikali haiwezi kujenga hospitali zote kwa mara moja kila kijiji na kuweza kupata wafanyakazi wa kutosha kwa mara moja.

Pamoja na ruzuku zinazotolewa kwa baadhi ya hospitali za binafsi au kidini, nashauri tupanue wigo huo. Nianzie kwa kuiombea msaada hospitali ya Misheni ya Maguu iliyopo Wilaya ya Mbanga, Hospitali hiyo ipo mstari wa mbele katika kuhudumia wagonjwa wakiwemo akinamama wa bonde lote la Hagati. Toka Maguu mpaka Litembo hospitali kubwa ni umbali wa kilometra 20 kwa gari na kilometra 7 wa miguu ambapo inabidi mgonjwa apande milima mikubwa sana ya Mikiga. Nilipotembelea hospitali ile mwaka 2006 Januari, Masista pamoja na akinamama wajawazito walitoa ombi la kupata *Utra Sound Machine* ambayo itasaidia kuonyesha kama mtoto amekaa vibaya ili aweze kuwashishwa hospitali ya Litembo kwa vile wao hawafanyi *operation*. Akisisitiza Sista alisema akinamama wengi wanafariki kwa kutokujua. Kama hivyo hospitali hiyo imo katika mpango wa kujenga chumba cha *X-ray* na baadaye chumba cha *operation*.

Hivyo basi kwa kuwa Tanzania tunazo hospitali nyingi ambazo zipo vijijini za kidini au watu binafsi ambazo zinafanya vizuri na ndizo zilizopo kwa sasa, basi bila kujali kuwa siyo za Serikali, zisaidiwe kuboreshwa kwa kuanzia wakakti serikal ikiwa inaendelea na juhudhi za kujenga zahanti zake. Umuhimu huo unatokana na ukweli kuwa sehrmu hizo ndizo wanazotibiwa wapigakura wengi waishio huko mbali na hospitali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, ajira kwa akinamama na vijana ni wazo tu, endapo kutakuwa na uwezekano wa kuanzisha *partnerships* za vijana wa Kitanzania na nchi za nje mfano Marekani na kadhalika. Naamini kuna vijana wengi ambao wako huko majuu, wana pesa za kutosha aidha, kutokana na urithi au zawadi kutoka kwa wazazi wao na marafiki na wengine wana nia ya kuwekeza pamoja na vijana wenzao. Tuangalie jinsi ya kuwashirikisha kwa njia ya mitaji na utaalam, kwani sisi ardhi tunayo na nguvu tunayo na nia tunayo. Naomba wazo hili lifanyiwe ukarabati kwa kuongezewa thamani, lakini hatimaye tupate kitu cha namna hiyo ambacho kitapanua wigo wa ongezeko la ajira na utajiri kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuhamasisha jamii katika kuongeza tija, ufanisi na maendeleo. Waheshimiwa Wabunge tufanye ziara za kuongea na wananchi pamoja na makundi mbalimbali ya jamii katika mikutano na semina mara kwa mara katika maeneo yetu ili kuhamasishana na kujenga urafiki ambao utawezesha kupeleka taarifa muhimu zinazolenga kuboresha jamii, kwa mfano tukitoka hapa tunaweza kupeana *agenda* moja ya Kampeni dhidi ya Malaria na sisi kama Wabunge tutoe taarifa ya utendaji pia kwa Bunge letu kwani tunalipwa mishahara na tunawajibika kuripoti tumewatendea nini wananchi wetu. Hii itasaidia pia kunyanya hadhi ya Bunge letu kiutendaji. Nimejaribu kufanya hivyo kwenye shule na nimeona *impact* yake kwa jamii ni kubwa na nzuri. Naomba nijipigie makofi mwenyewe!

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI:- Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kutoa pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupata kura nyingi za kuwa Mwenyekiti wa Chama Tawala, hongera sana. Vile vile pongezi za Sekretarieti mpya ya CCM.

Pongezi kubwa kwa bajeti ya Waziri wa Fedha na hoja ya Waziri Mkuu kwa kuwa na bajeti inayoendana na ahadi za Rais wetu wakati wa kampeni yake, imegusa kero nyingi za Watanzania. Hii inaonyesha jinsi Serikali ya Awamu ya Nne inavyojali maslahi ya wananchi.

Baada ya kusema hayo sasa niungane na wenzangu kuunga mkono bajeti hii kabla sijapigiwa kengele, ninaiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia.

Sasa nije kuangalia kitabu kizima cha bajeti na hoja za Waziri Mkuu nikianzia kwa kumshukuru Waziri Mkuu kwa chakula cha njaa, kwa kweli umefanya kazi kubwa ya kutulisha ni budi kumshukuru binadamu mwenzio basi hata Mwenyezi Mungu utashindwa kumshukuru kwa hiyo ahsante sana kwa chakula cha njaa.

Mheshimiwa Spika, suala la kilimo ninaona linearudi nyuma hii ni kutokana na kutegemea mvua na sasa mvua hazipo lazima tuanze kuweka mikakati ya kubadilisha mwelekeo na kuongeza tena kitu ambacho kitakuwa mbadala na mvua, na si kingine ni kilimo cha mwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, tuna mabonde mengi nchini, Bonde la Mto Rufiji, mabonde ya mto Ruvuma, mabonde ya mto Malagalasi, mabonde ya Maziwa Natron, Eyasi, Nyasa, Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika, mabonde ya ufa na hasa Bonde la Mto Lukuledi ambao unalisha mikoa ya Lindi, Mtwarra, mabonde ya Ruangwa (Mkowe, Chikoko, Mnacho na kadhalika).

Mabonde yote haya yanafaa kwa kilimo cha kiangazi na sasa hutumiwa na wakulima wadogo wadogo tu ambao huzalisha vitu vichache tu. Serikali sasa wayatumie mabonde hayo kwa miradi mikubwa ya kilimo ili kuzalisha zaidi kwa kujitosheleza kwa chakula cha nchi nzima. Wakulima hawa wakiwezesha watapata zaidi na uchumi wetu

katika kilimo utaongezeka, vijana wapangwe wapewe zana tuone kama hatujafanikiwa kupata mazao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hifadhi ya chakula. Kuhifadhi chakula ni muhimu sana kama Waziri Mkuu alivyotaja katika hoja yake, watu sasa wameongezeka, ni muhimu sasa kuongeza kituo kingine cha kuhifadhia chakula kuliko kutegemea vichache tulivyonavyo. Ongezeni vituo vya hifadhi ya chakula.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme. Suala la umeme nchini limekuwa ni tatizo kubwa, hatuwezi tena kutegemea umeme wa maji, katika nchi nyingine duniani hawategemei umeme wa maji *Hydro Electric Power*, huu ni umeme hafifu sana ndiyo maana tunahangaika. Sasa njia pekee ya kupata umeme ni njia ya mkaa wa mawe tu.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Wizara kwa kutambua hilo, tunayo makaa ya mawe, tunayo gesi ya *Mnazibay*, Mtwara na Songosongo, Kilwa Mkoani Lindi. Kwa nini tupate taabu ya kukodi mitambo kununua umeme wa Afrika ya Kusini, tuanze sasa kutumia raslimali yetu.

Mheshimiwa Spika, hakuna kitu kitakachotukomboa katika giza kama elimu. Elimu ya chekechekea, elimu ya msingi, elimu ya sekondari na elimu ya juu hizi ni muhimu kwa maendeleo yetu. Tutafute, tukope, tuombe ili mradi wananchi wetu wapate elimu. Tunayo matatizo katika kuendeleza elimu katika sekta mbalimbali nayo ni uhaba wa walimu, ninashukuru tumepewla lakini watakuja? Uhaba wa nyumba za walimu, vyoo vya shule, walimu, pia samani za shule.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru *MMES* na *MEMM* wametusaidia lakini bado kuna tatizo hayo juu sasa twende tukakope katika nchi za nje ili kuendeleza elimu, kama sisi hatuwezi katika *World Bank* zinatolewa mkopo kwa nchi maskini *Highly Indebted Poor Countries (HIPC)*, kukopa ni heshima, twende tukakope tuwape elimu watoto wetu. Tunahitaji shule kila Kata sasa kwa kuanzia wengine wamefanikiwa kuwa na shule kila kata, sasa wanaenda katika kila kijiji, wengine wapo nyuma sana.

Mheshimiwa Spika, tumeshukuru sana kwa maandalizi mazima ya Uchaguzi ambao ulishirikisha vyama vya kisiasa, ninaona sasa Tanzania imekomaa kisiasa na kuwa na demokrasia kamili (wengi wape) uchaguzi ulishirikisha vyama vyote 10 kwa wagombea urais na 18 kwa wagombea ubunge na udiwani. Ninawapogeza vyama vilivyoshinda. Hongera kwa CCM kupata asilimia 80.28 ya kura zilizopigwa Rais na pole walioshindwa kama *NCCR 12%* na *PPT Maendeleo 1%*.

Tunaishukuru pia Serikali kwa kufikiria wanawake na kuwaweka katika ngazi za maamuzi kutupa Ubunge wa Viti Maalum vinginevyo hatungekuwa Wabunge. Mimi nimeona sasa ni wakati wa Serikali kutupa njia maalum ya kutuendeleza wanawake katika shughuli za Ubunge, Wabunge 75 wanawake katika ngazi za maamuzi ambao kuongeza 22 wa majimbo na kufikia asilimia 30.4, ikilinganishwa na 20 ya mwaka 2000. Kwa kweli tunapiga hatua sasa lengo ni 50% kwa 50%, tunafanyaje maanuzi yatoke mapema ili tuweze kujianaa, maana mwisho wa uchaguzi ndiyo mwanzo wa uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Muungano. Tunaishukuru Serikali imejali sana suala la Muungano wetu na sina shaka matatizo yatashughulikiwa. Tuwe na subira wapinzani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bunge, tuna matatizo ya ofisi za Wabunge zifanyiwe hima kutukabidhi ofisi kwa kila Jimbo ili tuweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, Ulinzi na Usalama. Tunaipongeza Serikali na sekta husika kwa kushughulikia uhalifu, kazi kubwa imefanywa ya kushughulikia wahalifu wakubwa na wadogo. Tuendelee hivyo hivyo, tusichoke. Ulinzi na usalama wa raia na mali zao ni muhimu katika uchumi wa nchi, mtu hawesi kuendeleza kilimo, viwanda, uchumi kwa ujumla kama hakuna Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, ni muhimu sana.

Wizi ultaka kushamiri sana ulianza kuja hadi vijiji sisi Wilaya yetu ndogo mpya walitaka kuvamia tarehe 24/12/2005 walikuja wezi 10 na silaha zao wakitokea Mtwara. Mtwara kuna wezi waitwao Tukale Wapi, wanatokea vilevile Msumbiji, wanaiba usiku na kurudi kwao. Kwa hiyo, raia wema, wananchi wakatupigia simu kuwa kuna wezi 10 wanaume wote wanakuja kuteka silaha zilizopo katika Kituo cha Polisi. Ilipofika tarehe ile kweli wezi wakafika. Kwa vile tulija tukawawinda kwa hiyo walipotokea tukawakamata, na zile purukushani wezi 6 waliawa hapohapo wengine walikamatwa hai na sasa kesi zao zipo Mahakamani kwa hiyo wezi sasa wamehamia vijiji, tuwaelimishe wananchi wetu vijiji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Utawala Bora. Kwanza nianze na suala la Mahakama. Kuna uhaba sana wa Mahakimu vile vile ofisi za Mahakama. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006 tumeona jitihada za kukarabati Mahakama na kutunza mazingira nchi nzima, hongera sana sasa zijengwe mpya hakuna ofisi za kutosha zijengwe mpya zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Magereza. Magereze zetu zimejaa sana utaratibu ufanywe ili kuangalia upya magereza yetu, magereza ni machache na pingu ni chache zilizotumika zamani wakati wa ukoloni hadi sasa ni vile zile sasa hivi badala ya kutumia pungu basi hutumia kwa kufunganisha nguo, mashati watu watano watano. Hiyo siyo haki za binadamu vilevile suala la kutunza watu ndani ya gereza, watoto watenganishwe na wakubwa ili kuepusha maovu zaidi, yanayofanywa na wakubwa kwa watoto.

Mheshimiwa Spika, sekretarieti za Mikoa katika baadhi ya Mikoa bado kutimia hasa katika sekta ya ya Ushirika, Serikali za Mitaa na Afya utaratibu ufanywe ili kutatua hilo.

Utaratibu ungeelekezwa ili maafisa wafuatao waweze kusikiliza kero za wananchi angalau kila mwezi watenge siku za kusikiliza kero za wananchi Ma-RAC, Ma-DC, Ma-DED, Wabunge na Madiwani. Kero kubwa kwa wananchi na kusubiri kiongozi mkubwa aje. Hii inaleta picha mbaya. Safari za viongozi zimekuwa nyingi hivyo kukosa kujua matatizo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, utumishi wa umma. Nchi ina uhaba wa watumishi wa umma katika sekta mbalimbali. Makaimu ni wengi. Sasa kumekuwa na jina la makaimu juu ya

makaimu tuzibe mapengo, makaimu wapasishwe wawe wakuu wa idara badala ya kuitwa Kaimu wa Kaimu. Nyumba za watendaji, magari na ofisi za Ma-RC na Ma-DC zikarabatiwe, *OC* ya *RC* na *DC* ni ndogo sana. Wao huo omboomba tu kwa Ma-DED. Kazi haitakuwa nzuri kama utawala wanakuwa ombo ombo tu. Upungufu wa *VEO* na kutopata malipo yao. Kuna tatizo la watendaji kazi hawatoshi na tatizo la mishahara yao katika baadhi ya vijiji nchini kama Wilaya ya Ruangwa kuna vijiji 75, ni vijiji 31 hawajapatiwa mishahara yao tangu waanze kazi. Hii ni kero kubwa. Katika butchet hii tujaribu kuondoa tatizo hilo. Kuna tatizo vile vile la baadhi ya *K.A. R.* hawajalipwa pensheni zao hawa walioagizwa walipwe.

Mheshimiwa Spika, semina kwa viongozi na mafunzo. Kwanza napenda kuipongeza Serikali ya awamu ya nne kwa kuanza kutoa maelekezo ya kazi kabla hatujafika mbali. Mheshimiwa Rais alitoa semina elekezi kwa viongozi wakuu hapo Arusha mwezi Machi, 2006. Tumeambiwa semina kama hizi zitaendelea katika ngazi za Mikoa na Wilaya. Semina hizi ni muhimu sana kwa ma-RC na ma-DC, ma-DED na ma-DAS viongozi hawa wanafanyakazi kwa akili zao tu. Inategemea wewe umelalaje sasa utapata maelekezo kutoka juu. Kwa hiyo, kukiwa na semina za maelekezo zitasaidia sana kwa ngazi za mikoa Wilaya na Tarafa, sekta ya ma-DC, Wakuu wa Wilaya iendelee kuwepo.

Mheshimiwa Spika, ugawaji wa maeneo ya utawala, kuna umuhimu sasa wa kuongeza kurekebisha maeneo ya utawala katika maeneo yote kuanzia Mkoa, Wilaya, Jimbo, Tarafa, Kata, Vijiji hadi Vitongoji. Watu sasa wameongezeka. Ili tuweze kuwatawala ni lazima maeneo ya utawala uongezwe. Ili kurahisisha huduma ni budi maeneo hayo yaongezwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu UKIMWI, tunaomba elimu ya UKIMWI sasa ielekezwe kwa wazee. UKIMWI sasa unakwenda kwa wazee *NGO* zinazohusika na kuelimisha udhibiti wa UKIMWI zielekeze nguvu zao katika vijiji waliopo walengwa hawa kwa wazee na wale mavu.

Mheshimiwa Spika, naomba nzungumzie ushirika. Ushirika sasa umekufa, sasa hufanya uwakala wa matajiri katika ununuzi wa mazao. Mazao yananunuliwa katika vyama vyaya msingi tu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma za jamii, kilimo, tunaishukuru Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuwa na kilimo cha umwagiliaji maji. Mimi naunga mkono kabisa. Sasa tuangalie kilimo cha kiangazi kwa kutumia mabonde tuliyonayo.

Mheshimiwa Spika, tunayo mabonde mazuri sana nchini ambayo yangeweza kutumika kwa kilimo kama mabonde ya mto Rufiji, Ruvuma, Kilombero, Lukuledi, Malagalasi, Pangani, vile vile mabonde ya Ziwa Victoria, Tanganyika, Nyasa, Eyasi, Natron, mabonde ya Ufa. Hata kule Ruangwa kuna mabonde ya Mkowe, Ngolongolo, Mnacho, Chikoko na kadhalika. Mabonde haya yote yanaweza kuzalisha mazao kadhaa na kuendeleza uchumi. Tunaomba mpango maalum na mikakati ya kuendeleza kilimo

cha mabondeni, kupata mbegu husika, kupata pembejeo hasa zana za kilimo. Mabonde haya yanaweza kuzalisha zaidi ya kukuza uchumi wetu nchini.

Mheshimiwa Spika, mifugo nayo ipewe pembejeo kwa Mikoa ya wafugaji, josh, dawa, maeneo ya ufugaji watengewe maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanda nya kusindika chakula. Kuna umuhimu wa kusindika vyakula ili kuongeza thamani ya mazao yetu. Tunazo rasilimali nyingi sana za kilimo ambapo zinawezwa kusindikwa kama korosho. Korosho ukisindika nchini unapata faida ya mali ghafi kadhaa maganda ya korosho hutumika kwa mafuta, gundi, fuele za viwanda. Makapi yatokayo katika nut korosho hutumika kwa chakula cha mifugo. Nut yenye ni chakula safi kwa atu. Wamerika matajiri ndio wanaokula korosho. Nut hutumika kwa kutengeneza biscut, cake na aina mbalimbali za chakula. Kwa hiyo, ni muhimu kuwa na viwanda nya korosho Lindi.

Kwa hiyo, Tanzania ina malighafi nyingi za kilimo ambazo zikisindikwa hapa uchumi utaongezeka badala ya kupeleka malighafi nje. Kwa njia hiyo ya viwanda nya usindikaji tunaweza kuzalisha uchumi zaidi badala ya kutegemea kilimo peke yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanda nya saruji. Saruji Tanzania ina uwezo wa kutengeneza saruji kwa wingi sana. Ina malighafi udongo mzuri kwa ajili ya kutengeneza saruji kwa hiyo sasa tuongeze uzalishaji wa simenti kwani kuna mahitaji mengi ya saruji sasa. Majengo mengi yanajengwa na kutegemea tu saruji ya Tanga, Mbeya na Dar es Salaam, haitoshi kuna udongo mwingi mzuri kwa ajili ya utengenezaji wa saruji, kama vile kuna udongo mzuri mzuri Kilwa mkoani Lindi ungeweza kutumika kwa ajili ya kuanzisha *cement*, kiwanda cha *cement* kingine, Kusini.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Mbolea gesi inayotoka Lindi na Mtwara kianzishwe kiwanda cha mbolea kwani gesi ni malighafi ya kutengeneza mbolea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Madini, Tanzania inayo madini mengi sana kiasi kwamba kama yangedhibitiwa, uchumi wa nchi ungekuwa zaidi. Kwa hiyo, Serikali iangalie suala la kudhibiti madini yasiondoke ovyo, migogoro ya madini itatuliwe, tuangalie tatizo ni nini? Vile vile tuwasaidie nyenzo za kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, tunayo madini mengi. *Tanzanite*, dhahabu, makaa ya mawe, chuma, almasi, *Green Tomaline* na vito nya aina mbalimbali. Hivi karibuni, Tanzania yamegundulika madini mapya yapo ndani ya chuma cha *Liganga* iitwayo *Titanium* na *Vandawium* ambayo itatumika kwa ajili ya *nuclear* au kutengeneza mabati ya ndege (mbawa, bodi madini hayo hupatikana katika nchi tatu tu duniani, Amerika, Afrika Kusini na Tanzania, huu ni utajiri mkuu sana.

Kuhusu miundombinu, barabara ni kiungo muhimu sana vijiji na nchi mzima. Tunaishukuru *TANROAD* na mifuko ya barabara kwa kutengeneza barabara zetu. Ila sasa kuna tatizo moja, mfuko wa barabara hujali kutengeneza barabara zile zile zilizo katika mpango wake, hawajaweza kuweka fursa ya mipango mingine ya utengenezaji wa barabara mpya hii ni kero kubwa sana barabara zinazoachwa kutengenezwa ni za

kupitisha mazao ya wakulima za vijiji kwa hiyo, tunaomba Serikali iruhusu *council* kuweka mipango mipyä ya utengenezaji wa barabara mpyä. Sisi Wilaya ya Ruangwa, kuna kero kubwa kwa wananchi kwa kutotengenezwa barabara ya zaidi ya zile zilizopo katika mpango wao wa mfuko wa barabara za Mandawa -Mputwa kilometa 27, Luchelegwa - Nandanga kilometa 8, Manokwe - Chienjele kilometa 9, Namichiga - Matambarare na vile Milola – Mandawa kilometa 30, kilometa 15 karibu shilingi 225,950 zinahitajika.

Vile vile barabara ya Ruangwa - Nanjilinji - Kilwa la shilingi milioni 200 ili barabara ipite hapo. Tunaomba tusaidie barabara hizo vile vile suala la ukaguzi wa madaraja ufanyike mara kwa mara ili kuondoka idadi za ajali zinazotokea barabarani.

Kuhusu upimaji wa viwanja, kumekuwa na kigugumizi sana katika upimaji wa viwanja. Watu sasa wameendelea na wana pesa, wanataka kujenga nyumba, Wizara hiyo ipewe na watu wajenye kwa utaratibu ili kuondoka usumbufu wa bomoabomoa ambao unakuwa kero kwa wananchi. Sasa tuanzishe miji mipyä badala ya bomoabomoa, miji ambayo itakuwa na *plan* nzuri za barabara. Tunaishukuru Serikali kwa kushughulikia migogoro ya ardhi. Ni heshima kubwa sana kwa kuondoa kero hizo.

Mheshimiwa Spika, maji ni chakula, maji ni uhai. Kumekuwepo na matatizo ya maji karibu nchi nzima. Kama kungekuwa na uwezekano wa kuwa na *operation* ya maji nchi nzima hasa katika Mikoa ya Lindi hasa Nachingwea, Liwale, Kilwa, Lindi na Ruangwa. Wilaya hizo watu wameongezeka, mabomba yaliyopo ni yale yale ya ukoloni hayajakarabatiwa kwa miaka mingi. Katika Mkoa wa Lindi waliahidi shirika la *JICA* mwaka 2000, wamefanya vijiji vichache tu, sehemu kubwa yenye matatizo makubwa bado kama vijiji vya Chinongwe, Litama, Likwachu, Ipingo, Chillangalile, Liugulu, Chibula na Machang'anja. Hadi leo tangu mwaka 2000 miradi hiyo haijaanzwa. Tunaomba Serikali iwakumbushe wenzetu wa shirika la *JICA*, Japan.

Mheshimiwa Spika, eneo la afya. Katika sekta hii tumeambiwa kuwa kuna mradi maalum uitwao mradi wa ukarabati wa vituo vya afya. Mimi ninaomba sana mradi huu uelekeze nguvu zake katika Mkoa wa Lindi ambako kuna matatizo makubwa ya vituo vya afya, Hospitali na zahanati katika Mkoa wa Lindi kuna Wilaya ambazo hazina hata hospitali ya Wilaya kama Wilaya ya Ruangwa haina hospitali yenye hadhi ya Wilaya. Wananchi wake waliambiwa kama mnataka kuwa na hospitali basi jengeni majengo husika na sasa wananchi hao tayari wamejitlea kujenga majengo 6 ni kama ifuatavyo, majengo ya *ward* ya wanawake, jengo la upasuaji (*theatre room*), nyumba ya *X-ray*, *waiting maternity room*, *ward* ya wazazi na kukarabati *ward* zilizopo.

Majengo hayo yote hayana vifaa, hata *X-ray* haina ambayo inahitaji shilingi 199,870,430. Wananchi wanashindwa sasa kujitolea kwa kununua kwani wamejenga nyumba nyingi. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali, isaidie vifaa vya Hospitali ya Wilaya ya Ruangwa, vile vile kuifanya Hospitali ya Wilaya iweze kumudu kutumikia wananchi ambao huja pale kutoka Wilaya zote jirani za Mkoa wa Lindi ambazo ni Liwale, Kilwa, Nachingwea, Lindi Vijijini na Wilaya ya Masasi huja pale kutibiwa pia.

Kuhusu vifo nya akinamama na watoto. Vifo nya watoto na akinamama wakati mwingine hutokeza ni kwa sababu ya akinamama kujifungulia kwa wakunga wa jadi ambao wengine hawakupatiwa mafunzo maalum ya uzazi. Ni karibu asilimia 40 ya wanawake hujifungulia kwa wakunga wa jadi. Wakunga hawa hutumia vifaa ambavyo si salama kwa hiyo tunaomba Serikali katika mpango wake wa miaka mitano katika kuwajali wakunga wa jadi kwa kuwapa mafunzo vifaa na watambuliwe vituo vyao.

Kuhusu mahusiano na nchi za nje, kwa kuwa Tanzania ni wananchi wa jamii mbalimbali za nchi za jirani kama mwanachama wa Afrika ya Mashariki, mwanachama wa nchi Kusini mwa Afrika, mwanachama wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na shughuli za wanawake. Sasa tunaomba wakati uwakilishi unapokwenda katika mikutano hiyo tunaomba maazimio yanayowekwa yaletwe Bungeni kwa taarifa ili tuweze kufuutilia. Kuna hatari ya baadhi ya maazimio yanayowekwa, hayatakekelezwa kama katika Mkutano wa mwaka 1997 na mkutano wa tarehe 15/12/2004 ambao ulishirikisha nchi za Malawi, Mozambique, Zambia na Tanzania iliweka maazimio kadhaa ikiwepo ujenzi wa *Mtware Corridor* ili kuendeleza ujirani na kwa mawasiliano ya nchi hizo, kufungua biashara katika ya nchi hizo na kuendeleza sekta ya kilimo, utalii na uchimbaji wa madini nchini Tanzania, Liganga chuma na makaa ya mawe ya Mchuchuma. Miradi kadhaa 16 iliaishwa katika programu ya *Mtware Corridor* lakini hadi leo hii hatusikii utekelezaji wake. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ijali masuala ya utekelezaji wa maazimio ya jamii zetu za nchi za nje, sisi kama wanachama kwa utekelezaji, vinginevyo mikutano inayoendeshwa nje ya nchi itakuwa haina maana kwa sababu ya kutotekeliza maasimio yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maendeleo ya jamii, jinsia na watoto, tunaishukuru sekta hii kwa kuweka kipaumbele jinsia ya wanawake kwa kutatua matatizo mbalimbali ya wanawake. Wanawake wanawenza, kwa hiyo, jitihada zinazofanywa na Serikali kwa kuwasaidia wanawake iendelee, ninasema tunaishukuru Serikali ya Tanzania kwa kukubali kwao vile vile kusaini mikataba kadhaa inayoondoa ubaguzi wa kijinsia vile vile na tunaishukuru Serikali kwa kutoa nafasi kadhaa katika uongozi wa ngazi za juu kwa kuwa na Mawaziri sita, Manaibu Waziri tisa, Wakuu wa Mikoa kadhaa, Wakuu wa Wilaya zaidi ya 22, Ma-RAS, DED, Wakurugenzi na kadhalika wanawake pia na kweli wanafanya vizuri na tunawapongeza sana. Wanawake waliobaki nyuma si kupenda tu bali ni kwa sababu ya mfumo wa kikoloni uliorithiwa kwa kutowapa wanawake elimu ya kutosha, wa kuwatenga wanawake kisiasa, kiuchumi na kijamii. Lakini kwa kusema kweli wanawake wana mchango mzuri sana katika nyanja zote kiuchumi, kisiasa na kijamii. Matatizo yetu sisi ni nyenzo za kufanya kazi kwa hiyo tupewe mikopo, nafasi zaidi za kazi, nafasi za Ubunge 50/50 na tuambiwe mapema njia gani itatumika ili tuiandae mwisho wa uchaguzi ndiyo mwanzo wa uchaguzi.

Mwisho ni kuhusu wazee na walemovu. Hapa nizungumzie afya za wazee na walemovu ziangaliwe hasa katika suala la UKIMWI nao wapewe elimu ya UKIMWI kwani wanasa hauliwa sana. Vile vile walemovu washiriki katika maamuzi mbalimbali hasa Ubunge kwa kuwapa nafasi. Nafasi walizonazo sasa ni za hisani kutoka nafasi za CCM kwa hiyo, sasa ni wakati muafaka wa walemovu kupewa nafasi zao za Ubunge kama kundi maalum. Walemovu wanahitaji watu wao wa kuwatetea katika huduma

mbalimbali za afya, elimu, mikopo, uchumi na masuala mazima ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja ya Waziri Mkuu. Ahsante sana.

MHE. DAMAS P. NAKEI: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa hotuba nzuri ambayo ni dira sahihi inayolenga kumjali mwananchi wa kawaida, suala la uwezeshaji likiwa limepewa umuhimu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika baadhi ya maeneo hususan katika kujitosheleza kwa chakula, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ulinzi na Usalama wa Raia, migogoro ya ardhi na viwanja.

Mheshimiwa Spika, kujitosheleza kwa chakula, suala la kuhifadhi chakula lisiachwe tu hivi katika dhana ya soko huria. Hali ilivyo ni kwamba wananchi wanatumia uhuru walionao katika kuiza chakula chote walichonacho na hatimaye kabla hatujafikia hata nusu ya mwaka wa fedha wanakuwa wameishiwa chakula na njaa inaanza kuwakabili. Kwa kuwa Serikali yetu isingependa kuona mtu anakufa njaa, huanza kuhangaika kwa bajeti ya dharura kusaka chakula.

Nashauri Serikali isisite kudhibiti mwenendo mzima wa soko huria ambapo hivi sasa zoezi la kuhamisha chakula linafanyika. Heri kinga kuliko tiba, pamoja na udhibiti wa kiutawala, *SGR* ifanye kazi yake pia ya kununua chakula cha akiba.

Mheshimiwa Spika, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, katika suala la uwakilishi wa maeneo ya uongozi kama vile Kata na Majimbo, ningeshauri Serikali kuangalia upya namna ya wakilishi hao Madiwani na Wabunge kuwa karibu zaidi na wananchi wanaowawakilisha, kuna haja ya kugawa majimbo na kata zilizo na maeneo mapana/makubwa. Katika jimbo la Babati Vijijini, Kata zifuatazo zinahitaji kugawanywa ambazo ni Bashanet, Madunga, Magugu, Dareda, Ufana, Dabil na Gidas.

Aidha, jimbo la Babati Vijijini ni kubwa mno kwa Mbunge mmoja kwani lina wakazi (wananchi) zaidi ya 240,000 kwa mujibu wa Sensa ya 2002. Naishauri Serikali kugawa jimbo hilo kuwa Babati Magharibi na Babati Mashariki. Kwa sasa jimbo hilo (Babati Vijijini) linapakana na Hanang, Kondoa, Mbulu, Karatu, Monduli na Simanjiro. Naomba sana Serikali iligawe jimbo hilo katika majimbo mawili.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 32 na 33 Waziri Mkuu ameitaka Halmashauri kupanga ratiba zao za vikao ili Waheshimiwa Wabunge waweze kushiriki vikao hivyo.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana na kumshukuru Waziri Mkuu kwa maelekezo hayo. Wakurugenzi wa Halmashauri, Madiwani na watendaji wengine ndani

ya Halmashauri wanapaswa kuheshimu nafasi ya Mbunge na ushauri na uelekezi wake kama daraja kati ya Serikali Kuu na Halmashauri au Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika aya ya 43 ukurasa wa 34 imeelezwa kuwa miradi mbalimbali inatekelezwa katika Halmashauri za Wilaya. Mojawapo ni ujenzi na/au ukarabati na matengenezo ya miundombinu. Kazi hizi mara nyingi zinatumia wakandarasi katika utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri nyingi zinaweka viwango vya chini vya *Bill of Quantities* wakati wa tenda na kwa sababu hakuna mkandarasi ambaye angependa kukosa kazi muda wote wakandarasi wengi nao wanafuata *rates* hizo za kupati kazi. Matokeo yake utekelezaji wa kazi kama ni barabara au majengo na kadhalika unakuwa wa viwango hafifu (*low quality*).

Mheshimiwa Spika, ajabu ni kwamba *rates* za mwaka 2004 zinakuwa kigezo cha kupatia kazi (ukandarasi) mwaka 2006. Halmashauri ziangalie suala zima la kuboresha mazingira ya kufanya kazi Wakandarasi wadogo, Wakandarasi wa ndani.

Mheshimiwa Spika, Ulinzi na Usalama wa Raia, kwa kuwa Wabunge kimsingi wako karibu sana na wananchi kwa namna mbalimbali, mawasiliano na kwa kuwa suala la ulinzi na usalama wa raia linahusu wananchi hao, naishauri Serikali katika ngazi za Wilaya iwafanye Wabunge wa Majimbo kuwa Wajumbe wa Kamati za Ulinzi za Wilaya. Matatizo mengi ya kiusalama yanatokea vijijini na Mbunge akiwa mwenyeji, ushauri wake kwenye Kamati utakuwa muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi pamoja na wananchi wengi kumfuata Mbunge wao kwa masuala hayo hayo ya kiusalama wa raia, Mbunge wao huyo anabaki pembezoni mwa viako muhimu vya ulinzi na usalama Wilayani. Naomba Serikali ipokee ushauri huu na kuufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu migogoro ya ardhi na viwanja, hivi karibuni Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, alitoa agizo kwa viongozi husika ili kumaliza utatuza wa matatizo ya viwanja na aliwapa mwezi mmoja kufanya kazi hiyo. Wengi wetu tulifurahi hasa mimi ambaye nin matatizo/migogoro mingi sana jimboni kwangu katika kata za Ufana, Arri, Kiru, Magara, Naiti na kadhalika. Lakini nilichoona baadaye ni kwamba wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya na Miji wanashughulikia migogoro inayohusu *double allocation* ya plots/viwanja tu.

Mheshimiwa Spika, naomba agizo la Mheshimiwa Rais lisaidie kutatua matatizo na migogoro sugu katika Jimbo langu la Babati Vijijini hususan katika kata nilizotaja hapo juu. Migogoro inayohusu mipaka ya maeneo ya ardhi, mashamba vijijini na viwanja ni kero sugu ambalo lingefanyiwa kazi kwa kuunganisha na agizo la Mheshimiwa Rais bado wananchi wanaambiwa waende kwenye mabaraza ya ardhi ya vijiji na kata ambayo hayapo katika Wilaya ya Babati. Baraza la ardhi la Wilaya ambalo lina hadhi ya

Mahakama ya Wilaya limekuwa na *impact* kufuutilia/kupeleka mashauri yao barazani. Watawala wameacha kabisa wajibu wao wa kiutawala hata kwenda kwenye *site* za migogoro kuamua au kushauri tu wahusika wa migogoro.

Mheshimiwa Spika, kama agizo la Mheshimiwa Rais lilimaanisha viwanja tu mijini, naiomba ofisi ya Waziri Mkuu isaidie kupanua wigo wa maeneo ya migogoro kutoka *double allocation* ya viwanja mijini hadi migogoro ya ardhi na mashamba katika ujumla wake vijijini. Wananchi watashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MOHAMED RAJABA SOUD: Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza napenda nikupongeze wewe mwenyewe kwa uwezo aliokupa *Allah* wa kuweza kuendesha Bunge letu hili kwa mafanikio yenyé kasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, pia sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuweza kuwasilisha hotuba yake mbele ya mpango wa matumizi katika Bunge hili ambao unaonyesha jinsi Serikali inavyowajali watu wake ambao wengi wao ni maskini na kwa kweli wananchi wengi wamezidi kuwa na imani na Serikali yao kwa kuona kasi mpya ilivyoanza kwa nguvu.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa uamuzi wake wa kutoa fedha 500,000,000/= kwa ajili ya maendeleo ya kila mkoa, hii ni hatua kubwa sana kwa Serikali ambayo ndio kwanza inaingia madarakani ni mategemeo ya wananchi wengi kuwa ikiwa mwanzo ni huu basi huko mbele tunakoendelea hali ya nchi hii itakuwa nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuthamini elimu na kuwatachia mema vijana wetu ili wapate elimu, Serikali imeamua maamuzi thabiti ya kuiongezea Wizara hiyo fedha za kuendeleza elimu katika nchi hii huo ni uamuzi wa busara na wenye kuonesha mwanga wa kutaka maendeleo.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali wa kuamua kuweka bayana kwa kiasi gani Serikali itapambana na vitendo vyote vya uvunjaji wa sheria hasa kuhakikisha ujambazi uliokithiri hapa nchini utatafutwa mpaka mizizi yake yote ipatikane kwani kupata mizizi ya wahusika kwa ujambazi ni ukombozi kwa Watanzania wote. Imekuwa nchi ya ajabu sana kwani ni nchi iliyogubikwa sana na vitendo vya uhalifu kiasi ambacho inatawalika mchana kwa nguvu zote, lakini inapofika usiku nchi hii huwa na vituko vya ajabu kiasi ambacho wananchi hawajiamini kufanya kazi au kusafiri kwa kuhofia kupigwa na kunyang'anywa mali zao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuthamini kazi nzuri iliyoanza katika awamu hii ya nne ambayo inaonesha mwelekeo wa kupata mafanikio katika vita hii ya kupambana na majambazi na kuwapa imani wananchi waone kwa kiasi gani Serikali yao inawajali na waweze kuwa huru ndani ya nchi yao na kuweza kuamua kuzalisha mali ikiwa usiku au mchana.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri sana ambayo iwapo sote tutaiunga mkono kwa vitendo na kuifanya itekelezeke basi Tanzania yetu itazaliwa upya.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuzifikiria barabara za kuunganisha tambarare na mlimani. Awamu ya nne ilipoingia madarakani tu kupitia Benki ya Afrika (*AMSDP*) ambayo inasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu imenipatia fedha za kutengeneza barabara toka Maore tambarare kwenda Vuje, Tarafa ya Gonja. Hatua hii imenipa matumaini makubwa kwamba Serikali sasa inaanza kuziona barabara za mlimani. Jimbo la Same Mashariki wakazi zaidi ya asilimia 60 wanaishi mlimani. Kati ya kata 14 ni kata zangu 4 ndizo ziko tambarare. Kata zangu 10 zote ziko mlimani.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa mlimani ni wachapakazi sana na ni watu ambao kati ya siku 6 za kufanya kazi wananchi hawa wanafanya kazi siku 4 tu mashambani mwao siku 2 zote ni za kazi za kutengeneza barabara zao. Kazi za kutengeneza barabara mlimani ni ngumu sana kwani barabara hizo ili zipitike ni lazima kuvunja miamba.

Mheshimiwa Spika, wananchi wangu wa mlimani ni wapenda maendeleo sana. Maisha yao ni ya kazi tu. Hakuna kupumzika, upande wa barabara kuna wanayoyaweza lakini kuna mengine lazima upite mkono wa Serikali (*State role*) miamba mengine hawana uwezo nayo kwa hivyo wanakuomba, niombe Serikali kwa kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu iniboreshee barabara zangu za Wilaya ya Same Milimani kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ipo barabara ya Mamba Myamba hadi Hedaru yenye urefu wa kilometra 45 isimamiwe kikamilifu na *TANROAD* kwani kinachohitajika hapa ni kuipanua barabara hii kama ambavyo Ofisi ya Waziri Mkuu inapanua barabara ya Maore na kuweka changarawe iwapo Serikali itaboresha barabara hii itakamilisha mzunguko (*Network*) wa barabara za mlimani katika Wilaya yetu.

Mheshimiwa Spika, niombe tena Serikali itupie macho na kunyoosha mkono kuiona barabara ya Mwembe - Mbaga - Myamba hadi Hedaru.

Mheshimiwa Spika, katika milima hii kuna hekta 2040 zinazolimika miezi yote 12. Wananchi wa mlimani wanalima mazao muhimu sana na ya nadra. Kata zangu zote za mlimani wanalima Tangawizi yenye ubora wa hali ya juu. Iliki inapatikana kwa wingi sana mlimani, kahawa, ndizi, kwa wingi mno, viazi mbatata kwa wingi mno, tena vya aina pekee na aina zote za matunda.

Mheshimiwa Spika, mazao ya mlimani Same ni mengi mno na ziada ni kubwa mno lakini wananchi hawana uwezo wa kusafirisha mazao yote haya kwa vichwa vyao. Wananchi wa mlimani wanatembea mno kwa miguu kupeleka mazao yao sokoni

tambarare uwezo wao wa kubeba mazao yao ya ziada kwa vichwa ni mgumu sana. Niombi Serikali kuu itupie macho sana barabara za milimani.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kumuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa makusudi kabisa afanye ziara Same Mashariki Milimani kwani tangu tupate Uhuru hakuna Waziri Mkuu wala Rais aliyewahi kufika Same Mashariki milimani kuchochea maendelo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri Mkuu.

MHE. OMAR S. KWAANGW': Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri Mkuu pamoja na malengo ya ofisi yake.

Maeneo ya mchango wangu ni kwanza kujitosheleza kwa chakula. Kwa fundisho la njaa na ukame tuliuopata, hifadhi ya chakula ngazi ya kaya na familia ndio suluhu. Kila kaya iwe na kihenge/ghala au stoo na jambo hili litungiwe sheria ndogo na zisimamiwe kikamilifu. Pia hifadhi ya chakula ya Taifa inunue sasa nafaka.

Pili, fedha shilingi milioni 500, fedha zigawanywe moja kwa moja kwa kila Halmashauri na Halmashauri nazo zihuushwe kata zake. Ni kwa njia hii tu Waheshimiwa Madiwani na Wabunge wanaweza kufuatilia matumizi ya fedha hizi kwa waliokopa. Fedha hizi zikipitia mikroani hazitagawanywa sawa sawa na zitakwenda kwa vikundi vichache tu na pengine kwa upendeleo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuhusu maslahi ya watumishi hasa walimu, ipo mianya mingi sana inayofanywa na watendaji wa Halmashauri katika kulimbikiza madai ya walimu/watumishi, Serikali Kuu ikomeshe mianya ya matumizi yasiyolenga wahusika. Mianya ya malimbikizo ya madai ya walimu itafufua sana ari ya walimu na hivyo kupata elimu bora.

Mheshimiwa Spika, nne ni kuhusu *MMEM/MMES*. Bado kuna matatizo ya uwajibikaji ambao sasa unaleta majengo yasiyo imara. Ni muhimu kuangalia utaratibu mzuri zaidi wa usimamizi wa viwango na matumizi ya fedha. Kwa *MMES* ni tatizo zaidi kwani Kamati za ujenzi zilizoanza kazi ya kuanza ya ujenzi wa majengo ya sekondari zinawekwa pembeni mara tu fedha za *MMES* zinazotolewa. Upungufu huu unaondoa wawakilishi wa wananchi na unaweka fedha kwenye mikono ya wachache tena wateule wa Serilai yaani Bodi za Shule.

Tano ni kuhusu watendaji wa Halmashauri za Mji/Wilaya na kadhalika. Mabadiliko ya msingi yafanyike sasa. Wapo ambao wapo tu na wamejichokea tu. Hawataweza kasi ya sasa. Wengine wabadilishiwe mazingira ili waone pia tofauti ya wakati wa sasa. Serikali sikilizeni sana ushauri wa Wabunge. Wajibu wa Wakurugenzi uangaliwe upya kwa vile kwa sasa kazi yao kubwa ni mikutano na semina na safari, hawakai ofisini na Serikali ndio imewafanya wasikae ofisini kusikiliza matatizo ya wananchi na kuratibu kazi za Halmashauri. Pia Serikali iondoe utaratibu wa watumishi wa Halmashauri hasa wa idara ya fedha kwenda Dar es Salaam kila mwezi kufuatia

Warrant of Fund's na mengine. Jambo hili linaongeza sana matumzi ya Halmashauri na kupunguza shughuli za maendeleo.

Mwisho, Halmashauri mpya ziingizwe mara moja katika vitabu vyote vyta Serikali na wapewe migao yao ya fedha na pale ambapo fedha zimewekewa kwenye Halmashauri iliyokuwepo mgawanyo ufanyike haraka ili Halmashauri husika ndio ipange shughuli zake. Hili limejitokeza Babati kwenye migao ya *MMEM* na afya, lirekebishwe haraka. Natanguliza shukrani zangu na naunga tena mkono hoja na kumtakia kila la kheri Waziri Mkuu na wote.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, maelekezo haya yanahusiana na ruzuku ya vyama vyta siasa kama ilivoainishwa na mafungu yaliyo chini ya Wizara yako hasa fungu la msajili wa vyama vyta siasa, kasma namba 27, kasma ndogo 280700.

Mheshimiwa Spika, kiutaratibu kama ilivyoainishwa na sheria ya vyama vyta siasa, sheria namba 5 ya mwaka 1992 (*The Political Parties Act, Act no. 5 of 1992*) kama ilivyofanyiwa marekebisho na sheria namba 18 ya mwaka 1995 na kifungu cha 2 jedwali 11 cha mwaka 1996.

Sheria husika, kifungu 16(1) na 16(2) imezungumzia ruzuku za aina mbili ambazo Serikali inatakiwa kuzitoa kwa vyama vyta siasa, ruzuku iliyotengwa maalum kwenda kwa ofisi ya msajili wa vyama vyta siasa ambayo kwa mujibu wa kifungu 16(1) inatakiwa isizidi asilimia 2 ya bajeti yote. Fedha hii inagawiwa kwa kuzingatia matakwa ya kifungu namba 17(1) na (2) na ruzuku itakayotolewa na Serikali kama itakavyoamuliwa na Waziri anayehusika na usimamizi wa ofisi ya usajili (ambayo hapa ni ofisi ya Waziri Mkuu).

Mheshimiwa Spika, licha ya matakwa tajwa hapo juu ya kisheria kasma ya msajili wa vyama vyta siasa kasma namba 27, kasma ndogo 280700 fedha zilizotengwa kwa ajili ya vyama vyta siasa ni fedha ambazo zimebainishwa na kifungu 16(1) tu, ambazo ni shilingi 13,677,100,000. Hakuna kasma yoyote katika ofisi ya Waziri Mkuu inayoelekezea mgawo wa ruzuku kwa vyama vyta siasa kama ilivyoainishwa na kifungu 16(2).

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia utata huo uliojitokeza, tunaomba katika mawasilisho ya hotuba yako utueleze utupe ufanuzi kwa nini kasma husika (ambayo lazima iwepo kwa mujibu wa sheria) haipo? Ni matarajio yetu kuwa fedha iliyotengwa katika fungu 16(1) haitatumika kufanikisha malengo ya fungu 16(2) kwani kisheria ni mafungu mawili tofauti. Nawasilisha.

MHE. AMINA C. MPAKANJIA: Mheshimiwa Spika, nakuomba sana tena unisaide katika hili vijana na wanawake wanaofanya biashara zao katika soko la Kariakoo, wanalamika sana na wanaskitishwa sana na kitendo cha wafanyabiashara wa Kichina kutoka China ambao wamekuja kufanya biashara zao tena za reja reja hapa nchini. Vijana na wanawake yaani wafanyabiashara wa Kariakoo wanalamika kwa sababu wanaenda China kununua bidhaa, wanalipa nauli ya kwenda na kurudi China dola

1,000/= wanalipia malazi na chakula nchini China, wanunua bidhaa shilingi 2,000/= wakitegemea kuja kuuza nchini kwa bei ya shilingi 4,000/= au shilingi 5,000/= baada ya kutoa garama zao walizozitumia China.

Lakini cha kushangaza Wachina hao hao wanakuja hapa nchini kuuza bidhaa hizo hizo ambazo wanazinunua China Watanzania, wao Wachina wanakuja kuziuza hapa kwa bei ile ile wanayouzia China. Ina maana Wachina hawa hawalipi kodi yaani ushuru? Hawa Wachina ni kwa faida ya nani? Nani amewapa kibali cha kufanya biashara Kariakoo? Hivi kweli Watanzania wanaweza kwenda China na kuanza kufanya biashara za reja reja China? Tumeahidi ajira zaidi ya milioni moja kwa vijana wetu, zitapatikana kweli?

Kama Wachina ndio wameanza kuchukua ajira za vijana wetu? Sina ugomvi na wachina najua wametusaidia sana kwenye shughuli mbalimbali za kimaendeleo, nchini mwetu ukiwemo uwanja wa siasa (uwanja wa Taifa) wametujengea Bunge letu yaani wamesaidia kwenye ujenzi. Kwa hilo nawashukuru sana. Na ninawaomba waje nchini mwetu wajenge viwanda ili Watanzania wapate ajira lakini wasifanye biashara za reja reja, watuachie wazawa.

Mheshimiwa Spika, Wachina wamepiga hatua kubwa sana kimaendeleo kutushinda sisi, leo wao kuja hapa nchini mwetu kufanya biashara ndogo ndogo ni kutuonea na kuwanyanya wananchi wazalendo. Nawaomba waje nchini kwetu kwa miradi mikubwa mikubwa, hii midogo wawaachie wazawa, ukizingatia wamekopa mikopo wanahitaji kuirudisha kwenye mabenki na wameamua kujajiri wenyewe (MKUKUTA). Watanzania wanaenda China na kuleta bidhaa hapa nchini hiyo inatosha sana, inaonyesha ni jinsi gani tunawajali na tunashirikiana nao ndio maana tunakwenda kwao kuwaunga mkono.

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo la muhimu sana na nimetumwa na wafanyabishara wa Kariakoo wakiwemo vijana na wanawake. Mimi kama mwakilishi wao nakuomba uwasaide na ninaomba ufanuzi wa suala hili wakati utakapokuwa unajibu hoja za wachangiaji. Chonde chonde Mheshimiwa Waziri Mkuu, jambo hili ni muhimu sana na linahitaji ufanuzi wako ili wananchi wasikie na wajue Serikali yao inasemaje. Tukumbuke walitupigia kura na tuliahidi kuwapa ajira.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii mia kwa mia, ahsante sana.

MHE. SALIM YUSSUF MOHAMED: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kutoa mchango wangu huu mfupi kwa maandishi kutokana na hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Pili nakupongeza wewe Mheshimiwa Spika, pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika, wako kwa kushika nyadhifa hizo. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kupata nafasi hiyo na kuipongeza hotuba yake yenye mwelekeo wa kuleta maendeleo kwa Watanzania. Mwenyezi Mungu na azidi kumtia imani ili azma yake njema ifanikiwe. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kwa MKUKUTA. Katika kitabu cha hotuba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ukurasa wa tano ameeleza kuwa wastani wa pato la kila mtu ni shilingi 360,865, mwaka 2005. Kwa mahesabu ya haraka haraka ni kiasi cha shilingi 1,000/= kwa siku. Hii ni hali mbaya sana na tunategemea juhudu kubwa sana zitachukuliwa na watendaji wakiongoza na yeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kuona kwamba kwa kiasi kikubwa hali iliyo inabadilika.

Lakini hapo hapo kwenye ukurasa wa kumi wa bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, sentensi ya mwisho inasema: "Asiyeweza kucheza ngoma hiyo kwa midundo inayopigwa na Serikali itabidi atupishe." Hii ni kauli nzito sana, mimi nisingefikiria licha ya kuandika bali hata kuzungumza tu isingekuwa busara, ingeonekana katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mazoea ya ubadhirifu wa fedha za Serikali na kutojali utendaji wa kazi na hii hofu yangu kwamba bado hiyo itaendelea, hivyo kuikatisha mara moja ni vigumu sana na hakuna utamaduni wa kuwajibika. Sasa kauli hiyo nzito labda itakuwa vigumu kuitekeleza. Mwenyezi Mungu akusaidie Mheshimiwa Waziri Mkuu ili MKUKUTA usiendelee kuwa MKUKUBI (Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Binafsi).

Mheshimiwa Spika, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, kwa kuanzisha tena mazungumzo kati ya Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri Mkuu na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Waziri Kiongozi. Nazidi kumtanabaisha Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba kuna mpasuko Visiwani Zanzibar. Nadhani sambamba na juhudu hizo za kutatua kero za Muungano, mpasuko huu ungepewa umuhimu wa pekee ili kuepusha tofauti ndogo ndogo hapo baadae ambazo labda zinaweza zikatokezea.

Mheshimiwa Spika, UKIMWI ni janga kubwa linalotukabili nchini na kila siku waathirika wanaongezeka. Tume ya Kudhibiti UKIMWI pamoja na *NGOs* nyingi kwa maoni yangu ni vitega uchumi. Nia ya kukabiliana na janga la UKIMWI ni ndogo. Kwa mfano Tume ya Kudhibiti UKIMWI hadi Aprili 2006 (Miezi 10) wametumia 59% ya bajeti yao na hadi Mei 2006 wametumia 65% ya bajeti (mwezi mmoja 6%). Wamesema katika maelezo yao kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuwa hadi Juni 30 (mwezi mmoja tu) watamaliza 35% zilizobaki. Sasa hata kuwe na maelekezo gani kwa mwezi mmoja kutumia 35% ya bajeti hasa ikizingatiwa kuwa ni mwezi wa mwisho wa bajeti ni ubabaishaji mkubwa. Tunaiomba Serikali kuitia Wizara inayohusika kufuatilia kwa karibu sana utekelezaji wa mikakati ya kupambana na janga hili. Vinginevyo fedha zitaendelea kupotea na UKIMWI utaongezeka. Tuzidi kumwomba Mwenyezi Mungu atuondolee janga hili. Nashukuru, ahsante sana.

MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuteuliwa kwake na Rais kuwa Waziri Mkuu. Mimi Profesa Sarungi namfahamu Mheshimiwa Waziri Mkuu, tangu mwaka 1990 tulipoteuliwa na Rais wa Awamu ya Tatu katika Baraza la Mawaziri.

Uchapaji wake wa kazi, uzalendo na uadilifu wake ni mifano ya kuigwa. Nampongeza kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongozi hizo napenda kuchangia eneo ambalo limekuwa kero kwa wananchi wa Jimbo la Rarya kwa muda mrefu nalo ni Jimbo la Rarya kupandishwa daraja kuwa Wilaya. Historia kabla ya Uhuru wa nchi yetu Mkoa wa Mara uligawanywa kuwa Wilaya mbili, Wilaya ya *South Mara* na Wilaya ya *North Mara*. Baada ya Uhuru Wilaya ya *South Mara*, iligawanywa katika Wilaya ya Bunda, Serengeti, Musoma na Jimbo la Musoma Vijijini. Wilaya ya *North Mara*, ilibaki kuwa Wilaya ya Tarime na baadaye Jimbo la Rarya.

Mheshimiwa Spika, ombi maalum kwa Jimbo la Rarya lina sifa zote za kuwa Wilaya. Idadi ya watu ni zaidi 200,000. Kulingana na takwimu ya mwaka 2004 idadi hiyo imefika watu 250,000. Utawala, Jimbo la Rarya lina Tarafa 4 kata 21, vijiji 98 na vitongoji zaidi ya 40 ambavyo vitapandishwa hadi kuwa vijiji. Jimbo la Rarya lina ukubwa wa kilometra 9,472 za mraba.

Kwa upande wa elimu, shule za msingi ni 110, shule za sekondari ziko 15 na katika mwaka ujao 2007 shule za sekondari 5 zitafunguliwa hivyo kufanya shule za sekondari kuwa 20. Uchumi wa Jimbo la Rarya ni imara kutokana na uvuvi, ufugaji, kilimo na biashara. Vikao vya Halmashauri Wilaya na RCC Mkoa vilipitisha mapendekezo yaliletwa Wizarani.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, katika kampeni yake alipofika Jimbo la Rarya, katika Mkutano wa hadhara aliwaauliza wananchi kuhusu kero yao kubwa. Wananchi walijibu kuwa kero yao ni moja tu, Jimbo la Rarya kupewa hadhi ya kuwa Wilaya. Mheshimiwa Rais, aliwajibu kuwa kazi yake ya kwanza atakayofanya akiingia Ikulu ni kutangaza Jimbo la Rarya kuwa Wilaya. Pamoja na upinzani uliokuwepo Wilaya ya Tarime, wananchi wa Jimbo la Rarya, walimpa kura asilimia 76 wananchi wamenikaba koo. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu niokoe, naomba unipe tu ahadi ili niweze kuwatuliza wananchi.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, kutujalia sote Waheshimiwa Wabunge, kuwa wazima. Napenda kumshukuru mtoa hoja hii Mheshimiwa Edward Lowassa.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru wananchi wote wa Jimbo langu la Mtambile kwa kunichagua kwa kura nyingi na ninawaahidi sitowaangusha.

Napenda nianze mchango wangu na suala zima la lengo la Kitaifa la UKIMWI, ambapo umekuwa ukiendelea kuua maelfu ya Watanzania, huku maambukizo yakiongozeka mbali na jitihada za Serikali na wafadhili kutoa elimu na fedha kupambana na janga hilo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali mambo yafuatayo, fedha zinazotolewa na wafadhili za kupambana na UKIMWI washirikishwe kikamilifu viongozi wa dini yaani

Mashehe, Maaskofu au Mapadri ili kujaza imani ndani ya watu walio na imani tofauti bali dini zote zinapiga vita zinaa.

Mheshimiwa Spika, pia naipongeza Serikali kwa jinsi inavyoendelea na huduma za utoaji wa dawa za kurefusha maisha ila naiomba Serikali kuwe na angalizo lifuatalo ambalo ni muhimu sana, kwa nini ni kwa jinsi gani Serikali inawadhibiti waathirika wanaotumia dawa za kurefusha maisha wasiweze kuwaambukiza wengine na je, kuna utafiti wowote umefanyiwa juu ya ongezeko la maambukizo ya virusi vyta ukimwi hautokani na waathirika hao?

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuwezesha utaratibu wa kutoa vitambulisho vyta uraia, ila naishauri Serikali kuangalia yafuatayo, kuwatambua wageni wote hasa sehemu za mipakani ili kuepuka udanganyifu wa kutoa haki isiyostahiki.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa mkakati wa kudhibiti uharibifu wa mazingira kama inavyojulikana kwamba miti inakatwa ovyo, misitu inachomwa moto na hatimaye vyanzo vyta maji vinaathirika. Lakini cha kushangaza uharibifu unafanywa huku watendaji wa vijiji wanashuhudia, watendaji wa kata wanajua na kushuhudia na hata wale wa Tarafa. Sasa ushauri wangu mbali na kuwadhibiti wahusika lakini Serikali ni vema iwe na mkakati wa kuwaadhibu watendaji wote niliowataja watakaoshindwa kudhibiti mazingira katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara ya Usalama wa Raia (polisi) kwa kudhibiti ujambazi ila ninaishauri Serikali kutotoa kabisa mikakati yake hadharani ya kupambana na ujambazi, mikakati iwe siri kwa lengo la kukamilisha kazi.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi linakabiliwa na matatizo mengi ila ninaiomba Serikali kulikarabati jengo la Polisi la la Makao Makuu Kusini Pemba, ambalo linavuja na hilo ninaiomba Serikali kuangalia upya maslahi ya Askari wa Jeshi la Polisi na pia ninaiomba Serikali kuongeza posho za chakula (*ration allowance*) toka shilingi 50,000 angalau kufikia 100,000/=.

Mheshimiwa Spika, suala la ajira binafsi katika sehemu mbalimbali zimechukua nafasi ya kukabiliana na tatizo la ajira nchini. Ila kwa masikitiko makubwa wafanyakazi hao katika sehemu mbalimbali mfano nyumba za wageni, mahotelini, kwenye mabaa wanalipwa fedha zisizolingana na kazi zao ambapo hufanya kazi mpaka saa 4.00 au 5.00 za usiku. Hivyo naishauri Serikali kuandaa sheria maalum ya wamiliki wa sehemu hizo kutoa haki inavyostahili kwa wafanyakazi hao.

Mheshimiwa Spika, katika baadhi ya migahawa baadhi ya wamiliki wanabadilisha wafanyakazi kwa muda usiozidi miezi miwili kwa sababu tu ya kudai haki ndogo ndogo zinazowahu wafanyakazi hao maskini, ni vyema Serikali ikaangalia kero hii kwa undani kwa kulipatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. DR. ALI TARAB ALI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nataka kuchangia kuhusu Daftari la Kudumu la Wapigakura. Daftari hili lilianzishwa ili

kuwawezesha wananchi wote nchini kutekeleza haki yao ya msingi ya kuchagua viongozi wawatakao. Daftari hili pia linazuia upigaji kura mara mbili kwa wakorofî wanaotaka kuharibu juhudhi ya kujenga demokrasia ya kweli nchini. Ingawaje, inasikitisha kuona ya kuwa wapiga kura wengi hususan kwa upande Zanzibar wameshindwa kutekeleza haki yao hii ya kupiga kura kwa ukosefu wa taratibu nzuri ambazo ziliwekwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, hivyo ni vema ikiwa daftari la kupiga kura kuchagua Serikali ya Jamhuri ya Muungano liwe tofauti na lile la Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nataka kuchangia ni kuhusu utawala bora. Nchi yetu hii inaendeshwa kwa misingi ya Katiba na Sheria. Hivyo tusingelitazamia wananchi kunyanyaswa na kuonewa na vyombo vyta dola bila ya sababu.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa ni miezi nane tangu umalizike uchaguzi wa Oktoba, 2005 wa Zanzibar. Katika kipindi hiki tungetazamia ya kuwa kesi zote zinazohusiana na uchaguzi huo zingekuwa tayari zimeshasikilizwa na uamuvi kutolewa. Waliokosa wakaadhibiwa na wasio na makaso wakaachiwa. Kuchelewesha kutoa hukumu kunawafanya wananchi wafikirie ya kuwa kuna mkono wa wakubwa ambaa unaingilia maamuzi ya mahakama. *Justice delayed is justice denied.*

Mheshimiwa Spika, hivyo ni vizuri kesi hizi zikaisha haraka ili wahusika watakaonekana hawana hatia wakaendelea katika shughuli za ujenzi wa Taifa bila ya usumbufu.

MHE. HASSAN C. KIGWALILO: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa asilimia mia moja, pia nawapongeza watalaa kwa kuandaa hotuba hiyo nzuri na kamilifu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri Mkuu, kwa ufuatiliaji wa hali ya juu ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na pia kwa ufuatiliaji wa haraka yanapotokea majanga mbalimbali ya Kitaifa kama njaa na ajali kama ile iliyotokea Mererani mapema mwezi huu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikwenda haraka kwenye tukio na kuwafariji ndugu wa marehemu katika ajali ya basi iliyopoteza maisha ya wananchi zaidi ya ishirini na majeruhi kadhaa. Kitendo hiki kilichofanywa na Waziri Mkuu mara tu baada ya tukio kimepokelewa kwa imani kubwa na wananchi. Ninaomba kasi hiyo iendelee.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kupeleka kila Mkoa shilingi milioni 500 kwa ajili ya uwezeshaji. Nashauri Serikali ifuatilie kwa karibu kuona kila Wilaya inapata mgao wake ipasavyo na yatolewe wazi maelezo ya namna fedha hizo zitakavyotumika kwa manufaa ya wananchi wa Wilaya husika. Ninaamini kwamba ikitekelezwa vizuri huu utakuwa mwanzo mzuri wa safari yetu ndefu ya awamu ya nne kufikia hatua ya maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, Liwale ni mojawapo ya Wilaya yenye elimu duni, ili kujikwamua wananchi wamehamasika kwa kujenga shule tano mpya za sekondari. Ni

Wilaya ya kwanza katika Mkoa wa Lindi kwa kujenga sekondari nyingi za kata. Hivi sasa ina jumla ya sekondari sita ikiwemo sekondari ya awali ya Liwale yenye *Form I* mpaka *Form IV* yenye mikondo minne. Vijana wote waliofuzu darasa la saba katika Wilaya ya Liwale, wameingia *Form I* katika shule hizo za kata. Nafasi za ziada zimejazwa na wanafunzi kutoka Wilaya jirani za Kilwa, Ruangwa, Nachingwea na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa katika sekondari hizi ni upungufu wa walimu, hakuna hosteli kwa wanafunzi wanaotoka nje ya Wilaya na hakuna nyumba za walimu hata huduma za afya, maji salama kwa baadhi ya sekondari hizo. Naishauri Serikali ifuutilie kwa karibu sana shule hizi ili ziboreshwé kwa kushirikiana na wananchi. Vinginevyo shule hizi za kata hazitafanikisha malengo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, hali ya Madiwani ni duni sana wanategemea posho la Halmashauri. Baadhi ya Halmashauri kama Liwale haina uwezo, haina vyanzo vizuri vya fedha. Hakuna viwanda/makampuni au bandari na kadhalika kama vile ilivyo katika Halmashauri za Mijini kama Dar es Salaam. Liwale inategemea ushuru wa Korosho na ufuta ambaao pia inategemea soko na hali ya hewa hivyo Halmashauri hii haina kipato maalum cha uhakika. Hivyo naomba Serikali ichukue hatua za kuzichangia kipato ili kuinua hali ya Madiwani.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ifuutilie kwa karibu malalamiko yanayohusu baadhi ya watendaji katika Halmashauri zetu. Si vizuri kupuuza malalamiko hayo na wala siyo vizuri kuzilaumu Halmashauri au vikao vya Madiwani vinapotoa uamuzi wa kumsimamisha mtendaji yoyote. Wao wapo karibu sana na mtendaji huyo na wamemvumilia kwa kipindi kirefu kabla ya kufikia uamuzi huo. Hata kama hatua zilizochukuliwa hazikufuatwa vizuri lakini ni ushahidi tosha kwamba kuna mgogoro dhidi ya mtendaji huyo awe daktari mwenye sifa au mtumishi yeoyote mwengine. Baadhi ya hao wanaolalamikiwa wameshafanyakazi katika maeneo hayo kwa muda mrefu, zaidi ya miaka mitano. Inatosha kabisa muda aliokaa sio lazima aendelee kufanya kazi katika mazingira ya chuki. Mbona Wabunge tunaomba ridhaa kwa wananchi kila baada ya miaka mitano iweje mtumishi awe katika kituo kimoja kwa zaidi ya miaka mitano?

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimia Waziri Mkuu, kwa bajeti nzuri inayogusa maeneo yote ya wananchi kwa niaba ya wananchi wa Busanda. Napenda nikushukuru sana tena sana kwa kuipatia Wilaya ya Geita chakula cha njaa. Tunashukuru sana kwa kuingilia kati tatizo la ujenzi wa barabara ya Usagara -Geita - Kyamnyolwa. Tunashukuru kwa hekima na busara uliyotumia kutatua suala hilo kwani tulianza kujisikia wanyonge haki na tuna imani na utendaji wako.

Mheshimiwa Spika, maombi, tunaomba vituo vya afya viongezwe kwani idadi ya watu ni kubwa kulinganisha na vituo vilivyopo. Pia naomba wafugaji nao wapewe heshima yao. Suala la kuwaita wavamizi ni kuwanyanyasa na kutowatendea haki katika nchi yao. Pia wao wanauliza je, Wapemba ambaao wamekuja kulima na kufanya biashara Shinyanga si wavamizi? Wachaga waliotapakaa maeneo yote ya nchi wakilima na

kufanya biashara siyo wavamizi? Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba sana mliweke vizuri hili ili dhana potofu iliyopo kwa wafugaji ibadilike. Kwa kweli wanahitaji elimu na si kuwafukuza au kuuza mifugo yao. Ni kweli kwamba wana matatizo, lakini wamekuwa wakikimbia kuachia nafasi maeneo yao ya kuchungia kwa wahamiaji wakulima.

Kuhusu suala la wafugaji naomba sana hekima na busara ya Serikali iliangularie upya. Maeneo mengine wamefukuzwa na wengine kunyang'anywa mali zao kwa mfano Wilaya za Mkoa wa Kagera. Watendaji wametumia mwanya huo kuuza mifugo ya wafugaji kwa kisingizio kuwa ni wakimbizi. Ikiwezekana tume iundwe kuangalia utekelezaji wa zoezi hilo katika Mkoa wa Kagera, ulivyoendeshwa wafugaji wengi wanalia.

MHE. DORAH H. MUSHI: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii mbele ya Bunge lako Tukufu na kuchangia hoja. Kwa heshima na taadhima nimpongeze sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana kukiongoza Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, aidha, nimpongeze sana Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kuwasilisha hotuba nzuri kwenye Bunge lako pamoja na Baraza lake lililoendana na falsafa ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

Mheshimiwa Spika, nachangia kwa kuanza na suala la kilimo. Kilimo ndio mwajiri mkubwa wa Watanzania. Pamoja na malengo mazuri kukuza Pato la Taifa ambalo kwa kiasi kikubwa huchangiwa na sekta ya kilimo. Nina wasiwasni sana kutokana na janga la ukame linaloendelea kukua mwaka hadi mwaka kwa kikwango kikubwa na kilimo chetu kimekuwa kikitegemea mvua. Kama tunataka kukuza sekta hii ni vema mpango kabambe wa kilimo cha umwagiliaji uandaliwe sasa, sambamba na upatikanaji wa pembejo na huduma za ugani (*extension services*).

Mheshimiwa Spika, aidha, kuwepo na mpango wa kuendeleza viwanda vidogo vidogo na vikubwa na hili litawezekana ikiwa Serikali, itakuwa tayari kuanzisha benki za maendeleo ambazo zitakuwa na viwango vya riba nafuu ili kuwawezesha wakulima, wafanyabiashara ndogo ndogo na wachimbaji wadogo wadogo wa madini kuweza kukopa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara ndogo ndogo Tanzania (MKURABITA). Aidha, mpango huu ni mzuri lakini unakwenda taratibu sana, huu ungewawezesha wanawake wengi zaidi kutumia mali zilizorasimishwa kama dhamana ya mkopo kutoka benki mbalimbali. Pia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, utumike kuziimarisha *SACCOS* na *SACCAS* na hatimaye kuwawezesha kuundwa kwa Benki Kata. Ili kuboresha jitihada zilizopo za kuwawezesha wanawake wajasiriamali kupata masoko ya ndani na nje. Pia Serikali iwawezeshe wanawake kushiriki katika maonyesho ya Kimataifa ili kupanua wigo wa masoko ya bidhaa zao.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Simanjiro, Mkoa wa Manyara, hauna huduma ya benki kuna wafugaji, wakulima wakubwa, wachimbaji wadogo wadogo, makampuni

makubwa ya wachimbaji, vikundi nya akinamama nya kuweka na kukopa *SACCOS* na kadhalika, lakini yeote anapohitaji huduma inabidi aifuate Mkoa wa Arusha.

Mheshimiwa Spika, naomba nzungumzie suala la Mererani. Mji huu wenye sifa nyingi mbali na kwamba ni Mji pekee unaochimbwa madini ya *Tanzanite* duniani. Pia ni mji mpya uliojengwa kihisia na tangu Mererani ipate baraka ya kuwa Mji mdogo nashindwa kuelewa ni nini kinachochelewsha utaratibu wa sheria za mji kufanyika, ingekuwa vema basi kuandaliwe mipango thabiti na miundombinu mizuri kwa kuwa huu ndio Mji wa Watanzania amba haukuachwa na Mkoloni.

Mheshimiwa Spika, ajira mbaya ya watoto. Naipongeza sana Serikali kwa kubuni mbinu mbalimbali za kuweza kuwaondolea watoto walioko katika mazingira magumu na kuwapatia mbadala kama elimu ya msingi kwa waliokaa *MEMKWA* na stadi za kazi *VETA*. Aidha, naipongeza Serikali pia kwa kuanzisha mpango wa *MMES* mpango huu unaendelea vizuri na utekelezaji wake na pia mafanikio yameanza kuonekana. Lakini bado nasisitiza Serikali iangalie jinsi ya kuwaendeleza watoto wanaomaliza elimu ya msingi amba hawakuchaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari kabla hawajaingia katika mazingira magumu kwa kufanya hivyo ninaamini kwamba tatizo hili linaweza kupungua kabisa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004 Serikali kwa kushirikiana na taasisi ya *Good Hope Programme* katika Wilaya ya Simanjiro ilifanikiwa kuwaondoa watoto 370 katika mazingira magumu na kuwapatia stadi za kazi kwa kushirikiana na *VETA*. Baada ya watoto hawa kumaliza tulitegemea kwamba wangepatiwa mitaji kwa sababu tayari walikwishaunda vikundi ili waweze kujiajiri. Hadi sasa hakuna kinachoendelea. Ikiwa wataachwa hivi hivi ni kama hawajasaidiwa na kama kuna mpango uliyoandalila kwa ajili yao ni vema uharakishwe. Naomba jamani suala hili liangaliwe kwa makini.

Mheshimiwa Spika, watoto hawa wapewe vitendea kazi au mitaji ili waweze kujiendeleza, wasirudi tena kwenye mazingira waliyokuwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kueleza kuhusu watoto wa kike wanaopata mimba shulen i wakiwa na umri mdogo. Watoto wa kike wanaopata mimba wakiwa bado hawajamaliza elimu ya msingi au wale walioko sekondari. Naomba Serikali iwasaidie watoto hao ili kwamba wanapomaliza kujifungua, warudi shulen wajiunge na wenzao kwa sababu wanapopata mimba hujikuta wamekata tamaa ya maisha kwa kuona kwamba hawana maana wala kujiendeleza hawawezi. Kipato hawana na yule mtoto anayezaliwa utakuta hana jinsi ya kumtunza wala kumsomesha ndipo utakuta wote wanaingia kwenye mazingira magumu, mtoto chokoraa na mama chokoraa, naomba Serikali iangalie tatizo hili la wasichana kupata mimba wakiwa shulen na kuweza kusaidia ili kukomesha ajira mbaya kwa watoto.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kupeleka fedha nyingi katika ngazi ya Serikali za Mitaa, mpango huu ni mzuri sana lakini kuna wasiwasi mkubwa juu ya matumizi ya fedha hizo kwa sababu Halmashauri nyingi hazina uwezo wa kumudu kusimamia fedha hizo, uwezo wa kiutawala na kihasibu bado ni mdogo kwa hiyo fedha

zinazopelekwa kwenye Halmashauri kuna uwezekano mkubwa wa kutumika vibaya na hivyo kushindwa kutimiza malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ifanye maandalizi ya kutosha katika maeneo ya watumishi wa Halmashauri, wapate vitendea kazi na elimu ya mipango yenye.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na naomba kuwasilisha.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri na makini sana. Kwa hakika Serikali ya awamu ya nne imejipanga kweli kweli maana ukianzia hotuba ya Mheshimiwa Rais alipokuwa akilifungua Bunge hili, halafu hotuba za Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, hotuba ya Waziri wa Fedha na sasa hii ya Waziri Mkuu, zote zinaonesha kuwa Serikali imejipanga vyema kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kupeleka maendeleo vijijini karibu na mwananchi wa kawaida. Miradi kama *MMEM*, *MMES* imeleta mafanikio makubwa sana katika kupiga vita umaskini kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, napenda niseme machache kuhusu Wilaya ya Chunya, Mkoani Mbeya. Kama hapa nchini kuna Mikoa ambayo tutasema iko pembezoni au mipakani basi kwa Mkoa wa Mbeya, Wilaya ya Chunya iko pembezoni sana. Kimaendeleo katika nyanja zote Chunya iko nyuma sana kuliko Wilaya zote. Pamoja na hayo mipango yote inayoletwa na Serikali kupiga vita umaskini, Chunya inakuwa ni ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, mpango wa *MMEM* ulipoanza kwa majaribio, Chunya haikuwemo pamoja na umaskini uliopo na sasa hivi Serikali inatekeleza huduma za fedha vijijini, programu ambayo itagharimu dola za Marekani milioni 23.8 cha ajabu ni kwamba katika Mkoa wa Mbeya ni Halmashauri ya Wilaya ya Chunya na Ileje tu ndizo hazimo kwenye programu hii! Pia Serikali inatekeleza programu ya uendelezaji wa mifumo ya masoko ya mazao ya kilimo. Programu hii nayo itagharimu dola za Marekani milioni 42.5.

Mheshimiwa Spika, sitashangaa kama Wilaya ya Chunya haimo kwenye programu hii pamoja na kuwa Mkoa wa Mbeya umo.

Mheshimiwa Spika, lingine ni fedha zinazotolewa kuendesha Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya. Wilaya ya Chunya ina ukubwa ambaou unakaribia nusu ya Mkoa wote wa Mbeya, cha kushangaza ni kuwa fedha anayopewa Mkuu wa Wilaya ya Chunya inakaribiana na ile ya Rungwe au Mbozi. Matokeo yake ni kuwa sababu ya ukubwa wa Wilaya, fedha hiyo inaisha haraka na kumfanya Mkuu wa Wilaya kuwa omboomba wa mafuta ya gari anapotakiwa kusafiri kiutendaji Wilayani.

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote, waiangalie Chunya kwa macho ya huruma kama vile walivyoamua kuiangalia Mikoa ya pembezoni au mipakani kwa macho ya huruma. Naunga mkono hoja.

MHE. JANET B. KAHAMA: Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Taifa. Nampongeza pia Mheshimiwa Yusuf Makamba kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi pamoja na Waheshimiwa wengine waliochaguliwa.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na maelekezo ya Serikali kwamba ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la upungufu wa chakula nchini ni kuhakikisha kwamba kila kaya inahamasishwa ili iwe na utaratibu wa kuweka (kuhifadhi) chakula kila baada ya mavuno hadi mavuno ya msimu unaofuata.

Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kupendekeza kwamba pamoja na hatua hii, Serikali ingechukua hatua za makusudi kutambua vyakula vikuu na kuhakikisha kwamba Tanzania inajitosheleza. Vyakula hivyo ni vifuatavyo, mchele, Tanzania haina sababu ya kutojitosheleza kwa zao hili hata kuwa na ziada ya kuuza nje. Tunayo mabonde mengi yenye maji kwa mfano Mkoa wa Shinyanga, Kyela, Morogoro, Pwani na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mihogo inaota kwa wingi katika mikoa mingi Bara na Visiwani, kuhusu ulezi na mtama, mazao haya pia yanaota katika sehemu nyingi nchini.

Kuhusu zao la ndizi,, maeneo ya zao hili pia ni mengi, wananchi katika maeneo haya wahimizwe kuyaangalia na kuyatunza vizuri ili yasiathirike na magonjwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mahindi, zao hili linalimwa katika maeneo karibu yote nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango wa ajira na uwezesaji kiuchumi, naipongeza sana Serikali kwa kubuni mpango hu wa kutenga shilingi milioni 500 kwa kila mkoa kwa kuanzia. Napendekeza utaratibu ufuatao ili kuhakikisha mpango huu unafanikiwa kwanza, wakopaji wachunguzwe kwa makini kuhakikisha wanayo miradi yenye tija na faida ili wakopaji waweze kurejesha mikopo.

Pili, kwa kadri inavyowezekana, mikopo ipitishwe kwenye *SACCOS* ambazo zinawaelewa vizuri wakopaji wazuri na waaminifu wakopaji hao vile vile wanaweza kuunganisha mkopo kutoka *SACCOS* na kutoka Serikalini.

Kuhusu ajira kwa jumla, Serikali ingeweka utaratibu wa kujua mwaka hadi mwaka nafasi mpya zinazoundwa katika kila sekta na kujua ni zipi zinatoka *Private Sector* na zipi zinatokana na shughuli za Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa Makao Makuu, Dodoma, kwanza nafurahi kwamba Ilani ya Uchaguzi imeagiza itungwe sheria mahsusini ya kuthibitisha Dodoma itakuwa Makao Makuu ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kwamba barabara za lami zinajengwa kuunganisha Dodoma na Makao Makuu ya Mikoa yote pamoja na barabara ya kutoka Arusha hadi Iringa na kutoka Mwanza hadi Dodoma.

Mheshimiwa Spika, ili kuharakisha ujenzi wa Makao Makuu ya Dodoma, napendekeza utumike mkakati ule ulitumika wa kujenga ukumbi mpya wa Bunge na pia utaratibu wa *Contractor Finance*, makampuni mengi ya humu nchini na nje yako tayari kushiriki ili ujenzi wa Makao Makuu Dodoma utekelezwe, kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Hii ni pamoja na uwanja wa ndege wa Msalato.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri juu ya mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa ajili ya Ofisi.

Mheshimiwa Spika, hotuba imefafanua na kuweka wazi mambo yote, utekelezaji wa shughuli za Serikali. Naomba nichangie kuhusu yafuatayo:-

(i) Kuhusu *LAPF*, naipongeza Serikali kwa uamuzi wa kutoa ruzuku ya shilingi bilioni 107.3 ili kuwezesha watumishi kupata pensheni pindi watakapostaafu. Lakini kuna mchezo mchafu ambao hufanywa na Halmashauri kutowasilisha makato ya toka mishahara yao kwenda *LAPF*. Kwa kuwa sheria inazitaka Halmashauri kuwasilisha makato hayo mara yanapofanyika. Sheria iwekewe mkazo ili kulinda mali na haki ya mfanyakazi ili anapostaafu isionekane makato yalikuwa hayajawasilishwa.

(ii) Mfumo wa kutoa ruzuku kwa Halmashauri. Mfumo huu una kasoro kwa maana vigezo vingine vinasababisha adhabu kwa mwananchi asiye na hatia kwa mfano Halmashauri kunyimwa ruzuku kwa sababu mahesabu kuandikwa vibaya na hivyo kutolewa hati chafu, hapa mwananchi au wananchi wanakuwa wamehusika vipi mpaka fedha kwa ajili ya maendeleo yao kutotolewa?

Mheshimiwa Spika, kutokuwa na watumishi wenye sifa (Mkurugenzi, Mweka Hazina na kadhalika) hiki nacho ni kigezo cha Halmashauri kutopata ruzuku, hili ni kosa la nani? Serikali kama haijaleta watumishi wenye sifa zinazostahili kwa nini fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya wananchi izuiliwe. Naomba Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu iangalie upya vigezo vya kutoa ruzuku kwenye Halmashauri ili adhabu itolewe kwa yule anayestahili.

(iii) Kuhusu posho ya Madiwani. Posho ya Madiwani ni ndogo sana, lakini majukumu yake ni makubwa na mazito kwa vile yuko karibu sana na wananchi lakini pia husimamia utekelezaji wa miradi na mipango ya maendeleo. Suala hili tumelizungumza sana hivyo naomba Serikali Kuu ifike mahali pa kuamua kuwalipa posho kubwa zaidi ya

vikao na ile ya mwezi. Wajibu haki na maslahi vikienda pamoja ufanisi nao unapatikana. Nazidi kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa umahiri na umakini wa kutekeleza na kufuatilia na kusimamia shughuli za Serikali. Naunga mkono hoja.

MHE. RAJAB AHMED JUMA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ya Makadirio ya Matumizi ya mwaka 2006/2007 aliyoitao tarehe 26/6/2006 hapa Bungeni. Naipongeza hotuba hiyo kwa sababu imekidhi haja katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, kuwa na lengo imara la kubadili maisha ya Watanzania kuwa bora zaidi na pili, Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa karibu na watu sana na huo ndio uongozi bora kwa sababu matatizo yaliopo atayafahamu na kuyachukulia hatua.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuyashughulikia matatizo ya Muungano kwa kukaa pamoja na viongozi wa SMZ na hatimaye kuyatafutia ufumbuzi wake na Serikali kutenga shilingi 500 kwa kila Mkoa kwa ajili ya mikopo ya maendeleo kwa wananchi jambo ambalo litasaidia sana kuboresha maisha.

Tano, Mheshimiwa Waziri Mkuu kusaidia sana msukumo wa elimu na hatimaye watoto wengi wamepata nafasi ya kusoma darasa la tisa (*Form I*) na kuongeza madarasa mengi ya darasa la kwanza na sita, Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa na mpango maalum wa kuwa na mkataba na Halmashauri za Wilaya kwa nia ya kuboresha maendeleo ya kazi.

Mheshimiwa Spika, saba, Serikali imekusudia kwa dhati kuweka mfumo mzuri katika sekta ya madini jambo ambalo litasaidia sana kuboresha maisha ya wananchi wetu.

Mheimiwa Spika, namalizia kwa kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kusimamia vizuri ahadi hizi kama ilivyo kawaida yake.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja.

MHE. MARIAM S. MFAKI: Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kwanza napongeza hotuba ya Waziri Mkuu kwani ni hotuba na bajeti hii imezingatia matatizo na kero za wananchi. Ombi la kwanza ni Serikali iangalie utaratibu wa kupanua hospitali ya Dodoma katika maeneo ya kuongeza kujenga *ward* ya watoto ili kupunguza msongamano katika *ward* zilizopo, kuongeza *ward* ya wazazi na kupanua au kujenga jengo lingine ili kuwa *ward* ya daraja la kwanza kwani iliyopo ina vyumba viwili tu.

Mheshimiwa Spika, mapunjo ya watumishi yanayotokana na mishahara imekuwa ni kero ya muda mrefu, hawajalipwa. Tunaishukuru Serikali kwa kupandisha mishahara ambapo itaongeza mapunjo naiomba Serikali itueleze lini itawalipa watumishi hawa mapunjo yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekubali kutoa posho ya mazingira magumu ya kazi kwa watumishi wa Wizara ya Afya. Niikumbushe Serikali ijue watumishi wa Wizara ya Usalama wa Raia kwani kazi wanayoifanya ya kukimbizana na majambazi ni ku-*risk* maisha yao hivyo ni vizuri Serikali itueleze lini itatoa posho hiyo.

Mheshimiwa Spika, *teaching allowance* kwa walimu ni muhimu kwani kulingana na kazi ya walimu hawana nafasi ya kufanya shughuli nyingine yoyote ya kujiongezea kipato hivyo mishahara wanayopata haiwezi kukidhi mahitaji muhimu hivyo umefika wakati wa kuwapa walimu *teaching allowance* ili kuwapunguzia makali ya maisha na kuwawezesha kufanya kazi zao vizuri na watoto watafaulu kwa wingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mfumuko wa bei za bidhaa. Uwezekano wa wafanyabiashara kutumia mwanya wa kupanda kwa mishahara bei za bidhaa zikapanda. Tunaamini Serikali imeshatoa Ilani ila tunaomba Serikali iwe macho zaidi katika kusimamia bei za bidhaa. Pia shilingi milioni 500 kwa kila Mkoa. Tunaishukuru Serikali kwa kutoa fedha hizo kwa ajili ya mikopo kwa akinamama na vijana. Tunaomba Serikai itupe maelekezo ya utaratibu utakaotumika kukopesha fedha hizo. Ningeshauri Serikali, taratibu, kanuni na sheria hizo zitolewe na zipelekwe vijijini zenyelugha ya Kiswahili na rahisi ili wanaohitaji mikopo waelewe. Riba ndogo na isimamie mkopaji. Tunaomba mikopo hiyo itakapotolewa iweze kununua hata trekta, nyumba za kupangisha, vitu ambavyo vitazalisha na kuwapunguzia umaskini. Vile vile dhamana za kupata mikopo hiyo iangaliwe kulingana na maeneo mbalimbali. Naunga mkono hoja hii.

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA: Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa Mwenyezi Mungu kutujaalia tukiwa wazima na salama. Pili natoa pongeza kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama chake. Vile vile napenda nimpongeze Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kuchaguliwa kuwa Waziri Mkuu wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mimi napenda kuchangia hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mbunge wa Jimbo la Micheweni na wao tatizo lao kubwa linalo tukabili ni huu mpasuko wa kisiasa ulioko huko Zanzibar ambao Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano aliahidi kuushughulikia.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa upande wangu ninamuomba Mheshimiwa Rais suala hili alishughulikie haraka sana kwani wananchi wa Zanzibar wanalisubiri kwa hamu kubwa sana na wanasema kuwa tayari wao wameshachoshwa na hali iliyoko huko Visiwani kwa ujumla. Suala la kukaa kimya kipindi kirefu ni kuwaumiza Wazanzibar.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo napenda kuchangia ni kuhusu Tume ya Uchaguzi na hili nasema kwa dhati yangu kuwa napenda kuipongeza kwa sehemu moja tu ambayo ilinigusa mimi sehemu yenyewe ni namna walivyo zishughulikia pingamizi za wagombea, kweli sehemu hii walifanya vizuri, hakukuwa na upendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hiyo napenda kutoa dosari moja ambayo ninaiona kwa Tume hii nayo ni kuwashirikisha Usalama wa Taifa katika vyumba vyakuhesabu na kujumlisha kura wakati hawamo katika sheria ya uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, hapa nitamtaka Mheshimiwa Waziri anipe maelezo ya kina kwa nini hawa jamaa wakauangalia uchaguzi na wao hawakutajwa kwenye sheria ya uchaguzi.

Kuhusu kuhamia Dodoma mimi sina tatizo ila tu naona Serikali haina uharaka wa kufanya hivyo isijilazimishe kuwa haijawa tayari, iendelee kukaa Dar es Salaam kwani mtu nyumba aliyoizoea, kuihama inakuwa taabu na hata ikiwezekana hapa Dodoma iwe ni Makao Makuu ya Bunge tu na makaburi ya wakubwa kama tulivyopitisha Muswada wa Sheria wa Mazishi ya Viongozi. Kwa sababu suala hili watu wanaliangalia kwa kifupi, lakini ni refu sana hata likikamilika ni muda mrefu sana, kwani saa hizi Dodoma haina hata uwanja wa ndege wa Kimataifa, ndio sasa uwanja wake uko katika upembuzi yakinifu huko Msalato. Kwa hiyo, mimi nasema hili lisitusumbue. Ahsante sana.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani zangu kwako kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie. Mchango wangu utakuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, elimu, mazingira ya kazi kwa walimu wa shule za msingi hasa maeneo ya vijijini. Nyumba ni mbovu wanazoishi haziendani na hadhi ya taaluma yao, kushuka kwa hadhi ya walimu, hupunguza maadili ya kazi yake na wanafunzi hukosa haki yao ya msingi ya muhula na hatimaye mtoto kutofanya vizuri katika mtihani wa mwisho wa muhula.

Pili, mazingira ya kufuata mishahara makao makuu ya Wilaya, umbali na ugumu wa kupata usafiri unaostahili, walimu hutumia muda mrefu kusubiri mshahara kwa siku kadhaa mara afikapo Makao Makuu ya Wilaya na huwajibika kupanga nyumba ya kulala wageni kwa siku zote anazosubiri kupata mshahara wake. Hivyo analazimika kulipia chumba pamoja na chakula kwa kutumia mshahara wake. Kwa hiyo anaporudi nyumbani, pesa zote za mshahara anajikuta amemalizia kwa kuufuatilia mshahara.

Mheshimiwa Spika, pia, wanafunzi hukosa vipindi kwa muda wote wa walimu wao wanapokuwa safarini kufuatilia mshahara, Serikali iangalie kwa makini maeneo ya shule za vijijini ili ipunguze au kuondoa kabisa kero hii na adha wanazopata walimu hata wanafunzi pia.

Kuhusu elimu ya sekondari (*MMES*), mfumo wa mpango wa *MMES* sio mzuri katika upelekaji wa fedha kupitia Hazina ndogo hadi kwa Wakuu wa Shule, wakuu wa shule kujichukulia madaraka wao wenye bila kushirikisha Bodi ya Shule kikamilifu, nashauri pesa za *MMES* zifuate mpango wa *MMES*, Wakuu wa Shule wanapobainika kuwa wamekubali jambo hili humpa nafasi mhalifu huyu kuendeleza tabia hii ya ubadhilifu katika shule atakayopelekwa, tena kwa ufundi zaidi ili asigundulike.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, wakuu wa shule watakaobainika kula fedha za *MMES* wasihamishwe, wachukuliwe hatua za kisheria na kama hakuna ushahidi wa kutosha, basi wafukuzwe kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu ya watu wazima, kuna matatizo makubwa sana katika utoaji wa elimu ya watu wazima vijijini. Kwanza, walimu wa kutosha hakuna, maslahi ya watumishi hao ni madogo sana, hali duni ya maisha mionganoni mwa wananchi hasa walengwa wa elimu ya watu wazima na Serikali iweke mikakati mizuri katika kuboresha mazingira mazuri ya watoa elimu na wanafunzi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mfuko wa Bima ya Afya, bado mfuko huu haujawa na mfumo mzuri wa kutoa huduma kwa wanachama wake hasa watumishi walioko vijijini. Vituo vyote walivyovisafiri havina vitendea kazi vingi walivyovitaja.

Mheshimiwa Spika, matatizo hayo n pamoja na vipimo vya msingi haba, dawa yoyote iliyomo katika orodha ya Taifa ya madawa muhimu hazipatikani, kuhusu kulazwa vituo vingi havina madaktari na hata vitanda vya kutosha, suala la upasuaji wengi hulazimika kusafiri kufuata huduma kwenye hospitali kuu na gharama za kufuatilia huduma ya Bima ya Afya inakuwa kubwa toka mfukoni kwake, na pengine hukata tamaa na kuamua kujilipia na mwanachama hukatwa mshahara kila mwezi, lakini anaweza asiugue kwa miaka mitatu, lakini anapungua, huduma haipo, ni dhambi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kukoma kwa uanachama ni kufukuzwa kazi, kuacha kazi, kustaafu kazi, haya yarekebishwe angalau waendelee kwa miaka miwili.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

MHE. JUMA SAID OMAR: Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba kwanza nitumie nafasi hi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa leo tukiwa sote ni wazima na wenye afya njema. Namuomba Mwenyezi Mungu atuzidishie uzima na afya hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo napenda nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi.

Pia nampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu na kuthibitishwa na Wabunge wote kwa kura nydingi.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kukupongeza wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuchaguliwa na Wabunge wote kwa kura nydingi. Hii inatokana na imani kubwa tuliyonayo juu yenu kutokana na utendaji wenu wa kazi bila ya upendeleo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa namna ilivyoanza kufanya kazi hasa katika kukabiliana na suala la njaa pamoja na suala zima la ujambazi nchini. Naomba utendaji kazi kwa ufanisi uendelee katika sekta na taasisi mbalimbali zinazochangia uchumi na maendeleo yanchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kazi ya Jeshi la Polisi ni kulinda raia na mali zao, lakini kwa bahati mbaya imejitokeza kwa baadhi ya askari wa Jeshi hilo kutokutekeleza wajibu huo kwa baadhi ya maeneo hasa kwa wafuasi wa vyama vya upinzani (zaidi *CUF*) hasa unapofika wakati wa uchaguzi mkuu kama uchaguzi wa mwaka 2000 na 2005. Jeshi hilo litashirikiana na vikosi vya SMZ wamekuwa wakiwanyanya wananchi (wapinzani) kwa kuwapiga, kuwakamata na kuwaweka ndani kwa muda mrefu, kuwabunia makosa yasiyokuwa ya kweli na hata wakati mwininge kuwaharibia mali zao mfano kijiji cha Piki katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, kuna wananchi wasiopungua 20 katika kijiji cha Piki ambao hadi sasa wameshindwa kurudi kijijini kwao kwa hofu kuwa wakirudi watakamatwa ingawa wale waliokamatwa na kuwekwa ndani kwa tuhuma ya mauaji wa askari mmoja wa JKU wameshaachiwa huru. Je, hali hii itaendelea mpaka lini kwa wananchi hawa?

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iliangalie suala hili ili wananchi hao waweze kurudi kijijini kwao, waishi na familia zao bila ya usumbuwa wa aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, suala la maji safi na salama limekuwa kero kubwa kwa wananchi wote wa nchi hii hasa wale wanaoishi vijijini. Naiomba Serikali iandae mpango wa makusudi utakaohakikisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wote huku Serikali ikijua wananchi wanatumia maji yasiyo safi na salama.

MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimmia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri, iliyogusa maeneo mengi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika yafuatayo, kwanza kuhakikisha mipaka ya nchi yetu ipo salama. Hili ni suala muhimu sana kwa usalama wa nchi yetu ukiangalia Ziwa Tanganyika yapo maeneo karibu na Kongo, hakuna *infrastructure* yoyote ya kutekeleza suala hilo. Hakuna barabara, *patrol boat* na mawasiliano. Shughuli hizo zikiboreshw Serikali itaweza kuimariswa hizo uwezo wake wa kulinda maisha na mali za raia wake.

Mheshimiwa Spika,pia, kuboresha uchumi wa nchi yetu na kuondoa umaskini. Bado sekta ya uchukuzi na usafirishaji katika nyanja zote (reli, viwanja na magati) hazijapewa msukumo. Tunatoa fedha kwa barabara na kusahau reli na viwanja vya ndege. Ukitengeneza reli unatengeneza mara moja ile barabara. Kila baada ya miaka miwili lazima tufanye matengenezo. Hebu tufumbe macho na kutoa fedha za kutosha katika kuboresha miundombinu hii.

Kuhusu usimamizi na uratibu wa maafa. Napongeza mipango madhubuti ya uundwaji wa Kamati za Maafa za Mikoa. Sasa ipo haja ya kuziwezesha Kamati hizi kwa kuzipatia nyenzo (vifaa vyote) Kamati ziwe na *center* inayoeleweka na wananchi na wananchi waelewe wapi watapata huduma za haraka mara maafa yakijitokeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza, viongozi wa Ulinzi na Usalama daima wawe tayari kuwa wa kwanza katika kuwafikia katika eneo.

Pili, tunaweza kuwashajiisha vijana na kupewa elimu ya vitendo katika mambo mbalimbali ya majanga na namna ya huduma zinazotakiwa kutolewa.

Tatu, tutoe kipaumbele katika maeneo ya visiwa vidogo vidogo kwa vile kuwafikia kwa urahisi zaidi wakati wa maafa ni ngumu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vita dhidi ya maradhi ya UKIMWI. Ninahangaika sana nikisia wenye UKIMWI kwa makusudi kabisa wanaendelea kusambaza virusi hivyo kwa vijana wadogo sana, *responsible people* na wanaojijua wana UKIMWI wanaendelea kufanya mauaji ya makusudi kwa vijana wetu. Ipo haja ya kuwa na sheria ya kuwagusa wadhalimu hawa au lile suala la *confidentiality* liachwe na jamii ilezwe nani mgonjwa japo ni kinyume na *ethics*.

Mheshimiwa Spika, je, huo mfuko wa shilingi 500 milioni utafika Pemba na nani atakuwa *responsible* wa kuhakikisha zinatumika ilivyokusudiwa?

MHE. ALI AMEIR MOHAMED: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu, wadhifa muhimu kwa Taifa. Pili, nampongeza Waziri Mkuu kwa kuchapa kazi kwa ari, nguvu na spidi mpya.

Mchango wangu ni katika maeneo yafuatayo, kwanza ni kuhusu Muungano, hatua za Serikali mbili kukutana ni nzuri lakini muhimu zaidi ni kusaidia urchumi wa Zanzibar. Kelele zote za kero za Muungano zitakwisha pale urchumi utakuzwa kwa njia mbili kama vile kupeleka viwanda vikubwa Zanzibar ili watu hasa vijana wapate ajira. Utaratibu wa kazi wa *TRA* uangaliwe upya kuondoa maudhi yanayowapata watu. Gari zenye usajili wa Zanzibar kwa nini zizuiliwe kutembea Bara wakati *TRA* ipo Zanzibar?

Kuhusu uwezeshaji wananchi kiuchumi usiishie Mikoa ya Bara tu. Wastani wa shilingi milioni 500 kwa kila ukoo uhusishe pia mikoa ya Zanzibar kama ilivyo fanyika kwa mradi au mpango wa *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu shughuli za Bunge, naipongeza Serikali ya Muungano kwa kuliwezesha Bunge kukamilisha ujenzi wa jengo lake huko Zanzibar na kwa kweli ni jengo zuri linalotosha ushahidi kuwa Bunge la Jamhuri ya Muungano. Hata hivyo suala la Ofisi za Wabunge bado linaonekana halijapata ufumbuzi. Zanzibar inazo Wilaya kumi. Angalau kila Wilaya ingepatiwa Ofisi ambapo Wabunge wa Wilaya wangeweza kwenda kufanya kazi za ofisini. Ofisi kama hizo zingejengwa na kuwekwa vifaa vyakisasa zingesaidia sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri ya bajeti inayotoa matumaini mema katika harakati zetu za kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. Naunga hoja hii.

Napenda kutoa maoni yangu kuhusu hoja hii kama ifuatavyo, kwanza ni kufufua Mabaraza ya Usuluhishi ya Kata. Sheria zetu zinaruhusu kuundwa kwa Mabaraza ya Usuluhishi ya Kata (*Ward Tribunals*) lakini katika Kata nyingi sana hazijaruhusu Mabaraza hayo, hayafanyi kazi. Moja ya sababu ni kukosekana kwa fedha za kuwalipa Katibu wa Baraza, Mwenyekiti wa Baraza. Matokeo yake kazi zote vijijini hata zile ndogo ndogo zinapelekwa Mahakama za Mwanzo na kurundikana sana huko. Mahakama za Mwanzo nyingi hazina Mahakimu hivyo kesi zinakaa muda mrefu bila kusikilizwa hivyo inacheleweshwa na mahabusu wanarundikana Magerezani. Serikali itafute ufumbuzi na tatizo hili ili Mabaraza haya yafanye kazi kama ilivyokusudiwa.

Kuhusu utenganezaji wa barabara vijijini, zipo chini ya Halmashauri na matengezo kupitia fedha za *Road Fund*, barabara hizi zinategenezwa na makandarasi ambao huchukua fedha nyingi za matengenezo na hayana viwango. Pendekezo ni kwamba matengenezo ya barabara za vijijini ziige utaratibu wa *TASAF* ambapo wanaviji wanashiriki kwa ubora, wanalipwa chini ya usimamizi wa injinia. Utaratibu huo umetupatia barabara nzuri za vijijini, kwa bei nafuu, na wanaviji wanapata ajira. Kazi za madaraja ndizo zipewe makandarasi kwa vile ni za muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, naipongeza na kuishukuru Serikali kwa msaada mkubwa wa chakula cha njaa Mkoa wa Singida na hususan Wilaya ya Manyoni kipindi cha msimu uliopita. Msimu huu maeneo mengi ya Wilaya ya Manyoni hayakupata mvua za kutosha hivyo hali ya chakula ni mbaya sana hasa Tarafa za Kintinku, Kilimatinde na Nkonko. Kwa hiyo, kitengo cha Maafa katika Ofisi ya Waziri Mkuu na Serikali kwa jumla ijiandae kutoa msaada wa chakula kwa Wilaya ya Manyoni. Kwa kuwa huu ni msimu wa pili wa kukosa mavuno, itoe fedha za kununua chakula cha bei nafuu kwani wananchi wengi hawana.

Mheshimiwa Spika, ushauri ni kuwa sasa Serikali ileté chakula cha kazi (*food for work*) kwa vile wenye nguvu na chakula cha bure na wasio na uwezo kabisa hasa wakongwe, walemovu na watoto yatima. Narudia kuunga mkono hoja hii.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na yenye mantiki kwa wingi. Namshukruu sana kwa kurudisha Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa chini ya ofisi yake. Nina matumaini makubwa sana kwamba Mikoa, Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji la Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Arusha na Tanga yatapata maendeleo makubwa na hivyo kasi ya maendeleo sasa itafika mpaka kwenye Tarafa, Kata, Vijiji na Vitongoji.

Mheshimiwa Spika, kazi ya sasa ya kufanya ni kupanga upya safu za viongozi wa Wilaya, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Maendeleo na Wakuu wa Idara, lengo likiwa ni kuwapata viongozi ambao wataendana na kasi ya Serikali ya Awamu ya Nne. Kuna baadhi ya viongozi hawana uwezo wa kazi, wengine wamekaa kwenye vituo vyao vya kazi kwa kipindi kirefu hivyo kutawaliwa na mazingira ya eneo na kusahau wajibu wa kazi.

Napenda kumshauri Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba kasi mpya iwekwe kwenye kubadili mfumo wetu wa kilimo, tujitahidi kuachana na jembe la mkono na kuhamia kwenye matumizi ya wanyamakazi na kiwango kikubwa wakulima wetu waanze kutumia matrektta. Tuhakikishe wakulima wetu wanapewa mikopo kuitia kwenye *SACCOS* ambazo zimeanzishwa karibu kila Kata. Wananchi wetu watakiwe kulima mazao yanayoendana na hali ya mvua kwenye eneo husika.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano Mikoa ya Dodoma, Singida, Shinyanga na kadhalika, watakiwe kulima mtama, uwele badala ya kulima mahindi ambayo yanahitaji mvua kubwa. Sheria ya nguvukazi ianze kutumiwa sasa ili kila mtu afanye kazi. Kwa vijijini kazi kubwa iliyopo ni kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mifugo, wafugaji watengewe maeneo maalum kwa ajili yao. Malambo yachukuliwe ili maji yapatikane wakati wote wa mwaka, madawa ya mifugo yapatikane kwa urahisi na karibu na maeneo yao. Pia elimu iwe inatolewa mara kwa mara juu ya ufugaji bora. Maafisa Kilimo na Mifugo wapelekwe kila Kata. Pia Maafisa Kilimo na Mifugo Wilayani wawe wanatembelea Kata na Vijiji kutatua matatizo ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha zinazotolewa kwa ajili ya matengenezo ya barabara kwenye Halmashauri zetu, naomba sana Serikali itafute uwezekano wa kuongeza fedha hizo. Pia kuna wakuu wengi wa Kitengo cha Ujenzi Wilayani hawana uwezo, wengine wameanzisha kampuni zao ambazo kwa ujanja kazi za barabara hutolewa kwa kampuni hizo.

Mheshimiwa Spika, mtindo wa Afisa kuharibu Wilaya moja anapewa uhamisho kwenda Wilaya nyingine au kupelekwa TAMISEMI Makao Makuu uachwe mara moja. Mtumishi akikosea achukuliwe hatua kwenye kituo hicho hicho alichoharibu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sasa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa jitihada inayofanya kupata walimu wengi kwa ajili ya shule zetu za Msingi na Sekondari. Naomba pia jitihada zifanywe kupata waganga wa kutosha kwa ajili ya zahanati zetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MWADINI ABBAS JECHA: Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa tumekuwa tunaelezwa na tunafahamu kwamba kilimo ndio uti wa mgongo wa

uchumi wa Taifa letu, kwamba, Sekta ya Kilimo inachangia jumla ya asilimia 45.6 na inatoa ajira kwa takriban asilimia 80 ya Watanzania

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa inafanya kila juhudi kuimarisha kilimo ikiwemo na sekta ya mifugo kwa kuwapatia wakulima na wafugaji ruzuku katika pembejeo za kilimo, dawa, zana mbalimbali na kadhalika. Lakini ni lazima tukiri kwamba pamoja na juhudi zote zilizolekezwa kumkomboa mkulima na mfugaji, bado watu hawa wameendelea kuwa maskini wa hasa kipato. Ni vyema basi tukarudi nyuma kuangalia wapi tunakosea na wapi tumeteleza.

Mheshimiwa Spika, nadhani pamoja na mambo mengine, tumekuwa na changamoto kubwa zifuatazo, kwanza ni ukosefu wa upatikanaji wa mikopo na pili ni elimu duni au ukosefu wa elimu bora za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, tukizingatia hali ya kipato cha mkulima wa kawaida na kule kokosa dhamana ya kuweza kujipatia mikopo, kunawafanya wakulima na wafugaji kutumia mbinu zisizo za kisasa kuongeza uzalishaji, matokeo yake ukulima wetu unakuwa duni na wenye tija hafifu kila uchao.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali sasa ikaandaa utaratibu ulio madhubuti ukiwemo na ule wa kutambua umiliki wa ardhi ya Kijiji, utakaowawezesha wakulima na wafugaji kupata mikopo yenyeye riba nafuu ili kukuza uzalishaji hatimaye kuondokana na umaskini. Kadhalika hatua hii ni pamoja na mabenki na Taasisi za Fedha ambazo zinamilikiwa na wakulima wenyewe kuititia vyama vyao vya ushirika ambazo zitajielekeza kuwapatia mikopo nafuu wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine kubwa linalowasumbua wakulima na wafugaji hasa katika kuingia katika kilimo cha kiasa ni taaluma duni wanayopata au ukosefu wa taaluma hiyo kunakowafanya waendelee kuzalisha bila kuzingatia mbinu za kisasa za kukuza uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu sasa Serikali imekuwa inasomesha wataalam mbalimbali na kuapeleka vijijini kusaidia kuwaelimisha wakulima mbinu za kupambana na changamoto zinazokwaza ongezeko la uzalishaji wa bidhaa duni. Maafisa Ugani wanaopelekwa Mikoani, Wilayani na Vijijini huwa wanawajibika moja kwa moja katika Halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, madhumuni makubwa ya kuchukuliwa hatua hii ilikuwa ni kuongeza uwajibikaji. Tatizo linalojitokeza na ambalo sasa limeshaota mizizi ni ukosefu wa uwajibikaji unaotokana na ufuutiliaji hafifu wa kuona ni namna gani Maafisa Ugani wanatekeleza kazi zao. Matokeo yake wakulima wanalamika kuwa Maafisa Ugani hawaonekani kabisa mashambani, usimamizi wao ni mbovu na kwamba wakulima wanakosa elimu inayostahili kukuza uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mawazo yangu naona kuna mambo mawili makubwa yanahitaji kushughulikiwa ipasavyo.

Kwanza Serikali ni lazima sasa iandae utaratibu utakaowezesha kufuatilia ipasavyo utendaji wa Maafisa Ugani na pale ambapo panatokea kasoro basi hatua madhubuti na za haraka zichukuliwe kurekebisha hali hiyo. Aidha, kutokana na mabadiliko ya mazingira na mbinu za uzalishaji, Serikali lazima iandae namna ya kuwapatia elimu hizo Maafisa Ugani ili waendane na mabadiliko hayo hatimaye kukabili vyema matatizo ya mkulima na mfugaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali ihakikishe inawapatia Maafisa Ugani nyenzo na vitendea kazi vitakavyowezesha kuwa karibu na wakulima na kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa. Aidha, mishahara yao na maslahi mengine yaangaliwe upya kulingana na hali ya uchumi ilivyo, lakini pia na umuhimu wa kazi yao na mazingira wanayokabiliana nayo. Pia pawepo na ufuutiliaji wa karibu sana katika utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wao Maafisa Ugani wahakikishe wanatekeleza wajibu wao ipasavyo na kwa kuzingatia hali ya mkulima wa Kitanzania. Aidha, kila Afisa Ugani lazima aandae ratiba yake ya kazi (*calendar and plan of work*) na kuziwasilisha kwa uongozi unaohusika (iwe ni *RAS* au *DAS* na kadhalika) ili kurahisisha ufuutiliaji, lakini pia kuandaa mapema upatikanaji wa nyenzo zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, Maafisa Ugani wawe tayari mara kwa mara kujiongezea taaluma hasa tukizingatia mbinu za uzalishaji zinabadilika siku hadi siku na kwamba wawe na uhusiano wa karibu na Vituo vya Utafiti.

MHE. ANNE S. MAKINDA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Waziri Mkuu. Naomba maelezo kuhusu mambo yafuatayo: -

Kwanza, wale Watendaji wa Vijiji ambao walikuwa hawajalipwa mishahara yao hadi sasa watalipwa lini? Wengine toka utaratibu wa kulipa mishahara *VEO* uanze hawajalipwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

Mheshimiwa Spika, pili, tangazo la kuanzisha Halmashauri ya Mji wa Njombe lilipokelewa kwa shangwe kubwa na wananchi, mbona bajeti yake sijaiona katika makabrasha haya? Inawezekana kuwa uamuzi huu umefutwa kimya kimya? Kama haujafutwa, ni lini Halmashauri hii itaanza rasmi?

Katika Wilaya ya Njombe, Kata na Tarafa nyingine ni kubwa sana, kabla ya uchaguzi wa mwaka 2005 tulielezwa kuwa tutoe mapendekezo ya kugawa Kata na Tarafa, je, utaratibu huo pia umesitishwa? Kama bado upo, basi tungepewa mwongozo mapema wa kugawa Kata na Tarafa ambazo ni kubwa sana, mfano Tarafa ya Igominyi kama Tarafa ni kubwa sana na Kata zake nyingine mfano Kata ya Kifanya, Kata ya Uwemba na Kata ya Matola.

Mheshimiwa Spika, tafadhali naomba majibu na ufanuzi wa maswali niliyouliza na ninawasilisha na kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

MHE. JACKSON M. MAKWETTA: Mheshimiwa Spika, kuhusu uundaji wa Mikoa, kwa miaka mingi viongozi na wananchi wa Wilaya za Ludewa, Makete na Njombe wamekuwa wakiomba kupewa Mkoo wa Njombe bila mafanikio. Viongozi wa awamu zote wanajua na mara ya mwisho walifkisha maombi yao kwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na pia kwa Wizara ya TAMISEMI na Ofisi ya Waziri Mkuu. Jibu la mwisho tuliambiwa maombi yote yamepelekwa kwa Rais kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, je, tuendelee kungojea au vipi? Tuliambiwa kuwa huenda suala hili likashughulikiwa na uongozi wa Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya Wilaya husika ni kwamba kuna milima mingi na mabonde mengi, umbali kutoka Iringa, gharama za kufika Mkoani, kutotembelewa kwa urahisi na viongozi wa Taifa na Mkoo, watu wengi na *potential* kubwa kwa pendekezo la kugawa Wilaya ya Njombe na kadhalika.

MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA: Mheshimiwa Spika, *Assalaam Aleykum.*

Kule jimboni kwangu ni Mji Mkongwe kweli *Germans* walitusaidia kuweka *tiles* Jimbo lote. Bahati mbaya yapo maeneo mafupi mafupi tu ambayo yanahitaji vipande vyta barabara za lami. Si zaidi ya kilometra 10, zote kwa ujumla. Naelewa hili si suala la Muungano, lakini je, Mheshimiwa Waziri Mkuu haoni katika utaratibu wa kutusaidia sisi Zanzibar, akatupia jicho lake Jimbo langu kwa hili.

Mheshimiwa Spika, Mji Mkongwe ni Mji wa Utalii, iwapo tutafumbua tatizo hili itakuwa mmetusaidia kwa kiasi fulani. Hata kama mimi ni mpinzani, lakini heshima itarudi kwenu walau watu kuona kuwa CCM inajali watu na maendeleo hasa katika kipindi chetu hiki kifupi kilicholeta matumaini mapya kwa wananchi. Ni dhahiri inataka ujasiri, lakini penye nia pana njia.

Mheshimiwa Spika, kujenga barabara vile vile ni jambo la thawabu kubwa kesho mbele ya Mungu. Tutajenga imani kuwa kumbe kweli Serikali ya Muungano inajali matatizo ya Zanzibar. Ahsante.

MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu yenye kujaa hekima tele. Sisi tunaomfahamu tuna imani atasimamia kwa ufanisi mkubwa kazi za Wizara yake na Serikali kwa jumla. Ningependa kutoa ushauri na maombi kama ifuatavyo:-

(i) Nashauri sheria na madaraka ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya vitazamwe upya hasa katika uwezo wao wa kusimamia Halmashauri za Mitaa, vinginevyo tutakuta hawana kazi. Niko tayari kutoa maoni zaidi nikitakiwa.

(ii) Mheshimiwa Waziri Mkuu alipoitisha mikutano ya Mikoa inayolima Pamba, Tumbaku, Kahawa na Korosho alitoa malengo. Huo ndiyo mwelekeo sahihi. Nashauri kuwa Mikoa yote husika itakiwe kuweka mipango na *programmes* za utekelezaji zenyet malengo yanayoonyesha malengo kwa wingi wa tani.

(iii) Nashauri pia Mheshimiwa Waziri Mkuu aitishe mkutano wa Mikoa inayolima mazao ya chakula kwa wingi ili kweza kutoa mwongozo utakaozingatia kujitosheleza kwa chakula Kitaifa na ikiwezekana kuwa na ziada katika ghala la Taifa kwa kuwa na chakula cha kutosha miaka mitatu mpaka mitano.

(iv) Ianzishwe mipango ya masomo/mafunzo kwa watendaji wa Serikali za Mitaa.

(v) Zianzishwe kozi kwa Madiwani za kujenga uwezo kwa Madiwani ili waweze kuwa na upeo kwa ajili ya kumudu madaraka yao.

(vi) Nashauri kuwa Taifa lianzishe Kanda za Maendeleo. Iwepo mipango ya kilimo ambayo itaelekeza baadhi ya Kanda kupewa majukumu maalum hasa katika kulima mazao yanayokubalika katika Kanda hizo ili kuachana na kilimo holela.

(vii) Mikoa yote itakiwe kukamilisha maelekezo ya muda mrefu ya kuwa na *Regional Profile* zao, hasa itakayosaidia kuvutia wawekezaji.

(viii) Mheshimiwa Spika, Rais wa Awamu ya Tatu alitoa ahadi ya kutengenezwa kwa barabara ya Mnyangalua mpaka Kilyamatundu (Kipeta) ili iweze kupitika wakati wote. Ahadi hii haijatekelezwa ingawa tumekuwa tunatoa maombi kila mara. Mwaka jana tuliambiwa tumechelewa kuwasilisha wakati wa makisio. Mwaka huu tuliwahi kuleta muafaka tukajibowi kwa maandishi kuwa tutawekwa katika maombi ya fedha za misaada kutoka nje. Lakini mpaka sasa hatujui ni msaada kiasi gani na kutoka wapi. Eneo hilo ndilo linalozalisha chakula kwa wingi na mifugo kwa ajili ya uchumi wa Taifa.

MHE. HEMED MOHAMMED HEMED: Mheshimiwa Spika, sina budi kukushukuru wewe binafsi kwa kuweza kuwa mwalimu mzuri ambaye kwa jitihada zako unatuongoza kama sote ndugu moja katika Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani kwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake iliyo na mwelekeo mwema kwa Watanzania. Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ni kiongozi aliyeiweka historia katika nchi yetu, kwani ni Rais pekee aliyeweza kukaa na Wabunge wa Upinzani na kupokea maoni ya Upinzani. Mwenyezi Mungu amjaalie maisha mema, *Amin*.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nieleze mchango wangu na ninaanza katika sekta ya elimu. Serikali kila leo inahubiri kuwepo kwa uhaba wa walimu nchini. Kuwepo uhaba wa walimu ndio kusema kuna baadhi ya masomo katika shule zetu hayana walimu. Kukosekana kwa walimu wa somo fulani ndio maana wanafunzi hawasomeshwi. Kutokusoma kwa wanafunzi ndio kusema wanafunzi wanafanya vibaya na hivyo kufeli. Tatizo hili linahitaji ufumbuzi wa kina kwani hadi leo kufeli kwa wanafunzi kunasababishwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda nizungumzie sekta ya afya. Kwa kweli Serikali inapaswa iwajibike juu ya hali ya hospitali zetu nchini. Kwa kweli hospitali zetu

haziwezi kupewa jina Kituo cha Afya. Nasema hili kwa sababu hospitali ni mbovu sana tena sana. Kuna baadhi ya hospitali kama vile hospitali ya Songea, hospitali hii ni ya Mkoa na haifai kupewa sifa ya Mkoa

Mheshimiwa Spika, hii inatokana na bajeti ya Wizara kuwa ndogo, jambo ambalo linasababisha Wizara kushindwa kukidhi mahitaji ya hospitali zetu. Bajeti ya Wizara ya Afya inapaswa kuwa na mtazamo mpya. Wizara hii ndio inayopaswa kusimamia usafirishaji wa wagonjwa nje ya nchi. Kukosekana kwa fedha katika Wizara, ndipo Watanzania wanapojitokeza katika *TV* kuomba msaada wa kumsafirisha mgonjwa.

Mheshimiwa Spika, kama Wizara hii bajeti yake ni nzuri, nasema asingeweza kujitokeza mtu kuomba msaada binafsi. Sasa wakati umefika Wizara kujitegemea kwa kufuatana na ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA: Mheshimiwa Spika, Serikali inatarajia kutoa shilingi milioni 500 kwa kila Mkoa ili kusaidia mitaji ya wale walio na vipato vyta chini uwezeshaji. Fedha hizi zinahitaji maandalizi ili ziwe na *impact*. Tatizo kubwa tunalolipata ni upungufu wa *Credit Officers* katika maeneo yetu wa ku-manage na kufuatilia fedha hizi. Hili ni vyema likapewa umuhimu ili Serikali ipate *value for money*.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza hotuba kwa *comprehensive coverage* ya maeneo yote muhimu na ninaunga mkono hoja.

MHE. MWINCHOUM A. MSOMI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kumpongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri Mkuu kwa hotuba yake yenye mwelekeo sahihi wa Serikali yetu ya Awamu ya Nne, yenye matarajio mema kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naiomba Ofisi ya Waziri Mkuu na Serikali kwa jumla kuweka mikakati itakayowezesha zoezi la kuendeleza miji yetu, upimaji wa viwanja kwenda sambamba na upelekeji wa mahitaji muhimu ya ujenzi wa viwanja hivyo utaratibu ambaa hivi sasa haupo.

Nashauri mwananchi anapopatiwa kiwanja na Serikali miundombinu aikute imeshafikishwa. Hii itasadia wananchi kucheleva kujenga kutokana na kukosekana kwa huduma/miundombinu kwenye viwanja hivyo kama vile kupasua barabara kuwawezesha waliomilikishwa viwanja kufika kwa urahisi na kutunzwa barabara hizo, umeme, maji na kadhalika. Wakati umefika tulitazame hilo.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Kigamboni kuna tatizo la ukubwa wa Kata tatu ambazo naiomba Ofisi ya Waziri Mkuu kuangalia uwezekano wa kuzikata Kata hizo angalau kila moja iongezewe Kata moja. Kata zenyewe ni Charamble, Mbagala Kuu na Mbagala. Kata hizo zina wakazi wengi sana na kuleta usumbufu/ugumu kiutendaji kutokana na wingi wa watu na ukubwa wa maeneo.

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo kubwa linalotukabili kwa Wenyeviti wa Mitaa na wananchi. Suala la wananchi kutozwa fedha kwa ajili ya kupata barua kutoka kwa Mwenyekiti wa Mtaa kati ya shilingi 2000/= mpaka shilingi 3,000/= ni kero kubwa. Naishauri Ofisi ya Waziri Mkuu kuwasaidia Wenyeviti wa Mitaa vifaa muhimu vya kutendea kazi ili kero za aina hii zitoweke.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Ofisi ya Waziri Mkuu kwa jinsi inavyosimamia suala la ulinzi wakati wa kipindi cha uchaguzi. Hii inawawezesha wananchi kutoka kwa wingi kwenda kupiga kura na kutumia demokrasia yao. Fujo za Vyama vya Upinzani zilidumaa, hivyo zoezi hilo ni muhimu sana kuendelezwa na kudumishwa kwa kila chaguzi na kwa kila ngazi.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya Wizara ya Mipango na Uwezeshaji, pamoja na Wizara ya Fedha na Uchumi nilizungumzia suala la kuwafikiria wananchi wa Mbagala hadi Kongowe na waathirika wote wa bomoa bomoa wa barabara ya Kilwa kulipwa fidia kwa kuwa (i) wananchi wenye ni maskini sana (ii) wengi wao walikuwa wanategemea nyumba hizo zilizovunjwa (nyumba moja) kwenye maisha yao (iii) kwa kuwa Serikali tayari imepata msaada wa fedha wa kujenga barabara hiyo, tayari Serikali imepata nafuu, hivyo ni vyema nguvu zake zikapelekwa kwenye kufikiria kuwalipa fidia wapiga kura wetu ambao tunawahitaji sana. Tumewaelimisha wakafahamu na hatimaye kutupatia kura kwa wingi katika Uchaguzi Mkuu wa 2005. Tukishindwa kabisa kuwafidia, basi angalau tuwapatie viwanja katika mradi wa upimaji viwanja 20,000.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mpango na mkakati wa awali wa kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kutenga kiasi cha Shilingi milioni 500 kwa kila Mkoa kwa mwaka huu wa fedha 2006/2007. Naiomba Ofisi ya Waziri Mkuu kwanza kuteua Wajumbe wa Bodi itakayosimamia utoaji wa mikopo hiyo. Wateuliwe Wajumbe waadilifu na pili ni vyema hatua za kuunda Bodi hiyo zikachukuliwa kwa umuhimu unaofaa. Aidha, kwa Dar es Salaam, napendekeza Benki ya Wananchi wa Dar es Salaam itumike katika uendeshaji wa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Kigamboni, Kata ya Charame eneo la Mponda kumekuwa na tatizo kubwa la kipindipindu cha kudumu (kila mlipuko) kutokana na kutokuwepo maji salama katika eneo hilo. Zinahitajika hatua za haraka zichukuliwe kuchimba kisima kirefu eneo hilo ili kuwanusuru wananchi wa Mponda, huko Charame Jimbo la Kigamboni.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, napenda kwa dhati kabisa kumpongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri sana, hotuba yenye maelezo ya wazi na yanayoelewaka na yaliyogusia maeneo muhimu ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo. Aidha, hotuba ina takwimu muhimu ambazo zinajibu hoja za Wabunge kikamilifu. Hongera sana na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, napenda kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Nchi, Makatibu Wakuu wa Ofisi hiyo pamoja na wasaidizi wao kwa kumsaidia Waziri Mkuu kwa uaminifu, umahili mkubwa na nidhamu ya dhati na kuweza kuwasilisha hotuba nzuri sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hongera sana na naunga mkono hoja hii kwa dhati.

MHE. BERNADETA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri iliyotoa matumaini makubwa na mwelekeo wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nilichangia Hotuba ya Waziri wa Fedha sitapewa nafasi kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu, ila naomba uniruhusu niulize swali moja. Kwa vile juhudzi za Rais na usimamizi wake thabiti viliwezesha wanafunzi kwa asilimia 62.1 kuingia kidato cha kwanza, je, tumejiandaaje kwa mwakani (Desemba 2006)?

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu ili tupokea kiasi hicho au zaidi cha wanafunzi katika shule za sekondari, yanahitajika madarasa mengine mengi zaidi; je, tusipohamasisha wananchi kuanzia sasa waanze kujenga madarasa, (Juni – Desemba 2006) je, tutawezaje kuhakikisha hawa *Form I* wanapokelewa mashulenzi kati ya Januari – Machi 2007? (Angalizo mwaka huu 2006 *Form I* wengine wameanza Mei mpaka Juni).

Mheshimiwa Spika, napendekeza kampeni za kujenga madarasa ya *Form I* mwaka kesho zianze sasa ili wasije wakachelewa kuanza na kusababisha kutokamilishwa kwa *syllabus*.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuendelea kusikiliza michango mizuri ya Wabunge kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini sitawenza kwani naenda Dar kumuona mume wangu anaumwa.

MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa maana ya kuafiki mipango mizuri iliyokusudiwa kutekelezwa katika kipindi hiki cha bajeti ya mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, labda niweke msisitizo katika suala zima la kilimo chenye tija. Kilimo chenye tija ni kile ambacho kina uhakika wa kuvuna kwa mwaka mzima yaani cha umwagiliaji. Njaa ambayo tunapata katika nchi yetu sio tu kwamba ni aibu ikilinganishwa na nchi yetu kimazingira, lakini pia ni *challenge* ya vipi tutumie akili zetu kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tulipokea msaada wa chakula toka Serikali ya China, Serikali ya China ilisema: “Tunajua marafiki zetu mmepata tatizo kubwa la ukame, hivyo nchi yenu hivi sasa inakabiliwa na njaa, lakini sisi tunaamini viongozi wenu wanajua namna ya kulikabili tatizo hili, tunaamini halitakuwepo tena siku za

usoni.” Hivyo, naamini Waziri Mkuu ataandaa mipango mizuri katika utatuzi wa suala hili.

Mheshimiwa Spika, suala la afya ni muhimu sana kwa wananchi wetu. Vipo vijiji ambavyo havina zahanati za kutoa huduma kwa wajawazito na hata watoto hivyo kusababisha vifo visivyo vya lazima kwa watu wetu. Binafsi napendekeza Serikali wakati inatafuta fedha za kuboresha huduma hii, basi angalau liwepo zoezi la kuwafunza Wakunga wa Jadi kwa kuwapa mafunzo ya kisasa ili kuepusha janga hili.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali katika mipango mizuri ya kupambana na ujambazi, lakini bado naishauri iweke udhibiti katika Kambi za Ukimbizi kwani nahisi ndiko kwenye vyanzo vya upatikanaji wa silaha, kwani zipo tetesi silaha katika Kambi za Ukimbizi zinauzwa kama karanga na katika kiwango kinachohitajika.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ndio Msimamizi Mkuu wa shughuli zote za Serikali, naishauri iangalie sana kwa ufuatiliaji wa barabara za Mjini Dar es Salaam ambaao ni Mji Mkuu (*City*) kwani ni aibu kuona jinsi zilivyo ukilinganisha na hadhi yenyewe kwani Dar es Salaam ni kitovu cha mambo yote ukiachilia mbali ni njia kuu za wageni watokao nje ya nchi na Mabalazi wetu ambaao hutathmini kila kitu, hivyo kupelekea dosari katika mambo tofauti.

Mheshimiwa Spika, kupanga ni kuchagua, lazima tuwe na mipango ya sehemu ya kuzikana kwani hivi sasa Kinondoni na Ilala ni dhahiri kumejaa na kusababisha matatizo makubwa ya stara baada ya mwisho wa uhai wa binadamu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuunga mkono hatua ya maamuzi ya Serikali kujenga Chuo Kikuu Dodoma. Maamuzi hayo ni muhimu sana ukizingatia hali halisi ya Jiji la Dar es Salaam lilivyo hivi sasa. Pia, napenda Taasisi zote mpya basi maamuzi yatumike kibusara kuja kujengwa Dodoma,

Mheshimiwa Spika, mwisho, namuomba WaziriMkuu kwa kuwa ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, basi awe na ofisi ndogo Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, naomba tena niunge mkono hoja. Ahsante.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Lowassa (Mbunge), Waziri wa Nchi katika Ofisi hiyo, Mheshimiwa Juma Akukweli (Mbunge) na Waheshimiwa Manaibu Waziri wote wawili kwa kutuletea hotuba safi yenye mwelekeo katika utendaji wa Awamu ya Nne ya Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi mpya.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu katika hotuba hii nauelekeza zaidi katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Hapo awali kabisa mwaka 2002 nilileta swalii katika Wizara hiyo kutolipwa fidia wananchi wa Vijiji vya Miwale, Rukohe, Mpanyani, Mihima, Mkang’u na kadhalika, wakati walipohamishiwa maeneo

mapya baada ya eneo lao kufanya Hifadhi (*Makonde Plateau Forest Reserve*) na baadaye eneo hilo kuharibiwa na mafuriko yaliyotokea mwaka 1990.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, wenzao wa Kijiji cha Majembe, Tarafa ya Lulindi walilipwa fidia hiyo. Wanavijiji katika vijiji vitano nilivyovitaja hawajalipwa mpaka leo fidia ama kifuta machozi. Huu ndio msingi wa swali langu hapo mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, kuanzia wakati huo mpaka leo hakuna jawabu lililopatikana lenye maana. Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Mizengo Pinda analifahamu suala hili vyema kwani ndiye aliyenijibu swalii al msingi. Tulikubaliana kuwa wananchi hawa walipwe kifuta machozi badala ya fidia, kwani fidia ingekuwa kubwa sana na pengine kuzua mizozo ya aina hii sehemu nyingine nchini. Tulionana pia na Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib (Mbunge), ambaye alishauri kuwa TAMISEMI ileté orodha ya waathirika ili Wizara ya Fedha ifanye taratibu za kulipa kifuta jasho. Kazi ya kutayarisha orodha walipewa TAMISEMI ambao mpaka leo naamini hawajakamilisha kazi hii kwani mimi sijaona.

Mheshimiwa Spika, mimi kama mwakilishi wa wananchi hawa nimekwenda mara nyingi ofisi ya *DC* Masasi na *RC* Masasi kufuatilia jambo hili, lakini sijapata mafanikio ya kuridhisha. Suala hili nililipeleka pia katika Kamati, ilimwagiza *RC* wa Mtwara akamilishe orodha ya waathirika ili TAMISEMI ipeleke Hazina kwa ajili ya malipo ya kifuta machozi. Sielewi kinachoendelea mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, walileta suala hili kwa Waziri Mkuu ili aingilie kati wananchi hawa waweze kulipwa kifuta machozi chao. Tulikuwa tumefikia mahali pazuri ambapo kinachotakiwa ni orodha ya majina ya waathirika kwani Hazina wanaisubiri ili walipe.

Mheshimiwa Spika, wananchi wamechoshwa na ahadi hii ambayo sasa inakuwa kitendawili. Walipata *Bush Lawyer* ambaye aliwaahidi kupeleka shauri hili kwenye Tume ya Haki za Binadamu na Utawala bora, kwa bahati nzuri walikubaliana nami kuwa hiyo haingekuwa busara waniachie mimi mwakilishi wao ili nimalize suala hili na Serikali. Wapinzani nao walikuja juu ili wapate manufaa kisiasa, lakini nguvu za hoja yangu pamoja na imani waliyonayo wananchi kwangu na kwa CCM, wapinzani hawa hawajafanikiwa, sasa nimeacha fukuto la baadhi ya wananchi kupeleka shauri Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Spika, hakuna sababu ya kufikishana Mahakama Kuu, suala lenyewe ni la urasimu tu. Serikali ilikwishakubali kuwapa wananchi hawa kifuta machozi, kinachochelewesha ni TAMISEMI kukamilisha orodha ya waathirika na kuipeleka Hazina ili walipwe. Wananchi wamekubali walipwe walau kifuta machozi badala ya fidia.

Mheshimiwa Spika, naomba suala hili likamilike katika kikao hiki cha Bajeti kinachoendelea. Naunga mkono hoja ya Waziri Mkuu, namuomba kwa kutumia vyombo vyake, suala hili la miaka mingi (toka 1990) sasa likamilike na ikiwezekana atoe

ahadi Bungeni ili wananchi wa Rukohe, Miwale, Mpanyani, Mihima na Mkang'u waendelee kuwa na imani na CCM na Serikali yake.

MHE. GIDEON A. CHEYO: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia ndani ya Bunge lako Tukufu kwa awamu hii ya nne, napenda kwanza kutoa pongezi nydingi kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Amani Abeid Karume na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa ushindi mkubwa wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005. Aidha, nawapongeza sana kwa uongozi wao mahili ambao wamekwisha uonyesha tangu washike madaraka yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na nawapongeza wasaidizi wake wote kwa utekelezaji wao mzuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika maeneo machache. Kwanza, napenda kuipongeza Serikali katika ujumla wake kwa kushughulikia suala la ukame na upungufu wa chakula vizuri na kuepusha maafa kwa wananchi katika maeneo husika. Ili kujiepusha na janga la ukosefu wa chakula nchini, nashauri Serikali iendelee kuwa makini zaidi kushirikiana na wananchi kuanzia ngazi ya Taifa hadi kijijini kuchukua hatua zifuatazo: -

- (i) Kuelekeza nguvu zaidi katika meneo yenyewe uwezo wa kuzalisha mazao ya chakula kwa wingi ili kupata ziada ya kusambaza katika maeneo yenyewe upungufu wa chakula.
- (ii) Kuchukua hatua madhubuti za kuendekeza kilimo cha umwagiliaji na kuongeza bajeti katika eneo hili mwaka hadi mwaka.
- (iii) Kuboresha na kufufua hifadhi ya mazao ya chakula kuanzia ngazi ya Taifa hadi ngazi ya kaya ili kujitosheleza kwa chakula wakati wote.

Mheshimiwa Spika, pili, naipongeza Serikali kwa mpango wa *MMEM* na *MMES*. Pongezi maalum kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa changamoto yake ya kuhimiza ujenzi wa shule za sekondari nchini. Changamoto hiyo imetuwezesha kukamilisha ujenzi wa shule za sekondari tano katika kipindi cha miezi mitano iliyopita. Tatizo ni upungufu wa walimu. Deni sasa ni kwa Serikali kutimiza wajibu wake wa kuhakikisha walimu wa kutosha wanapatikana.

Tatu, napenda kuikumbusha TAMISEMI ombi la Wilaya ya Ileje kuhusu mgawanyo wa Tarafa na Kata. Ombi letu ni kuzigawa Tarafa mbili zilizopo za Bulambya na Bundali kuwa Tarafa nne na kupewa majina ambayo hayana hisia ya ukabila kama ilivyo sasa. Pia, lipo ombi la Kata mpya ya Kalembo ambalo liliwasilishwa miaka mitatu iliyopita, tunasubiri idhini ya Serikali. Maombi yote haya yanazingatia hali halisi ya kijiografia ya Wilaya yetu. Naomba kutumia nafasi hii kumuomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi (TAMISEMI) aje Ileje ili apate maelezo ya kina na kuona mazingira yalivyo.

Nne, tunaishukuru *TANROADS* kwa jitihada za kushughulikia barabara za Mkoa katika Jimbo langu. Hata hivyo, kutokana na mvua nyingi za msimu huu, tunaomba hatua za ziada zichukuliwe kutengeneza barabara hizo. Aidha, napenda kuikumbusha Serikali (Miundombinu) ombi letu la kuipandisha hadhi barabara ya kutoka Mpemba (Mbozi) hadi Isongole (Ileje) iwe ya Kitaifa na iwe kwenye mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami. Barabara hii inaunganisha nchi yetu Tanzania na nchi jirani ya Malawi. Ombi hili linazingatia mwelekeo wa Kitaifa kwa barabara zote zinazounganisha nchi yetu na nchi jirani kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia kwa kushauri kwamba utumishi wa umma uendelee kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa. Viongozi na watendaji wasisubiri kushtuliwa na kuagizwa. Tujipushe na utendaji wa hofu. Tuwajibike na kufurahia kazi zetu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja.

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia maeneo yafuatayo katika hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, ningependa nipate ufanuzi kuhusu mpango wa MMES. Wananchi walihamasishwa sana na shule nyingi zilijengwa ili wanafunzi waanze shule kwa mwaka wa elimu 2006. Hadi sasa fedha zilizoahidiwa hazijatolewa hata senti moja. Je, tatizo ni nini? Mpango huu bado upo? Kama upo, fedha hizo sasa zitatolewa lini ili kukamilisha majengo na madarasa yaliyokuwa yakamilike Januari 2006 pamoja na majengo mapya kwa ajili ya mwaka 2007?

Mheshimiwa Spika, ningependa Ofisi ya Waziri Mkuu iingilie suala la *WEO* wa Kansay, Wilaya ya Karatu Bwana Samson. Bwana Samson alipelekewa na wananchi na Mwenyekiti wa Kijiji mtu aliyembaka mwanamke ambaye walimkamata *ready handed*. Alipopelekewa *WEO* kama mlinzi wa amani akawatukana wananchi na baadaye akafanya mpango wa kumtorosha mbakaji. Hadi sasa mbakaji hajapatiwana. Jitihada za Baraza la Madiwani kumtaka *DED* kama mamlaka ya kumchukulia hatua *WEO* huyo zimegonga ukuta. Kwa vile suala la kubaka ni zito, tunaomba Serikali isaidie kumchukulia hatua za kinidhamu *WEO* huyo iwapo hatua za kisheria zimeshindikana.

Mheshimiwa Spika, wakati wa hotuba ya Rais nilieleza tatizo la Hakimu wa Mahakama ya Eudabash na Hakimu Shayo wa Mahakama ya Mwanzo Karatu. Wote wawili wanatuhumiwa kwa rushwa, kutoa hukumu bila kufuata sheria na hata Mawakili wa *Legal and Human Rights Centre* waliofutilia kesi na hukumu kadhaa zimeonyesha hivyo. Wizara husika iliahidi kufuutilia, lakini hadi sasa hakuna taarifa wala hatua iliyochukuliwa na Mahakimu hao ndio kwanza wamezidisha ukiukwaji huo. Nina nia ya kutoa Shilingi wakati wa vifungu iwapo sitapata maelezo ya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali kutenga Shilingi milioni 500 kwa ajili ya kila mkoa ili kusukuma miradi ya kujenga ajira kwa vijana ni nzuri.

Hata hivyo ninapenda kushauri kuwa, kuweka fedha hizo benki mkoani kutawanyima nafasi vijana wengi wa vijiji nafasi na uwezo wa kupata fedha hizo. Uzoefu wa *SIDO* ulionyesha kuwa Mkoa uko mbali sana na wadau na matokeo yake wale wenye uwezo na uzoefu tu ndio watakaonufaika na Mfuko huo ambao si walengwa hasa.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kuwa, fedha hizo zipelekwe kwenye Halmashauri ambako tayari kuna uzoefu wa mikopo kwa vijana ila tatizo lilikuwa mkopo ni mdogo sana. Mfumo huo wa Halmashauri ukiwezeshwu zaidi, wahusika wakapewa mafunzo ya uendeshaji wa Mifuko ya aina hiyo na mikataba kuimariswua, nina hakika tutawafikia vijana wengi zaidi bila urasimu; tutakuwa karibu na maeneo ya *Local investments* za size ya wahusika na tutapata *multiplies effect* zaidi.

Naomba tufanye utafiti wa kina wa namna ya kuendesha Mfuko huo kuliko kuzipeleka benki ambazo Watanzania wengi vijana hawawezi kuzifikia kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani za dhati.

MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS: Mheshimiwa Spika, ufgaji uboreshwe sio kufujwa. Naomba Serikali kupitia kwako Mheshimiwa Waziri Mkuu suala hili lisimamiwe vyema na wafugaji wapewe uwezo kama kupewa sehemu maalum sio kunyanyaswa. Pia, wapewe dawa za wanyama na mambo yote wanayohitaji wafugaji wa kileo kwa wakati tulionao.

Mheshimiwa Spika, afya nzuri inapatikana kwa mazingira mazuri na Mheshimiwa Waziri Mkuu amelisemea sana suala hili la afya, nami nampongeza sana na ninaungana naye.

Namwomba sana chini ya Ofisi yake na Serikali kuiboresha Wizara ya Afya kwa majengo bora, madaktari wazuri, wauguzi, dawa na vifaa vya kileo na mazingira mazuri ya kufanya Tanzania ya leo Visiwani na Bara chini ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Halmashauri za Wilaya, naomba ziwezeshe sana ili ziweze kufanya maendeleo ndani ya sehemu zake, pia Serikali za Mitaa, Vijiji vipewe uwezo na kusimamiwa na Wilaya, Mikoa kama ilivyo Serikali Kuu inavyojitahidi kutaka maendeleo Tanzania nzima kutaka kupata maisha bora kwa kila mtu au Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira kwa vijana, bado ni tatizo kubwa Tanzania kwa ukosefu wa ajira kwa wenye elimu na wasio na elimu. Wote ni vijana wa Tanzania na kila kijana au mtu tunahitaji michango na nguvu zao wala hatuna mahali pa kumpeleka au kuwagawa isipokuwa ni wetu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali sasa kwa makusudi ilione na kutafutia njia ya muhimu ili tuepukane kwa vijana wetu na ujambazi, wizi, uhuni na kadhalika na wawe watumishi bora na walete maendeleo ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nauga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. BAHATI ALI ABEID: Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwapongeza wale wote walioteuliwa katika nyadhifa mbalimbali katika Chama chetu cha Mapinduzi hivi karibuni. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri, pia ninawashukuru watendaji wote walioshiriki kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu na mazingira. Ni kweli uchafuzi wa mazingira upo na kwa kiasi kikubwa tukijipanga vizuri tunaweza tukapiga hatua. Hii ni kwamba, kila Kijiji kionyeshe mikakati yake ya kupambana na mazingira. Lakini katika nchi yetu tunao wakimbizi na wakimbizi ni wachafuzi wakubwa wa mazingira ya ukataji wa miti.

Mheshimiwa Spika, ninamuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na watendaji wake waende Kigoma, waende wakashuhudie mamia ya mahekta ambayo yamekatwa miti na mpaka mizizi imeng'olewa. Hata ule uoto wa zamani wa asili hauwezi kuota tena, hii ni mbaya zaidi. Nenda Mkoa wa Rukwa kule Mpanda kuna wakimbizi walidumu pale kwa kiasi cha miaka inayozidi thelathini, sasa wanachokifanya ni kwamba, kuna miti mingi ambayo haifai kwa matumizi ya mba, wakimbizi wanakata miti hiyo na badala yake hupata mashamba ya kulima muhogo na baada ya miaka miwili huacha shamba hilo na kukata miti mingine ili apate penye rutuba. Hivi Serikali haijui kuwa wakimbizi hawa wanatumiza sana kwenye mazingira?

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali ifanye mazungumzo na hawa wafadhili amba ni Mashirika yanayoshughulikia wakimbizi kabla hawa wakimbizi hawajaondoka kurudi makwao, basi waweze kutusaidia upandaji wa miti katika maeneo hayo niliyoyataja tena wawashirikishe wakimbizi hao kupanda miti hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu ya juu, wanafunzi wetu wa elimu ya juu huwa wanaomba mikopo na Serikali imepiga hatua kwa kuwapatia wanafunzi hao mikopo hiyo, lakini mikopo hiyo inavyotolewa haitolewi kwa uangalifu kwani hucheleva kufika kwa wakati unaohitajika na hii husababisha kumbabaisha, yaani kumtia hofu mwanafunzi juu ya uendelezaji wa masomo yake. Lakini pia kwa kuwa Serikali imeamua kumkomboa mwanamke, basi maombi ya mikopo ya elimu ya juu yanapoletwa hebu tuwekeni kipaumbele wanawake ili ile azma ya Serikali ikamilike na wanawake wajue kweli Serikali inawajali sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninaunga mkono hotuba hii mia kwa mia.

MHE. BAKAR SHAMIS FAKI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia na kuwa na afya njema na kuniwezesha leo hii kuchangia walau kidogo kuhusiana na hotuba ya Waziri Mkuu juu ya mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwashukuru wapigakura wa Jimbo langu la Ole, kwa kunipa ridhaa yao kwa mara ya pili kuwa Mbunge wao kwa kipindi cha 2005 - 2010.

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la kupanda bei ya mafuta nchini kwa kupanda bei ya bidhaa hiyo katika Soko la Dunia. Pamoja na kwamba bei ya mafuta imepanda, lakini inaelekea wafanyabiashara wanaitumia fursa hiyo kupandisha bei bila kulingana na uwiano wa bei ya Soko la Dunia. Ni vyema sana Serikali kuitia Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji kuwa macho na wafanyabiashara wa aina hiyo maana wanachojali ni kupata faida kibao (*super profit*).

Mheshimiwa Spika, suala la matumizi ya simu za mkononi si suala la anasa. Sote tunajua kwamba simu imekuwa ni kichocheo kikubwa cha maendeleo kwani wafanyabiashara wadogo wadogo ambao hawawezi kumudu kusafiri kwenda huku na huko wanaweza kuwasiliana tu na mambo yao yakaenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana leo hii Watanzania ambao wengi wao hawatimizi milo miwili kwa siku, wanaambiwa kwamba ushuru wa huduma za simu umepandishwa kutoka asilimia 5 hadi kufikia asilimia 7, kweli hivi Tanzania tumekusudia kuondoa umaskini au tunaupalilia umaskini?

Mheshimiwa Spika, Serikali imepandisha ushuru wa huduma za simu eti kwa kukabiliana na asilimia 10 ya nchi za Kenya na Uganda, lakini mbona Serikali haikueleza vipato vyetu Watanzania kama vinakaribiana na vile vya Wakenya na Waganda? Je, *exchange rates* za Tanzania zinakaribiana na zile za Kenya na Uganda? Na ongezeko la thamani (*VAT*) za nchi hizi zinakaribiana?

Mheshimiwa Spika, kodi ya ongezeko la thamani (*VAT*) kule Kenya ni asilimia 16 wakati kule Uganda ni asilimia 18 na ni hakika *exchange rates* zetu hazilingani na za kwao. Sasa itakuwaje tujilinganishe na sisi? Ni vyema Serikali itafute vyanzo vingine zaidi au kpandisha kodi katika mambo ambayo hayana athari sana kwa wananchi kama vile ulevi, mambo ya anasa na kadhalika. Kwa hivyo basi, tunaitaka Serikali kama hakuna uwezekano wa ushuru huu wa huduma za simu kufutwa, basi angalau ushuke hadi kufikia asilimia 3 au 4 au kama hapana budi kabisa, basi ibakie ile ile asilimia 5.

Mheshimiwa Spika, mazingira ya siasa hasa katika Uchaguzi Mkuu hayajawa safi na yenye mlingano sawia. Pamoja na kuwa Serikali inadai kwamba vyama vilipewa nafasi ya kujinadi kwa wananchi, lakini kwa baadhi ya maeneo jambo hili halikuwepo kabisa. Baadhi ya Majimbo hasa ya Zanzibar wagombea wa Ubunge wa Vyama vya Upinzani hawakupewa nafasi ya kujinadi kwa wananchi, mfano Jimbo la Donge kule Mkoa wa Kaskazini Unguja, hata siku moja kati ya muda wote mrefu wa kipindi cha Kampeni Vyama vya Upinzani kikiwemo Chama cha Wananchi (*CUF*) hakikuruhusiwa kwenda kule na kufanya kampeni zake.

Mheshimiwa Spika, kama hilo halitoshi, baadhi ya maeneo hasa yale ambayo Vyama vya Upinzani vinaungwa mkono, kwa kweli ilikuwa ni pata shika nguo tatua.

Vyombo nya dola vilitumia kuwachapa na kuwanyanya wa pigakura kama vile wao hawana haki ya kuchagua na kuchaguliwa.

Mheshimiwa Spika, kila mmoja wetu tunapenda kuona Muungano wetu kati ya Zanzibar na Tanganyika unanawiri, unaendelezwa na hatimaye unadumu. Lakini inakera mno kuona (watu) au Serikali mbili zilizoungana kuleta umoja wa kweli kama unavyoongeleta, lakini sehemu moja ya Muungano huo unaulalia upande mwingine. Mimi nashangaa kwa hii asilimia 4.5 ya misaada ya nje kwa Serikali ya Muungano inayopelekwa Zanzibar! Mimi najiuliza, hivi ni *formula* gani iliyotumiwa katika kupatikana tarakimu hii? Hivi asilimia hii ya 4.5 si sawa na kasoro ya asilimia ya Mkoa mmoja tu?

Mheshimiwa Spika, ipo haja kubwa sana ya pande hizi mbili katika jitihada za kuimarisha Muungano kulipa angalizo maalum suala hili vinginevyo itakuwa upande mmoja wa Muungano hautendewi haki inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. DR. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu kuhusu wafugaji, utendaji wa mikataba pamoja na ujenzi wa shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri, ya busara na inayojenga matumaini kwa wananchi na viongozi pia. Nawapongeza Mawaziri na viongozi walio chini yake.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza vile vile kwa kuelekeza na kuhimiza mikataba ya utendaji ndani ya Serikali hususan Serikali za Mitaa. Utendaji wa matokeo unahitaji mikataba na vile value for money will be realized.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuelekeza wafugaji walioondolewa kutoka katika vyanzo nya maji, milimani na maeneo owevu kupatiwa maeneo mbadala ili nao haki yao ya *survival* ihakikishwe kuwepo. Kama hatua ya kudumu, kila Wilaya yenyeye mifugo itenye maeneo ya wafugaji kama Wilaya ya Chalinze ilivyofanya. Huduma zaidi za mifugo kama maji, dawa na masoko ziimarishe.

Pengine ni vyema Kamati ya Mazingira iwashirikishe wafugaji kuhusu ujenzi wa Shule za Sekondari, sasa hivi wananchi kwa kushirikiana na Serikali wamejenga madarasa, nyumba za walimu na matundu ya vyoo machache hivyo inabidi tuwe na mipango kabambe ya kukamilisha ujenzi wa shule hizi katika mwaka huu na miaka michache ijayo ili tusijifikishe mahali ambapo wanafunzi kadri wanavyoendelea na madarasa ya juu wakakabiliwa na uchache wa madarasa, nyumba za walimu na matundu ya vyoo. Napendekeza kila Halmashauri itoe mpango wa ujenzi wa shule zilizosajiliwa kwa kuonyesha fedha zitakazotumika zikishirikiana na Wizara ya Elimu na wananchi. Nina wasiwasi kuwa shule nyingi zitakuwa *half-done*.

Mheshimiwa Spika, namtakia Waziri Mkuu kila na kheri, ninashukuru na kuwasilisha.

MHE. ERNEST G. MABINA: Mheshimiwa Spika, naomba kuanza kwa kuunga mkono hoja hii ya Waziri Mkuu kwa asilimia mia moja. Pia, nimpongeze Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri aliyoiwasilisha kwa niaba ya Wizara yake, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Asasi zilizo chini yake na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, katika kuipitia bajeti hii kuna mengi yamenigusa kama ifuatavyo: -

Kwanza, Wilaya yetu ya Geita ina idadi kubwa sana ya watu. Ukichukulia sensa ya mwaka 2002, Geita ilikuwa na watu zaidi ya laki saba. Hadi kufikia sasa nina imani kuwa tumefikia laki nane. Lakini tatizo kubwa ni kwamba kuna hospitali moja na vituo vya afya vinne tu. Vituo hivi havitoshi kabisa. Ninaiomba Serikali itusaidie kutuunga mkono kuimarisha vituo vya Kasamwa, Nzera, Katoro na Bukoli.

Mheshimiwa Spika, pili, hakuna gari la kubeba wagonjwa na katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nimesikia kuwa kuna magari kumi ya kubebea wagonjwa. Naomba sana gari moja tupatiwe Hospitali ya Wilaya ikizingatiwa kuwa jiografia ya Wilaya yetu ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004 Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, wakati akiwa Waziri wa Mambo ya Nje, alitusaidia kupata gari la wagonjwa kutoka Ubalozi wa Korea aina ya *KIA*. Gari hili limeshindwa kuhimili mikikimikiki ya barabara zetu hivyo hadi sasa Wilaya yetu haina gari kabisa. Kutokana na umuhimu wa Wilaya hii na idadi kubwa ya watu wanaongezeka siku hadi siku, naomba kati ya magari hayo kumi, angalau moja basi lije Geita.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Geita kama Miji mingine ina idadi ya watu zaidi ya 50,000 lakini tatizo lililopo hapo ni maji. Idadi kubwa ya wananchi hawa haipati maji safi, wanachota maji kwenye mabwawa na visima vifupi. Kwa mantiki hiyo, ni wananchi elfu 5 tu ndio wanaopata maji safi na salama. Hii ni asilimia kumi tu.

Naomba na nazidi kuiomba Serikali yetu ya Awamu ya Nne, waifikirie Wilaya hususan Mji wa Geita upate maji kutokea Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama ulivyonieleza na ahadi ulizokuwa umetupatia wakati ukiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kuwa Mji wa Geita ungepata maji ifikapo mwaka 2005, lakini hadi sasa hakuna maji, tatizo ni kuokoa wananchi kutokana na baa la njaa. Napenda kuipongeza Serikali kwa kutatua tatizo hili kwa makini. Tumefanikiwa upande huo, lakini ujue kuwa miradi uliyoianzisha na kuahidi mingine kama maji mjini Geita imekwama. Kama imekwama, kwa umakini ninaoujua na

ufuatiliaji wa masuala mbalimbali huwa hushindwi labda uanzie kwetu Geita kukosa maji.

Mheshimiwa Spika, najua kabisa Mradi wa Maji Geita ni wa gharama kubwa sana unakadirwa kama Shilingi milioni 17. Hivyo basi, utuone nasi kwamba tunahitaji huduma kama hii muhimu kulingana na Watanzania wenzetu. Tunaona aibu wawakilishi wa wananchi hapa Bungeni, Wilaya yetu kutolewa mfano wa umaskini na kuonewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, nitashukuru sana kama haya yatakelezwa au kutiliwa maanani katika bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. FETEH SAAD MGENI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa sina budi kutoa pongezi zangu za dhati kabisa, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Bumbwini, kwa ushindi wa kishindo alioupara Rais Jakaya Kikwete. Aidha, Mkutano Mkuu wa CCM wa tarehe 24 hadi 25 Juni, 2006 kumchagua kwa kishindo kikubwa kuwa mwenyekiti wa CCM Taifa. Pia, sina budi kwa moyo wa furaha na upendo kumpongeza Rais wa Zanzibar kwa ushindi mkubwa alioupara katika Uchaguzi Mkuu uliopita.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa mchango wangu katika maeneo machache.

Kwanza ni kuhusu elimu. Elimu ni ufunguo wa maisha, elimu ni nuru au ni mwanga wa maisha ya binadamu wote. Viongozi wetu wakuu kwa pamoja wanazungumzia kuimarishe elimu kuanzia Msingi, Sekondari na hata Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, umaskini mkubwa ni kukosa elimu, kwa maana hiyo lazima viongozi wetu pamoja na wananchi tuwe pamoja katika kampeni ya elimu na Serikali kusaidia kwa kila kinachowezekana. Umefika wakati sasa kila Mkoa uwe na Chuo Kikuu chake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya uchumi, Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango, wote hotuba zao zilitueleza kuimarike vizuri kwa uchuni wetu. Ni jambo la kufurahisha na kutupa matumaini viongozi na wananchi wote. Lakini bado tunaomba kusisitiza kwamba nyanja zote zinazovujisha uchumi wetu, kodi na vinginevyo, ninaomba zizibwe.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amelingumzia sana suala la hali mbaya ya uchumi wa Zanzibar. Huo ndio Muungano wa kweli na ndio unaopaswa kutiliwa maanani, kwani Zanzibar haina uchumi mkubwa zaidi ya karafuu. Duniani kote sasa inajulikana kwamba karafuu hazina bei na nchi ya Indonesia sasa imepunguza sana kununua karafuu kutoka Zanzibar. Indonesia sasa wanavuna karafuu zao wenyewe. Kama ndugu wawili, sasa imefika wakati ndugu mkubwa amsaidie mdogo wake kwa hali na mali ili kuvunja wale wakorofu wa Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukubali kwamba hali ya ulinzi na usalama mipakani mwetu ni nzuri na utulivu wa nchi pamoja na kupungua kwa kiasi kikubwa hali ya vurugu la majambazi, bado nashauri kutilia mkazo wa hali ya juu zaidi juu ya ulinzi wa nchi yetu. Vyombo vyetu vya ulinzi ni lazima tuongeze bidii katika kuviwezesha, tuendelee kuvipatia zana mbalimbali za ulinzi wa uhakika pamoja na kuwa hali yetu ya uchumi bado haijawa nzuri, lakini tuwe tayari kununua amani na utulivu wa nchi kwa bei yoyote.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Bumbwini, tunaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa asilimia mia moja. Ahsante.

MHE. AMEIR ALI AMEIR: Mheshimiwa Spika, naomba kumpongea Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Mwenyekiti wa CCM. Pia, niwapongeze Wabunge walioteuliwa kushika nafasi mbalimbali za uongozi katika CCM.

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ifuatavyo: -

Kwanza ni kuhusu dawa za kulevyta. Dawa hizi ni tatizo kubwa na lina mtandao mkubwa sana unaolingana au kuliko mtandao wa majambazi. Mtandao huu unahatarisha maisha ya vijana wetu wadogo ambao ndio tegemeo la kesho.

Pia, mtandao huu ndio mama wa maasi yote yanayofanyika nchini na duniani kote. Ninaishauri Serikali kuweka mikakati ya kulishughulika suala hili kama tulivyoshughulikia suala la ujambazi ambao sasa umepungua. Majambazi yanatumia silaha na kuua ili wafanikishe walilolikusudia, lakini mtandao huu wanatumia fedha nyingi wakati wanapopitisha na wakati wanapokamatwa na bidhaa hii haramu katika vyombo vilivyowekwa kushughulikia uzuaji wa dawa hizi kuanzia bandarini, viwanja vya ndege, polisi na mahakamani na ndiyo maana kesi haziendi na ushahidi haukamiliki wakati mhusika kakamatwa na bidhaa hiyo na inaonekana.

Mheshimiwa Spika, waagizaji na maajenti wakuu wanajulikana, lakini hali ndiyo hiyo. Mkakati wa kukomesha dawa unataka uwe wa mbinu za hali ya juu. Kwa hiyo, kuna haja ya kuongeza vifaa vya kuangalia mizigo, pia wafanyakazi wa maeneo hayo wasikae mahali pamoja kwa kipindi kirefu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Muungano, nazishukuru Serikali zetu mbili kwa uamuza wa kukaa kwa makusudi kutafuta ufumbuzi wa vipengele ambavyo vinaonekana vina kasoro katika Muungano wetu ambao ni wa kupigiwa mfano barani afrika na duniani kote. Naomba mijadala hii iendeshwe kwa njia ya kidiplomasia na siyo kwa jazba kwani ndugu hawagombani bali kufahamishana na kuelewana kwa sababu lengo ni mahusiano mema.

Mheshimiwa Spika, kuhusu shughuli za uchaguzi, pamoja na matatizo mengi yaliyoelezwa hasa katika Kambi ya Upinzani kuhusu uchaguzi, sina budi kuzipongeza Tume za Uchaguzi za NEC na ZEC kwa kazi ngumu na kubwa walizofanya kwa kufanikisha uchaguzi ambao ndio uliotufikisha hapa kwa kushinda katika uchaguzi huo na Marais wamepatikana kwa kupata kura halali kabisa. Pia, niwapongeze Wabunge wenzetu wa Kambi ya Upinzani kwa kukubali matokeo na kukubali kuwa Rais Kikwete ni Rais wa nchi hii na ushirikiano walionao na Wabunge wa CCM kwa lengo la kujenga nchi yetu kwa manufaa ya Watanzania wote. Lakini pia nina masikitiko makubwa kwa upande wa Zanzibar, Wapinzani hawaitambui Serikali. Suala hili ni la kuvunja moyo na kurejesha nyuma maendeleo ya nchi na inaonyesha ni mpango wa makusudi ulioandalialiwa kwa kuvuruga Utaifa wetu na kujaribu kuipaka matope nchi yetu. Lakini ninaziomba Serikali zetu zisije tetereka kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, hali hii imejitokeza kwa kuwa mtu fulani hakushinda uchaguzi na kuanza kushawishi wenzake wasiitambue Serikali na Rais. Watu hawa ndio wale waliozungumwa na Mheshimiwa mmoja kuwa kuna watu wanataka wawe wao tu! Inafaa wadhibitiwe mapema wasije wakatutia katika matatizo na kuondosha amani na utulivu wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante, ninaomba radhi kama kuna kosa nimelifanya katika mchango wangu. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa (Mbunge), kwa hotuba nzuri na yenyewe mwelekeo na dhamira.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya CCM imeonyesha wazi majukumu makuu ya msingi kwa Awamu hii ya Nne. Kwanza, ni kuitoa Tanzania kutoka kwenye dimbwi la uchumi ulio nyuma na tegemezi na kuiingiza katika mkondo wa uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea na pili, kuwashirikisha wananchi wote kwa njia ya uwezeshaji katika ujenzi wa uchumi na kuutokomeza umaskini.

Mheshimiwa Spika, naamini sana iwapo mikakati ya utekelezaji wa majukumu hayo itatekelezwa vizuri, basi Tanzania tajiri inakuja, kwa kipindi cha miaka 20 tiliyojiwekea katika Dira ya Maendeleo ya Tanzania tayari tutakuwa nchi tajiri. Kwa maana nytingine na kwa kifupi ni kuwa, nchi yetu imejikita katika vita dhidi ya umaskini kwa awamu hii ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, napongeza sana Serikali kuhimiza wananchi wapambane na umaskini. Nashauri njia zifuatazo zitumike ili kuhamasisha wananchi wote washiriki vita dhidi ya umaskini: Kuwepo na mradi wa kuelimisha jamii juu ya MKUKUTA na malengo yake matatu yaani (i) kuongeza kipato kuboresha uchumi, (ii) kuboresha ustawi wa jamii na (iii) uwajibikaji na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, mradi huu ungesaidia sana katika kuzifanya familia/kaya na mtu mmoja mmoja kushiriki na kutekeleza malengo ya MKUKUTA na hivi kama kila mtu angeongeza kipato, angeboresha ustawi wa familia yake na angewajibika na kuwa na Utawala Bora, basi Taifa lingekuwa limetimiza malengo ya MKUKUTA ifaavyo na hivyo kuendelea.

Mheshimiwa Spika, MKUKUTA hautekelezwi katika ngazi ya familia. Wananchi wanajua MKUKUTA katika *MMEM*, *MMES* zahanati, barabara na kadhalika. Lakini haya yote ni kuondoa umaskini usio wa kipato. Tatizo kubwa ni namna ya kuondoa umaskini wa kipato na hii ni lazima kila mwananchi afanye kazi na aongeze uzalishaji, ndipo kipato kitaongezeka.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kwa kupeleka kwa kila Mkoa Shilingi milioni 500. Hii ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu kila ukurasa ametambua na kutamka wazi kuwa kuna vikundi vya uzalishaji mali mfano ukurasa wa 37, 38, 39, 50 na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, vikundi hivi havitambuliki na Mabenki yetu na Asasi nyingine za Fedha, hivyo hawasaidiwi. Naomba kutoa mfano wa vikundi 131 vya uzalishaji mali, vikundi vya *VICOBA* havitambuliki hivyo havisaidiwi moja kwa moja na Serikali na Asasi za Fedha.

Naomba kushauri Serikali iandae utaratibu wa kuvisajili vikundi hivi katika ngazi ya Halmashauri ili vitambulike kama Mheshimiwa Waziri Mkuu anavyovitambua. Wakurugenzi wa Halmashauri wapewe jukumu hilo la kuvisajiri na hii itasaidia sana kutambua makundi mbalimbali ya wananchi yaani wakulima, wafanyabiashara, wavuvi na kadhalika, hivyo itakuwa ni rahisi kupeleka mitaji, misaada hata utaalam katika vikundi kisekta na hii itatusaidia tunaposema mkulima tutajua ni nani, yupo wapi na analima nini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Programu ya Uendelezaji wa Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo, napongeza sana Serikali kwa kubuni programu hii muhimu kwa wananchi. Programu hii ina matatizo kidogo katika utekelezaji wake.

(i) Mawakala wanaotekeliza *program* hizi wana majina yao, hivyo *program* haileleweki vizuri kwa wananchi. Watu wanaita miradi hii majina ya mawakala mfano Songea, wananchi wanaita mradi wa *Technoservice*, *Daipesa* na kadhalika.

(ii) Mawakala wa miradi hii hawawajibiki katika vikao vya Serikali mfano *RCC, Full Council* na kadhalika. Hivi ni kwa namna gani Serikali itasimamia na kutathmini utekelezaji wake?

(iii) Nashauri mawakala wawajibike moja kwa moja katika Halmashauri na Mkoa ili wananchi waelewe vizuri miradi hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uendelezaji wa viwanda, nia ya Serikali katika kuendeleza viwanda vya kusindika mazao ya kilimo, naipongeza kwani naamini itaongeza thamani ya mazao hayo, ajira, fedha za kigeni na utaalami. Usindikaji wa mazao kama mahindi ni muhimu hasa kama kiwanda kikijengwa mkoani Ruvuma wananchi watanufaika na ajira, thamani ya zao hilo la chakula itapanda na kulingana na mazao nafuu ya biashara.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Mkoa huu wa Ruvuma umetupa heshima ya uzalishaji mkubwa wa zao la mahindi na kusaidia Mikoa mingine katika Tanzania kwa chakula na hata nje ya nchi. Wakulima wa Ruvuma wakijengewa kiwanda cha usindikaji mahindi wataongeza ari ya kuongeza uzalishaji wa chakula na hivyo nchi yetu haitakumbwa na tatizo la njaa kali.

Mheshimiwa Spika, napongeza sana hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hasa kwa sababu imeangalia wanyonge.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono bajeti kwa asilimia mia moja.

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete; Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kwa kura za kishindo na Mkutano Mkuu wa CCM kuwa Mwenyekiti wa CCM. Nasema hongera sana.

Mheshimiwa Spika, nampongea Mheshimiwa Yusuf Makamba (Mbunge), kwa kuteuliwa na kuwa Katibu Mkuu wa CCM, Mheshimiwa Aggrey Mwanri kuwa Katibu Mwenezi na Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe kuwa Katibu wa *Organization* wa CCM. Hongereni wote pamoja na Mheshimiwa Rostam Azizi na Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, TAMISEMI ina chuo chake Hombolo ambacho kinatoa Maafisa watakoapelekwa katika Halmashauri zetu. Kwa kuwa Chuo cha Mipango ni kimoja nacho kinatoa Maafisa Mipango katika Halmashauri za Wilaya zetu, kwa uzito huo naomba Waziri wa TAMISEMI na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji washirikiane na kuungana kutoa wataalam wote wa Halmashauri za Wilaya. Chuo cha Hombolo kiwe Chuo cha pamoja ili kitoe Afisa Mipango, Utawala na Utumishi, hii itasaidia Chuo cha Mipango kusomesha wanafunzi wengi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ana mamlaka hayo, naomba atusaidie ili vijana wengi wanaomaliza *Form IV* na *Form VI* wajiunge na taaluma nilizozitaja.

Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, anaongoza Serikali sikivu kwa wananchi na Tanzania, tuko pamoja katika usimamizi wake mzuri. Ninamtakia kheri katika kazi zake na Mungu atamwongoza.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono, apewe fedha zote kwa asilimia mia moja.

MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA: Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti mpya wa CCM kwa kura zote kasoro moja tu. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa wote walioteuliwa kuunda Sekretarieti ya CCM ikiongozwa na Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba, (Mbunge).

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Waziri Mkuu wetu; Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa (Mbunge), kwa hotuba yake nzuri sana yenye kutia matumaini makubwa kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, katika utumishi wa umma kuna kanuni ya kudumu inayotoa adhabu kwa watumishi wanaokaa nje ya kituo cha kazi pasi na kutumwa na Serikali kwa zaidi ya siku 60 kwa mwaka. Hivi karibuni Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wao wanaweza kukaa nje ya vituo vyao vya kazi kwa zaidi ya siku 120 kwa mwaka kwa mambo binafsi tu. Naomba Waziri Mkuu kudhibiti hali hii, ili viongozi wa namna hiyo katika Wilaya wakae katika vituo vyao vya kazi na wafanye kazi zao za kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kule Rufiji barabara ya kufika Makao Makuu ya Wilaya, Utete inapitika kwa tabu. Hakika wakati wa mvua haipitiki kabisa, nayo ni Utete – Nyamwage - Daraja la Mkapa - Ikwiriri - Kibiti kilomita 84. Taabu iko kati ya Nyamwage kwenda Utete. Aidha, kuna barabara iliyotolewa ahadi na Mheshimiwa Rais yaani barabara ya Utete - *Utete Ferry* (Pantoni) - Kibiti, urefu km 44 tu. Barabara hii haipitiki kabisa. Ilani ya CCM ukurasa wa 53 (c) inasema kila Makao Makuu ya Wilaya ni lazima yafikike wakati wote. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu asimamie utekelezaji wa (i) Ahadi ya Rais na (ii) Ilani ya uchaguzi 2005 ya CCM ukurasa wa 53 (c).

Kuhusu Makao Makuu ya Rufiji ni Utete. Sasa Utete imepata hadhi ya kuwa Mji Mdogo. Hivi karibuni matukio ya uhalifu, ujambazi, uwindaji haramu na wizi wa nyara za Serikali umezidi na kuripotiwa mara kwa mara. Lakini mpaka sasa Utete haina ofisi rasmi ya Polisi ya Wilaya.

Aidha, kuna uhaba mkubwa wa nyumba za kuishi Askari Polisi mjini Utete. Barua ya maombi haya lilipelekwa kwa Waziri. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaomba asimamie ili Utete Makao Makuu ipate Ofisi ya Polisi ya Wilaya. Aidha, nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakualika utembelee Rufiji.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazopelekwa kwenye Halmashauri zetu kwa ajili ya kujenga barabara za wilayani hazitoshi. Aidha, kuna ubadhilifu mkubwa katika matumizi yake. Kandarasi feki hutolewa na hakuna uhakiki wa mali yaani *value for money*. Maafisa Wakuu katika Halmashauri hizo wanashirikiana na hao makandarasi feki. Nchi nzima barabara za wilayani ni mbovu sana na hii ndio sababu kubwa.

Tunaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aiambie Serikali kuwa kazi ya barabara zote nchi nzima (Wilaya zote) zijengwe na *TANROADS* yaani kuwe na (i) *TANROADS - Trunk Roads* (ii) *TANROADS - Regional Roads* na (iii) *TANROADS - District Roads*.

Pia nzungumzie suala la Madiwani wetu ni nguvu kazi, Madiwani wetu tunawategemea na hawa nao wafikiriwe hata kukopeshwa pikipiki ili mradi ziwasaidie kwenye ufanisi wao wa kila siku kwenye Kata. Kwani, kuna Kata tatu za Jimbo langu, ukubwa wa Kata moja, hata Jimbo la Kibaha ni dogo. Fikiria Diwani huyo atafanyeje ufanisi huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini, pia magari ya Ma-DC yamechoka. Yana nguvu, kasi hayana. Yalijitahidi sana kushughulika na jambo kubwa la uchaguzi. Magari yameishachoka, hivi sasa na wao wapatiwe magari ili waendane na kasi mpya hii tunayokwenda nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu la Chalinze, nasema nalo ni kubwa. Basi pale itakapobidi, Serikali iangalie kwa jicho la huruma pale itakapoona sasa kuna mgawo wa Wilaya, basi Jimbo langu nalo si vibaya likatizamwa kwa jicho la huruma lipate Wilaya. Kama suala la kuona ni jinsi gani vigezo vyta Jimbo la Chalinze kuwa Wilaya, nina imani vigezo vingine vilishakamilika. Lakini kama ni idadi ya watu, basi nitaenda kukaa na wananchi wangu wale nione jinsi gani kuongeza idadi ya watu ili iweze kuwa Wilaya. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, nimalizie suala la kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu kwa jinsi tunavyoshirikiana nao na nawaomba sana wanizidishie kunipa ushirikiano ili niweze kuwatumikia na nawahakikishia sitowaangusha, Mbunge sasa wamepata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja ya hotuba ya Waziri Mkuu kwa zaidi ya asilimia 100. Ahsante sana. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. RICHARD S. NYAULAWA: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri Mkuu kwa matayarisho makini na hotuba nzuri aliyoitoa Bungeni. Hotuba hii imeainishwa barabara na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ambayo ni maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Serikali kutenga fedha za kutosha kwa programu mbalimbali kwa ajili ya kuleta maendeleo na kuinua maisha ya wananchi wanaoishi vijijini. Ili kuleta mageuzi ya kilimo ni lazima kuendesha viwanda vidogo, vyta kati na vikubwa kwa kuwashirikisha wananchi wenyewe kumiliki viwanda hivyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nawasilisha.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ninawapongeza Waziri Mkuu na Waziri wa Nchi, TAMISEMI, kwa kazi nzito wanazofanya, wanadhihirisha umahiri na umakini.

Mheshimiwa Spika, naomba mambo yafuatayo: -

(i) Suala la kupata hadhi ya Mji Mdogo wa Nzega ili iwe Halmashauri ya Mji wa Nzega lipewe uzito unaostahili na hasa katika bajeti.

(ii) Halmashauri mfano ya Nzega kupewa adhabu ya kunyimwa fedha za maendeleo kwa ajili ya hati chafu, kosa ni la watendaji siyo la wananchi, hivyo fedha zilipwe na waliosababisha hati chafu waadhibiwe.

(iii) Napongeza hatua za kulazimisha wachimbaji wa madini (dhahabu) kulipa Halmashauri kodi. Mkazo uongezwe kwa makampuni wabishi, mfano *Resolute* ya Nzega kuchelewa kuilipa Halmashauri.

(iv) Mradi wa maji toka Ziwa Victoria, Awamu ya Pili uzingatie katika tatizo la maji Wilaya ya Nzega (mkazo uelekezwe vijijini).

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, hapo ndio mwisho wa uchangaji kutoka kwenye *floor*. Sasa watakaozungumza ili kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kutoka hii Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kwa mpangilio ufuatao, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, atazungumza kwa nusu saa yaani dakika 30. Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Celina Kombani, atazungumza kwa dakika 15. Hii, sikupanga mimi, hivi ndivyo walivyojipanga. Natangaza tu ili Wabunge waelewe na wasishangae pale inapokuwa kuna tofauti. Ni namna wlivyopanga kulingana na uzito wa hoja zilivyokwenda katika eneo mhusika, Naibu analisimamia au Waziri wa Nchi analisimamia. Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Juma Akukweti atafuatia, ataongea kwa dakika 30 na hatimaye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mheshimiwa Mizengo Pinda, ataongea kwa dakika 45. Hapo tutakuwa tumefika saa 7.00. Sasa namwita Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. LUKE J. SIYAME): Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nichukue fursa hii nami niungane na wenzangu ambao wamekwisha kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Pia, napenda nichukue fursa hii kuwapongeza wale wote ambao wameteuliwa na kuchaguliwa kwa nafasi mbali mbali za Chama chetu cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitakuwa ni mdogo wa fadhila kama wakati huu sitachukua fursa hii kuweza kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye kwa miezi hii sita niliyofanya kazi katika Ofisi yake nimejifunza mengi kwake, nimepata ujasiri kutoka

kwake na ninaamini nitajitahidi kwa uwezo wangu ili niweze kulitumikia hili Taifa vilivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja zilizotolewa na ambazo inabidi nianze kuzijadili, ziko katika makundi matano, hoja ya kwanza ni kuhusu chakula cha njaa, hoja ya pili ni dawa za kulevyo, hoja ya tatu ni Tume ya UKIMWI na UKIMWI wenyewe, hoja ya nne inahusu walemaruvu na hoja ya tano Programu ya Uendelezaji wa Mfumo wa Masoko ya Mazao ya Kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuanza, Mheshimiwa John Malecela Mbunge wa Mtera alitaka Serikali iongeze akiba ya chakula, *SGR*, kwani kiwango cha sasa cha tani 150,000 kimepitwa na wakati kufuatana na ongezeko la idadi ya watu. Serikali ingependa kumjibu kwamba kama ilivyokwisha kutamkwa kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, Serikali itaimarisha Hifadhi ya Chakula cha Taifa ili kuwezesha kuwepo kwa chakula cha kutosha kwa angalau miezi mitatu wakati wa njaa. Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika itaandaa utaratibu wa kutekeleza maelekezo hayo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa alitoa taarifa kwamba Wilaya ya Kongwa bado inakabiliwa na njaa na inahitaji chakula cha msaada na mbegu za mtama kwa ajili ya kujianaa kwa kilimo cha msimu ujao. Hoja hii ilifanana na hoja ya Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mbunge wa Singida Kusini na pia Mheshimiwa Felister Bura, Mbunge wa Viti Maalum.

Jibu la Serikali ni kwamba tunakubaliana kwamba bado kuna maeneo nchini ambayo hali yake ya chakula siyo nzuri. Serikali inafanya tathmini ya hali ya chakula ilivyo sasa na hatua zitachukuliwa. Kwa Mikoa ambayo kutakuwa na mavuno mazuri ya chakula, viongozi wahimiza utaratibu mzuri wa kila kaya kujivekea chakula cha kutosha kama hifadhi. Tuchukue fursa hii kuwakumbusaha viongozi kuwahimiza wananchi kupanda mazao ambayo yanaendana na hali ya eneo husika. Pia, Mheshimiwa Felister Bura, alitaka *SGR* isibague mazao ya kununua hasa kwenye maeneo ambayo Mtama na Uwele unalimwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sera ya Serikali na utaratibu ni kwamba sisi tunanunua nafaka zote bila ubaguzi, ila mwaka 2005/2006 Serikali ilipanga kununua tani 10,000 za Mtama lakini haukupatikana. Hivyo wananchi wanahimizwa kulima Mtama na Serikali itanunua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, naye aliuliza swalı linalofanana na lile la Mheshimiwa Job Ndugai, alitaka Serikali iendelee kuzipa chakula Tarafa za Kwamtoro na Farkwa kwani zina njaa. Jibu ni lile lile kwamba Serikali itafanya tathmini na hatua zitachukuliwa kama hali hiyo ndivyo ilivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mbunge wa Kilombero, alitaka Serikali iuwezeshe Mkoa wa Morogoro kuzalisha chakula cha kutosha kwa Tanzania nzima. Kwa hakika Serikali itaendelea kutoa utaalalm, pembejeo, kutafuta

masoko na uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji na barabara ili kuendeleza kilimo. Aidha, viongozi wote wanatakiwa kuhamasisha wananchi kwenye maeneo yao katika uzalishaji wa chakula. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mbunge wa Temeke, alitaka Serikali iupatie Mkoa wa Dar es Salaam, msaada wa chakula cha njaa kama ilivyo katika Mikoa mingine. Ningependa kumjibu Mheshimiwa Abbas Mtemvu, kwamba kiutaratibu chakula cha njaa hutolewa kwa wananchi ambao shughuli zao za kilimo zimeathiriwa na janga kama ukame na mafuriko na vile vile mwananchi huyu anakuwa hana mbini nyingine ya kupata chakula. Kwa kawaida, wananchi wengi wa Dar es Salaam si wakulima, hivyo hawawezi kuhusika katika utaratibu wa kupatiwa chakula cha njaa na utaratibu huu unaihusu pia miji mingine yote nchini, si Dar es Salaam peke yake.

Mheshimiwa Spika, fungu la pili la hoja zangu kama nilivyokwisha kusema ni kuhusu dawa za kulevyta. Katika kundi hili nina hoja tano, kwanza kabisa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ilitaka Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevyta iwafuatilie walioathirika na dawa hizo na iendeleze mikakati ya kupambana na janga hilo. Jibu letu ni kwamba Tume imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali katika kudhibiti dawa za kulevyta. Hata hivyo Tume inakusudia kuboresha ushirikiano na wadau hao katika kuweka utaratibu wa kufuatilia walioathirika na kupambana na janga hili kwa nguvu zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, alitaka Serikali ifanye juhudhi za kusaka wanaojihusisha na madawa ya kulevyta na iandae mkakati wa kusaidia waathirika.

Ningependa kwanza kuelezea hoja hii katika makundi mawili, kwanza, ni kuzagaa kwa dawa za kulevyta. Serikali imekuwa ikifanya jitihada za kupambana na tatizo la biashara ya dawa za kulevyta kwa kuwakamata wahusika. Kwa mfano, mwaka jana watuhumiwa 4,532 walikamatwa na kesi 3,368 zilifunguliwa Mahakamani. Tatizo hili linahitaji ushirikiano wa wananchi kutoa taarifa kwa vyombo vinavyohusika kuwafichua wahusika.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ni kuhusu tiba ya waathirika wa dawa za kulevyta. Ningependa kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba waathirika wa dawa za kulevyta wanaojitokeza wanapata tiba katika hospitali mbalimbali. Hata hivyo kuna tatizo la wazazi na ndugu wa waathirika kutokuwapeleka waathirika hospitalini kupata tiba. Wazazi ama walezi wanahimizwa kuwapeleka waathirika hospitalini. Aidha, Serikali itaangalia upya sheria inayohusika, ili suala la tiba kwa waathirika isiwe hiari kama ilivyo sasa. Serikali imeandaa rasimu ya mwongozo kwa waathirika ambao utasambazwa katika hospitali. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mbunge wa Viti Maalum alitaka Serikali iweke mkakati utakaodhibiti kilimo cha bangi. Mheshimiwa Spika na Bunge lako Tukufu, Serikali imeweka mkakati wa kutokomeza kilimo cha bangi kuitia mpango kabambe wa Taifa wa kudhubiti dawa za kulevyta unaojumuisha mikakati ifuatayo,

kwanza, kutilia mkazo kilimo cha mazao mbadala yatakayowaingizia kipato wakulima. Pili, kuendesha operesheni maalum, kugundua, kukamata na kuteketeza bangi popote inapolimwa nchini na tatu, kuelimisha wakulima madhara yatokanayo na kilimo cha bangi pamoja na athari za utumiaji wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mbunge wa Fuoni, alitaka Serikali iweke mkakati wa kuvunja mtandao haramu wa madawa ya kulevya zinazohatarisha maisha ya vijana. Kama nilivyokisha kueleza, Serikali itaendelea kufanya operesheni maalum kupambana na wote wanaojihusisha na dawa za kulevya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, katika fungu hili, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mbunge wa Fuoni alitaka vyombo vy'a dola vinavyoshughulikia madawa ya kulevya vitekeleze majukumu yao ipasavyo. Ningependa kumhakikishia kwamba vyombo vy'a dola kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wanafanya hiyo kazi vizuri sana kama ipasavyo, kama nilivyokwisha kueleza kwenye taarifa kuhusu waliokamatwa na wale waliopelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, fungu la tatu katika hoja ninazojadili sasa hivi ni kuhusu Tume ya Kudhibiti Ukimwi na Huduma za Ukimwi. Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilitaka Tume ya Kudhibiti Ukimwi iendelee kupanua shughuli zake zaidi ili ziwafikie wananchi wengi vijijini na iweke mikakati ya kufikia wananchi walioathirika na Virusi vy'a Ukimwi pamoja na yatima.

Mheshimiwa Spika, ningependa kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba Tume ya kudhibiti UKIMWI ina utaratibu wa kufikia jamii kwa kutumia wakala wao ambao wameingia mkataba wa kuzijengea uwezo Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Wakala hawa ndio wanaosaidia wanaoishi na virusi vy'a UKIMWI pamoja na yatima. Wakala hawa wanapatikana kwa mchakato wa uwazi kwa kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Serikali ya mwaka 2004 na kwa kushirikisha Halmashauri na wadau wengine. Pamoja na hilo, Tume itaendelea kuboresha na kupanua shughuli zake kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati na wadau mbali mbali. Katika uboreshaji huo, Halmashauri na Asasi zinazohusika, wanashauriwa kutoa ushirikiano wa dhafi katika kuwatambua na kuwafikishia misaada walengwa wa virusi vy'a UKIMWI na yatima. Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala pia ilitaka Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania ishirikiane na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Zanzibar kupambana na janga la UKIMWI kila inapowezekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba Tume zote mbili za Tanzania Bara na Zanzibar zimekuwa zikishirikiana katika masuala mbalimbali ya kudhibiti UKIMWI. Hata hivyo, ushauri wa kuimarisha ushirikiano, umezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, wakati akiongea kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, alitaka Serikali iangalie upya mfumo mzima wa uendeshaji wa shuguli ndani ya *TACAIDS*, utumiaji wa mawakala kushughulikia suala la UKIMWI nao uangaliwe upya. Ni kweli Serikali inatumia mpango wa mawakala ili kuongeza nguvu za Kamati za Halmashauri na asasi zisizo za Kiserikali. Wakala hawa wamepangiwa

kufanya kazi katika Halmashauri zote nchini. Tunawaomba Waheshimiwa Wabunge washirikiane na Halmashauri pamoja na wakala ili kuongeza nguvu katika kupambana na UKIMWI nchini. Hata hivyo, kasoro zinazojitokeza katika utaratibu huo, zinafuatiliwa na kushughulikiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum alitaka wananchi wahamasishwe juu ya kujikinga na UKIMWI ili wachukue tahadhari. Aidha, Serikali isadie kuwapatia dawa za kupunguza makali ya UKIMWI waathirika. Ningependa kumjibu Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah kama ifuatavyo: Serikali imekuwa ikielimisha wananchi kwa kutumia njia mbalimbali za utoaji elimu ya kujikinga UKIMWI kwa kutumia vyombo vya habari, vijarida, elimu kwa njia ya semina, warsha na nyenzo mbalimbali. Serikali ilianzisha mpango wa tiba ya bure kwa waathirika tangu mwaka 2004. Sasa hivi, waathirika 27,000 wanapata dawa hizo bure.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi watakuwa wanafadhaika kwamba mbona tunaambiwa kuna waathirika 2,500,000. Taratibu za utoaji tiba zina kanuni maalum kwamba mwathirika wa UKIMWI awe ametimiza vigezo kadhaa ikiwa ni pamoja na kuwa na *CD4* chini ya 200. Aidha, Serikali itaendelea kuongeza juhudhi za kuwahudumia wale ambao watapimwa na kuonekana wameathirika na kuwa na *CD4* chini ya kiwango hicho.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mbunge wa Viti Maalum, naye pia alitaka mashirika yasiyokuwa ya Serikali (*NGOs*) yanayojinufaisha na fedha za kampeni dhidi ya UKIMWI yaangaliwe na kuchukuliwa hatua. Ningependa kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba *NGOs* zinazoshughulika na Kampeni dhidi ya UKIMWI zinatakiwa kutumia fedha zilizotolewa kwa manufaa ya wananchi. *NGOs* zinapata fedha kwa njia mbali mbali. Kuna zile zinazopata fedha moja kwa moja kutoka kwa wafadhili na zile ambazo fedha zake zinapatikana kutoka Serikalini.

Hata hivyo, mamlaka za Serikali za Mitaa zinawajibu wa kujua bajeti ya *NGOs* zilizo katika maeneo yao pamoja na kufuatalia utekelezaji wa shughuli zote za kupambana na UKIMWI katika maeneo husika. Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuchukua hatua endapo inaonekana *NGOs* hizo hazitekelezi mipango kama ilivyopangwa. Katika hili, samahani naomba hapa nipitilize kwa sababu Mheshimiwa aliyejewa ametayarisha suala hilo lilikuwa linafanana na yale ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum alitaka semina kwa ajili ya kampeni dhidi ya UKIMWI zipunguzwe na badala yake huduma za dawa na lishe zitolewe hasa vijijiji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, napenda kurudia tena kwamba semina kuhusu vita dhidi ya UKIMWI, hutolewa kwa kuangalia masuala mapya yanayojitokeza kama vile mahitaji ya dawa za kupunguza makali ya UKIMWI, ongezeko la maambukizi kwa makundi mbalimbali katika jamii na suala la lishe. Kwa jumla ningependa kusema kwamba semina zitafanyika pale zinapohitajika ili kuweza kupata taarifa mpya, kuweza kupata maendeleo katika uvumbuzi wa kinga na baadae tiba ya

UKIMWI. Hivyo basi ushauri wa kupunguza semina, utazingatia uwiano kati ya mahitaji ya elimu na upelekaji huduma kwa walengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mbunge wa Makete alitaka Serikali iande mkakati wa kutoa elimu ya kupambana na UKIMWI kwa wakazi wa Wilaya ya Makete, kwani sababu za kueneo kwa UKIMWI Makete ni pamoja na ujinga na umaskini.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imeunda Kamati za kudhibiti UKIMWI katika mamlaka ya Serikali za Mitaa nchini ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Makete. Kamati hizi huanda na kusimamia utekelezaji wa mipango ya kudhibiti UKIMWI. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii, tayari imeandaa mpango wa kutoa elimu ya UKIMWI katika shule zote nchini. Elimu hii ilitolewa shulenii, itaifikia jamii kwa haraka na kwa upana mkubwa. Serikali inatambua tatizo la UKIMWI Wilaya ya Makete na itaendelea kushauriana na viongozi wa Makete wakiwemo Waheshimiwa Wabunge ili kutatua tatizo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, alitaka Serikali isisitize zaidi katika malezi ya vijana kama njia mbadala ya kupambana na UKIWI badala ya kusisitiza matumizi ya kondomu kama kinga. Suala hili lilichangiwa pia na Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka. Ushauri umekubaliwa na utazingatiwa kwani hatua zote ni muhimu na zinasaidia katika kupunguza ongezeko la UKIMWI nchini. (*Makofi*)

Hoja inayofuatia ambayo ni moja tu, ilitolewa na Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge wa Viti Maluum aliyetaka Serikali iandae mkakati wa kuwasaidia wale mavu badala ya kuacha jukumu hilo kwa watu binafsi. Kama ilivyo katika hotuba ya Waziri Mkuu, Serikali ina Sera ya Taifa ya Watu wenye Ulemavu na itaendelea kuitekeleza ili wapate fursa za kiuchumi, kisiasa, ajira, elimu, afya na mikopo kama watu wengine katika jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya mwisho ni kuhusu mawakala wa programu ya uendelezaji wa Mfuko wa Masoko ya Mazao ya Kilimo (*AMSDP*). Hii ilitoka kwa Mheshimiwa Devota Likokola, Mbunge Viti Maalum. Yeye alitaka mawakala wa programu hii wawajibike kwenye Halmashauri za Mikoa ili wananchi waelewe vizuri mradi huo. Ili kuipa Wilaya husika mamlaka ya usimamizi wa utakelezaji wa programu ya *AMSDP*, kamati ya ushauri imeundwa na Wilaya. Kamati hii inayojulikana kama *Folk Area Advisory Group*, ndiyo yenye mamlaka ya kushauri, kusimamia na kukubali mipango yote ya wakala mwezeshaji. Kamati hii ndiyo inayopitia malipo, mpangokazi na bajeti ya wakala mwezeshaji. Kazi ya programu hii ni kulipa kile kinachokubaliwa na kamati hii na kutoa ushauri wa kitaalam ikibidi. Ushirikiano huu uko ndani ya mkataba maalum ambao unaainisha wajibu wa kila mdau kati ya Halmashauri ya Wilaya, wakala maalum ambao unaainisha wajibu wa kila mdau. Waheshimiwa Wabunge wanaweza kuuona mkataba huu kwa Mkurugenzi Mtendaji wa kila Wilaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongea haya naomba nitoe shukrani zangu maalum kwa wananchi wangu wa Wilaya ya Mbozi hususan wale wa Wilaya ya Mbozi Magharibi ambao waliniwezesha kufika katika Bunge hili Tukufu na baadae kuweza kuteuliwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu. Hivyo basi naomba shukrani zangu ziwafikie kwa dhati. Nitaendelea kulitumikia Taifa hili kama ambavyo nitaendelea kuwatumikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote kama ilivyo ada, kwanza naomba kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyungui na wananchi wa Tanzania. Wakati huo huo namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kunitfea kuwa Naibu Waziri.

Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Naibu Mawaziri pamoja na Wabunge wenzangu wote kwa kuchaguliwa kuingia katika Bunge hili Tukufu.

Mwisho, naomba niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Ulanga Mashariki kwa kunichagua kwa kura nyngi, yaani za asilimia 85. Kwa kweli ninawashukuru sana na nasema kwamba nitawatumikia kwa nguvu zangu zote na pia nitatumikia huo wadhifa mwingine ambao nimepewa na Mheshimiwa Rais. Naomba kuwapongeza Wabunge wote ambao wametoa hoja mbalimbali katika kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Sisi tumezipokea, hizo ni changamoto na mengi tutayachukua na kuyafanya kazi. Tunaamini kwamba wao ndio wako karibu na wananchi wengi, kwa hiyo tunawapongeza na tunawashukuru kwa michango yao yote. (*Makofi*)

Naomba niende moja kwa moja katika hoja mbalimbali ambazo zimechangiwa na Wabunge mbalimbali. Hoja tatu za kwanza, zilichangiwa na Mheshimiwa George Lubeleje na Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji. Ya kwanza, TAMISEMI ijenge hoja ya kuongeza Bajeti ya mwakani ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Jibu letu ni kwamba ushauri huo utazingatiwa na pili tunasema kwamba zipo taratibu zinazozingatiwa na Serikali katika kugawa fedha kwa Wizara, Mikoa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili, Ofisi za Wabunge zipatiwe vitendea kazi vya kisasa ili kuendana na falsafa ya kasi na viwango. Ushauri huo unazingatiwa na kwamba katika bajeti ya mwaka 2006/2007, Ofisi za Mikoa zimeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuhudumia Ofisi za Wabunge. Jumla ya shilingi milioni 146 zimetengwa kwa ajili ya madhumuni hayo.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu, Ofisi ya Waziri Mkuu iandae semina kwa Wabunge wote kuelimisha kwa undani shughuli za utekelezaji wa mikoa na juu ya maboresho ya Serikali za Mitaa. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba,

uelimishaji wa Wabunge kuhusu maboresho yanayoendelea, umeanza kutekelezwa. Tarehe 16 na 17 Juni, 2006, semina imefanyika kwa Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala na kwa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa ili kuwaelewesha Wabunge kuhusu uboreshaji wa Serikali za Mitaa. Ofisi yetu inawasiliana na Ofisi ya Bunge ili kupanga semina kwa Wabunge wote ili waelewe maboresho ya Serikali za Mitaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna hoja nyingine nne ambazo zimetolewa na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa na Mheshimiwa John Malecela. Hoja ya kwanza, Ofisi ya Waziri Mkuu ihmize kuanzishwa kwa Mifuko ya Elimu ya Mikoa na Wilaya. Napenda kujibu kwamba, ofisi yetu imepokea ushauri huo na utaratibu huu upo kwa baadhi ya Mikoa kwa mfano, Kilimanjaro, Shinyanga, Rukwa na kadhalika. Nawashauri Mikoa mingine, iende kwenye Mikoa hii, ikajifunze wenzao wamefanya nini.

Suala lingine Serikali ianzishe mashindano ya kimaendeleo kati ya Halmashauri zinazoongozwa na Chama cha Mapinduzi na zile zinazoongozwa na Vyama vya Upinzani. Tunapenda kujibu kwamba, idadi ya Halmashauri zilizo chini ya Vyama vya Upinzani ni ndogo mno, kuweza kushindana na Halmashauri zilizo chini ya Chama Tawala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya Halmashauri zote yanapimwa katika utekelezaji wa Ilani ya Chama Tawala. Halmashauri zinafanyiwa tathmini kwa kuzingatia vigezo vya Utawala Bora na utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine Serikali itoe tamko kufuatia kuhamishwa kwa kituo cha mabasi cha Mwenge kwenda Makumbusho, kwa kuwa wananchi wanapata shida sana. Serikali imehamisha huduma za kituo cha mabasi Mwenge kwenda Makumbusho kwa muda ili kutoa nafasi ya shughuli za ukarabati wa Kituo cha Mwenge. Serikali inawaomba wananchi wawe na subira wakati kazi hiyo inaendelea. Kituo cha Mwenge, kitatumika kama kawaida, baada ya ukarabati huo kukamilika.

Hoja nyingine ni tatizo la uhaba wa maji katika mikoa kame, litatuliwe haraka. Serikali itaendelea kutekeleza programu ya maji na mazingira ili kutatua tatizo la uhaba wa maji katika Mikoa kame. Pia tunashauri chini ya mfumo wa kutoa ruzuku ya maendeleo kwa Serikali za Mitaa, Halmashauri bado zina fursa ya kupata hela hizo na kuzitenga katika miradi ya maji.

Mheshimiwa Spika, masuala mengine matatu yamechangiwa na Mheshimiwa Luhanga Mpina na Mheshimiwa Samuel Chitalilo. Moja utendaji kazi wa Maafisa Watendaji wa Kata, uangaliwe upya kwani kuna baadhi wanabandika watu kesi pindi wanapokataa kutoa rushwa. Hoja hiyo ilitolewa na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa. Tunasema kwamba, ushauri huo unazingatiwa, sisi pamoja na Mheshimiwa Mbunge, tutafuutilia suala hili kwa karibu.

Suala lingine ni vituo vya afya katika Halmashauri ya Meatu, vipatiwe vifaa na Waganga. Jibu letu ni kwamba, ni kweli vituo hivyo vya afya havina vifaa na waganga wa kutosha. Kwa kuzingatia uamuzi wa Serikali wa kuajiri watumishi mara tu

wanapomaliza masomo yao, ni tumaini letu kuwa, nafasi zilizo wazi zitajazwa kadri wahitimu watakavyopatikana. Pia Serikali inaendelea kutoa fedha kila mwaka kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya zahanati na vituo vya afya. Halmashauri tunaomba zifuatilie vifaa hivyo muhimu kutoka *MSD*.

Hoja nyingine ni Wilaya ya Sengerema haina Hospitali ya Wilaya. Suala hili lifanyiwe kazi ili kuondokana na tatizo hili. Kwa sasa Wilaya ya Sengerema inashauriwa kuendelea kutumia huduma zitolewezo katika Hospitali Teule iliyopo, hadi hapo uwezo wa Serikali utakaporuhusu kujenga hospitali katika Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Spika, masuala mengine mawili yalichangiwa na Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mbunge wa Muleba Kusini na Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mbunge wa Viti Maalum, kuhusu ukarabati wa Kituo cha Afya cha Nshamba Wilayani Muleba. Halmashauri ndizo zenye jukumu la kwanza la kujenga kituo cha afya kwa kutumia mapato yake. Pia Halmashauri ingetoa kipaumbele katika ujenzi wa Kituo cha Afya cha Nshamba, ingeweza kupatiwa fedha kutoka Hazina. Mwisho, Halmashauri inaweza pia kupata fedha kutokana na Mpango wa Kuzisaidia Serikali za Mitaa ili kujenga Kituo cha Afya cha Nshamba, ikiwa inakidhi masharti ya kupatiwa fedha.

Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa mwaka wa fedha 2006/2007, jumla ya shilingi milioni 198.8 zilipelekwa Wilaya Muleba, kwa ajili ukarabati wa vituo vya afya na zahanati. Hivyo, ni jukumu la Halmashauri husika kupanga kulingana na vipaumbele vyake.

Suala lingine ni wodi ya wazazi katika Mkoa wa Mara, haina vitanda vya kutosha kiasi kwamba akina mama wazazi wanalala wanne wanne katika kitanda kimoja. Serikali ina mpango maalum wa kuboresha vituo vya afya na zahanati ili kupunguza msongamano wa wagonjwa katika Hospitali za Mikoa. Mkoa wa Mara, unashauri kuliweka hitaji hilo katika vipaumbele vyake.

Masuala mengine matatu yalichangiwa na Mheshimiwa Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo. Moja ni kuhusu taa za barabarani ziwekwe katika Manispaa ya Dodoma. Jibu, ni kuwa uwekaji wa taa za barabarani ni mionganoni mwa miradi ambayo inapaswa itekelezwe na Halmashauri. Manispaa ya Dodoma, kwa mwaka huu imetenga jumla ya shilingi milioni 12 kwa kuanzia, ili kuweka taa barabarani.

Suala lingine ni Serikali itoe fedha kwa ajili ya upanuzi wa Kituo cha Afya cha Sokoine Mjini Singida. Upanuzi wa Vituo vya Afya kama ilivyo kwa shughuli nyingine za maendeleo, ni jukumu la Halmashauri husika kuliweka kwenye mipango yake ya maendeleo. Halmashauri ya Manispaa ya Singida, ipo chini ya programu ya ukarabati wa vituo vya afya na zahanati. Halmashauri pia inaweza kupata fedha chini ya Mpango wa Kuzisaidia Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Mbunge, anashauriwa awasilishe pendekezo hili kwenye Baraza la Madiwani ili litolewe maamuzi.

Hoja nyingine ni maombi ya kupandisha daraja Barabara za Kilindi, ambazo hazijafanyiwa kazi. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, Katibu wa Bodi ya Barabara Mkoa wa Tanga, amekwisha iandikia Wizara ya Miundombinu, ili kuzipandisha daraja barabara za Wilaya ya Kilindi.

Mheshimiwa Spika, masuala mengine mawili yalichangwa na Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini na Mheshimiwa Ernest Mabina, Mbunge wa Geita. Moja, Serikali itenge maeneo mapya ya makaburi hasa katika Manispaa za Wilaya za Jiji la Dar es Salaam. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, Halmashauri zote za Manispaa za Dar es Salaam, zimetenga maeneo ya makaburi kwa kuzingatia ongezeko la watu kama ifuatavyo: Manispaa ya Ilala eneo la makaburi ni Mwangati, ambalo lina eka 6.8. Manispaa ya Temeke eneo la makaburi ni Kibada na Ungindoni, eneo hilo lina eka tano. Manispaa ya Kinondoni eneo la makaburi ni Kwembe, Kibamba, Mbezi Luisi, Kiruvya, Mbezi Temboni, Mbezi Luguruni, Kimara Matangini na Kimara Bonyokwa. Maeneo haya yana jumla ya eka 72.

Mheshimiwa Spika, hoja ya mwisho ni Hospitali ya Wilaya ya Geita, ipatiwe moja ya magari ya wagonjwa, yanayonunuliwa kwa kipindi hiki cha sasa. Jibu ni kwamba, kwa mwaka 2005/2006, Serikali imenunua na kugawanya magari 30 ya wagonjwa kwa kufuata vigezo vifuatavyo: Wilaya ambazo ni mpya, Wilaya zilizo mpakani mwa nchi na Halmashauri zenyet matatizo makubwa ya kijiografia, kwa mwaka wa fedha 2006/2007, Serikali pia itanunua magari mengine 22 ya wagonjwa na yatagawanywa kwa kutumia vigezo hivyo nilivyovitaja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika na mimi niungane na wenzangu, awali ya yote, niseme kwamba, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Naunga mkono kwa sababu hotuba hii na hoja hii, imekuwa dira kubwa na maelekezo ndani ya Serikali. Kwa hiyo, naunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia na mimi naomba niungane na wenzangu, kumpongeza sana Rais Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Wengi tutakubaliana na mimi hasa waliokuwa kule na waliosikia hotuba yake baada ya kuchaguliwa, ilitoa matumaini makubwa sana kwa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, ninawapongeza Mheshimiwa Yusuf Rajabu Makamba, kwa kuchaguliwa kuwa Katibu Mkuu, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, kwa kuchaguliwa kuwa Katibu Mwenezi na Mheshimiwa Rostam Azizi, kwa kuchaguliwa kuwa Mweka Hazina. Vile vile napenda kuipongeza Kamati ya Katiba na Sheria, tuliokwenda mbele ya Kamati hii, tulipewa ushauri mkubwa sana na maelekezo. Napenda kuchukua nafasi hii kwa dhati kabisa, kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa George Lubeleje, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Tatu Ntimizi na Wajumbe wa kamati hii. (*Makofi*)

Sisi tuliokuwa pale na wenzangu tulifaidika sana kwa ushauri wao na maelekezo ambayo walitoa. Kwa kweli ningependa kuwahakikishia kwamba, yale yote ambayo mltushauri siku ile, yote kabisa yalizingatiwa na yamezingatiwa. Mengine mnaweza kupata majibu kwa sasa, lakini sisi tuliporudi ndani ya Serikali, tulishauriana na mengi mtayaona katika bajeti zinazokuja. Kwa hili tunawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kama alivyosema Mheshimiwa Ramadhani Athumani Maneno, alipokuwa anachangia hapa, ilitupa maelekezo. Moja ya maelekezo ni kwamba, Serikali iandae tena ratiba itakayoainisha Wizara zitakazohamia Dodoma, hatua kwa hatua. Mimi napenda kurudia hili ambalo lilisemwa na Kamati, hatua kwa hatua hata kama utekelezaji wake utachukua muda mrefu. Hili nawashukuru sana kwamba, waliliona na sisi kwenye Kamati pia walituambia na humu ndani walilieleza. Sasa jibu lake ni kwamba, ushauri umezingatiwa na baadhi ya Wizara zimeanza kuhamia Dodoma, hatua kwa hatua, kwa kadri hali ya uchumi inavyoendelea, wote mtaona jitihada ambazo zinafanyika.

Lakini pia nia ya Serikali iko wazi kwa wale ambaو walimsikiliza Mheshimiwa Rais, siku alipokuja hapa Dodoma, kuwashukuru wananchi wa Dodoma, alisisitiza sana hili kwamba, tutahamia Dodoma na hili hakuna tena mjadala maana ni maamuzi na ndiyo Ilani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Ningependa kulirudia kwamba, hii ni Ilani ya Chama cha Mapinduzi, toka mwanzo Chama cha Mapinduzi na *TANU* kule ndiyo viliviyobuni utaratibu wa kuhamia Dodoma. Haiwezi kuwa Sera ya Chama kingine, wengine wanaweza kuwa nayo kweli, lakini Chama cha Mapinduzi ni sera yake, ndiyo wanaoisimamia.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Katiba na Sheria pia ilitoa maelekezo yake kwamba, Jengo la Ofisi ya Waziri Mkuu Dodoma, ambalo ni kuukuu na halistahili kutumiwa na Waziri Mkuu, lifanyiwe ukarabati mkubwa ili lilingane na hadhi ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Mimi nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mko hapa, tembeleeni pale mpaone, si jengo zuri hata kidogo. Kwa hiyo, kwa ushauri huu ambaو Kamati imesema kimsingi Serikali imeshaamua kukarabati Jengo la Ofisi ya Waziri Mkuu Dodoma, ukarabati utaanza mwaka 2006/2007 na kiasi cha shilingi bilioni moja kimetengwa ili kuanza kazi hiyo, kwani hili ni kati ya majengo ya kale yanayotakiwa kuhifadhiwa kwa mujibu wa sheria. Ukarabati huo ukikamilika, utatoa nafasi za ofisi nzuri kwa Waziri Mkuu na watendaji wake, zinazolingana na hadhi ya Waziri Mkuu, hili litafanyika. (*Makofi*)

Kamati ya Katiba na Sheria, ilitoa maelekezo yake kuhusu Tume ya Uchaguzi, iangalie uwezekano wa kupanga tarehe ya Uchaguzi Mkuu iwe katikati ya wiki badala ya siku ya ibada. Ni kweli imekuwa ni utaratibu wa Tanzania, kupiga kura siku ya Jumapili. Utaratibu huo umetumika wakati wote, isipokuwa uchaguzi wa mwaka 2005, ambapo haukutumika kwa sababu maalum. Katika chaguzi zote, mwitikio wa wananchi umekuwa ni mzuri sana. Hata hivyo, Serikali italifanyia kazi suala hili. Lakini kwa miaka yote toka Uhuru, uchaguzi tumefanya siku ya Jumapili na hatukuwa na matatizo yoyote kabisa,

wananchi wamehudhuria kupiga kura mpaka tukapata mafanikio. Kama nilivyosema, bado litaangaliwa maana ni hoja ya kuitazama, hatuna sababu ya kuikataa moja kwa moja, bila kuitazama vizuri. (*Makofî*)

Kamati ya Katiba na Sheria na Utawala, ilisema hapa ndani kuwe na Mkakati Maalum wa Kuwaelimisha Wananchi juu ya Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa, hasa utaratibu wa kupiga kura. Mkakati wa Kuelimisha Wananchi kuhusu Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa na hasa utaratibu wa kupiga kura, utawekewa msukumo mkubwa na mpya. Tume ya Uchaguzi, itaendelea kushirikiana na wadau wote, wakiwemo wa Vyama vya Siasa vyote, Mashariki yasiyo ya Kiserikali na vyombo vya habari, ili kufanikisha suala hili. Wote ni mashahidi, katika chaguzi tunaona matatizo ya hapa na pale, yanayohitaji elimu, ili wananchi wanapokwenda kupiga kura, kusiwe na matatizo. Suala hili Serikali inalikubali kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa alisema, vyombo vya dola vimeduwa vikiwakandamiza wananchi wakati wa uchaguzi, kwa kutumia mabomu ya machozi, marungu, hata risasi za moto, kwa mfano, matukio yaliyotokea Tarime, Karatu, Bariadi Mashariki, Unguja na Pemba na kadhalika na kufanya upigaji wa kura usiwe wa haki na huru.

Mheshimiwa Spika, wakati wa uchaguzi, vyombo vya dola vina wajibu wa kuhakikisha kunakuwepo na hali ya amani na utulivu, kuwawezesha wananchi kutumia haki yao ya Kikatiba ya kupiga kura bila kubughudhiwa na mtu yeoyote. Vyombo vya dola vimeduwa vinatekeleza wajibu huo kikamilifu, pale ambapo pametokea vurugu zinazoashiria uvunjaji wa amani, vyombo vya dola vimechukua hatua zinazostahili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, wote hapa sisi ni mashahidi tumetoka kwenye uchaguzi, kuna maeneo ya ghasia, ambayo hayawezi kuleta utulivu kwa wapiga kura. Wito wa Serikali kwa hili, inawataka na kuwaomba wananchi wote, siku ya kupiga kura tuwe watulivu, tutulizane twende taratibu. Hakuna askari atakayekubugudhi kama wewe unakwenda kiungwana, taratibu na kwa amani. Lakini ukiamua kufanya fujo, wajibu wa Serikali ni kuhakikisha yule mtulivu, analindwa na analindwa kwa kuhakikisha wewe wa fujo, unatulizwa na hili ndilo mara nydingi linatoka. Lakini bado jitihada zitaendelea kama nilivyosema awali, kutoa elimu kwa Watanzania wote kwamba, uchaguzi si uhasama, uchaguzi ni kitu cha amani, tunachagua viongozi wetu kwa utulivu ili yule anayechaguliwa, achaguliwe kwa mapenzi ya wote. Lakini unapoamua kwa nguvu, unayemtaka wewe rohoni ndiyo achaguliwe, basi unawaleta karaha watu wengine, kwa hiyo, ni kazi ya vyombo vya dola, kuhakikisha jambo hili halitokei. Kama ninavyosema, elimu itaendelea kutolewa kwa Watanzania wote, ili tuwe na mafanikio mazuri katika upigaji wa kura. (*Makofî*)

Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa alisema, Tume ya Uchaguzi, imeegemea zaidi kulinda maslahi ya Chama Tawala, kwani wasimamizi na wasimamizi wasaidizi wote ni watendaji wa Serikali. Pendekezo alilotoa yeye, Tume ya Taifa iwe na maafisa wake kwenye ngazi ya Wilaya, wasio na mgongano kimaslahi. Kwa mujibu wa Katiba na

Sheria za Uchaguzi, Tume ya Uchaguzi, inaendesha shughuli zake bila kuegemea upande wowote wa kisiasa, wala upande wa chama chochote. Hii ni Tume Huru, nayo iko huru wakati wote. Wasimamizi wa uchaguzi huteuliwa kwa kuzingatia sheria za uchaguzi, ambazo kwa sasa zinawataka wawe Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa, ambao hawaegemei upande wowote.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ilisema, uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, ufanywe kwa uwazi ili kuondoa dosari ndogo ndogo. Tume imeandaa utaratibu wa kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, ambao utatekelezwa katika mwaka 2007/2008. Wakati wa uboreshaji, wale wote ambao watakuwa wamepoteza sifa, wataondolewa na wale ambao wamekuwa na sifa za kujiandikisha au hawakujandisha hapo awali, wataandikishwa. Aidha, dosari zilizoko kwenye Daftari kwa sasa, zitarekebishwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Wote ni mashahidi, tunapoandikisha wapiga kura ni zoezi la wazi kabisa. Kila chama kinaweka wakala wake na wananchi au wakazi wa eneo hilo, nao wanathibitisha kwamba, huyu tunamjua, ni raia na ni mkazi wa eneo letu. Hata hivyo, hii ni mara ya kwanza tumetumia Daftari la Wapiga Kura, litaendelea kuangaliwa, kuboreshwa na kuweka mazingira yake yawe sawa sawa. Zoezi hili litafanywa kwa uwazi bila kificho, kama ilivyofanyika wakati wa uandikishaji wa wapiga kura.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, pia ilisema mwaka 2004/2005, Bunge liliambiwa kuwa Jengo la Chimwaga, litakarabatiwa kwa ajili ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhamia. Lakini sasa hakuna kinachozungumzwa na Serikali juu ya hilo badala yake imeomba fedha jumla ya shilingi 792 milioni, kwa ajili ya jengo hilo la Chimwaga. Serikali itoe maelezo ya kina kuhusu malengo ya matumizi ya jengo hilo. Kwa kweli nina furaha sana juu ya maamuzi yaliyofanywa na Serikali kuhusu jengo lile. Serikali baada ya kulitazama lile jengo na kulijenga, kwa wale ambao mmekwenda pale, narudia tena, kwa wale ambao hamjafika pale, mtafute muda wa kwenda kuliangalia, ni jengo zuri sana, ni jengo la Serikali. Kwa hiyo, Serikali imeamua kutoa jengo lile kwa ajili ya kuanzisha Chuo Kikuu cha Dodoma. Haya ni matumizi mazuri sana, kwa ajili ya maisha ya Taifa letu. Ananiambia Mheshimiwa Profesa Msolla, ambaye ndiye Waziri wa eneo hili kwamba, yeye angependa hata mwakani tuanze, kwa sababu jengo lile linatosha kabisa, vyumba vinatosha, vinawenza kuanza kutumika. Kwa hiyo, kama kulikuwa na wazo, kuifanya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, wazo hilo halipo tena, tunataka kulitumia kama Chuo Kikuu. (*Makofsi*)

Waheshimiwa Wabunge, ndio maana tumeomba fedha katika bajeti hii, ili tupate jengo lingine au tukarabati lile kwa ajili ya matumizi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Waheshimiwa Wabunge, ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa Dodoma, wote mnaiona, sio nzuri. Kwa wale ambao mmetembelea Ofisi ya Waziri Mkuu pale Dar es Salaam, maofisa wengi wanakaa kwenye vibanda vya mbao tu kule nyuma, si zuri ndio maana Serikali imeamua kujenga ofisi nzuri na yenye heshima, kwa ajili ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa, alisema Bunge lisimamie Bajeti yake lenyewe, tofauti na ilivyo sasa. Utaratibu unaotumika,

kuandaa Bajeti ya Bunge, unazingatia Sheria Na. 14 ya mwaka 1997. Utaratibu huu ndiyo unaotumika katika baadhi ya nchi za Jumuiya ya Madola, ambazo zina mfumo uitwao *West Minster*, Bunge lina fungu lake kama ilivyo kwa Wizara na Taasisi zingine.

Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe umetuma Tume nchi mbalimbali, kwenda kuangalia taratibu za namna njema ya kuwa na matumizi sahihi ya bajeti ya Serikali. Mimi ningependa kuwashakikisha kwa niaba ya Serikali kuwa, Serikali itaisadia Bunge kuhakikisha inafanya kazi yake vizuri, bila kikwazo. Serikali haina sababu hata kidogo, kuwa na Bunge ambalo linapata tatizo katika utekelezaji wa shughuli zake. Kwa hiyo, huu ni utaratibu ambao sheria tuliyokuwa nayo, ndiyo inayotumika na wote wanatumia taratibu hizo. Bunge, Mahakama, taratibu ni hizo hizo, lakini kama nilivyosema, ni jambo ambalo linazungumzika, pengine mkilieleza, hoja hizo zitachambuliwa. Lakini kwa hivi sasa, utaratibu unaotumika ni huo kwamba, Bajeti iwe ya pamoja. Lakini pamoja na hayo, pesa zinazotengwa kwa ajili ya Bunge, anayeamua nini kinunuliwe ni Bunge lenyewe. Zile ambazo zimetengwa, zimeletwa Bungeni, anayeamua nani atumie kipi, aende wapi, nauli kiasi gani, ni juu ya Bunge lenyewe. Kamati gani iende wapi, kwa fedha kiasi gain, ni juu ya Bunge lenyewe mpaka hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Meshimiwa Job Ndugai, alilieza suala lingine ambalo sina hakika kama Mheshimiwa Dr. Siyame amelijibu, maana lilikuwa ni eneo. Amesema Wilaya ya Kongwa bado inakabiliwa na njaa na inahitaji chakula cha msaada na mbegu za mtama kwa ajili ya kijiandaa kwa kilimo cha msimu ujao. Tunakubaliana kwamba, bado kuna maeneo nchini, ambayo hali yake ya Chakula siyo nzuri, hili Serikali inalijua. Maeneo mengine tunaweza kuvuna vizuri, haya atayaeleza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

Lakini ni kweli baadhi ya maeneo tunatazamia kuwa na matatizo na kama Serikali ilivyo fanya, mwaka huu tumehakikisha, Rais mwenyewe alihakikisha, Mheshimiwa Waziri Mkuu, alihakikisha kwamba, sisi wasaidizi wao tunatumwa kila mahali kuhakikisha kwamba, hakuna mtu anayekufa kwa sababu ya njaa. Maeneo mengi tumetoa mbegu. Pale ambapo patathibitika pana matatizo ya namna hii, Serikali haitasita na kwa kweli ni wajibu wake kuhakikisha wananchi hawa wanapata chakula na mbegu. Wito ambao Serikali inautoa kwa wananchi wote, maeneo yale ambayo kuna upungufu wa mvua, tafadhali tuzingatie kupanda mazao ambayo yatakoma haraka, ili tuweze kuuepukana na njaa. Maeneo ambayo mtama unastawi, hata kama unadhani mtama si mzuri, lakini lima mtama ili uweze kuuepuka njaa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Job Ndugai, ni kweli Wizara ya Kilimo na Watalaam kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, wametumwa nchini, hivi sasa wanafanya tathimini ya mavuno katika Taifa letu na pindi ikithibitika kwamba, kuna tatizo hilo, hapana shaka kabisa, hatua za Serikali zitachukuliwa ili kuondoa tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, alilirudia tena suala lile la ujenzi wa Ofisi ya Waziri Mkuu, anasema kwa nini Ofisi ya Waziri Mkuu ijengwe Dar es

Salaam na siyo Dodoma, wakati kuna uamuza wa msingi wa Makao Makuu kuhamia Dodoma?

Waheshimiwa Wabunge, kwa hali ilivyo sasa, kuna umuhimu wa kuwa na Ofisi Dar es Salaam na Dodoma. Ofisi hizo za Dar es Salaam na Dodoma, kwa sasa ni chakafu sana, kama nilivyosema. Dar es Salaam kuna Ofisi na mabanda ya mbao, ambayo yamechakaa sana, hayafai hata kukarabatiwa, isipokuwa kuyaondoa na kujenga upya. Wote ambaao wamefika Dar es Salaam, mnajua ukifika ile Ofisi ya Waziri Mkuu kule nyuma, Maofisa wetu wengi (*Senior Officers*), wanakaa kule kwenye mabanda mabanda tu. Haya ndiyo yanayokusudiwa, kwa kweli kuhakikisha kwamba, tunawapa mahali pazuri pa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa amesema, kwa kuwa *CDA* wanatengewa fedha kidogo za maendeleo, kwa nini iendelee kuwepo. Nilidhani angesema inatengewa fedha kidogo, kwa hiyo, waongezewe. Umuhimu wa kuwa na *CDA* Dodoma ni mkubwa sana. Kwa hivi sasa hicho Chuo Kikuu, ambacho nilikuwa naeleza pale Chimwaga, wakati wenzetu wa Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, walipokwenda pale wakaona eneo lile halitoshi. Wakaitaka *CDA* iwapimie. Kwa hiyo, ni wajibu wa *CDA* kwenda ku-survey na imefanya kazi nzuri sana, ime-survey kwa yale majengo ambayo Waheshimiwa Wabunge, tumehamia pale Kisasa, ni eneo ambalo limepimwa na *CDA* na wanaendelea kupima maeneo mbalimbali.

Kwa hiyo, kuna umuhimu sana wa kuwa na chombo ambacho maalum kitaendeleza Makao Makuu ya Taifa letu. Ukichanganya Halmashauri kwa maana ya Manispaa ukachanganya na ule uendelezaji wa Makao Makuu, moja lazima itafifia. Lakini lazima kuwe na chombo ambacho kazi yake kubwa kila wakilala wakiamka ni maendeleo ya Mji Mkuu wetu wa Tanzania. Kwa hiyo, *CDA* ni muhimu iwepo pale. Serikali inaendelea kujitahidi kuwapa pesa kidogo kidogo, kwa kadri mahitaji wanayohitaji na kwa kweli nia ya Serikali ni kuhakikisha *CDA* inakuwepo na inaendelea kupata *resources* za Serikali aweze kufanikisha kazi yao.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mbunge wa Muyuni, alisema Serikali ihakikishe kuwa, kero za Muungano zinapatiwa ufumbuzi, hili ni zito atalizungumzia mwenyewe Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini itoshe tu kusema, Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikutana na Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, wakazungumza na hayo waliyozungumza, Mheshimiwa Waziri Mkuu, atapata nafasi ya kuyazungumzia hapa.

Mheheshimiwa Spika, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mbunge wa Bumbwini, alisema Serikali iviendeshe vyombo vya ulinzi ili kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu. Haya yataelezwa vizuri na Waziri wa Usalama wa Raia na Waziri wa Ulinzi, jinsi gani vimewezeshwa. Nia ni kweli kuviwezesha. Tunakubaliana sana na alichosema Mheshimiwa Mbunge, kuviwezesha vyombo hivyo ili viweze kufanya kazi yake na kutekeleza kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo maeneo ambayo mimi niliona niyasemee, nimsaidie mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri Mkuu, maana yalikuwa mengi, yeze peke yake asingepata muda hata wa kuyaelezea na angesema peke yake angeweza kuchoka zaidi. Sisi Wasaidizi wake tumemsaidia mpaka hapo.

Mheshimiwa Spika, narudia tena, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, kwa ufanuzi mzuri na uliowasilishwa kwa lugha ya Kibunge, ya kistaarabu na iliyoleweka wazi wazi na nampongeza sana Waziri wa Nchi. Sasa tumalizie na Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Peter Pinda.

WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba niungane na Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye katika hotuba yake, ametoa pongezi kwa viongozi wote wa Kitaifa na viongozi ambaao hivi majuzi wameteuliwa katika ngazi mbalimbali ndani ya Chama cha Mapinduzi. Naungana naye kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, naomba kwa kweli nitumie nafasi hii, kuwashukuru sana viongozi hawa wa Kitaifa, kwa maana ya Rais, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa heshima kubwa sana waliyonipatia ya kulisaidia Taifa hili katika wadhifa ambaao sasa ninao. Najua wanafanya kazi kwa mujibu wa Katiba, kwa kushauriana. Kwa hiyo, kwa kweli wamechangia kwa kiasi kikubwa sana na hasa Rais mwenyewe, ambaye finally ndiye anayetoa uamuvi. Nawashukuruni sana.

Lakini naomba vile vile kuwashukuru sana wananchi wa jimbo langu la Mpanda Mashariki. Najua nawapokonya muda wao mwangi ambaao walitaka niwe nao, lakini nawashukuru kwa uvumilivu wao, kwa sababu wanatambua kwamba, dhamana hii nayo ni muhimu kwa Taifa letu. Kama alivyosema Naibu Waziri na mimi nitajitahidi kadri nitakavyoweza, kusaidia wananchi wangu.

Lakini kubwa naomba kwa kweli nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye ndiyo kiongozi wangu katika ofisi yake, kwa namna ambayo anatusaidia sana kutuongoza na kutuelekeza, kweli ni mtu wa kasi kubwa, lakini tutajitahidi sana kwenda naye, kwa kadri itakavyowezekana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nina hakika tutakuwa Wasaidizi wako, tutajitahidi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja 137 zimeelekezwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ni nyingi na sidhani kama tutaweza kuzijibu zote. Lakini kwa kweli naungana na Mheshimiwa Waziri, kuwashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge, kwa yale yote ambayo mmetueleza. Mengi kwa kweli ni kwa manufaa ya kuimarisha Ofisi ya Waziri Mkuu na tutajitahidi kuyazingatia sana ili tuweze kuboresha kazi katika maeneo ambayo, mengi mmeiyasema kwa nia ya kutusaidia. Naibu Waziri amejitahidi, amejibu hoja 22. Nataka nijitahidi nione kama naweza kujibu hoja angalau 50. Hizo nyingine tutazijibu kwa maandishi na tutawapeni kwa wakati muafaka.

Sasa naomba nianze na eneo ambalo lilizungumzwa hasa na Mheshimiwa George Lubeleje, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, lakini vile vile na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, kuhusu uendelezaji wa Mikoa ilio nyuma kimaendeleo. Jambo hili ni dhahiri ni la kisera na wengi katika vikao, mmekuwa mkilieleza na Serikali kwa kiasi kikubwa, imekuwa nayo ikijitahidi sana kujaribu kulizingatia jambo hili. Kwa maneno mengine, ni suala la vipaumbele katika utekelezaji wa bajeti zetu. Naamini jambo hili litaendelea kupewa umuhimu kadri uwezo wa Serikali utakavyokuwa unaongezeka. Lakini si hilo tu, katika bajeti ya mwaka huu wa 2006/2007, Mikoa kama vile Rukwa, Tabora, Lindi, Mtwara na Kigoma, kwa makusudi kabisa, imetengewa shilingi bilioni moja na milioni mia mbili, yaani kwa kila mkoa kama shilingi milioni 200 zaidi, kwa ajili tu ya kusaidia kuimarisha miundombinu katika maeneo hayo.

Mikoa ya mipakani, yaani Arusha, Mara, Kagera na Wilaya ya Mafia - Mkoa wa Pwani, nayo imeongezewa shilingi bilioni 2,605 katika kuzingatia rai hii nzuri ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kwa mwaka 2006/2007, Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara, umetengewa jumla ya shilingi 709 milioni na milioni 1,000 kwa ajili ya uendelezaji wa majengo katika Mkoa huo katika kujaribu kutoa msukumo zaidi wa ukamilishaji wa Makao Makuu.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili linahusu utumishi katika Halmashauri kwa ujumla. Eneo hili lilikuwa na wachangiaji wengi na mimi nawashukuruni sana, kwa sababu baadhi ya maeneo mliyoyagusa ni maeneo ambayo tunaamini kabisa tukiyazingatia, tutaweza kuyafanyia kazi vizuri zaidi. Mheshimiwa Lubeleje, Mheshimiwa Chitalilo, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Mkonga Ruhwaya. Kwa idadi hiyo, hawa wote wamechangia kwa namna moja au nyingine katika eneo hili.

Sasa naomba niseme maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge walitaka tuyazingatie. Moja, wanasema TAMISEMI iendelee kutatua tatizo la watumishi katika Halmashauri na viongozi wanaokaimu kwa muda mrefu wathibitishwe kama wana sifa. Aidha, Serikali ifuatilie upungufu katika hospitali ya Bombo ya Mkoa wa Tanga. Kila Halmashauri itatengewa ikama ya Wahasibu wanane na Wakaguzi wa Ndani watatu, ili kuziwezesha kufanya kazi kwa ufanisi. Mwaka wa fedha wa 2006/2007, Wahasibu 878 watapangwa kwenye Halmashauri mbalimbali ili kupunguza uhaba wa watumishi uliopo, kwa utaratibu ulioandaliwa kwa pamoja kati ya Hazina na TAMISEMI. Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI itashirikiana pia na Wizara ya Afya, kutafuta mbinu mbalimbali za kujaza nafasi wazi katika Hospitali ya Bombo, ambacho ni kilio chake cha kweli na nadhani itabidi tufanye kila linalowezekana. Serikali imeamua kuwapeleka watumishi wa Afya na Elimu moja kwa moja, bila kufanya tena usaili kama ilivyokuwa hapo awali. Hili nalo tunaamini litasaidia sana, kuongeza kasi ya kujaza nafasi zilizo wazi.

Mwisho, Wizara zote za kisekta zimetakiwa kufanya tathmini ya upungufu wa watumishi katika ngazi ya Halmashauri, Kata na Vijiji na kisha kwa pamoja, tutachukua hatua ambazo tunaona zitaweza kupunguza tatizo hilo kwa kiasi kikubwa. Ipo hoja kuhusu Hospitali ya Mkoa wa Mara kwamba, haina Daktari Bingwa. Eneo hili ni la Sekta ya Afya, lakini kwa upande mwingine na sisi tunahusika vile vile, kwa sababu liko katika Mikoa yetu. Tutashirikiana na Wizara ya Afya, kujaribu kuona ni namna gani jambo hili linaweza likapata ufumbuzi.

Serikali ina mkakati gani katika kupunguza uhaba wa walimu wa shule za msingi? Nalo hili ni la Sekta ya Wizara ya Elimu, lakini sisi ni wadau wakubwa sana katika eneo hili. Ni vizuri nikatangulia kuishukuru Wizara hii na Serikali kwa ujumla kwamba, chini ya Mpango wa MMEM na Waheshimiwa Wabunge ninyi wote ni mashahidi, kumekuwa na jitihada kubwa sana kutoa mafunzo kwa walimu, ambayo kwa kiasi fulani wametusaidia kupunguza tatizo la walimu katika shule za msingi. Kama nilivyosema, Waziri anayehusika pengine atatoa ufanuzi wa kina atakapokuwa ajibu wakati wa Bajeti yake. Wakurugenzi wa Halmashauri wapunguze safari za kuhudhuria semina. Tunalikubali lipo na kwa kweli kwa sasa ni tatizo kubwa na limepunguza uwajibikaji katika Halmashauri kwa kiasi kikubwa sana. (*Makofî*)

Mara zote wanapoondoka, leo ataachiwa Afisa Utumishi kukaimu, kesho ataachiwa Mweka Hazina, keshokutwa Mkuu wa Idara. Kwa utaratibu huu ni vigumu sana kupima uwajibikaji kwa karibu wa Mtendaji Mkuu katika Halmashauri. Kwa sehemu kubwa inawezekana na sisi Serikali katika mipango yetu, hatukujipanga vizuri. Kwa hiyo tumekubaliana kwamba, tutajitahidi tutafute utaratibu mzuri zaidi, wakati Wakurugenzi hawa watakapoitwa kwenye jambo moja, basi na Wizara nydingine zitumie mwanya huo kukutana nao, kujaribu kutoa maelekezo mengine, ili kupunguza safari hizi zilizo nydingi. Lakini kwa upande mwingine, tumeamua kwamba, tutapeleka maelekezo mahsus kwa Wakuu wa Mikoa wote ili jambo hili liweze kudhibitiwa kwa karibu zaidi, kwa kuhakikisha kwamba, Mkuu wa Mkoa atakuwa ndiye anayeidhinisha safari za kila Mkurugenzi anapotaka kutoka nje ya kituo chake. Lakini vile vile kwa kujua kwamba, inawezekana tusipunguze kabisa tatizo hili, ofisi yangu inaangalia utaratibu wa kuwa na Naibu Mkurugenzi, ili mmoja anapotaka mwingine abaki pale, tujue kwamba uwajibikaji uko kati ya mtu mmoja na wa pili na siyo kama ilivyo hivi sasa. (*Makofî*)

Watendaji wa Serikali wasijihushe na siasa, jambo hili likitokea ni uvunjaji wa taratibu tu. Upo Waraka Na. 1 wa 2000, upo bayana kabisa, ambao umeweka mtumishi anayeweza kujihusisha katika masuala ya kisiasa. Lakini kamwe hatutegemei kwamba, kutakuwa na Mtendaji, ambaye ameamua kujiingiza moja kwa moja na kujaribu kupanga nani awe kiongozi wakati wa uchaguzi wowote ule. Kwa hiyo, tutaifanyia kazi kwa kujaribu kubaini maeneo ambayo pengine jambo hili limejitokeza kwa nguvu ili kuweza kurekebisha kasoro hiyo kwa siku zijazo.

Lakini tumewataka Wakurugenzi, kwa maandishi, wahakikishe wanasimamia Waraka huo vizuri kwa sababu wao ndiyo wanasimamia watumishi katika Halmashauri husika. Watumishi wa Umma katika ngazi mbalimbali, wazingatie wajibu wao na wasisubiri kusukumwa na viongozi. Ushauri umepokelewa na tayari tumeshaanza

mipango mbalimbali ya kujaribu kusimamia jambo hili ili kwa kweli tija inayotegemewa iweze kupatikana.

Maslahi ya Maafisa Watendaji wa Mitaa na Maafisa Watendaji wa Vijiji, yaangaliwe upya na kuboreshwa na mishahara yao ilipwe kwa wakati ili kuepusha urasimu, ambao sasa kwa kweli umekuwa ni kero katika baadhi ya Halmashauri. Nia ya Serikali ni kuboresha maslahi ya watumishi wake wote, wakiwemo Watendaji hawa. Kwa mwaka 2006/2007, Serikali itahuisha mishahara ya wafanyakazi wa Serikali za Mitaa ili ilingane na watumishi wa Serikali Kuu, kwa ngazi zile zinazoenda sambamba.

Kwa upande mwingine Waheshimiwa Wabunge, Serikali ilikwishatoa maelekezo hapa kwamba, mishahara ilipwe kila tarehe 25, lakini jambo hili bado mnaona linajitokeza, linakwenda zaidi ya tarehe 25. Kwa hiyo, tumedhamiria kupunguza tatizo kama si kulikomesha kabisa, ingawa tumegundua kwamba, moja ya sababu ya ucheleweshaji ni wao wenyewe kuchukua *pay roll* kutoka Hazina. Maana kila mkoa unapewa mtu mmoja, akichelewa kwenda, basi maana yake Mkoa mzima utakuwa umechelewesha jambo hili. Tumedhamiria kabisa kulimaliza jambo hili na hatudhani kwamba, tutaendelea tena kuhojiwa juu ya tatizo hili kucheleweshwa.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Watendaji katika Halmashauri ya Kilindi, wana lugha chafu. Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, tumelipokea jambo hili. Tatalifuatilia kwa karibu na bahati nzuri nilipokuwa kwenye ziara, nilipata nafasi ya kusikia minong'ono minong'ono kama hiyo na kuahidi kwamba, itarekebishwa mapema kadri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ratiba ya vikao, tutalisimamia vizuri, tutatoa maelekezo kwa mara nyingine tena. Ili wakati itakapowezekana, vikao vya Halmashauri, vizingatie kwa kiasi kikubwa, vikao vya Bunge ili muweze kupata nafasi ya kushiriki katika vikao hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu watumishi kukaa kwa muda mrefu katika vituo, mimi mwenyewe nimeshuhudia hilo, nimekwenda maeneo mengine watu wamekaa kwa miaka 25, baadhi ya maeneo miaka 28, walishapoteza hata sura ya utumishi wa umma. Kwa hiyo, tunalifanyia kazi jambo hilo na tunadhani ndani ya kipindi si kirefu sana, basi tutakuwa tumeshachukua hatua za kurekebisha kasoro hiyo, ambayo kwa kweli kwa kiasi kikubwa, inaathiri utendaji. Lakini naomba tu niseme, kwa sababu zoezi litakuwa karibu la nchi nzima, la kuwahamisha watu ambao wamekaa kwenye vituo kwa muda mrefu na ni la gharama, tatalizingatia vile vile. (*Kicheko*)

Baadhi ya viongozi hawana uwezo wa kazi, ofisi yetu inaendelea na utaratibu wa kutoa mafunzo kuwajengea uwezo Watendaji wote na viongozi wote. Lakini nataka nikiri tu kwamba, pamoja na juhudhi hizo, tunaathirika sana na chaguzi ambazo zinalazimisha sasa kuwepo na viongozi wapya, kila baada ya miaka mitano na sehemu nyingine zaidi ya asilimia 50. Kwa hivi sasa tunaandaa tena utaratibu wa kutoa mafunzo ili kujaribu kuwawezesha hawa wapya nao waweze kwenda pamoja na wenzao.

Mtumishi akiharibu katika kituo kimoja awajibishwe pale pale alipo. Nakubaliana kabisa na kwa kweli ndiyo juhudini tunazofanya sasa lakini kwa kuwa baadhi ya Wabunge walilisemea sana jambo hili, naomba tu niongezee kwamba, nia ya maelekezo tuliyoyatoa kwa Wenyeviti na Mameya, haikuwa kuwanyamazisha kuwachukulia hatua watumishi wabovu, tulichokuwa tunawasaidia ni kwamba, sheria, taratibu na kanuni, lazima zizingatiwe wakati mnapitisha maamuzi yenu. Rai yangu ni kwamba, hawa ni watumishi na lazima muda wote tutajaribu haki zao kwa kuwatendea kile ambacho inatakiwa tuwatendee kisheria. Nimewaambia Wenyeviti wote, chukueni hatua, lakini zingatieni utaratibusi huo.

Mheshimiwa Spika, ninalo tatizo ambalo Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, alilieleza la Kata ya Kansari, kuhusiana na Mtendaji wa Kata ambaye alimtorosha mtu ambaye alikuwa ni mhali. Tunaomba tuseme kwa kweli tu kwamba, Mtendaji huyu alituhumiwa kumtorosha mbakaji, sheria ikachukua mkondo wake akashtakiwa. Lakini Mahakama ikamwachia kwa vile ushahidi haukutosha. Tunachoweza kusema hapa, tutajaribu kulifua tilia kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria, kama uwezekano wa rufaa upo, basi tutafanya hivyo, ingawa muda kwa kweli umepita sana. Hili la mahakimu ambalo Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa alilieleza, kwa kweli tutaliwasilisha tu kwenye Wizara ya Sheria na Katiba, wanaweza kuwa na ufumbuzi juu ya eneo hili.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni viongozi wa kuchaguliwa katika Halmashauri na namna ambavyo Waheshimiwa Wabunge, tulitaka tuwasaidie au kuwahudumia. Moja, ni la posho ya Madiwani. Naomba tu tulipokee, ni mapema sana kusema jambo lolote lakini tunaamini Serikali itakapofikia mwisho, tutapata majibu ya namna gani pengine jambo hili linawenza likashughulikiwa. Lakini *process* inaendelea na tunaamini haitachukua muda mrefu, kutoa kauli ya mwisho. Baadhi yao inaonekana kwamba, uwezo wao ni mdogo, tunalikubali na sababu ziko wazi. Kigezo kikubwa kwa kweli kwa chaguzi zetu zote hizi ni kujua kusoma na kuandika, lakini ni dhahiri kuwa, kazi kubwa iliyomo katika Halmashauri, fedha nyingi zinazokwenda huko na utaalam unaotakiwa katika maeneo haya, jambo hili linahitaji mafunzo zaidi ili tuweze kuwasaidia Waheshimiwa Madiwani, kuweza kusimamia majukumu yao.

Kulikuwa na hoja vile vile ya kuwawezesha kimaslahi Wenyeviti wa Vitongoji, Vijiji, pamoja na Masheha, ili kuweza kuboresha mambo yanayohusu maslahi yao. Hili la Masheha, naomba pengine walitazame kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa sababu sisi Bara tunao Madiwani, kule Zanzibar wanao Masheha. Lakini kwa hawa viongozi wengine wa Serikali za Mitaa, tunaloweza kusema ambalo tumekuwa tunalisema muda wote, tumeshazia Halmashauri lakini tutazia tena kwamba, zamani walikuwa wanapata asilimia 20 kutokana na vyanzo walivyokuwa wanakusanya. Serikali inawarejeshea vyanzo ambavyo tumefuta. Viongozi hawa ni chachu kubwa sana katika maendeleo. Tumekwisha washauri, tatarudia kuwaambia watafute taratibu zitakazowezesha kurejesha ule mfumo wa posho ile ndogo, walivyokuwa wanapata kwa sababu ilikuwa ni motisha kubwa kwao.

Eneo la nne ni TAMISEMI na Mikoa kuimariswa. Tumepokea ushauri ambao ulitoka kwa Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, lakini nilitaka nimhakikishie tu kwamba, kwa sasa tayari katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikao na Serikali za Mitaa, tumekwisha unda Idara ya Uendelezaji Taasisi na chini ya Idara hii, kiko kitengo cha ukaguzi wa shughuli za Serikali za Mitaa na Kitengo cha Ufuatiliaji wa utoaji huduma katika Serikali za Mitaa (*Service Delivery*). Kwa kutumia vitengo hivi viwili, ndiyo tutaboresha kabisa usimamizi wa mikoa yetu na sisi wenyewe katika ofisi yetu.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine, utaratibu wa Wakuu wa Mikoa kuwa Washauri wa Halmashauri uangaliwe upya. Mheshimiwa Waziri Mkuu, pengine atalizungumzia kidogo. Tunaendelea kuliangalia hili ili tuweze kuimariswa usimamizi wa karibu kupitia mikoa na wilaya katika halmashauri zetu. Nafasi ya Wakuu wa Wilaya walivyo sasa, hawana kazi. Ilitolewa hoja hii na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Serikali inaomba kutofautiana naye na sababu ziko nyingi tu. Kwa ukubwa wa nchi ya Tanzania ulivyo, itakuwa kweli ni kujidanganya kama tunafikiri tunaweza kufuta Wilaya na Mkuu wa Wilaya. Huyu ni mwakilishi wa Rais katika ngazi hiyo. Anasaidia sana sana katika kusimamia suala zima la ulinzi na usalama, lakini wengi wenu ni mashahidi Wakuu wa Wilaya hawa ndiyo wanaotembea vijijini, pengine kuliko hata Wakurugenzi wao. Ukiwaondoa hawa, muwe na uhakika mtaanza kurudi nyuma kwa kiasi kikubwa sana. Ni kiungo muhimu sana na ninaomba sana wazo hili si vizuri mkaliendeleza. Tutafute namna ya kuboresha utendaji wao. Lakini ni dhahiri, haiwezi kuwa ni kufuta nafasi ya Mkuu wa Wilaya. (*Makofii*)

Wakuu wa Mikoa wawe viongozi wa kuchaguliwa ili wananchi waweze kupata fursa ya kusimamiwa na watu ambao wamewateua wao wenyewe. Nalo hili haliwezekani, kwa sababu kwa mkondo wa *Executive Arm*, Rais anawakilishwa katika Mkoaa na Mkuu wa Mkoaa na katika Wilaya na Mkuu wa Wilaya. Sasa na Rais mmemkubali kwamba, anayoyatenda yale ni dhahiri ni kwa ajili ya kusaidia umma, sioni tatizo kwa nini Mkuu wa Mkoaa muwe na mashaka naye. Sioni kwa nini muwe na mashaka na Mkuu wa Wilaya, mtakalolifanya ni kuimariswa ofisi hiyo, ili yale maeneo ambayo yanaonekana kuwa na upungufu yaweze kuimariswa vizuri zaidi.

Eneo la tano linahusiana na mahusiano zaidi kati ya TAMISEMI na Wizara za Kisekta na hili Mheshimiwa George Lubeleje, ametaka sana Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ishirikiane kwa karibu na Wizara nyingine. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa George Lubeleje kwamba, upo ushirikiano mkubwa sana kati ya TAMISEMI na Wizara za Kisekta na hata mambo mengine ambayo mnayaona yanakwenda kwa *speed*. Sasa kupitia Wizara ya Fedha na Wizara nyingine za Kisekta kama Utumishi, ni kwa sababu ya mashirikiano makubwa ambayo yapo sasa. Tutakachofanya ni kuyakuza na kuyaendeleta ili hili alilolisema, liweze kufikiwa kwa asilimia kubwa.

Vigezo vya kugawa fedha za maendeleo, tumepata mchango kutoka kwa Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Estherina Kilasi na wengine ambao walichangia eneo hili. Mimi naelewa Waheshimiwa Wabunge wanachosema na nina hakika hata Waheshimiwa Wabunge wote mnaelewa wanachosema. Inaonekana kana kwamba, wanaponyimwa ile fedha ya maendeleo, wanaoumia ni wananchi na ni jambo la

kweli, kwa sababu linagusa maendeleo yao. Naomba niseme tu kwamba, fedha hizi ni mkopo tumetoa Benki ya Dunia. Imani yao ni kwamba, fedha ile itatumika vizuri, itatokana na umahiri wa Halmashauri kuweza kuonyesha kwamba, ina uwezo wa kusimamia fedha vizuri. Vigezo vyake si vikubwa sana, ni vya kawaida kabisa. Kwa hiyo, tunachotaka kusema hapa ni nini?

Tunataka tujitahidi kuhakikisha hawa watendaji ambaو wanashindwa kutimiza vigezo vidogo kama hivi, wanachukuliwa hatua. Naomba niseme kwa dhati kwamba, Madiwani halali kwao vile vile ingawa ni kweli Madiwani Kamati ya Fedha na Uongozi, inakutana kila mwezi kupitia maeneo haya, lakini kama mwisho wa safari, utapata Hati Chafu ni dhahiri wataalam hamkumshauri vizuri. Kwa hiyo, nadhani hili tutajitahidi sana kuwabana ili jambo hili liweze kufika mahali na kumalizika katika kipindi kijacho.

Najua yapo mawazo kwamba, kigezo cha hati safi si vigezo pekee na mimi nalikubali kwa sababu hali halisi wakati mwingine kwenye miradi sivyo ilivyo, unapotazama kiwango cha fedha kilichopo. Lakini kwa sasa kigezo hicho ndicho kinachotumika Serikali Kuu, kigezo hicho ndicho kinatumika Serikali za Mitaa. Sasa safari hii ni Halmashauri nne tu ndizo zimekosa kigezo hicho. Tutajitahidi tuzisukume zote hizi, awamu ijayo na zenyewe ziweze kunufaika na jambo hili. Lakini kwa ujumla wake, Serikali na hasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, pengine atalidokezea vile vile, tumedhamiria kujaribu kama linaweza likazungumzwa tena na wahisani, ambaو ndio tulikubaliana nao, kuona kama tunaweza kupata *feasibility* ili wananchi kwa hoja mlizozitoa, waweze kunufaika moja kwa moja na tupambane na hawa ambaو ndiyo kikwazo katika maendeleo ya Halmashauri husika.

Mheheshimiwa Luhaga Mpina, alitaka zile halmashauri ambazo hazikufanya vizuri, basi pesa zilizotoka kwa wale waliofanya vibaya, ziende kwa wale waliofanya vizuri zaidi. Anatumia msingi ule ule, aliyenacho aongezewa zaidi. Utaratibu ulioko si kwa maana hiyo ya Mheshimiwa Luhaga Mpina, hapana, ni kwamba chini ya utaratibu huu ikio *bonus* inayotolewa kwa wale waliofanya vizuri, ni kuwatia moyo ili wasirudi nyuma tena kwa yale ambayo wamesha-*achieve* ili waweze kusaidia wananchi wao. Kwa hiyo, tunadhani ni utaratibu mzuri, hauna nia hata kidogo ya kujaribu kupokonya kwa wale ambaو wameshindwa, lakini ni kuwataka na hao wengine waweze kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika na mimi nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, nimefurahi sana nilipopita katika baadhi ya mikoa hivi majuzi kuona kwamba, Madiwa sasa wanawacharukia kweli kweli Wakurugenzi, kwa nini tumekosa fedha ya maendeleo. Ni jambo zuri na mimi nataka niwatie moyo, waendelee kuwacharukia hivyo hivyo ili waweze kujua kwamba, wananchi hawako tayari tena kuendelea na Mkurugenzi, ambaye hawezi kutimiza wajibu wake vizuri.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingi kuhusiana na hali za barabara za Jiji la Dar es Salaam, ni jambo kubwa na zito, naomba basi Mheshimiwa Waziri Mkuu, pengine ukipata nafasi, ulizungumzie hili ili tuweze kuwasaidia Waheshimiwa Wabunge, kuelewa jitihada zinazoendelea.

Uanzishwaji wa maeneo mapya ya utawala, nalo hili limechangiwa na Wabunge wengi; Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Benedict Losurutia, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi na wengine, ambao pengine naweza kuwa siku-*take note*.

Tunaloomba hapa tueleze ni kwamba, jambo hili kwanza ni kubwa, kwa maana *implications* zake kila unapoamua kuongeza eneo moja, maana yake umeongeze mzigo wa kifedha kwa upande wa Serikali. Hizi Halmashauri chache tulizoziazisha na wilaya hizi chache ambazo zimeanzishwa na Rais mara ya mwisho, bado unaona zinatuletea tatizo hata kwenye bajeti hii.

Kwa maana ya miundombinu nyumba zao za kuishi, ofisi zao, magari ya kuwawezesha kuhudumia vizuri wananchi, imegeuka sasa imekuwa ni kikwazo katika kujaribu kuendelea na zoezi hili. Lakini kwa maana ya kupata maamuzi ya msingi, naomba niseme kwa ujumla kwamba, tumeamua kufanya zoezi hili kwa upana wake wote, bila kusubiri maombi. Tutachambua mikoa, Wilaya, Halmashauri, Kata, Vijiji na hata Vitongoji, kulingana na vigezo. Kwa sababu maelezo na takwimu kwa sehemu kubwa tunazo, pale tutakapokosa tutaomba msaada kutoka kwenye maeneo husika. (*Makofii*)

Mtihani utabaki ni pale kusema sasa nani anaingia kwenye awamu ya kwanza na nani atafuata baadaye, kwa kulingana na uwezo wa Serikali yetu kwa siku zinazokuja. Lakini naomba niseme kwa dhati kabisa kwamba, jambo hili tumeona tulifanye kwa sababu hatuoni kwa nini tuendelee kuombwa wakati vigezo vinafahamika, tutakaposhindwa tutaomba msaada wenu.

Kuzuka kwa ugonjwa usioeleweka dhidi ya watoto kama mtakumbuka, Mheshimiwa Wilson Masilingi, alilieleza jambo hili kwa uchungu mkubwa sana. Naomba tu ni wahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, tulimtaka Mkuu wa Mkoo atupe taarifa juu ya jambo hili. Alithibitisha kwamba, kweli tatizo lipo na kwa hiyo, tukamwarifu Mheshimiwa Waziri Mkuu na akatoa maagizo wakati ule ule, kumtaka Waziri wa Afya, aende Kagera na Timu yake na ndio maana hamumwoni hapa Bungeni, kwa sababu yuko huko. Tunaomba tufanye subira Wabunge wote wa Kagera, atakaporudi Mheshimiwa Waziri, basi tunaamini, atatoa maelezo ambayo yatasaidia kuonyesha ni tatizo gani na ukubwa wake ni kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ilifuta baadhi ya vyanzo vya mapato katika Halmashauri zetu, lakini misingi mikubwa na ninyi wote siku ile mlishangilia sana, illikuwa ni kuondoa vyanzo ambavyo vilikuwa ni kero kwa wananchi wetu. Lakini tukisema vilevile baadhi ya vyanzo vilikuwa vinakusanya kwa gharama kubwa mno, wakati unachokwenda kupata ni kidogo sana, hakikuwa na tija hata katika Halmashauri, kwa hiyo, tukaamua tuziondoe. Lakini kwa kufanya hivyo, Waheshimiwa Wabunge, hatujasema Halmashauri haiwezi kuendelea kubuni vyanzo vingine vya mapato, la hasha,

bado wanaweza. Sisi tutakachowabana ni kuona kama chanzo hicho ni kero au kiko pale na kinaweza kutoa huduma bila kusababisha vurugu kwa wananchi. Kwa hiyo, raia wasidhani tumefunga mlango, waendelee na baadhi yao wamekuwa wakifanya hivyo.

Lakini cha msingi naomba niseme, tangu Serikali ilipofanya uamuvi huu na wakati ule ilikuwa ni kwamba, tulipofanya mahesabu ikaonekana kiwango cha fedha tulichoondoa ilikuwa ni kama theluthi moja ya mapato ya Halmashauri. Serikali ikaamua kuanza kutoa kiwango hicho chote. Kwa hiyo, tulipoanza mwaka 2003 tulitoa shilingi bilioni 22.9, mwaka 2004/2005 shilingi bilioni 25, mwaka 2005/2006 shilingi bilioni 40.1 na mwaka 2006/2007 zimetengwa shilingi bilioni 43. Tatizo kama nilivyogusia, wakati tulipokuwa tunaeleza jambo hili kwenye swalii, Halmashauri nyingi sasa baada ya kuona, maana fedha hii ni ya uhakika, sio kama ya kukimbizana na wananchi, hili ni suala la Serikali, muda ukifika inatoa. Sasa wengi wao wamelegeza kamba katika makusanyo ya mapato yao, wengi hawafikii asilimia 100 ya malengo yao na ndio maana ya kupitia sasa Mikataba hii ambayo tutawekeana nao, ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ataaelezea. Tunataka tuwabane, kila mmoja atimize wajibu wake, Serikali inatimiza wajibu wake na wao watimize wajibu wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, iko migogoro ya mipaka, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, aligusia ule wa Kilindi, lakini si Kilindi tu, tuna matatizo ya mipaka katika maeneo mengi kidogo na hivi leo umemsikia Mheshimiwa John Lwanji, naye alikuwa anazungumza juu ya mpaka wake kati ya Sikunge na Manyoni. Kwa hiyo, matatizo yanafahamika na tumedhamiria kwa kuwa tumekuwa tukifanya *piece meal*, tutashirikiana na Wizara ya Ardhi, sasa kujaribu kufanya kazi nchi nzima. Itakuwa gharama kubwa, lakini tumeona tukalifanye, tunawaomba tu Waheshimiwa Wabunge basi, mshirikiane kwa karibu sana na Wizara hizi mbili, pale tutakapofikia maamuzi ambayo pengine hayapendezi sana. Maana hatuamini kwamba, itabidi tuanze kunyoosha mipaka sasa kulingana na matakwa ya watu, mipaka hii ipo, kazi yetu itakuwa ni kuiweka bayana na wananchi wataamua kukaa upande wowote wanaoutaka, utadhani kwamba, kutakuwa na bughudha katika jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, tunaomba vilevile tuliarifu Bunge lako kuwa, tutaanza utaratibu mwaka huu wa fedha wa kuimarisha Mabaraza ya Ardhi Vijijini. Ni vyombo muhimu sana hasa katika kutatua migogoro midogo midogo ya ardhi, ili watu waweze kuishi bila matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni bajeti ya Halmashauri mpya. Mtakuwa mmesikia baadhi ya Wabunge wamelisema hili, Mheshimiwa Anna Makinda alilisema, lakini nadhani Korogwe, Manyara, Babati pale nalo limesemwa. Naomba tu nieleze kwa kifupi kwamba, hatujaamua kufuta uamuvi wa kuanzisha mamlaka hizo hata kidogo, ni utaratibu tu wa kufungua *accounts* kwa ajili ya Halmashauri hizo, ambao ndio umechelewesha jambo hili.

Kwa hiyo, kwa kipindi kijacho, pengine hiki tulichokianza, tunaomba Waheshimiwa Wabunge, wanaotoka katika maeneo ya Njombe na maeneo mengine

kama Mpanda kule, basi tufanye subira kidogo, ili *accounts* zile ziweze kufunguliwa kwa utaratibu unaokubalika chini ya maelekezo ya Wizara ya Fedha.

Kwa sasa fedha zile zitakwenda kwenye Halmashauri zile tunazozita mama, lakini zitakwenda kufanya kazi Halmashauri hizo tulizozianzisha na miradi ile itasimamiwa na Halmashauri hizo. Wao kazi yao ni kuondoa fedha kwenye akaunti na kupeleka kwenye mradi unaohusika. Nadhani nimejitahidi kulieleza jambo hili kwenye barua. Mheshimiwa Kwaangw' kinachotakiwa ni kuwaondoa wasiwasi na kama kuna tatizo, naomba tuwasiliane ili tuweze kufanya marekebisho yanayostahili.

Eneo lingine ni la wananchi kuhamishwa kutoka *Makonde Prattle*, suala hili lilisemwa na Mheshimiwa Raynald Mrope, nimeona niliseme hili kwa sababu lilikuwa ni jambo ambalo analizungumza mara nyingi. Kwa kifupi ni kwamba, tulifikia uamuzi wa Serikali kwamba, hawa wananchi hawawezi kulipwa fidia, ndio ulikuwa uamuzi wa Serikali. Mheshimiwa Raynald Mrope, akasema haiwezekani, naomba basi walipwe angalau kifuta machozi, tukamshauri ajenge hoja. Hoja haikujengwa, isipokuwa alionana na Naibu Waziri Fedha, akamwambia bwana, basi tuletee hiyo hoja pamoja na orodha ya majina ya wale wote amba wanastahili. Tatizo limekuwa ni hiyo orodha, TAMISEMI hatuitengenezei na wala hatujaletewa, tumeomba Mkoa utengeneze hiyo orodha ya majina ya wale wote amba waliathirika na zoezi hilo, tuweze kuliwasilisha Wizara ya Fedha na sisemi kwamba, tukiliwakilisha fedha hiyo itapatikana. Tutakuwa tunapeleka kama maombi, kama Wizara itakuwa na uwezo, *alhamdullilah*, wanaweza wakapata, kama haina itabidi tuendelee kuomba mpaka hapo jambo hili litakapokuwa limefika mahali pake.

Mheshimiwa Spika, ziko rai zilitoka kwa Waheshimiwa Wabunge kadhaa, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Samuel Chitalilo, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Mgana Msindai na Mheshimiwa Benson Mpesya, kuhususiana na sheria ndogo kwamba, ziangaliwe upya ili kuona kama zinakidhi mahitaji na mabadiliko yaliyopo hivi sasa. Aidha, Halmashauri za Wilaya, Manispaa, Miji na Majiji, ziangalie uwezekano wa kutumia sheria ndogo ili kudhibiti janga la UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutunga sheria ndogo za Halmashauri, kwa kawaida unaanzia kwenye Halmashauri zenyewe, Waheshimiwa Wabunge ni Wajumbe katika mabaraza hayo. Kama ambavyo tumekuwa tukisema muda wote, ninyi ni chachu kubwa sana, upeo wenu ni mkubwa kweli kweli, mkiwepo katika Mabaraza haya, naamini hakuna litakaloharibika. Kwa hiyo, raia yangu kwa hili, mjaribu kuwa karibu na Halmashauri zenu, hata kama kwa kupigiana simu, kuwataka wajaribu kuandaa hata rasimu baadaye mkazipitia, mkazirejesha na hatimaye zikaja kwetu. Ofisini kwetu tumejipanga vizuri, hakuna *by-law* inayokuwepo pale ikakaa siku hiyo ikalala, ni siku hiyo hiyo tunaondoa inarudi ilikotoka. Kwa hiyo, tunaomba hili jambo mlikazanie ili tuweze kusaidiana kwa pamoja, tuweze kulifanikisha. Lakini tumeona kwa kuwa kuna mapungufu katika Halmashauri hizi, tumeamua sisi kutengeneza sheria ndogo za mfano, kwenye maeneo yote ambayo tunafikiri yatasaidia Halmashauri. Tumekamilisha mazingira, tunaenda sasa maeneo mengine ya kilimo, UKIMWI, elimu na kadhalika, ili tuweze kuzisaidia sasa kwenda kwa haraka zaidi katika kuandaa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa George Lubeleje, alitaka vilevile Wakuu Wilaya tuwape magari, tunajitahidi tatizo ni uwezo wa Serikali. Mwaka 2005/2006, tumeweza kununua magari 28 tu na mwaka huu kwenye bajeti ya safari hii, tutaweza kununua magari 40. Tutaendelea kuongeza kadri uwezo utakavyokuwa unapatikana, ingawa kwa kweli tungependa wapate magari kwa mkupuo wote, ili usimamizi wa shughuli za maendeleo uweze kwenda kwa uwiano unaofanana. Lakini tatizo ni hilo la fedha.

Kuwepo programu za utekelezaji wa ajira kwa ajili ya vijana na wanawake katika Halmashauri na kutafuta rasilimali zinazohitajika kwa ajili ya makundi hayo. Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Benson Mpesa na Mheshimiwa Mgana Msindai, wote hao wamejaribu kutoa raia hiyo na kwa kweli tunachowenza kusema moja, ni kuishukuru Serikali na hasa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa uamuzi wake wa kuanza na zile shilingi milioni 500.

Kazi ya Halmashauri hapa kwa kweli itakuwa ni kujipanga vizuri ili tuweze kutimiza azma ya hoja ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wajumbe. Tunaendelea vilevile kuhimiza Halmashauri kuhusiana na asilimia kumi, iendelee kutengwa katika Mfuko wao, lakini tumesema vilevile tumekubaliana kiofisi, tutoe msukumo maalum kwa ajili ya *SACCOS*, kwa kushirikiana na Wizara inayohusika. Hapa tunaomba vilevile Waheshimiwa Wabunge, mtusaidie sana kutohana na uwezo wenu mkubwa katika eneo hili. Ofisi ya Waziri Mkuu, iweke utaratibu utakaowezesha kutolewa kwa ruzuku kwenye mbolea. Hili nadhani nitalizungumza na Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika na Ofisi ya Waziri Mkuu, iandae semina kwa Wabunge, kuwaelimisha kwa undani shughuli zitakazotekelawa mikoani. Hili kama tulivyosema, tumekwisha anza na tutalikamilisha baada ya muda si mrefu.

Eneo lingine ambalo nataka nilisemee kidogo, ni utendaji kazi wa Maafisa Watendaji wa Kata kwamba, uangaliwe upya kwani kuna baadhi wanabambikiza watu kesi. Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, tunaomba tukuhakikishie kuwa, tutajitahidi, tumekuwa tunalisema sana, lakini tutajitahidi kujaribu kuona hatua za dhahiri, ambazo zinaweza zikasaidia kuondokana na hawa miungu watu, watu ambaa wanaona wao ndio wakubwa kabisa pale na kikubwa katika eneo hili ni kuwa na watu wenye upeo wa kielimu. Ndio maana tunasisitiza awe darasa la 12 au la 14. Sasa hatunao sawa, lakini tumekubali wale wa darasa la saba waendelee kwa kipindi cha miaka mitatu, baada ya hapo ni bora tukachelewa lakini tukawa na watu wenye kiwango cha kutosha, hili tutalitilia mkazo ili tuweze kuwa na viongozi wenye uwezo wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri hazifanyi kazi vizuri, fedha zinazopelekwa ni nyingi lakini bado kama mnavyosema Waheshimiwa Wabunge, ni tatizo kubwa na mimi naomba niseme changamoto niliyonayo, kama Msaidizi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, hapa ni namna ya kujaribu kuimarisha uadilifu katika Serikali za Mitaa, wengi wana uwezo, lakini uadilifu ndio tatizo kubwa. (*Makofit*)

Sasa hili chini ya uongozi wake tunajaribu kuliangalia, kwanza, kutazama mikakati lakini hasa ni kuongeza uwazi zaidi katika ngazi ya Halmashauri na hili tumelianza. Tunaomba tuseme, tutawatumia sana hawa *internal auditors* katika eneo hili, kwa kuwa ndio wanaojua mambo mengi vizuri, lakini mara nyingi yanapuuzwa na Wakurugenzi. Tukiwatumia hawa vizuri, tunaamini tutafanya mambo makubwa katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Same, haikusanyi mapato yake. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Anna Kilango Malecela kuwa, tutalivalia njuga, tutataka kujua ni kwa nini na naamini tutapata ufumbuzi, kama si kwa njia hii ya mkato, lakini kwa kupitia *performance agreement* ambazo zitaelezwa hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, zipo Wilaya nyingi zenyenye majimbo zaidi ya moja, Halmashauri zijaribu kugawa miradi kwa usawa. Suala hili naliafiki kabisa, hujakosea Mheshimiwa Anna Kilango Malecela, katika jambo hili na kwa kweli ndio utaratibu. Lazima maendeleo ndani ya Wilaya, ambayo ina zaidi ya Jimbo moja, tujitahidi kuweka uwiano wa maendeleo. Miradi yetu lazima izingatie hilo. (*Makofî*)

Lakini changamoto kubwa ni kwamba, wale wanaopanga mipango hiyo ni Madiwani wenyewe, ukiona pameharibika, ni rahisi kujua kwa nini pameharibika. Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyo sema, kwa kuwa wote tuko katika gurudumu hilo, mkipata nafasi hasa wakati wa kuitisha bajeti zetu ni muhimu sana ili muweze kujua mipango ipo na wapi pamekwenda upande bila kuzingatia uwiano ninaousema.

Hili la Maafisa Ugani, wamelisema kwa kweli Wabunge wengi na mimi nawashukuru sana, kwa mawazo waliyoyatoa, lakini nadhani Waziri wa Kilimo, atalizungumzia vizuri zaidi, kwa kuwa ni jambo ambalo linatugusa wote. Hali kadhalika hili la kuweka msukumo mpya katika matumizi ya mbolea na kuwepo kwa malengo ya kilimo katika Kata, Wilaya na utaratibu madhubuti wa usimamizi, naamini kwa sehemu kubwa, Wizara ya Kilimo italisemea. Lakini nidokeze moja tu ambalo chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri Kuu, alituagiza tuandae Waraka mmoja, ambao utatoa maelekezo ya kina, kuhusiana na namna tunavyofikiria Wataalam hawa na Wakurugenzi wetu, wanavyopaswa kusimamia kilimo.

Waraka ule upo katika hatua za mwisho, tumejaribu kutumia *inputs* zote kutoka kilimo, ili tuweze kwa kweli kwenda kwa kasi inayotakiwa kwa kadri itakavyowezekana. Nina hakika Waheshimiwa Wabunge wengi, mtakuwa mnajua, mkiwa kwenye majimbo huko sijui ni mara ngapi, umesikia Mkurugenzi anasema anakwenda kukagua mashamba mahali popote. Wengi wao wanaona kama kilimo si eneo lao, halina mwenyewe. Kwa hiyo, tunataka tuwape kazi sasa ya kusimamia kilimo wao wenyewe. Katika Kamati tulizopendekeza, tunesema ni vizuri Mkurugenzi mwenyewe ama awea Mwenyekiti au awe Katibu wa hiyo Kamati ya kusukuma kilimo. (*Makofî*)

Wanafunzi ambao hawana uwezo wa kulipia gharama za shule za Serikali, wasaidiwe na Serikali. Serikali Kuu ina mpango wa namna hiyo, lakini na Serikali za Mitaa tunao mpango kama huo, nadhani kubwa ni wananchi kuelewa kwamba,

unapokuwa na mtoto na uwezo ni mdogo au ni yatima, pamoja na jukumu la Halmashauri kuwatafuta, ni vizuri wao wenyewe wakachukua hatua ya awali, kumwona Diwani na kueleza tatizo ili aweze kuingiza katika mpango ambao tunadhani unaweza ukasaidia kuondoa hilo tatizo.

Iko vilevile hoja kuhusiana na ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Mheshimiwa Halima Mdee, naona alilisema hili kwa nguvu sana na mimi naomba niseme tu kwamba, ni bahati mbaya kwamba, mambo kama hayo yakiulizwa sana kwa upande wa ofisi yetu, inabidi turudi Mkoani kuuliza kwamba, imekuwaje?

Jambo hili litakuwa lilzungumzwa kwenye RCC ya mkoa, ambao wajumbe ni sisi wote tulipo hapa na pale ndio wakati mzuri, kama ni kukataa au kutoa ushauri tofauti, pale hasa ndio mahali pake. Hata hivyo, tumeamua tu kwamba, tutalifuatilia na tuone kama kweli kuna tatizo au hapana, lakini ninavyojua mimi, inawezekana kweli mahitaji ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa bado yanahitajika. Kwa sasa ofisi ile inam-*accommodate* Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya, sasa *you can imagine*, idadi ya watumishi waliopo, ni kubwa na pengine itahitaji kuwa na ofisi za ziada kidogo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na barabara ambazo zimetajwa, sehemu nyingi ambazo tungesema tuzungumzie, tumeamua zitakwenda upande wa Wizara ya Miundombinu, ili waweze kuzijibu zote kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Serikali iongeze fedha za matumizi ya barabara kwenye Halmashauri na kudhibiti matumizi yake. Hili ni dhahiri kabisa linawagusa wengi kabisa na tumekubaliana kiofisi, tujaribu kujenga hoja ya Serikali. Nasema tujaribu, kwa sababu kwa kweli Serikali ni moja tu, Hazina ni ile ile moja, lakini tunajaribu kutaka kujenga hoja kwa kuzingatia hoja za Waheshimiwa Wabunge kwamba, pengine Serikali ingetazama pengine kurekebisha kidogo *formula* ya hivi sasa ya asilimia 30 kwa 70, kwa maana ya barabara ya Serikali Kuu. Lakini ni jambo ambalo inabidi tulijengee hoja, pengine Waraka wa Baraza ili tuone kama rai hiyo itaweza kukubaliwa, lakini kwa sasa tutaendelea na hicho kidogo tunachokipata ilimradi kisimamiwe vizuri. Tunaamini barabara bado zinaweza zikaonekana ni bora kuliko pengine katika maeneo mengine zinavyoonekana.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kila Halmashauri iwe na mpango endelevu katika ukamilishaji wa ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu, akishirikiana na wadau, tumelipokea. Ni jambo zuri na kwa kweli, ndio mwelekeo wenyewe, muda wote tangu tumeanza kutekeleza Mpango wa MMEM. Tatizo kama mnavyoliona wote, mahitaji ni makubwa, na sasa msisimko ni mkubwa zaidi katika elimu kwa hiyo ujenzi sasa umekuwa ni mkubwa zaidi lakini kama ambavyo mlikuwa mkiambiwa na Serikali, safari hii angalau mwelekeo umekuwa ni kuboresha, kuongeza nyumba za walimu, ili tuone kiasi gani tunaweza tukasaidia kupunguza jambo hili.

Sasa kama nilivyosema, tuna maeneo mengi ambayo tungeweza tukayasemea lakini muda haututoshi. Kwa haya ambayo tumejaribu kuyaeleza, tunawashukuru kwa kutusikiliza na kwa yale ambayo hatukuweza, basi tutaweka kimaandishi. Lakini nimalizie angalau kwa kumwambia Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya kwamba,

ahadi ya Rais kuhusiana na barabara ya Miangalua kwenda Bondeni kule, hatimaye imepata ufumbuzi kuitia mpango wa barabara za vijijini. Kwa hiyo, kwenye bajeti ya mwaka huu, tumeitengea barabara ile shilingi milioni 300, kuweza kukarabati kilomita 35. Nakushukuru lakini nakupongeza kwa juhudi kubwa sana ulizofanya, kutuomba pale ili iweze kuingizwa katika angalau progamu hii.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naomba kuunga mkono hoja moja kwa moja, tukitakiana kila la heri katika hayo yaliyobaki. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Nina hakika Waheshimiwa Wabunge, nitakuwa ninawawakilisha vema, nikisema kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu, amepata wasaidizi wazuri sana. Kwa dhati, majibu ya kuanzia Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Maafa na Kampeni Dhidi ya UKIMWI, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Mheshimiwa Celine Kombani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Juma Akukweti na Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Peter Pinda, yamekuwa ni majibu ambayo nilitarajia kufikia kiwango hicho. (*Makofi*)

Kwa maana hiyo, nadhani kazi yetu jioni itakuwa nyepesi kabisa, ila kwa sababu bado tuna dakika kumi, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, atoe hoja ili tuweze kusitisha Shughuli za Bunge kabla ya wakati.

KUAHIRISHA BUNGE KABLA YA WAKATI WAKE

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 21, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako liahirishwe sasa kwa dakika kama nane kabla ya wakati wake, ili likutane tena saa 11.00 jioni.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Mtihani utabaki ni pale kusema sasa nani anaingia kwenye awamu ya kwanza na nani atafuata baadaye, kwa kulingana na uwezo wa Serikali yetu kwa siku zinazokuja. Lakini naomba niseme kwa dhati kabisa kwamba, jambo hili tumeona tulifanye kwa sababu hatuoni kwa nini tuendelee kuombwa wakati vigezo vinafahamika, tutakaposhindwa tutaomba msaada wenu.

Kuzuka kwa ugonjwa usioeleweka dhidi ya watoto kama mtakumbuka, Mheshimiwa Wilson Masilingi, alilieleza jambo hili kwa uchungu mkubwa sana. Naomba tu niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, tulimtaka Mkuu wa Mkoo atupe taarifa juu ya jambo hili. Alithibitisha kwamba, kweli tatizo lipo na kwa hiyo, tukamwarifu Mheshimiwa Waziri Mkuu na akatoa maagizo wakati ule ule, kumtaka Waziri wa Afya, aende Kagera na Timu yake na ndio maana hamumwoni hapa Bungeni, kwa sababu yuko huko. Tunaomba tufanye subira Wabunge wote wa Kagera, atakaporudi Mheshimiwa Waziri, basi tunaamini, atatoa maelezo ambayo yatasaidia kuonyesha ni tatizo gani na ukubwa wake ni kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ilifuta baadhi ya vyanzo vya mapato katika Halmashauri zetu, lakini misingi mikubwa na ninyi wote siku ile mlishangilia sana, illikuwa ni kuondoa vyanzo ambavyo vilikuwa ni kero kwa wananchi wetu. Lakini tukisema vilevile baadhi ya vyanzo vilikuwa vinakusanya kwa gharama kubwa mno, wakati unachokwenda kupata ni kidogo sana, hakikuwa na tija hata katika Halmashauri, kwa hiyo, tukaamua tuziondoe. Lakini kwa kufanya hivyo, Waheshimiwa Wabunge, hatujasema Halmashauri haiwezi kuendelea kubuni vyanzo vingine vya mapato, la hasha, bado wanaweza. Sisi tutakachowabana ni kuona kama chanzo hicho ni kero au kiko pale na kinaweza kutoa huduma bila kusababisha vurugu kwa wananchi. Kwa hiyo, raia wasidhani tumefunga mlango, waendelee na baadhi yao wamekuwa wakifanya hivyo.

Lakini cha msingi naomba niseme, tangu Serikali ilipofanya uamuvi huu na wakati ule ilikuwa ni kwamba, tulipofanya mahesabu ikaonekana kiwango cha fedha tulichoondoa ilikuwa ni kama theluthi moja ya mapato ya Halmashauri. Serikali ikaamua kuanza kutoa kiwango hicho chote. Kwa hiyo, tulipoanza mwaka 2003 tulitoa shilingi bilioni 22.9, mwaka 2004/2005 shilingi bilioni 25, mwaka 2005/2006 shilingi bilioni 40.1 na mwaka 2006/2007 zimetengwa shilingi bilioni 43. Tatizo kama nilivyogusia, wakati tulipokuwa tunaeleza jambo hili kwenye swalii, Halmashauri nyingi sasa baada ya kuona, maana fedha hii ni ya uhakika, sio kama ya kukimbizana na wananchi, hili ni suala la Serikali, muda ukifika inatoa. Sasa wengi wao wamelegeza kamba katika makusanyo ya mapato yao, wengi hawafikii asilimia 100 ya malengo yao na ndio maana ya kupitia sasa Mikataba hii ambayo tutawekeana nao, ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ataaelezea. Tunataka tuwabane, kila mmoja atimize wajibu wake, Serikali inatimiza wajibu wake na wao watimize wajibu wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, iko migogoro ya mipaka, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, aligusia ule wa Kilindi, lakini si Kilindi tu, tuna matatizo ya mipaka katika maeneo mengi kidogo na hivi leo umemsikia Mheshimiwa John Lwanji, naye alikuwa anazungumza juu ya mpaka wake kati ya Sikonge na Manyoni. Kwa hiyo, matatizo yanafahamika na tumedhamiria kwa kuwa tumekuwa tukifanya *piece meal*, tutashirikiana na Wizara ya Ardhi, sasa kujaribu kufanya kazi nchi nzima. Itakuwa gharama kubwa, lakini tumeona tukalifanye, tunawaomba tu Waheshimiwa Wabunge basi, mshirikiane kwa karibu sana na Wizara hizi mbili, pale tutakapofikia maamuzi ambayo pengine hayapendezi sana. Maana hatuamini kwamba, itabidi tuanze kunyoosha mipaka sasa kulingana na matakwa ya watu, mipaka hii ipo, kazi yetu itakuwa ni kuiweka bayana na wananchi wataamua kukaa upande wowote wanaoutaka, utadhani kwamba, kutakuwa na bughudha katika jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, tunaomba vilevile tuliarifu Bunge lako kuwa, tutaanza utaratibu mwaka huu wa fedha wa kuimarisha Mabaraza ya Ardhi Vijijini. Ni vyombo muhimu sana hasa katika kutatua migogoro midogo midogo ya ardhi, ili watu waweze kuishi bila matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni bajeti ya Halmashauri mpya. Mtakuwa mmesikia baadhi ya Wabunge wamelisema hili, Mheshimiwa Anna Makinda alilisema, lakini nadhani Korogwe, Manyara, Babati pale nalo limesemwa. Naomba tu nieleze kwa

kifupi kwamba, hatujaamua kufuta uamuzi wa kuanzisha mamlaka hizo hata kidogo, ni utaratibu tu wa kufungua *accounts* kwa ajili ya Halmashauri hizo, ambao ndio umechelewesha jambo hili.

Kwa hiyo, kwa kipindi kijacho, pengine hiki tulichokianza, tunaomba Waheshimiwa Wabunge, wanaotoka katika maeneo ya Njombe na maeneo mengine kama Mpanda kule, basi tufanye subira kidogo, ili *accounts* zile ziweze kufunguliwa kwa utaratibu unaokubalika chini ya maelekezo ya Wizara ya Fedha.

Kwa sasa fedha zile zitakwenda kwenye Halmashauri zile tunazozita mama, lakini zitakwenda kufanya kazi Halmashauri hizo tulizozianzisha na miradi ile itasimamiwa na Halmashauri hizo. Wao kazi yao ni kuondoa fedha kwenye akaunti na kupeleka kwenye mradi unaohusika. Nadhani nimejitahidi kulieleza jambo hili kwenye barua. Mheshimiwa Kwaangw' kinachotakiwa ni kuwaondoa wasiwasi na kama kuna tatizo, naomba tuwasiliane ili tuweze kufanya marekebisho yanayostahili.

Eneo lingine ni la wananchi kuhamishwa kutoka *Makonde Prattle*, suala hili lilisemwa na Mheshimiwa Raynald Mrope, nimeona niliseme hili kwa sababu lilikuwa ni jambo ambalo analizungumza mara nyingi. Kwa kifupi ni kwamba, tulifikia uamuzi wa Serikali kwamba, hawa wananchi hawawezi kulipwa fidia, ndio ulikuwa uamuzi wa Serikali. Mheshimiwa Raynald Mrope, akasema haiwezekani, naomba basi walipwe angalau kifuta machozi, tukamshauri ajenge hoja. Hoja haikujengwa, isipokuwa alionana na Naibu Waziri Fedha, akamwambia bwana, basi tuletee hiyo hoja pamoja na orodha ya majina ya wale wote ambao wanastahili. Tatizo limekuwa ni hiyo orodha, TAMISEMI hatuitengenezei na wala hatujaletewa, tumeomba Mkoa utengeneze hiyo orodha ya majina ya wale wote ambao waliathirika na zoezi hilo, tuweze kuliwasilisha Wizara ya Fedha na sisemi kwamba, tukiliwakilisha fedha hiyo itapatikana. Tutakuwa tunapeleka kama maombi, kama Wizara itakuwa na uwezo, *alhamdullilah*, wanaweza wakapata, kama haina itabidi tuendelee kuomba mpaka hapo jambo hili litakapokuwa limefika mahali pake.

Mheshimiwa Spika, ziko rai zilitoka kwa Waheshimiwa Wabunge kadhaa, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Samuel Chitalilo, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Mgana Msindai na Mheshimiwa Benson Mpesya, kuhususiana na sheria ndogo kwamba, ziangaliwe upya ili kuona kama zinakidhi mahitaji na mabadiliko yaliyopo hivi sasa. Aidha, Halmashauri za Wilaya, Manispaa, Miji na Majiji, ziangalie uwezekano wa kutumia sheria ndogo ili kudhibiti janga la UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutunga sheria ndogo za Halmashauri, kwa kawaida unaanzia kwenye Halmashauri zenyewe, Waheshimiwa Wabunge ni Wajumbe katika mabaraza hayo. Kama ambavyo tumekuwa tukisema muda wote, ninyi ni chachu kubwa sana, upeo wenu ni mkubwa kweli kweli, mkiwepo katika Mabaraza haya, naamini hakuna litakaloharibika. Kwa hiyo, raia yangu kwa hili, mjaribu kuwa karibu na Halmashauri zenu, hata kama kwa kupigiana simu, kuwataka wajaribu kuandaa hata rasimu baadaye mkazipitia, mkazirejesha na hatimaye zikaja kwetu. Ofisini kwetu tumejipanga vizuri, hakuna *by-law* inayokuwepo pale ikakaa siku hiyo ikalala, ni siku hiyo hiyo tunaondoa inarudi ilikotoka. Kwa hiyo, tunaomba hili jambo mlikazanie ili

tuweze kusaidiana kwa pamoja, tuweze kulifanikisha. Lakini tumeona kwa kuwa kuna mapungufu katika Halmashauri hizi, tumeamua sisi kutengeneza sheria ndogo za mfano, kwenye maeneo yote ambayo tunafikiri yatasaidia Halmashauri. Tumekamilisha mazingira, tunaenda sasa maeneo mengine ya kilimo, UKIMWI, elimu na kadhalika, ili tuweze kuzisaidia ziweze sasa kwenda kwa haraka zaidi katika kuandaa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa George Lubeleje, alitaka vilevile Wakuu Wilaya tuwape magari, tunajitahidi tatizo ni uwezo wa Serikali. Mwaka 2005/2006, tumeweza kununua magari 28 tu na mwaka huu kwenye bajeti ya safari hii, tutaweza kununua magari 40. Tutaendelea kuongeza kadri uwezo utakavyokuwa unapatikana, ingawa kwa kweli tungependa wapate magari kwa mkupuo wote, ili usimamizi wa shughuli za maendeleo uweze kwenda kwa uwiano unaofanana. Lakini tatizo ni hilo la fedha.

Kuwepo programu za utekelezaji wa ajira kwa ajili ya vijana na wanawake katika Halmashauri na kutafuta rasilimali zinazohitajika kwa ajili ya makundi hayo. Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Benson Mpesa na Mheshimiwa Mgana Msindai, wote hao wamejaribu kutoa raia hiyo na kwa kweli tunachowenza kusema moja, ni kuishukuru Serikali na hasa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa uamuzi wake wa kuanza na zile shilingi milioni 500.

Kazi ya Halmashauri hapa kwa kweli itakuwa ni kujipanga vizuri ili tuweze kutimiza azma ya hoja ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wajumbe. Tunaendelea vilevile kuhimiza Halmashauri kuhusiana na asilimia kumi, iendelee kutengwa katika Mfuko wao, lakini tunesema vilevile tumekubaliana kiofisi, tutoe msukumo maalum kwa ajili ya *SACCOS*, kwa kushirikiana na Wizara inayohusika. Hapa tunaomba vilevile Waheshimiwa Wabunge, mtusaidie sana kutokana na uwezo wenu mkubwa katika eneo hili. Ofisi ya Waziri Mkuu, iweke utaratibu utakaowezesha kutolewa kwa ruzuku kwenye mbolea. Hili nadhani nitalizungumza na Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika na Ofisi ya Waziri Mkuu, iandae semina kwa Wabunge, kuwaelimisha kwa undani shughuli zitakazotekelzwa mikoani. Hili kama tulivyosema, tumekwisha anza na tutalikamilisha baada ya muda si mrefu.

Eneo lingine ambalo nataka nilisemee kidogo, ni utendaji kazi wa Maafisa Watendaji wa Kata kwamba, uangaliwe upya kwani kuna baadhi wanabambikiza watu kesi. Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, tunaomba tukuhakikishie kuwa, tutajitahidi, tumekuwa tunalisema sana, lakini tutajitahidi kujaribu kuona hatua za dhahiri, ambazo zinaweza zikasaidia kuondokana na hawa miungu watu, watu ambao wanaona wao ndio wakubwa kabisa pale na kikubwa katika eneo hili ni kuwa na watu wenye upeo wa kielimu. Ndio maana tunasisitiza awe darasa la 12 au la 14. Sasa hatunao sawa, lakini tumekubali wale wa darasa la saba waendelee kwa kipindi cha miaka mitatu, baada ya hapo ni bora tukachelewa lakini tukawa na watu wenye kiwango cha kutosha, hili tutalitilia mkazo ili tuweze kuwa na viongozi wenye uwezo wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri hazifanyi kazi vizuri, fedha zinazopelekwa ni nyingi lakini bado kama mnavyosema Waheshimiwa Wabunge, ni tatizo kubwa na mimi naomba niseme changamoto niliyonayo, kama Msaidizi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, hapa ni namna ya kujaribu kuimarisha uadilifu katika Serikali za Mitaa, wengi wana uwezo, lakini uadilifu ndio tatizo kubwa. (*Makofit*)

Sasa hili chini ya uongozi wake tunajaribu kuliangalia, kwanza, kutazama mikakati lakini hasa ni kuongeza uwazi zaidi katika ngazi ya Halmashauri na hili tumelianza. Tunaomba tuseme, tutawatumia sana hawa *internal auditors* katika eneo hili, kwa kuwa ndio wanaojua mambo mengi vizuri, lakini mara nyingi yanapuuzwa na Wakurugenzi. Tukiwatumia hawa vizuri, tunaamini tutafanya mambo makubwa katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Same, haikusanyi mapato yake. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Anna Kilango Malecela kuwa, tutalivalia njuga, tutataka kujua ni kwa nini na naamini tutapata ufumbuzi, kama si kwa njia hii ya mkato, lakini kwa kupitia *performance agreement* ambazo zitaelezwa hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, zipo Wilaya nyingi zenyenye majimbo zaidi ya moja, Halmashauri zijaribu kugawa miradi kwa usawa. Suala hili naliafiki kabisa, hujakosea Mheshimiwa Anna Kilango Malecela, katika jambo hili na kwa kweli ndio utaratibu. Lazima maendeleo ndani ya Wilaya, ambayo ina zaidi ya Jimbo moja, tujitahidi kuweka uwiano wa maendeleo. Miradi yetu lazima izingatie hilo. (*Makofit*)

Lakini changamoto kubwa ni kwamba, wale wanaopanga mipango hiyo ni Madiwani wenyewe, ukiona pameharibika, ni rahisi kujua kwa nini pameharibika. Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, kwa kuwa wote tuko katika gurudumu hilo, mkipata nafasi hasa wakati wa kuitisha bajeti zetu ni muhimu sana ili muweze kujua mipango ipo na wapi pamekwenda upande bila kuzingatia uwiano ninaousema.

Hili la Maafisa Ugani, wamelisema kwa kweli Wabunge wengi na mimi nawashukuru sana, kwa mawazo waliiyoyatoa, lakini nadhani Waziri wa Kilimo, atalizungumzia vizuri zaidi, kwa kuwa ni jambo ambalo linatugusa wote. Hali kadhalika hili la kuweka msukumo mpya katika matumizi ya mbolea na kuwepo kwa malengo ya kilimo katika Kata, Wilaya na utaratibu madhubuti wa usimamizi, naamini kwa sehemu kubwa, Wizara ya Kilimo italisemea. Lakini nidokeze moja tu ambalo chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri Kuu, alituagiza tuandae Waraka mmoja, ambao utatoa maelekezo ya kina, kuhusiana na namna tunavyofikiria Wataalam hawa na Wakurugenzi wetu, wanavyopaswa kusimamia kilimo.

Waraka ule upo katika hatua za mwisho, tumejaribu kutumia *inputs* zote kutoka kilimo, ili tuweze kwa kweli kwenda kwa kasi inayotakiwa kwa kadri itakavyowezekana. Nina hakika Waheshimiwa Wabunge wengi, mtakuwa mnajua, mkiwa kwenye majimbo huko sijui ni mara ngapi, umesikia Mkurugenzi anasema anakwenda kukagua mashamba mahali popote. Wengi wao wanaona kama kilimo si eneo lao, halina mwenyewe. Kwa hiyo, tunataka tuwape kazi sasa ya kusimamia kilimo wao wenyewe. Katika Kamati

tulizopendekeza, tumesema ni vizuri Mkurugenzi mwenyewe ama awea Mwenyekiti au awe Katibu wa hiyo Kamati ya kusukuma kilimo. (*Makofî*)

Wanafunzi ambao hawana uwezo wa kulipia gharama za shule za Serikali, wasaidiwe na Serikali. Serikali Kuu ina mpango wa namna hiyo, lakini na Serikali za Mitaa tunao mpango kama huo, nadhani kubwa ni wananchi kuelewa kwamba, unapokuwa na mtoto na uwezo ni mdogo au ni yatima, pamoja na jukumu la Halmashauri kuwatafuta, ni vizuri wao wenyewe wakachukua hatua ya awali, kumwona Diwani na kueleza tatizo ili aweze kuingiza katika mpango ambao tunadhani unaweza ukasaidia kuondoa hilo tatizo.

Iko vilevile hoja kuhusiana na ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Mheshimiwa Halima Mdee, naona alilisema hili kwa nguvu sana na mimi naomba niseme tu kwamba, ni bahati mbaya kwamba, mambo kama hayo yakiulizwa sana kwa upande wa ofisi yetu, inabidi turudi Mkoani kuuliza kwamba, imekuwaje?

Jambo hili litakuwa lilzungumzwa kwenye RCC ya mkoa, ambao wajumbe ni sisi wote tulipo hapa na pale ndio wakati mzuri, kama ni kukataa au kutoa ushauri tofauti, pale hasa ndio mahali pake. Hata hivyo, tumeamua tu kwamba, tutalifuatilia na tuone kama kweli kuna tatizo au hapana, lakini ninavyojuua mimi, inawezekana kweli mahitaji ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa bado yanahitajika. Kwa sasa ofisi ile inam-*accommodate* Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya, sasa *you can imagine*, idadi ya watumishi waliopo, ni kubwa na pengine itahitaji kuwa na ofisi za ziada kidogo.

Mheshimiwa Spika, kuhususiana na barabara ambazo zimetajwa, sehemu nyingi ambazo tungenesema tuzungumzie, tumeamua zitakwenda upande wa Wizara ya Miundombinu, ili waweze kuzijibu zote kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Serikali iongeze fedha za matumizi ya barabara kwenye Halmashauri na kudhibiti matumizi yake. Hili ni dhahiri kabisa linawagusa wengi kabisa na tumekubaliana kiofisi, tujaribu kujenga hoja ya Serikali. Nasema tujaribu, kwa sababu kwa kweli Serikali ni moja tu, Hazina ni ile ile moja, lakini tunajaribu kutaka kujenga hoja kwa kuzingatia hoja za Waheshimiwa Wabunge kwamba, pengine Serikali ingetazama pengine kurekebisha kidogo *formula* ya hivi sasa ya asilimia 30 kwa 70, kwa maana ya barabara ya Serikali Kuu. Lakini ni jambo ambalo inabidi tulijengee hoja, pengine Waraka wa Baraza ili tuone kama rai hiyo itaweza kukubaliwa, lakini kwa sasa tutaendelea na hicho kidogo tunachokipata ilimradi kisimamiwe vizuri. Tunaamini barabara bado zinaweza zikaonekana ni bora kuliko pengine katika maeneo mengine zinavyoonekana.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kila Halmashauri iwe na mpango endelevu katika ukamilishaji wa ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu, akishirikiana na wadau, tumelipokea. Ni jambo zuri na kwa kweli, ndio mwelekeo wenyewe, muda wote tangu tumeanza kutekeleza Mpango wa MMEM. Tatizo kama mnayyoliona wote, mahitaji ni makubwa, na sasa msisimko ni mkubwa zaidi katika elimu kwa hiyo ujenzi sasa umekuwa ni mkubwa zaidi lakini kama ambavyo mlikuwa mkiambiwa na Serikali,

safari hii angalau mwelekeo umekuwa ni kuboresha, kuongeza nyumba za walimu, ili tuone kiasi gani tunaweza tukasaidia kupunguza jambo hili.

Sasa kama nilivyosema, tuna maeneo mengi ambayo tungeweza tukayasemea lakini muda haututoshi. Kwa haya ambayo tumejaribu kuyaeleza, tunawashukuru kwa kutusikiliza na kwa yale ambayo hatukuweza, basi tutaweka kimaandishi. Lakini nimalizie angalau kwa kumwambia Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya kwamba, ahadi ya Rais kuhusiana na barabara ya Miangalua kwenda Bondeni kule, hatimaye imepata ufumbuzi kupitia mpango wa barabara za vijiji. Kwa hiyo, kwenye bajeti ya mwaka huu, tumeitengea barabara ile shilingi milioni 300, kuweza kukarabati kilomita 35. Nakushukuru lakini nakupongeza kwa juhudi kubwa sana ulizofanya, kutuomba pale ili iweze kuingizwa katika angalau progamu hii.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naomba kuunga mkono hoja moja kwa moja, tikitakiana kila la heri katika hayo yaliyobaki. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Nina hakika Waheshimiwa Wabunge, nitakuwa ninawawakilisha vema, nikisema kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu, amepata wasaidizi wazuri sana. Kwa dhati, majibu ya kuanzia Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Maafa na Kampeni Dhidi ya UKIMWI, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Mheshimiwa Celine Kombani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Juma Akukweti na Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Peter Pinda, yamekuwa ni majibu ambayo nilitarajia kufikia kiwango hicho. (*Makofi*)

Kwa maana hiyo, nadhani kazi yetu jioni itakuwa nyepesi kabisa, ila kwa sababu bado tuna dakika kumi, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, atoe hoja ili tuweze kusitisha Shughuli za Bunge kabla ya wakati.

KUAHIRISHA BUNGE KABLA YA WAKATI WAKE

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 21, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako liahirishwe sasa kwa dakika kama nane kabla ya wakati wake, ili likutane tena saa 11.00 jioni.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja hiyo iko mbele na imeungwa mkono, yaani ya kusitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni, ambapo Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye ndio mtoa hoja, atajibu hoja. Sasa naomba muiamue hoja. Asante.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Saa 06.54 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita mtoa hoja, nimepewa taarifa ya wageni, kwenye *Speaker's Gallery*, wapo Bob na Barbra Griffin, Mwenyekiti wa *Dodoma Tanzania Health Development*, wanaotoka *Minnesota United States*, ni hapo Mkono wa kulia. Hawa ndiyo wafadhili wanaokuja kuwezesha kujengwa kwa Mradi wa Hospitali ya Rufaa ya Dodoma (*Dodoma Christian Health Centre*), ambayo itamilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri. Pia waliopo pamoja nao ni John and Joan Tosso, amba ni Wakurugenzi wa hiyo *Dodoma Christian Health Centre*. (*Makofi*)

We are honoured by your presence, we pray that the project takes off because our country in Central Tanzania, really broadly needs a Referral Hospital. Thank you. (*Makofi*)

Pia wapo na Janeth kutoka Minnesota, karibu sana. (*Makofi*)

Kwa taarifa hizo nzuri za utangulizi, namwita sasa Mheshimiwa mtoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nyingine ya kuhitimisha hoja yangu, iliyoanza kujadiliwa toka Jumatatu. (*Makofi*)

Kwanza, napenda nichukue nafasi hii, kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa pongezi zao nyingi na sifa nyingi walizotumimina sisi Ofisi ya Waziri Mkuu, tunashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nikiri kwamba, ubora wa mjadala hapa umekuwa wa hali ya juu sana, nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge. Lakini vilevile naomba nitumie nafasi hii, kuwapongeza sana sana Kiongozi wa Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kwa kusema kwamba, wataunga mkono Serikali na tutabishana juu ya Sera za msingi za Serikali. Nawapongeza sana. Ninawapongeza tena kwa kuunga mkono bajeti yetu, ahsanteni sana. Naamini mtaendelea kutuunga mkono mpaka tumalize kipindi chetu cha miaka mitano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hotuba hii imejadiliwa na Waheshimiwa Wabunge 90 wamechangia kwa kuzungumza na 63 wamechangia kwa maandishi. Kama ulivyo utamaduni, naomba kuwatambua Waheshimiwa Wabunge, waliochangia nikianza na wale waliochangia kwa kuzungumza, mtaniwia radhi orodha ni ndefu.

Waliochangia kwa kuzungumza ni kama ifuatavyo: Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa John S. Malecela, Mheshimiwa Anne K. Malecela, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mheshimiwa Samuel M. Chitalilo, Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mheshimiwa William M. Ngeleja, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah,

Mheshimiwa Rosemary K. Kirigini, Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Jacob D. Shibili, Mheshimiwa Said J. Nkumba na Mheshimiwa Benson M. Mpesa.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Mohamed S., Mheshimiwa Benito W. Malangalila, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Benedict K. Losurutia, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Michael L. Lekule, Mheshimiwa Felister A. Bura, Mheshimiwa Estherina J. Kilasi, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa William J. Kusila, Mheshimiwa Aziza S. Ally, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Manju S. O. Msambya, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mheshimiwa Zaynab M. Vulu, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri na Mheshimiwa Halima O. Kimbau.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Mheshimiwa Joyce M. Masunga, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Prof. Feethan F. Banyikwa, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Kilontsi M. Mpologomyi, Mheshimiwa Anna M. Komu, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Anna R. Lupembe, Mheshimiwa Col. Saleh Ali Farrah, Mheshimiwa Adam K. Malima, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Sijapata F. Nkayamba, Mheshimiwa Eliatta N. Switi, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Dunstan D. Mkapa, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa John M. Shibuda, Mheshimiwa Laus O. Mhina, Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, Mheshimiwa Dr. Luka J. Siyame, Mheshimiwa Celina O. Kombani, Mheshimiwa Juma J. Akukweti na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mheshimiwa Anne S. Makinda, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa

Gideon A. Cheyo, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa James P. Musalika na Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu, Mheshimiwa Ernest G. Mabina, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa Lucas L. Selelili, Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Margreth Agness Mkanga, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Dewji, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Rajab Ahmad Juma, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mheshimiwa Janet B. Kahama, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Juma Said Omar na Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Damas P. Nakei, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Anne K. Malecela, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Amina C. Mpakanjia, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mheshimiwa Prof. Philemon M. Sarungi, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Manju S. O. Msambya, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Dorah H. Mushi na Mheshimiwa Col. Saleh Ali Farrah.

Mheshimiwa Spika, nadhani hao ndio waliochangia, kama kuna niliyemsahau, namwomba radhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutanguliza kwa kusema kwamba, kwanza, tumechukua hoja zote na tutazizingatia, hoja ambazo Mawaziri walionitangulia hawakuweza kuzijibu, zitajibiwa na Mawaziri kwenye Sekta zao. Kwa hiyo, hakuna hoja yoyote iliyotolewa hapa, ambayo itaachwa. Lakini vilevile ningependa kuwashakikishia kwamba, baadhi ya majibu mengine tutawapelekeeni, kila mmoja alichochangia tutampelekea kwa maandishi ili awe na *record* ya mazungumzo yake hapa Bungeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nijiunge nawe kukubaliana kabisa kwamba, nina timu ya Watendaji hodari katika Ofisi ya Waziri Mkuu, nawapongeza sana kwa umahiri waliouonyesha humu ndan, lakini vilevile kwa kazi wanazofanya pale Ofisi ya Waziri Mkuu. Nimepata Timu wa watu hodari sana. Ni hodari sana na mimi nawatakia kila la kheri ili tuvuke pamoja katika Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi nitapitia maeneo machache, ambayo yamejitokeza katika mjadala kwa ujumla, kwa sababu *details* zimeshajibiwa na Waheshimiwa Manaibu Mawaziri na Mawaziri.

Nianze na lile la kwanza la nafasi ya Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa katika uongozi wa nchi yetu, hii ni hoja ambayo iliwasilishwa na Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa na Mheshimiwa Halima J. Mdee. Namshukuru Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, asubuhi alilieleza na mimi nasisitiza maeneo yale ambayo yanahitaji kusisitizwa. Kwanza, tutaendelea kurudia kwamba, hawa ni Wawakilishi wa Rais katika maeneo yao. Pili, tunarejea hawa ni viongozi wa kisiasa si watendaji wa Serikali, ni viongozi wa kisiasa. Tatu, ni walinzi wa amani na nne ni kiungo kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa na Mheshimiwa Halima J. Mdee, walitaja kifungu cha ambacho naomba nikisome maelezo yake kama ifuatavyo:-

Ibara ya 63(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 toleo la mwaka 2005, ambalo linajumuisha mabadiliko yote ya Katiba hadi kufikia mwaka 2005, ilikuwa ni Ibara ya 23(4) katika toleo la mwaka 1980. Baada ya Mabadiliko ya tatu ya Katiba ya Nchi ya mwaka 1984, Ibara hii ilibadilika na kuwa Ibara ya 66. Kabla ya mabadiliko ya nne ya nchi yaliyofanywa kupitia Sheria Namba 4 ya mwaka 1992 Ibara ya 66(3), iliwatambua Wakuu wa Mkoa yote ya Tanzania kuwa Wabunge, kwa mujibu wa madaraka yao. Kutokana na mabadiliko ya Nne ya Katiba ya mwaka 1992, Wakuu wa Mkoa waliondolewa kwenye orodha ya Wabunge, wanaoingia Bungeni kwa nyadhifa zao za Ukuu wa Mkoa.

Ibara ya 66(3) inatoa ufanuzi wa akidi ya Mikutano ya Bunge, akidi yaani *quorum* ya Bunge. Kwa mujibu wa ufanuzi huo, Wakuu wa Mkoa waliochaguliwa kuwakilisha Majimbo ya Uchaguzi au Wabunge wanaowakilisha Majimbo ya Uchaguzi, wakati huo zikiitwa Wilaya za Uchaguzi, wanaoteuliwa kuwa Wakuu wa Mkoa, hawaathiri akidi ya Mikutano ya Bunge. Ufanuzi huo ultolewa chini ya Ibara ndogo ya 3 ya ibara ya 66 kwa kuzingatia uwezekano wa Wabunge kuteuliwa kuwa Wakuu wa Mkoa.

Uteuzi huo ungeweza kupunguza idadi ya Wabunge kama Wakuu wa Mkoaa wangekuwa ni Wabunge kwa nyadhifa zao, kwani nafasi moja ingepungua kwa kila Mkuu wa Mkoa aliyeoteuliwa kuwa Mbunge au Mbunge anapoteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa. Lakini kufuatia Mabadiliko ya Nne ya Katiba ya nchi yetu, yaliyofanywa mwaka 1992, sasa Wakuu wa Mkoa siyo Wabunge tena kwa nyadhifa zao. Hivyo, hata kama Mbunge atateuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa, ataendelea kuingia Bungeni kama Mbunge na siyo kama Mkuu wa Mkoa. Ufanuzi huu, hauathiri idadi ya Wabunge, akidi ya Mikutano ya Bunge, wala shughuli za Bunge lenyewe. (*Makofî*)

Masharti ya Ibara ya 66(3), hayana uhusiano na aya (g) ya Ibara ndogo ya 2 ya Ibara ya 66 wala Ibara ya 61, ambazo kwa pamoja, alizieleza Mwanasheria Mkuu wa Serikali alipotoa kauli ya Serikali kuhusu uteuzi wa Mkuu wa Mkoa Luteni Yusuf Makamba kuwa Mbunge. Kwa hiyo, kwa kweli mimi nashauri kifungu hicho hata kikifutwa, hakina kazi, kwa hiyo, hakuna mgogoro.

Mheshimiwa Spika, Suala la pili, ambalo limezungumzwa sana ni eneo la Halmashauri ya Serikali za Mitaa. Limezungumzwa, nina hakika kwa sababu ni eneo linalowagusa Wabunge wengi, lakini kwa kweli msingi wa maendeleo yetu kule vijijini ni Serikali za Mitaa. Sasa najua Madiwani kadhaa wanalamika wanasesma, Serikali Kuu inawakandia sana tungepunguza makali ya kuwakandia lakini hatuwakandii kwa nia mbaya, tunawakandia kwa sababu tunataka wafanye yanayowapasa kuyafanya na kama hawafanyi ni lazima yatasemwa.

Mheshimiwa Spika, sasa walio changia hoja hii ujue ilivyo na umaarufu ni hawa wafuatao: Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Samuel M. Chitalilo Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Benson M. Mpesa, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Anne K. Malecela, Mheshimiwa Ernest G. Mabina, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, William M. Ngeleja, Mheshimiwa Jacob D. Shibili, Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Rosemary K. Kirigini, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mheshimiwa Wilson M. Masilingi na Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Benito W. Malangalila, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mheshimiwa Anne S. Makinda, Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa Benedict K. Losurutia, Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Hemed M. Hemed, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa James P. Musalika, Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni na Mheshimiwa Ernest G. Mabina.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Serikali, tunakiri kwambab yapo matatizo kadhaa katika Halmashauri zetu na asubuhi Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, alipitia baadhi ya matatizo yaliyopo katika Halmashauri. Jukumu letu kama Serikali Kuu, ni kusaidia kuondoa matatizo hayo ili Halmashauri ziweze kufanya kazi vizuri na ndiyo maana katika bajeti hii, mtaona tunapeleka zaidi ya shilingi bilioni 700 kwenye Halmashauri za Wilaya. Kwa hiyo, ukiwa na Halmashauri za Wilaya ambazo ni makini na mahiri, una hakika fedha zitafanya kazi iliyokusudiwa. Lakini kama alivyosema Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda asubuhi, liko tatizo la uwajibikaji, kuna Wakurugenzi wengine, baadhi yao si wote, hawana kazi kubwa wanayofanya kama walivyosema wengine, ni safari kati ya Wilayani Dodoma, Dar es Salaam, Arusha na kwingine kila siku wako barabarani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Paul P. Kimiti, alisema wanaotoka Sumbawanga fikiria mafuta wanayotumia kutoka Sumbawanga kule Nkasi au Mpanda mpaka Dar es Salaam, ni dhahiri kwamba, kwa kweli uwajibikaji ni matatizo. Lakini kuna matatizo makubwa

vilevile ya matumizi mabaya ya fedha katika Halmashauri, ungeweza kusema kabisa kuna watu kule wamejipanga kupora fedha za Halmashauri, kazi yao ni kupora fedha za Halmashauri. Napenda nikiri kwamba, baadhi yao wanasaidiwa na viongozi kama Wenyeviti au Madiwani, wanasaidiana. Lakini hatuna vilevile taratibu nzuri, zinazotuwezesha kudhibiti kwa mfano, mapato ya Halmashauri, taratibu zetu zilizopo bado zina matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nitasemea kidogo Hati Chafu. Hati Chafu wanapewa ambao wameshindwa kufunga mahesabu yao, ni mabaya lakini bahati mbaya wanaopewa hizo Hati Chafu ni zile Halmashauri ambazo kuna matatizo vilevile ya kuwa na watumishi. Mwaka 2005, waliopata Hati Chafu ni Manispaa ya Mtwara, Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, Wilaya ya Handeni na Wilaya ya Misungwi. Kupata Hati Chafu maana yake nini? Maana kuna fedha za miradi ya maendeleo hazikwenda Mtwara Vijijini, Mtwara Mjini, Misungwi wala Handeni. Sasa unajiuliza hivi kosa la nani; yule mwananchi anayekosa maendeleo au huyu Mtumishi ambaye hakufunga Hesabu za Serikali? Jambo hili lina utata. Wenzetu wanaotupa misaada, wanafikiri sharti hili linatusaidia lakini wanasheru mazingira ya Serikali za Mitaa kule Ulaya ni tofauti kabisa na Serikali za Mitaa huku Tanzania. (*Makofi*)

Mimi na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, ukimpata Diwani aliyefika *form four* katika Halmashauri yetu, ni wawili au watatu, sana sana anajua kusoma na kuandika na kusoma kwenyewe ni kule kwa kuazima miwani na ndiyo aina ya watu unaowapata vijijini. Si kwamba, hajui uongozi, anajua uongozi lakini uwezo kwa kweli wa kuelewa mambo haya ya kisasa ni matatizo. Kwa hiyo, iko kazi ya kuwajengea kwanza Madiwani wenye uwezo. Lakini hii haitoshi, Hati Chafu peke yake siyo *agenda*, hata hao wanaopata Hati Safi zina matatizo, ni *Book Keeping* tu, unachukua hapa nimenunua hiki hata kama umetunga ile risiti nimeweka hivi na hivi, hesabu zinakubali, si *Value for Money*. Huna hakika kama kweli hizo shilingi milioni 100 unazosema zimejengea *dispensary* zimejenga *dispensary*. Kwa hiyo, tuna tatizo. (*Makofi*)

Yupo Mkuu wa Mkoa mmoja amekwenda katika Mkoa, amefanya kazi nzuri sana, amegundua *Internal Auditor* anaweza akasaidia sana lakini *Internal Auditor* huyu anawajibika kwa Mkurugenzi na ukishaondoka pale wanaendelea na mambo yao kama kawaida. Sasa mapendekezo yetu kwa kweli kwanza ni *Performance Contract*, ile ambayo tumeisema katika hotuba kwamba, ni lazima tuwe na Mkataba wa kazi kati ya Halmashauri na Serikali Kuu ili masuala haya Waheshimiwa Wabunge mnayoyatoa hapa kwenda kwenye Halmashauri, tujiridhishe kwamba, yamekwenda kufanya kazi za wananchi, ndiyo maana yake.

Mheshimiwa Wilson Masilingi, juzi alikuwa anasema hawa hawafai nenda vijijini, angalau tuanze hapa hapa, Halmashauri tunakowapelekea fedha zetu tuweke Mkataba. Anayeweka Mkataba ni Mwenyekiti wa Halmashauri na Mkurugenzi wa Halmashauri kwamba, fedha tulizoleta kwa ajili ya kujenga zahanati, zinajenga zahanati na zinajenga zahanati iliyo bora siyo hivi hivi tu.

Tulikwenda Kilwa, kule Kilwa kwenye mradi wa MMEM wakaamua kuwaajiri *contractors*, wale *contractors* wakajenga madarasa yale ya MMEM, Mwenyekiti yule Alhaji Mtopa anasema, ukipiga teke nyumba inaanguka lakini mamilioni yameshapotea. Wamekamatwa wakapelekwa Mahakamani, kesi badala ya kuwa upande wa wale ikaigeukia Halmashauri, fedha za Halmashauri zikakamatwa shilingi milioni 120 kwa uzembe wa viongozi wa Halmashauri.

Kwa hiyo, katika miradi hii vilevile tupate *Value for Money* na hii tunapendekeza kwamba, kuanzia sasa, kila Halmashauri iwe na Kamati ya Madiwani ya kuhakiki miradi katika maeneo yao. Kwa hiyo, juu tunaipa Mkataba chini kuna Kamati zinakwenda kuhakiki. Amesema Mheshimiwa kwamba, tunajitahidi kuweka Wahasibu wa kutosha kama tulivyosema, lakini vilevile nitangaze mapema kabisa kwamba, kwa mambo tuliyoyaona katika kipindi cha miezi sita, tafadhalil fumbeni macho, mkiona hatua tutakazokuwa tunazichukua, kwa sababu inabidi ziwe kali na kwa nchi nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la mifugo. Suala la Mifugo limechangiwa na Mheshimiwa John S. Malecela, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Estherina J. Kilasi, Mheshimiwa Benedict K. Losurutia, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa William M. Ngeleja, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha na Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu.

Waheshimiwa Wabunge naomba tulitazame suala hili kwa umakini sana. Kwanza, tuelewane kwamba, wafugaji ni Watanzania wenyе haki zao za msingi kama Watanzania wengine. Lakini tukubaliane kwamba, haiwezekani tukageuza nchi nzima ikawa ni malisho kwa ajili ya malisho, haiwezekani. Tunalo tatizo ngazi ya kwanza kule Mikoa ya Kagera na Kigoma, kuna mifugo mingi imevamia kutoka nchi za jirani.

Kagera peke yake kulikuwa na mifugo 70,000 kutoka nje ya Tanzania, wamevamia maeneo yale wamevamia kwenye ranchi za Taifa na wamekaa. Tumelazimika kuchukua hatua za kuwaondosha, tumefanya *operation* mpaka sasa hivi tumeondoa ng'ombe 50,000 kutoka Kagera. (*Makofi*)

Tumepata malalamiko mengi sana na magazeti ya nchi zile wametuandika vibaya sana kwamba, sisi ni nchi ambayo hatujali haki za binadamu. Sisi hatujali haki za binadamu wakati tunao huku wakimbizi kwa maelfu hapa katika nchi yetu, hatujali haki za binadamu? Sisi ni watu ambao hatuna uungwana, watu wetu waliofanya kazi hiyo wamefanya vitendo visiviyokidhi haki za binadamu, watu wetu wamefanya bunduki na silaha zinazoingia kutoka kwao kufanya ujambazi katika nchi yetu hatuzioni?

Kwa hiyo, tumefumba macho, tumeamua mifugo inaondoka na inaondoka kwa sababu ipo katika misitu au Mapori ya Akiba ambayo ni muhimu kwa ajili ya mazingira ya nchi yetu. Sasa tunaomba watuelewe na katika hili hatuna Msalie Mtume. (*Makofi*)

Tumepeleka wataalam wetu wiki iliyopita kule katika nchi moja ya jirani, wamekwenda kuzungumza nao, hatujadiliani juu ya kutoondoa mifugo, bali tunajadiliana juu ya utaratibu mzuri wa wao kupokea mifugo yao, ndiyo! Wenzetu kule Uganda, mimi

nilikaa Uganda Mbarara kule kwa wafugaji, kila mtu ardhi yake imewekewa uzio, kila mtu hata Kenya pale ardhi yake imewekewa uzio, sasa wanakuja Tanzania wanasema aah! unajua kwetu ni *private land*, tumeona nchi yetu ina maeneo ya kutosha kufuga mifugo yetu na ni mali ya umma, kwa hiyo na sisi tunakuja kulisha ng'ombe wetu. Aha! Mali ya Umma haina mwenyewe?

Mali ya Umma maana yake ni ya Umma wa Watanzania na kama wanataka kuingia Tanzania kwa utaratibu, basi wafuate taratibu za kisheria za kutafuta uraia ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo, nasema watuelewe hakuna Msalie Mtume, mifugo yote itaondoka kama ambavyo ya Watanzania inaondoka kwao na ya kwao itaondoka hapa kwetu. (*Makofi*)

Sasa nirudi nyumbani, wote ni mashahidi jinsi ambavyo mabwawa yetu yamekosa maji na wote pia ni mashahidi wa matokeo ya maji hayo kutopatikana na umeme ulivyoathiri uchumi wa nchi yetu. Kwa hiyo, hatuwezi kukaa kimya, tukishuhudia mazingira yanaharibika na uchumi unaathirika.

Lakini liko tatizo la pili, ardhi ina uwezo wa kubeba mifugo kadhaa tu, siku ile nilimsikia Mheshimiwa Raynald Mrope, akilalamika sana juu ya wale ng'ombe 200 waliokwenda kule kwao Mtwara. Rafiki yangu Mheshimiwa Raynald Mrope, ng'ombe 200 siyo nusu ya ng'ombe wa Mheshimiwa Lekule Laizer wala siyo nusu ya boma lake, lakini nasikia kule Mtwara walipofika mmlikimbia kweli kweli kukimbia ng'ombe. (*Makofi*)

Lakini hoja ya Mtwara eneo lao ni dogo na kweli Mtwara ni padogo pale kiasi kwamba, ikiingia mifugo mingi sana, itaathiri ardhi ile lakini si kweli kwa Tunduru na Ruvuma. Naomba nipitie baadhi ya takwimu, mwone matatizo yaliyopo katika baadhi ya maeneo mjue *carrying capacity* ya maeneo. Mbarari ukubwa wa eneo la malisho pale ni hekta 259,000, uwezo wa malisho ya ng'ombe ni 103,600, idadi ya ng'ombe waliopo ni 298.772.

Namwomba radhi, Mheshimiwa John Samwel Malecela, jina lake nililiruka, alichangia kwa maandishi, nisamehe sana. (*Makofi*)

Wilaya ya Iramba ukubwa wa eneo la malisho ni hekta 454,900, uwezo wa malisho 181,960, idadi ya ng'ombe waliopo ni 584,000. Wilaya ya Mpanda, ukubwa wa eneo la malisho ni hekta 104,990, uwezo wa malisho ni ng'ombe 34,998, idadi ya ng'ombe waliopo Mpanda ni 245,000.

Mheshimiwa Spika, nimalizie na Same kwa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, ukubwa wa eneo la malisho ni hekta 246,705 uwezo wa malisho ya ng'ombe ni 49,541 na idadi ya malisho ya ng'ombe waliopo ni 292,000.

Sasa we are joking, katika hali hii hivi tumlaumu nani, mazingira yakiharibika hii ndiyo hali halisi na iko sehemu nyingi nchini. Ndiyo maana ndugu zangu tuelewane,

mnajua kwamba, katika kuwaondoa wafugaji kuna baadhi ya maeneo watu wetu wamepita wamefanya kwa nguvu zaidi kuliko tulivytaka. Lakini kwa ujumla, nawapongeza sana Mkoo wa Mbeya, hasa Mkuu wa Mkoo na Timu ya Ulinzi na Usalama, wamefanya kazi nzuri sana.

Mkoo wa Mbeya ndiyo walikuwa na kazi kubwa kuliko wote, kwa sababu walikuwa wanawaondoa kwenye Bonde la Ihefu, ambako Pori lile la Akiba lilikuwa na ng'ombe 13,000 na kile ndiyo chanzo cha maji yanayokwenda kwenye mabwawa haya tunayoyazungumza. (*Makofi*)

Sasa nasema hatuna njia, tumetoa Ilani yetu kuhusu mazingira, ameitangaza Makamu wa Rais, tuna tatizo tunaloliona ni lazima mifugo iondoke katika maeneo ya vyanzo vya maji na maeneo ambayo hayafai kwa mifugo. Lakini tukishafanya hivyo, ni wajibu wa Serikali, Halmashauri za Wilaya na Wakuu wa Mikoa, kuhakikisha kwamba, wananchi hao kwanza wanaelimishwa, lakini wanaonyeshwa ukitoka Ihefu tunakupeleka mahali fulani na njia yake ni hii.

Ni kazi hiyo tumekubalina ifanywe kwa makini kwa sababu hatutaki wafugaji wajisikie ni yatima ndani ya nchi yao, lakini tukishawaonyesha njia tukapange pia matumizi ya ardhi katika maeneo yetu.

Mifugo ijue maeneo ya kufuga mifugo ni maeneo haya na ijulikane na kwa kweli tuwafundishe watu wetu kwamba, jamani hatuwezi kuendelea kufanya nchi nzima ni malisho ya mifugo, haiwezekani hakuna nchi inayofanya hivyo duniani, haiwezekani.

Lakini nasema tuifanye kwa uangalifu na kwa umakini na sasa nazitaka Wizara zinazohusika, Wizara ya Ardhi, Wizara ya Mifugo, Wizara ya Kilimo, Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Mazingira, kuanzia tarehe 1 Julai, 2006, wanashirikiana na Mikoa kuhakikisha kwamba, kazi hii inafanywa vizuri, kwa kuheshimu mazingira, lakini vilevile kwa kuheshimu malisho na maeneo ambayo wafugaji wanapaswa kuhamia.

Naomba katika kuwahamisha, wazingatie Waraka wa Rais Namba 1 wa mwaka 2002, Sheria ya Magonjwa ya Mifugo Namba 17 wa mwaka 2003, ili mifugo isiendo kienyeji, maana hata hivi tunavyofanya, unapomtoa mtu Singida na kumpeleka Mbarali, njiani huko unasambaza magonjwa na ukisha sambaza magonjwa.

Ndiyo maana nyama yetu haiwezi kuuzwa nje ya nchi, kwa sababu inaonekana ninyi bado mna magonjwa ya mifugo. Kwa hiyo, naomba lifanyike kwa uangalifu na kwa umakini, lakini kwa haraka, hatuwezi kurudi nyuma, ile ambayo imekwisha toka Usangu isirudi Usangu bali waonyeshwe mahali pa kwenda.

Mheshimiwa Spika, waliochangia eneo la kilimo ni Mheshimiwa John S. Malecela, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Rosemary K. Kirigini, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel, Mheshimiwa Gaudence

C. Kayombo, Mheshimiwa Castor R. Ligallama , Mheshimiwa William J. Kusila na Mheshimiwa Aziza S. Ally. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze na Mheshimiwa William Kusila. Nilimsikiliza jana akizungumzia juu ya mabwawa yaliyotengenezwa. Nimeamua Jumatatu saa 5.00 nitakwenda kuyaona kama kweli hayo aliyoyasema ni kweli ili tuchukue hatua kwa wote ambao wanahusika na jambo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kilimo, sina lugha ya kusema akina Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru wanaita uti wa mgongo. Ningependa kuita kwa jina zuri zaidi, “Roho ya Watanzania.” Maendeleo haya ya Tanzania yataanza kwenye kilimo. Kwa hiyo, ni lazima tukibadilishe kilimo chetu, hatuna *option*.

Mheshimiwa Spika, naomba mjifikirie Waheshimiwa Wabunge, mwangalie mwenzako, halafu fikiria adha ya kwenda kumwambia bwana naomba chakula, maana mimi sina chakula. Tazama *humiliation* unayoipata as an individual. Tafsiri *humiliation* hiyo kama Taifa, kwamba Watanzania tunakwenda kupiga magoti tunaomba chakula na tusipopata chakula kile watu watakufa, ndivyo tumefanya.

Mheshimiwa Spika, lakini tunaomba chakula nchi ambayo imejaa mito mingi sana, kuna mabonde ambayo yakilimwa vizuri tutapata chakula cha kutosheleza nchi yetu. Tunaomba chakula, nchi ambayo ina watu wenye uwezo wa kufanya kazi asilimia kubwa hapa vijana, sehemu nyingine huko ni wazee, sisi kwa asimilia kubwa hapa ni vijana wenye uwezo kufanya kazi. Awamu ya Nne tumeamua kulipa kipaumbele suala la kilimo. Tunawataka Wakuu wa Mikoa wote, Wakuu wa Wilaya Wote, Wakurugenzi wote, kazi kubwa, ajenda namba moja, ni elimu ikifuatiwa na kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri, kama atakavyofafanua Waziri wa Kilimo, Chakula na Masoko, tumepata mradi mkubwa sana unaoitwa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo kuanzia mwaka huu fedha 2006/2007. Muda wa programu hii ni miaka saba, kuanzia mwaka huu wa fedha na programu itatekelezwa katika ngazi ya Wilaya na Vijiji. Gharama za programu imekadiriwa kuwa Shilingi trilioni 2.5. Mgawanyo wa fedha hizi ni kama ifuatavyo:-

Uwekezaji katika kilimo cha umwagiliaji mashamba Sh.1,493,000,000/= ambazo zitapelekwa Wilayani kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Uendelezaji wa kilimo umetengewa Sh.135,795,000,000/= ambazo nazo zitapelekwa Wilayani. Uboreshaji wa huduma za kilimo kama vile huduma za ugani umetengewa Sh. 190,000,000,000/= ambazo nazo zitapelekwa Wilayani. Uendeshaji wa mafunzo ya wakulima, wafugaji na watumishi Sh. 15,794,000,000/= ambazo na zenyewe pia zitapelekwa Wilayani. Kwa mwaka huu wa fedha 2006/2007 zimepangwa Shilingi bilioni 33.17 kutoka kwa Wahisani na Shilingi bilioni 12.5 kutoka Serikalini. Mkakati ni kuhakikisha kuwa ipo mipango bora na shirikishi ya maendeleo ya kilimo Wilayani. Kuongeza tija, uzalishaji na mapato ya wakulima na kufanikisha lengo la kujitosheleza kwa chakula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukishapata mradi mkubwa kama huu, hatuna sababu ya kushindwa. Tumekubaliana na Waziri wa Kilimo, Chakula na Masoko kwamba itafanyika Semina maalum kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge wote waelewe maana ya Mradi huu katika Wilaya zao. Lakini wataitwa vilevile Wakurugenzi wote, Ma-DC wote, Wakuu wa Mikoa wote na Ma-RAS waje na wao wauelewe Mradi huu. Kwetu sisi suala la kilimo ni kufa na kupona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, moja ya vigezo vyta kupima viongozi wote walioko Mikoani na Wilayani ni jinsi walivyosimamia Elimu na jinsi walivyosimamia kilimo. Hilo ndilo lengo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukijilinganisha na nchi kama Kenya au Malawi tu, mazao wanayopata kwa ekari ni mara mbili tunachopata sisi, kwa nini? Hatuwezi kuendelea kukubali hali hii, hatuwezi kuendelea na suala la kuombaomba chakula wakati nchi imeja rutuba, mito na watu wa kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilipata nafasi ya kukutana na wadau wa mazao makubwa, najua wadau wa mifugo nao wananihitaji, nitakutana nao. Kwa zao la pamba, tulikubaliana kuongeza uzalishaji kutoka kilo 300 za sasa hadi kilo 1000 kwa ekari kwa kila mkulima ifikapo mwaka 2010, tunaweza kufanya hivyo. Kuhusu korosho kuongeza uzalishaji kutoka tani 90,385 za sasa hadi tani 180,000 mwaka 2010, kwa korosho nadhani tutawahi kabla ya mwaka 2010. Nimeona jitihada za Lindi kule na Mtwara, nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu tumbaku, kule Urambo tunataka kuongeza uzalishaji kutoka tani 56,500 sasa hadi tani 100,000 ifikapo mwaka 2010. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa tumbaku, kuna mambo machache sana ambayo tukiyafanya kufikia mwaka 2008 tutafikia lengo. Hili tunaweza kufanya. Kahawa kuongeza uzalishaji kutoka tani 54,000 mwaka 2004/2005 hadi kufikia tani 120,000 ifikapo mwaka 2010, ndugu zangu tunaweza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, narudia, Viongozi wote Mikoani na Wilayani tuna vipaumbele viwili, elimu na kilimo. Tukiwa wakali mtatusamehe, lakini lengo letu tuondokane na aibu ya kuomba chakula kama Taifa lenye uwezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamesemea sana suala la barabara. Waliochangia ni pamoja na Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Jacob Shibili, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Mohamed Said Sinani, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Abbas Mtemvu na Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa kuweka bayana. Nilimsikiliza rafiki yangu Gosbert Blandes jana akisema kwamba kama tunabisha atatuletea *video* tuone ahadi za Mheshimiwa Rais. Sisi ni waungwana, ahadi ni ahadi na zitatekelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, narudia kwa wote kwamba, popote pale ambapo Mheshimiwa Rais alipotoa ahadi, tutasimamia ahadi za Mheshimiwa Rais zitekelezwe, maana ni ahadi za Chama cha Mapinduzi. Lakini tutakwenda kwa awamu. Nyingine zitaanza sasa na nyingine zitafuata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jana nilimsikiliza Mheshimiwa Paschal Degera akilalamika sana. Lakini ningependa kumwambia kwamba barabara ya Singida - Babati - Minjingu inakwenda vizuri. Benki ya Maendeleo ya Afrika imeahidi kimsingi kutoa Dola za Kimarekani milioni 78.3. Barabara ya Babati - Kondoa - Dodoma - Iringa, mazungumzo yanakwenda vizuri na *inshallah* pengine na yenewe itaanza vilevile hivi karibuni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Dar es Salaam kama walivyosema wengine, kwa kweli kuna tatizo kubwa sana la barabara. Wale mlionika Dar es Salaam hivi karibuni ni taabu kweli kweli. Kama unataka kwenda Mbezi au kutoka Mbezi ni maudhi kweli kweli! Muda ambaa mtu anapoteza njiani kabla ya kufika kazini ni mwiningi sana. Ikitokea kuna Viongozi wageni wamekuja nchini, hata mimi wakati mwininge naona ni kero pale Dar es Salaam. Lakini ni kwa sababu magari yamejaa barabarani kweli kweli! *Dotcom Generation* kila meneja ana gari, sasa utafanyaje? Ni mafanikio, lakini tumetambua tatizo hilo, tumeamua kulishughulikia kwa namna kadhaa. Kwanza, Halmashauri za Dar es Salaam mwaka huu zimetenga Shilingi bilioni 3.2 kwa ajili ya barabara za Dar es Salaam. (*Makofi*)

Lakini vilevile, kuna ule Mradi wa Mabasi yaendayo kwa kasi uliofadhilliwa na Benki ya Dunia, umefikia hatua nzuri. Benki ya Dunia imeshatoa kiasi cha fedha na tunajaribu kutafuta wafadhili wengine watuwezeshe ili tupate *package* ya kutosha. Awamu ya Kwanza ya Mradi huo itahusisha barabara za Morogoro hadi Kimara, Mwenge hadi Ubungo, Makutano ya Barabara ya Morogoro na Sokoine hadi *Ferry* na Msimbazi hadi Kamata.

Mheshimiwa Spika, naamini mradi huu utakapokuwa umekamilika, utachangia kwa kiasi kikubwa sana kuondoa tatizo kubwa la msongamano wa magari pale Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, lakini TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu tunashughulikia barabara zifuatazo:- Ukarabati wa barabara ya Mandela, ujenzi na upanuzi wa barabara Kilwa kuwa njia nne, ujenzi na upanuzi wa barabara ya Sam Nujoma kuwa njia nne kuanzia Mwenge hadi Ubungo. Kwa kweli hapa Mheshimiwa Basil Mramba lazima achangamke kidogo. Huu mradi unachelewa na hatuoni sababu. Ukarabati wa barabara ya Shekilango unaendelea, nilimsikiliza Mheshimiwa Lucy Owenya juzi, lakini tutafuutilia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile, suala la kupambana na tatizo Mbezi, Meya wa Jiji la Dar es Salaam amekuja na mawazo mazuri sana. Kuna mradi tunautazama ambao nadhani tutakubaliana ili tupanue barabara ya kutoka makutano ya barabara ya Kawawa na Ali Hassan Mwinyi hadi Tegeta kuwa njia nne. Tunadhani itapunguza tatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tutaimarisha barabara ya *old Bagamoyo - Kawe - Oasis Club*, ukarabati wa Barabara ya Igesa kwa kiwango cha lami, ukarabati wa Barabara ya Uhuru, ukarabati wa Barabara ya Kichangani Mtoni kwa kiwango cha lami na ukarabati wa Barabara ya Mandela Wailesi mpaka Mahunda. Tunaamini hatua hizo zitatusaidia sana kupunguza angalau tatizo hilo la Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini liko lingine ambalo halihitaji kungoja miradi. Hili ni la Halmashauri kutunga sheria ndogo ndogo ili kuzuia magari makubwa na yale ya kusambaza bidhaa kuingia katikati ya Jiji wakati wa mchana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, muda wangu naona unakwenda. Sasa nije kwenye Muungano.

Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii ni pamoja na hawa wafuatao: Mheshimiwa Maida Abdallah, Mheshimiwa Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa na Mheshimiwa Haji Juma Sereweji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yameulizwa maswali mengi, mengine nayashangaa kidogo yanayosema watu wapewe nafasi ya kuamua juu ya aina ya Muungano wanaoutaka. Sasa naomba niwakumbushe historia tu kwamba, mwaka 1999 Jaji Samwel Kissanga alipitia katika nchi nzima na akatoa taarifa ambayo tulipokea na Taifa zima linajua. Taarifa ya Kamati ya Jaji Samwel Kissanga ilionyesha kuwa asilimia 88.87 ya Watanzania wa pande zote mbili za Muungano wanataka Muungano wa Serikali mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, katika taarifa ya Jaji Kissanga, asilimia 94.46 waliona hakuna haja ya kuhoji uhalali wa Muungano. Sasa jamani hii Sera ya Chama cha Mapinduzi inayokubalika na wananchi wa Tanzania, tumezunguka Tanzania nzima kunadi sera hiyo na Watanzania wameikubali kwa idadi ya Wabunge waliomo humu ndani na Madiwani walioko nje na kura 82.84 za Watanzania. Sasa anayehoji kwamba hii ni sera ya nani, awahoji Watanzania waliotupa kura. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jamani Muungano huu sio Muungano wa Viongozi, ni Muungano wa watu. Pimeni Muungano ulivyo kati ya Watanzania wenyewe kwa wenyewe. Wanaohoji sio Watanzania wale wa kawaida, wanaohoji ni watu wanaotaka vyeo labda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini tunakiri kwamba kama ulivyo Muungano mwingine wowote duniani, huwezi kukosa matatizo. Canada wameungana siku nyingi, wana matatizo, wanaendelea kuzungumza tu. Waingereza wale ni Falme zimeungana, wanaendelea kuzungumza tu. Sasa na sisi tukizungumza mambo ya Muungano, kwa nini ionekane ni nongwa? Kwani ni tatizo! Hata baba na mama huko nyumbani, jamani, si wanazungumza siku nyingine hawakubaliani lakini si wanazungumza tu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lakini ninakubaliana na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed alisema tuujadili Muungano, kujadili Muungano ruksa haki yako. Hata jana nimewaambia watu wa *University* wame-*organize* Mkutano kule Zanzibar wanazungumza habari ya Muungano. Ni mali yao. Hii ni mali yako. Una haki ya kuizungumza bwana, ni chako lakini chako kitunze siyo ukibomoe. Usizungumzie Muungano kwa minajili ya kuubomoa. Zungumza kwa namna ya kuendeleza Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo sisi tuna heshima duniani na Afrika kwa sababu ya huu Muungano. Tuko hapa wote tunafurahi kwa ulinzi na amani na utulivu shauri ya Muungano. Idadi ya kubwa ya Watanzania hawajui kitu kingine, wanajua Muungano, wamezaliwa ndani ya Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema yapo matatizo madogo madogo lakini ni matatizo ambayo tunaweza kuyashughulikia. Hayana matatizo makubwa sana ya kusema kwamba Muungano wetu una matatizo. Muungano wetu ni imara kama sisi Watanzania tulivyo imara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwezeshaji wa wananchi, waliochangia eneo hilo ni pamoja na Mheshimiwa Maida Abdallah, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mheshimiwa Abbas Mtemvu na Mheshimiwa Paul Kimiti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeombwa kumtambua vile vile Mheshimiwa John Shibuda ambaye pia alichangia kwenye mjadala huu. Samahani nilikusahau Mheshimiwa John Shibuda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili sisi vilevile ni la kufa na kupona. Tumewaaahidi Watanzania katika Ilani ya Uchaguzi kwamba tutapata ajira za watu wasiopungua milioni moja. *We mean business*, lazima tuzipate hizo ajira kwa watu milioni moja. Hatua zetu za kwanza ni pamoja na hii ya kutoa milioni 500 kwenda Mikoa kuanzisha ajira kwa wajisiriamali na watu wengine wa aina hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesikiliza mjadala hapa, kuna watu wanafikiri tutagawa kama njugu hizi fedha. Jamani hatuzigawi fedha kama njugu. Kwanza, tunataka zielekezwe kwa wajisiriamali. Tumewaambia jana Wakuu wa Mikoa hii ni mojawapo ya kazi zao ya kuwatafuta wajisiriamali katika Mikoa yao na katika Wilaya zao na

kuwaongoza. Tumefungua dirisha lingine dogo tu katika Benki, fedha hizi zitachukuliwa kwenye Benki. Isipokuwa masharti yake ni masharti nafuu na riba ile itakuwa ndogo kabisa, kwa sababu ugomvi wetu na mabenki hapa riba zao ni kubwa na wakichukua mikopo, watu wetu wanashindwa kurejesha kwa sababu riba ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jambo la kwanza, riba itakuwa ndogo. Jambo la pili, hizi fedha zitapatikana kwa urahisi bila *collateral* za lazima sana za kuaminiana, lakini kwa kasi. Tunataka ifikapo mwezi wa Agosti mwaka huu tunapoondoka hapa, mkienda huko mkazikute mhangaike nazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, alinipigia simu mfanyabiashara mmoja maarufu Mtanzania akaniambia, kwa mara ya kwanza Serikali sasa mmejua cha kufanya. Lakini akaniambia angalieni hizo fedha msiwapelekee watu amba siyo wajisiriamali. Mkiwapelekea watu amba sio wajasiriamali, zote zitakwisha hazitakuwa na *impact* kwenye uchumi. Tunataka kumpelekea hata mtu kama ana *container* yake mahali, ukimwongezea milioni tano ataajiri vijana wengine wawili, watatu, wanne, watano, ni ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wamenifurahisha sana watu wa Mkoa wa Lindi. Mkoa wa Lindi wameshajiandaa. Mkoa wa Lindi akinamama wengi sana wanashughulika na kubangua korosho. Mashine zile za kubagua korosho ni kama Shilingi milioni tano. Wao wanasema tunaomba sisi hizo fedha tununue mashine za kubangua korosho. Kwa hiyo, kuna uhakika wale akina mama wa Lindi, kwanza, tutaongeza ajira, tutaongeza uzalishaji, tutaongeza hata korosho za kupeleka nje ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesema katika hotuba yangu kwamba tutakuwa na *Advisory Board* na Bodi hii watakuwemo Waheshimiwa Wabunge katika Bodi. Lakini licha ya kuwepo kwenye Bodi, naomba muanze kwenda huko kuangalia mambo mhakikishie kwamba wapiga kura wenu wale wajasiriamali wanapata mikopo hii ili waongeze ajira na waongeze kipato chao. Wala msione aibu ndugu zangu, hiyo ndiyo kazi ya Mbunge. Ukipata wajasiriamali 20, wanabadilisha uchumi wa Jimbo lako. Kwa hiyo, nawaomba msione aibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini Mfuko huu msiufananishe na ule mwingine wa Jimbo tuliokubaliana. Tutaanza huo mwaka kesho, huu ni tofauti. Ule wa Jimbo ni tofauti na huu. Huu ni kwa ajili ya kuendeleza biashara na ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kupitia maeneo mawili madogo sana. Kwanza, nitoe shukrani za jumla. Kama nilivyosema, ubora wa hoja na mjadala ulikuwa wa hali ya juu kabisa. Nawapongeza sana. Lakini vilevile, umezingatia matatizo halisi tuliyonayo katika Majimbo yetu. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi Mawaziri kazi yetu ni kusikiliza pale palipo na matatizo mara moja, tunafika kusaidiana kuondoa hayo matatizo. Hii ni Serikali ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya, hatuna nafasi ya kungoja kwa lolote lile. Tukiambiwa, pale pale tunalishughulikia. Ndiyo maana juzi Mheshimiwa Wilson Masilingi alipolalamika

juu ya watoto karibu 1,000 waliolazwa katika Hospitali ya Rubya, tumemwondoa Waziri Bungeni kwenda kuwaangalia. Lakini vilevile lazima tujifunze kufanya maamuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine hapa nchini ni watu wanaogopa kufanya maamuzi. Mara nyingine hili tishio kwamba watasema umekula, linasumbua kweli! Nimeona tunahangaika pale Dar es Salaam kuagiza *turbine gas* kwa ajili ya gesi. Kila mtu akija ana mashaka, hata kivuli mtu anaogopa. Mimi nasema kheri ufanye uamuzi wa kuhukumu kwa kufanya uamuzi kuliko kutofanya uamuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Benson Mpesya ombi lako kugeuza eneo la Iwambi badala ya kuwa shamba la mifugo liendeshwe kwa shughuli za Halmashauri pamoja na wawekezaji waliokuja. Linakubalika na litatekelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia na wale ambao hawakuchangia hata kwa kukaa kimya nawashukuru sana kwamba mmechangia. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Makatibu Wakuu wote pamoja na wataalam wa Wizara wote, tumeshirikiana vizuri sana, nawashukuru sana. Kipekee namshukuru Ndugu Vicent Mrisho, Mama Maimuna Tarishi, Bwana Michael Mwanda na Wilson Mukama, Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu Ofisi ya Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahaa! Mcheza kwao hutunzwa. Nimefurahishwa sana na timu yako inayoongoza Bunge, wewe mwenyewe, Naibu Spika na Wenyeviti. Mheshimiwa Job Ndugai alikaa kwenye Kiti nikasema ni Mheshimiwa Job Ndugai ninayemfahamu yule! Alifanya vizuri sana! Hata kama alikuwa haeneienei kwenye Kiti lakini kichwa kikitoka ni busara. Alikaa kwenye Kiti Mheshimiwa Jenista Mhagama, haijapata kutokea! Hodari kweli kweli! Ndiyo maana kule CCM tunasema akinamama wanaweza. Naibu Spika, umahiri wake na umakini ni wa hali ya juu sana. Hongera sana Mheshimiwa Anne Makinda. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, maana unaendelea kuonyesha ni Spika wa viwango na kasi. Kwa hakika Bunge limepata mwenyewe na Kiti kimepata mwenyewe. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, kwa heshima na taadhima, nawaomba sasa mkubali kutupatia fedha tulizoomba tukafanye kazi tuliyokubaliana hapa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana. Nazipokea kwa shukrani kubwa pongezi zako zote kwa wale ambao tunakalia Kiti hiki umetuimarisha. Sasa Waheshimiwa Wabunge, hoja hiyo iko mbele yetu na imeungwa mkono.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

**KAMATI YA MATUMIZI
MATUMIZI YA KAWAIDA**

FUNGU 25 - OFISI YA WAZIRI MKUU

Kifungu 1001 – *Administration and General ...* Shs.4,014,623,000/=

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, sikusudii kupinga fungu. Lakini nataka maelezo kidogo kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati akijibu hoja, kuna hoja ya msingi tulimpa na bahati mbaya hakuweza kujibui wala Mawaziri hawakujibui. Kwa hiyo, sikuridhika na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwa ruhusa yako fungu hilo la 25, programme 10, Kifungu 5100 - *Basic Salary*, Mshahara wa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tulipokuwa tunawasilisha hoja zetu na Waziri wa Nchi aliwahi kujibu juu ya suala zima la Vyombo vya Dola vinavyotumia nguvu za ziada wakati wa uchaguzi, alitoa maelezo mazuri Mheshimiwa Waziri, lakini kuna eneo moja hili aliliacha nafikiri ni muhimu sana kwa Taifa letu kulifahamu. Ndiyo maana wakati tulipokuwa tukiwasilisha hoja zetu tulisema kwamba wakati umefika, kuna pande zote mbili zinachukua sheria mikononi mwao. Upande wa Vyombo vya Dola na upande wa raia unachukua sheria mikononi mwao. Tukasema ni vizuri basi Taifa likajielekeza katika kulishughulikia jambo hili *seriously*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi wa hayo, tuliwahi kumpa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Mungano video *cassette* inayoonyesha ni kwa kiasi gani Vyombo vya Dola vilitumia nguvu za ziada.

Mheshimiwa Spika, vilevile Mheshimiwa Waziri Mkuu ye ye binafsi tulimpa *documents* zote na hata wewe Mheshimiwa Spika tulikupatia *copy* na mpaka leo hatujapata majibu ya jambo hilo. Tulitegemea ingetumika *forum* hii kutoa msimamo juu ya pande zote mbili, wananchi wanaochukua sheria mikononi mwao, lakini vilevile Vyombo vya Dola vinapochukua sheria mikononi mwao. Ni hatua gani na malengo gani tunaweza kufanya? Nikipata maelezo ya hilo nitaridhika na fungu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli suala analozungumza Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed aliwahi kuliwasilisha Serikalini, lakini tumempa maelezo ambayo ningependa kurudia hapa kwamba, vyombo vinavyotuhumiwa katika

taarifa zile ni vyombo ambavyo viko chini ya mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Tukasema, busara zingepeleka jambo hilo kwenye Tume ya Haki za Binadamu ambayo itaangalia kwa pande zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande huu unaangalia vile vile Zanzibar, lakini kwa bahati mbaya kuna tatizo la kisheria. Tume ile ya Haki za Binadamu haiwezi kufanya kazi Zanzibar kwa sababu ya sheria fulani ambayo inahitajika tuibadilishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakusudia kuibadilisha sheria hiyo mwezi Oktoba ili Tume ya Haki za Binadamu iweze kufanya kazi vizuri Zanzibar. Nina hakika wakati huo masuala ya Zanzibar yatashughulikiwa na hiyo Tume. (*Makofî*)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 27 - Msajili wa Vyama vyaa Siasa

Kifungu 1001 – *Administration and General...* Sh. 15,229,892.000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu

Kifungu 1001 - *Administration and General ...* Sh.8,944,027,300/=

(Kifungu kilichotjwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ningewaomba njipange vizuri ili muwahi kwa sababu shughuli hii itatuchukua muda na mara nyingine wakishakubali Wabunge wote, itaniwia vigumu kurejea tena kukuona.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Mimi sina matatizo na Waziri Mkuu kimsingi, lakini nataka kusahihisha. Wakati wa asubuhi Waziri wa TAMISEMI wakati akijibu hoja mbalimbali alisema kwamba...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mrope inabidi utaje kifungu. Hatuzungumzi kwa ujumla tu.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Ahaaa!! Kifungu 1101, *Subvote 250100 - Mshahara wa Waziri.*

Wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu akijibu hoja mbalimbali, alisema kwamba mimi sikuwa nimeleta hoja yoyote na pia sikuwa nimeleta orodha ya wale ambao walikuwa wanadai fidia. Sasa naomba, hii barua nitakupa ili iwe Mezani, tarehe 10 Desemba, 2003 nilimwandikia barua Mheshimiwa Mizengo Pinda inasema hivi:-

**KULIPWA KIFUTA MACHOZI KWA WANANCHI
WALIOHAMISHWA TOKA MAKONDE
ESCAPEMENT WILAYANI MASASI**

Tulipokuwa Dodoma Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Tatu, niliwasilisha kwako tena, suala la wananchi wa Vijiji vya Mpanyani, Mihima, Mkang'u, Lukohe, Miwale na kadhalika katika Jimbo la Masasi ambao walihamishwa na Serikali kutoka maeneo yao yaliyokuwa karibu na *Makonde Escapement* kuanzia mwaka 1987 mpaka 1990 ili kuanzisha Hifadhi ya Misitu. Wenzao wa Kijiji cha Majembe Jimbo la Lulindi, wamekwishalipwa fidia ya mali walizopoteza.

Kwa kufuatilia ushauri ulionipa nilifikisha suala hili la kutokulipwa kifuta machozi kwa wananchi wa Jimbo la Masasi kwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba ambaye aliniagiza nikutane na Naibu wake Mheshimiwa Khatib ili tujadili kwa kina zaidi. Katika mazungumzo yangu na Mheshimiwa Khatib alinishauri kuwasiliana nawe, yaani Waziri Pinda ili Wizara yako impelekee makisio ya gharama ya kifuta machozi kwa nia ya kuona uwezekano wa kulipwa.

Lengo la barua hii ni kuiomba Wizara yako ikamilishe zoezi la makisio ya gharama na kuwasilisha kwa Mheshimiwa Naibu Waziri ili tuweze kufikia mwisho wa kero hii ya miaka mingi. Kama nilivyokueleza, suala hili limefikia mahali pabaya kisiasa hasa kwa kuwa wenzao wa Lulindi walikuwa wamelipwa miaka mingi iliyopita. CCM itapata wakati mgumu kutoa maelezo ya kuwaridhisha wananchi husika katika suala hili katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005. Naomba ufanye hima kulishughulikia.

Raynald A. Mrope
MBUNGE WA MASASI

Nakala: Mhe. Abdisalaam Khatib

Mhe. Isidore Shirima
Mkuu wa Mkoa

Bwa. Jacob Chitukuru
Mwenyekiti wa CCM

Bw. Ali Lufungo
Mkuu wa Wilaya.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilisemekana kwamba mimi sikuleta hoja hiyo. Sasa hii barua ya nini kama sikuleta hoja hiyo? Mimi nitapeleka orodha kwa ajili gani? Hiyo si kazi ya Serikali?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, kwa mujibu wa kanuni ya 81 (b), muda wa kusema katika Kamati ya Matumizi hauzidi dakika tano. Kwa hiyo maliza ili upate majibu.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Sawa, nami nilikuwa *in time* kabisa. Kwa hiyo, kutokana na *statement* hii naomba sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu aseme ndani ya Bunge hili kama wananchi hao watapata kifuta jasho ama hawatapata. Kwa sababu inaonekana tumekuwa tunavutana vutana tu na mpaka hivi sasa wananchi wanalamika sana. Naomba hoja yangu ijadiliwe na kutolewa uamuzi.

MWENYEKITI: Ni maelezo tu.

WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKIOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kusema kwa kifupi sana kwamba, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge maana ameshakuwa ni Mbunge ambaye ndiyo ilikuwa hofu kubwa wakati ule kwamba tusipolishughulikia mapema ingewezeckana pengine Uchaguzi ungekuwa mgumu. Lakini nashukuru, hilo limekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa hapa kwa kweli tulichokuwa tunaomba sisi, ilikuwa ni orodha tu na tulifikiri pengine Mbunge angeweza kuiwasilisha tukalifanyia kazi hizo haraka. Lakini mimi nafikiri tusiendeleze mjadala sana. Nimezungumza na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Meghji, kwa hiyo, tumekubaliana tukipata hiyo orodha tutalifanyia kazi hili jambo vizuri sana ingawa kwa Bajeti hii, kwa namna mambo yameshapita, hatutaweza, lakini amesema kwa Bajeti ijayo tunaweza tukalitazama mapema sana tukalingiza kwenye Bajeti kulingana na misingi tuliyokuwa tumekubaliana na kifuta machozi.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa ahadi hii, lakini kwa sababu limechukua muda mrefu, ningeomba angetupa muda. Halafu pia wakati huo huo nataka kumshukuru Waziri Mkuu kwa kusema dhahiri kwamba Mkoa wetu ni mdogo, kwa hiyo haufai kuletewa mifugo inayofukuzwa sehemu nyingine na kuletwa kule. (*Makofi*)

MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Subvote* 1101, kifungu 250100 - Mshahara wa Waziri. Lakini kabla sijasema, kwanza nikuombe radhi wewe mwenyewe kwamba inawezeckana wakati Waziri alipokuwa akijibu hoja za Wabunge atakuwa pengine ameелеzea jambo hili. Kwa hiyo, natangulia kuomba radhi. Lakini ni bahati mbaya kwamba nilikuwa nimepewa kazi nyingine ya kufanya, sikuwepo wakati anajibu.

Ni kwamba kuna ahadi ya Serikali ambayo ilitolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu barabara ya Miangaria Kinyamatundu na mwaka 2005

kwa bahati nzuri Waziri mwenyewe nilipozungumza na Waziri wa Fedha, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba alisema TAMISEMI wakiandika barua kuomba fedha, wangetazama namna ya kusaidia barabara ile. Badala ya kuandika barua kwa Wizara ya Fedha kuomba fedha TAMISEMI walituandikia barua kutuomba tuilete wakati wa mwaka wa fedha, bajeti ya mwaka 2006/2007. Tumeleta makisio ya barabara hiyo, badala yake tumeandikiwa barua na kujibiwa kwamba sisi hatukufikiriwa katika orodha ya wale walioleta maombi isipokuwa tukae tunangoja mpaka hapo marafiki watakapojalia Tanzania kupata fedha ndio tufikiriwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, kwa kuwa sikuwepo, inawezekana walishatoa majibu, lakini kwa kuwa sikuwepo naomba mwenyewe nisikilize majibu juu ya barabara hii, kwa sababu hii inapunguza heshima ya nchi, maana Rais wa Nchi mwenyewe alitamka na bahati nzuri wakati ule alipotamka Mheshimiwa Waziri wa Nchi, wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Peter Pinda tulikuwa wote, tulimsikia Mheshimiwa Rais wakati ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate maelezo. Barabara ilishaombewa gharama ya kitaalamu, imetengenezwa, imeletwa, hata kama fedha hazipo zote mia kwa mia, angalau tungepewa hata fedha za kuanzia maana maendeleo ni hatua kwa hatua. Lakini tumenyimwa kabisa, hatukupewa hata Shilingi moja. Kwa hiyo, naomba maelezo. (*Makofii*)

WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba taarifa hiyo tunayo na ni kweli tulimjibu hivyo kwa maandishi kwa sababu alikuwa ametegemea kwamba tungeweza tukapata fedha kutokana na fedha ya kawaida ya Mfuko wa Barabara. Kwa kipindi kile isingwezekana kwa sababu tulikuwa *tumesha-commit funds* zetu zote. Kwa hiyo, tukamwambia hebu tupe subira tutazame uwezekano wa nyanja nyingine tuone kama tunaweza. Ndiyo maana leo asubuhi nikathubutu kusema kwamba kwa barabara hiyo ambayo kwa kweli gharama zake ni Sh.1,500,000,000/=, Kwa Awamu ya Kwanza tumetenga Sh.300,000,000/= tena kwa kipindi hiki ambacho tunamalizia sasa.

Kwa hiyo, kutoka pale tunakwenda, tunajitahidi kidogo kidogo na pengine baadaye tutashirikiana kwa namna nyingine na Wizara ya Miundombinu tuone kama tunaweza tukasaidiana kuukamilisha mzigoto huu amba ni ahadi ya Rais mapema iwezekanavyo.

MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Nimeridhika.

MWENYEKITI: Umeridhika. Ahsante sana.

MHE. CHACHA Z. WANGWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nazungumzia *Sub votes* 1101 kifungu 250100. Mimi nilikuwa namwuliza Waziri Mkuu hatua ambazo amezichukua baada ya mimi kuwa nime-*raise issue* katika Kikao chake cha *briefing* cha tarehe 12 Juni, 2006 kwamba katika Jimbo la Tarime kuna hali mbaya sana ya mauaji yanayofanywa na watu amba ni Majeshi yasiyokuwepo kisheria na

akaniagiza kwamba nimwandikie barua Waziri wa Usalama wa Raia na nika-*compile* ripoti ambayo ndiyo hii na nimeisambaza kwa Viongozi wa Idara mbalimbali. Ningependa kujua kwamba Mheshimiwa Wazri amechukua hatua gani mpaka sasa kwa sababu sasa hivi tena haya mambo yamezidi na mpaka dakika hii watu wanaendelea kuuawa na nyumba za watu zimechomwa na mali zinaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika hii hii tunayozungumza hapa, tayari wameshakufa watu wanne na Miji 14 imechomwa moto na watu ambao wanafanya shughuli hizo nje ya Katiba na Sheria wakijiita Sungusungu. Kwa hiyo, ningependa njue kwamba amefikia wapi?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Wangwe kwa kutafuta mahali pa kupenyeza jambo lake. Ila ni kweli kama anavyosema, kumetokea matatizo kwenye Jimbo lake, wale wanaukoo wanaendelea kupigana, tena sio tatizo la Serikali, wanapigana wao. Lakini ningependa kumhakikishia tu kwamba Serikali inadhibiti hali hiyo na mpaka sasa imedhibitiwa, ila suala lake amelileta juzi tu, linashughulikiwa, asubiri tutampa majibu wakati muafaka.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts*... Sh. 258,653,700/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1003 - *Policy and Planning* Sh.1,883,784,600/=

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sina tatizo sana na Waziri Mkuu, nimeridhika na majibu yote niliyoyapata. Lakini kwa kutumia kifungu cha 81, ningependa nipate ufanuzi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipeleka swali kuhusu Mtendaji wa Kata aliyemtorosha mtu aliyebacka. Sasa najua Waziri asubuhi alijibu, mimi nilikuwa Ofisini, nimemsikiliza nikiwa Ofisini, ninakubaliana na majibu yake. Lakini labda kuna taarifa ambazo pia hakupewa kikamilifu. Kwanza ni kweli kesi ilipelekwa Mahakamani, lakini haikusikilizwa, mashahidi hawakuitwa. Hilo nadhani linaungana na lingine ambalo niliandika barua kuhusu Mahakimu ambao hawafuati taratibu. Nilikwishalileta, halikufanyiwa kazi mpaka leo.

Sasa wote tunakubaliana kwamba katika suala la *policy* na sheria tulipitisha kwamba kubaka ni kosa zito linakwenda kinyume na udhalilishaji. Huyu ni mtu ambaye amebaka, wananchi wamemkamata *red handed*, wamempeleka kwa Mtendaji, Mtendaji amemtorosha. Anapelekwa Mahakamani, Mahakama inamwachia. Wananchi ni mashahidi, wapo. Mtendaji huyo bado yuko kazini. Mahakama imemwachia, lakini hata kiutawala hakuchukuliwa hatua, anaendelea kwenye Kata hiyo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nipate uhakika, Serikali inachukua hatua gani? Lini? Kwa nini huyu mtu wakati wale walioumia bado wako na maumivu yao, mama aliyebakwa bado yupo, wanakijiji bado wanaendelea na machungu ya kumkamata, kumpeleka usiku, yeche bado yuko? Bado anasema yeche ndiye Mtendaji wa Kata hiyo, ndiyo mtawala. Taarifa nililetewa na ndugu wa huyo aliyetoroshwa.

Sasa katika haya yote, ningependa uhakika Waziri wa Serikali za Mitaa anisaidie. Najua kwamba inawezekana, Mahakama itaachia kwa taratibu zile na Mahakama tuiachie kwa uchunguzi niliouomba. Lakini kiutawala tunamfanyaje mtu huyu ambaye sheria nzito anaiweka pembeni wananchi anawatukana kwamba hamtofanya kitu, bado anaendelea kudunda hapo hapo! Ningependa kupata ufanuzi.

WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Slaa kwa maeleo ambayo amenipatia. Lakini naomba niseme tu kwamba Mtendaji wa Kijiji, Mtendaji wa Kata ni mtumishi mdogo sana ukilinganisha na uwezo wa Halmashauri mliyonao, ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maeleo anayonipa Dr. Slaa, napata tatizo kuona ni kwa nini katika mazingira hayo Madiwani ambaa ndio wenye uwezo asilimia mia moja, kwa mtumishi kama huyu washindwe kumchukulia hatua katika mazingira kama hayo. Lakini naomba nimhakikishie basi Mheshimiwa Dr. Slaa kwamba hebu atuachie TAMISEMI tulifuatilie jambo hili, mimi mwenyewe nitasaidia kulipatia ufumbuzi mapema iwezekanavyo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dr. Slaa, kwa nini Madiwani hamchukui hatua?

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo ndio Mheshimiwa Waziri ananitibua. Ni kweli kwamba Madiwani wana mamlaka, lakini ni kweli ndani ya Bunge hili tumelalamika kwamba Madiwani hawana mamlaka kwa sababu kuna mtu mwingine mwenye mamlaka. Sisi Karatu tumechukua hatua, tumeazimia, tumemwomba Mkurugenzi afanye uchunguzi hakuchukua hatua. Mkurugenzi tukimgusa, tunaambiwa yuko chini yako. Sasa tufanye nini? Ndiyo maana tumekuja kwako. Sisi tunajua tuna mamlaka, tuna uwezo wa kuazimia lakini sheria haitupi sisi mamlaka ya kumwondo. Mamlaka ya nidhamu kwa sheria, bado imebaki kwa Mkurugenzi. Mkurugenzi ni wa kwako na ndiyo maana nimeileta kwako. (*Makofii*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Watendaji wa Vijiji na Kata ni wengi sana. Tukigeuza Bunge hili kuzungumza habari ya Maafisa Watendaji wa Kata, tutashindwa kazi hapa. Mimi nakubali tatizo limetokea, lakini ndani ya uongozi wa Wilaya mlikuwa na nafasi ya kufanya jambo hili. Waziri amejibu kwamba tumelisikia, hamkuchukua hatua zenu kwa sababu kama Mkurugenzi anakataa sio Mwenyekiti wa Kikao, kuna Mwenyekiti wa Kikao ambaye ni Diwani, kwa nini hawakukaa wakazungumza? Kwa hiyo, nasema hamkuchukua wajibu wenu, Mheshimiwa Waziri wa

Nchi, TAMISEMI ameahidi kwamba tutafuatalia. Nadhani mngeridhika na ahadi hiyo kwamba tutachukua hatua. (*Makofii*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 1004 - *Information Education and Communication* ... Sh. 161,788,500/=

Kifungu cha 2001 - *Civil Affairs and Contingencies*... Sh. 584,724,000/=

Kifungu cha 2002 - *National Festivals* Sh. 412,470,800/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 3001 - *Parliamentary and Political Affairs*... Sh.349,810,200/=

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi katika kifungu cha 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi Waziri wa Nchi wakati anajibu hoja alisema kwamba baada ya fedha za Bunge kuwa *approved* katika Bunge, basi Spika au Ofisi ya Spika na Kamati yake ya Huduma za Bunge itakuwa na jukumu la kupanga matumizi na kadhalika. Lakini lipo tatizo la msingi la kutaka idhini kwa Katibu Mkuu Kiongozi kutoka Ofisi ya Spika kwa mambo mengi yanayoendea. Tunataka ufanuzi; Je, sasa hivi kuna maamuzi ya kubadilisha zile *Circulars* za kuitaka Ofisi ya Spika baadhi ya mambo kutaka idhini kwa Katibu Mkuu Kiongozi kwa utaratibu huu sasa kutokana na maelezo yako ya asubuhi? Nilitaka ufanuzi wa hilo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI WA WAZIRI MKUU: Mheshimiwa mwenyekiti, ingawa sina hakika kama ni kifungu hicho, maana nadhani kifungu cha Bunge kinakuja, sina uhakika kama ni hapa. Lakini itoshe tu kusema, nia ya maelezo yale ilikuwa kwamba utaratibu wa sheria ulivyo sasa ni kwamba Ofisi ya Bunge baada ya makisio yao na baada ya kupata vile viwango, *ceilings* zile za Kitaifa kwa Idara zote na kwa *Executive, Judiciary* na *Legislature*, ni Bunge lenyewe wanakwenda Hazina baada ya kugawiwa fedha, wao *wanazi-manage* wenyewe na kila mara wanapopata tatizo huwa wanakwenda Hazina kama wanavyokwenda watu wa *Executive* kwenda kuomba Hazina na kama wanavyokwenda watu wa *Judiciary*.

Kwa hiyo, nilichosema ni kwamba, wenzetu wa Bunge wanaweza kabisa kwa sheria iliyopo sasa hivi wakaitumia vizuri na wasikwame kwa shughuli zinazoendelea. Kama Mheshimiwa Mbunge ana namna bora ya kuboresha utaratibu mwingine, basi hilo ni wazo ambalo anaweza kulileta likajadiliwa na pande zote mbili. Narudia kusema Bunge, *Judiciary* na *Executive* ni nguzo ambazo wote tunategemeana. Tunategemeana kwa mahitaji ya fedha na kwa namna yoyote ile. Kwa hiyo, hakuna nia ya Serikali kukwamisha shughuli zozote zile. Hivi ndivyo sheria kwa hivi sasa ilivyo.

MWENYEKITI: Nadhani inatosha Mheshimiwa Hamad.

MHE. HAMAD R. MOHAMED: Nilikuwa nasema ahsante tu.

MWENYEKITI: Sawa. (*Kicheko*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 5001 - *Coordination of Government..* Sh. 550,624,200/=
Kifungu cha 7001 - *Government Printer... ..* Sh.1,361,680,700/=

(*Vifungu viliyyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 42 – Ofisi ya Bunge

Kifungu cha 1001 - *Administration and General.....* Sh. 6,817,741,600/=
Kifungu cha 2001 - *National Assembly... . .* Sh.27,767,222,400/=

(*Vifungu viliyyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI - 56

Kifungu cha 1001 - *Administration and General* Sh. 3,277,844,400/=

MHE. FATMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 1001 - *Administration and General Sub vote* 250100. Nilikuwa naomba kupata ufanuzi kwamba, kuna Watendaji Kata katika Mkao wa Lindi wale Ma-VEO katika Wilaya mbalimbali hawajalipwa mishahara yao. Kwa mfano, Wilaya ya Ruangwa kuna Watendaji 31, kati ya 75 hawajalipwa mpaka sasa na wengine wanalipwa. Je, kuna mpango gani kuhusu Watendaji hawa ambao hawajalipwa?

WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukiri kwamba bado tuna baadhi ya Ma-VEO ambao bado hawajaanza kulipwa mishahara. Lakini wakati najibu swali mojawapo, nilijaribu kulieleza hili na hatua ambazo tumekwischachukua. Kwa hiyo, tunadhani haitachukua muda mrefu tena kukamilisha zoezi hili. Tatizo ni kwamba taarifa ambazo tumekuwa tukizitaka kwa kipindi fulani baadhi ya Wakurugenzi wamekuwa wakileta lakini zinakuwa bado sio kamilifu. Kwa mara ya mwisho tulidhani tungekamilisha zoezi hili kabla ya Bajeti, lakini bado tumelazimika kurejesha hizi fomu ili zikamilishe vizuri. Kwa hiyo, naomba kumhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutajitahidi jambo hili limalizike sio kwa Wilaya yake tu, lakini tunazo Wilaya kadhaa ambazo bado tunadaiwa jambo hilo.

MHE. ADAM A. MALIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 1001, Subvote 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nazungumza hapa jana kwenye Bunge lako Tukufu, nilikuwa nimewomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wabunge wenzangu pia kama watatu, wanne kauli yake kuhusu ule Mradi wa Daraja la Kigamboni. Kwa sababu ya *spill over effects* kubwa zilizokuwanzo kwa Wilaya zote na kadhalika.

Sasa nilitaka nimwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu, atakubali ombi letu la kwamba Ofisi yake iratibu mradi huu moja kwa moja kwa sababu inaonekana umekwama katika ngazi nyingine zote, hali ya kwamba tayari kuna maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano na maagizo ya Ilani ya Uchaguzi na Mwenyekiti wa Chama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu inaratibu mambo yote ya Serikali lakini, kwa suala la Kigamboni, naomba majadiliano yafanywe kwenye Sector Ministry ndipo tuone kuna tatizo gani.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 1002 - *Finance and Accounts* ... Sh. 153,231,900/=

Kifungu cha 1003 - *Policy and Planning Division*... Sh. 543,796,300/=

Kifungu cha 1004 - *Management Information Systems Division*... ... Sh. 597,468,900/=

(*Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 1005 – *Legal Service Division*... Sh.209,698,500/=

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Sub vote 105 item 25...

MWENYEKITI: Hakuna Sub vote 105 hapa.

MHE. DR. ZAINABU A. GAMA: Sub vote 1005

MWENYEKITI: Ulisema 105.

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA: Okay, basi samahani Mheshimiwa Mwenyekiti. Naomba tu ufanuzi, katika Sheria ya *Tender Board* ya 2001 ilimweka Mkurugenzi kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya *Tender Board*, lakini kwenye Sheria ya mwaka 2004 ilimwondoa kutokana na Sheria yenye. Mpaka sasa, bado baadhi ya Wakurugenzi ni Wenyeviti wa *Tender Board*. Naomba maelezo kamili au usahihi wa hili jambo.

MWENYEKITI: Ni wapi huko? Pengine utusaidie. Kibaha!

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala limezungumzwa tukiwa katika Semina ya Kanda ya....

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge tutajie.

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA: Ni Kibaha, Dar es Salaam.

WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimeshanong'ona na Mheshimiwa Mama Gama, mengine haya tuyanong'one nong'one huko. Lakini naomba tu nimwombe kwamba pengine baada ya kumaliza, tuzungumze tuone tatizo likoje halafu nina hakika tutalimaliza sio kubwa sana hili.

MWENYEKITI: Ahsante. Kwa hiyo, Kibaha na wengine wanong'one na Waziri, basi yamekwisha hayo.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 2001 - *Regional Administration Coordination Division*... Sh. 3,857,892,200/=
Kifungu 2002 - *Local Government Coordination Division* ... Sh. 3,664,403,700/=
Kifungu cha 2003 - *Sector Coordination Division* Sh. 26,290,215,300/=
Kifungu cha 3001- *Organization Development Division* Sh. 5,243,910,800/=

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 61 – TUME YA UCHAGUZI

Kifungu cha 1001 - *Administration and General*... Sh. 4,950,617,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamatiya matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 91 – TUME YA KUDHIBITI MADAWA YA KULEVYA

Kifungu cha 1001 – *Administration and General*... Sh. 1,317,992,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 92 - TUME YA KUDHIBITI UKIMWI

Kifungu 1001 – *Administration and General.... Sh. 71,500,000/=*
Kifungu 1002-*Finance Administration and Resources mobilisation...Sh. 2,954,987,000/=*
Kifungu 1003 - *Monitoring evaluation Research and MIS Sh. 338,500,000/=*
Kifungu 1004 - *Advocacy Information Education and Comm... Sh. 638,300,000/=*
Kifungu 1005 - *District and Community Response... Sh. 313,500,000/=*

MIKOA

Fungu 70 – Mkoa wa Arusha... Sh. 32,936,011,000/=

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 71 – Mkoa wa Pwani... Sh. 28,730,337,000/=

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 71, *Program number 10, Sub vote 1001.* Ninaomba nipate maelezo, kwanini kila Bajeti inapopita nyumba ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani inatengewa fedha lakini huwa haitengenezwi na pia nyumba ya Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo nayo pia haitengenezwi ingawa fedha zinatolewa? Ni sababu zippi za msingi zinazosababisha nyumba hizo haziishi na wakati wote fedha zinatolewa?

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nilikuwa na hiyo *Vote 71, Sub vote 3001* kifungu kidogo 543 - *Construction of the District Hospital.* Nilitaka kujua ni hospitali ipi? Je, ile hospitali ya pale Kibaha iliyoungua, imo katika pesa hizi?

WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nitoe maelezo kuhusiana na swali la Mheshimiwa Nyami. Majengo yote mawili yamekuwa yakifanyiwa ujenzi wa namna moja au nyingine hasa ile ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani.

Kwa upande wa nyumba ya Mkuu wa Wilaya pale Bagamoyo, ni kweli tulikuwa na matatizo katika kutekeleza ule mradi. Lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Nyami kwamba tumeshamalizana na yale maswala yaliyokuwa yanatuchelewesha, tunadhani miradi yote miwili itakamilika haraka iwezekanavyo kulingana na hali tunavyoiona sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la Mheshimiwa Dr. Gama, ninaloweza kusema ni kwamba, *tuta-check* tuwe na uhakika maana sio vizuri tukasema bila kuwa na uhakika kama fedha zile ni kwa ajili ya ile hospitali iliyoungua, *I mean* Kituo cha Afya au hapana. Lakini nilikuwa nimezungumza naye kabla, kuonyesha tu kwamba kama waliweka jambo hili katika mpango wao kupitia Mkoa inawezekana fedha zikawa ni hizo. Lakini

tutamwanganzia baadaye ili tumthibitishie na hata kama siyo hivyo, bado tunafikiria tunaweza tukawa na njia nyingine ya kumsaidia kuhakikishia kwamba kituo hicho kinaweza kikasaidiwa kwa njia nyingine hasa kupitia fedha za ukarabati.

(*Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 72 - Mkoa wa Dodoma... Sh. 37,559,065,000/=

MHE. MOHAMMED RISHED ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, toka tumeanza kuzungumza, hii Mikoa *figure* zinazosomwa ni tofauti na zinazoonekana kwenye vitabu vyetu. Sasa je, kuna masahihisho? Kwa sababu imo ndani ya *Hansard*, ni vyema ikaeleweka vizuri.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, mtaona kwamba Katibu anaposoma, hasomi ile inayoitwa *net*. Anasoma *total of votes*, yaani ni *Sub vote* pamoja na *appropriation in aid* ambayo inatolewa kwenye idadi hiyo. Ndiyo maana unachotakiwa kutazama ni zile tarakimu juu ya *column* imeandikwa *Less appropriation in aid* hiyo ndiyo inayosomwa na Katibu.

(*Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Fungu 73 - Mkoa wa Iringa Sh. 42,204,991,000/=

Fungu 74 - Mkoa wa Kigoma Sh. 32,450,558,000/=

Fungu 75 - Mkoa wa Kilimanjaro Sh. 46,431,149,000/=

Fungu 76- Mkoa wa Lindi Sh. 23,709,043,000/=

Fungu 77- Mkoa wa Mara Sh. 33,863,309,000/=

Fungu 78- Mkoa wa Mbeya... Sh. 50,475,231,000/=

Fungu 79- Mkoa wa Morogoro... Sh. 41,809,678,000/=

Fungu 80- Mkoa wa Mtwara... Sh. 29,003,688,000/=

(*Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 81- Mkoa wa Mwanza Sh. 59,285, 980,000/=

MHE: ERNEST G. MABINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote* 81, fungu lote hilo. Nilitaka kuelewa tu kwamba Mkoa wa Mwanza fedha ilizopewa mwaka 2004 mpaka mwaka 2005 zilikuwa ni Shilingi bilioni 66. Mwaka 2005 mpaka mwaka 2006 tulipewa fedha Shilingi bilioni 82. Mwaka huu zimetoka bilioni 59, ni sababu zipi ambazo zimesababisha pesa hizi zikapungua? Naomba maelezo.

MWENYEKITI: Maelezo ya marudio tu. Lakini ilizungumzwa sana hii kuhusu miradi ambayo.... Nisijibie Serikali. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunisaidia. Sababu kubwa ni hiyo kwamba kulikuwa na miradi ambayo ndiyo ilikuwa ina- *boost up* Bajeti kwa kiasi kikubwa. Sasa baada ya muda wake kwisha *then* tumerudi sasa kwenye Bajeti kulingana na uwezo wa Serikali.

MHE. FAUSTINE K. RWIOMBBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu limejibowi. Ahsante sana.

(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 82- Mkoa wa Ruvuma Sh.34,706,841,000/=

Fungu 83- Mkoa wa Shinyanga... Sh.53,450,937,000/=

(Mafungu yalijotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 84 - Mkoa wa SingidaSh. 25,084, 318,000/=

MHE. MOHAMMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *vote 84 program 10, sub vote 1001* kifungu kidogo 250100, nilikuwa nimewasilisha kilio cha wananchi wa Singida juu wa kugawanywa kwa Wilaya ya Singida, nikalia na machozi hapa, wengine wamenifarji, nashukuru sasa. Sijafarijika kusikia kauli ya Serikali juu ya kilio ambacho nimekieleza na sina sababu ya kulia tena kwamba Mkoa wa Singida na Wilaya zake ni mionganini mwa Wilaya za zamani enzi za ukoloni ambazo hazijaguswa hata kidogo na kwamba idadi ya watu na vigezo vyote vinavyostahili vimefikiwa. Sasa ningependa kupata maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mohammed Missanga kwa hoja yake. Lakini asubuhi nilijaribu kulisema, labda kwa vile nilieleza kwa ujumla sikutaka kwenda kwa ombi moja moja ndiyo maana nikatoa kauli kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu tumeona badala ya kusubiri maombi ya mtu mmoja mmoja wacha tufanye *assessment* sisi wenyelewe tufanye mchanganuo wenyelewe kwa nchi nzima ili tuweze kuona hasa *requirements* zikoje katika maeneo yote ambayo Waheshimiwa Wabunge walikuwa wametoa hoja zao. Baada ya hapo kama tutakwama tutaomba msaada kutoka kwenye Mikoa inayohusika. Nadhani ndiyo maana pengine Mheshimiwa Missanga hakuipata moja kwa moja.

(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 85 - Mkoa wa Tabora Sh.34,991,247,000/=

Fungu 86- Mkoa wa Tanga Sh.41,879,524,000/=

Fungu 87- Mkoa wa Kagera... Sh.41,488,271,000/=

Fungu 88- Mkoa wa Dar es Salaam... Sh.48,344,350,000/=

Fungu 89- Mkoa wa Rukwa... Sh. 27,420,580,000/=

Fungu 95- Mkoa wa Manyara... Sh. 25,064,315,000/=

(*Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

MIPANGO YA MAENDELEO

FUNGU 37 – OFISI YA WAZIRI MKUU

Kifungu cha 1001 - *Administration and General*... Sh. 1,792,989,000/=

Kifungu cha 1003 - *Policy and Planning*... Sh. 13,299,899,400/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

FUNGU 42 – OFISI YA BUNGE

Kifungu cha 2001 - *National Assembly*... ... Sh. 300,000,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

FUNGU 56 – OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI

Kifungu 1001 – *Administration and General*... Sh. 100,000,000/=

Kifungu 2002 – *Local Government Coordination Division*... Sh. 109,331,335,700/=

Kifungu 2003 – *Sector Coordination Division* Sh. 35,348,928,700/=

Kifungu 3001 – *Organization Development Division*... Sh. 200,000,000/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

FUNGU 92 - TUME YA KUDHIBITI UKIMWI

Kifungu 1001 – *Policy, Planning and National Response* ... Sh. 1,373,200,000/=

Kifungu 1002-*Finance Administration and Resource Mobilisation*... Sh. 367,344,000/=

Kifungu 1003 – *Monitoring, Evaluation Research and MIS*... ... Sh. 1,762,055,000/=

Kifungu 1004 - *Advocacy, Information Education and Comm* ...Sh. 7,953,000,000/=

Kifungu 1005 – *District and Community Response* Shs. 14,581,295,000/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 70 - Mkoa wa Arusha... Sh. 1,104,036,000/=

(*Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati*

(ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dr. Gama, nimeonya hii tabia ya kusimama hata hatujatajiwa chochote. Sasa hii ni mara ya mwisho, ukisimama tena kwa chochote itakuwa ni matatizo. Kwa hiyo, subiri kwanza, mimi naangaza. Usiwe na wasiwasi nitaangaza ikishatajwa tarakimu ili uweze kutaja.

Fungu 71 – Mkoa Wa Pwani Sh. 3,568,700,000/=

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, naomba msamaha. Uzoefu ni mbaya kwa sababu zamani tulikuwa tunafanya hivyo. Naomba *Vote 71, Subvote 1001*, Kifungu kidogo cha 6339 - *Rehabilitation of Government Houses*. Mara nyingi pesa zilikuwa zinatolewa, kati ya *Government Houses* ni pamoja na Nyumba za Wakuu wa Wilaya. Tukiwa katika Mkutano wa RCC, imethibitishwa nyumba ya Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo imejengwa kwa pesa nyingi, lakini kwa bahati mbaya inavuja sasa hivi ikiwa mpya. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kusaidiana na sisi kuitizame hii nyumba? Kweli ina thamani ya pesa zilizotolewa?

WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleza hapa kwamba, Serikali inatambua kwamba tulikuwa na matatizo katika ujenzi wa ile nyumba. Lakini, nimelihakikishia Bunge lako kwamba kwa sasa matatizo hayo kwa sehemu kubwa yamekwisha. Kwa hiyo, tunaamini nyumba ile ya Mkuu wa Wilaya itakamilika kwa sababu tunaendelea kuimalizia, isipokuwa tumechelewa sana katika kuikamilisha.

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 72 – Mkoa wa Dodoma Sh. 1,246,100,000/=
Fungu 73 – Mkoa wa Iringa Sh. 3,989,536,400/=
Fungu 74 – Mkoa wa Kigoma...Sh. 3,436,800,000/=
Fungu 75 – Mkoa wa Kilimanjaro Sh. 1,360,598,000/=
Fungu 76 – Mkoa wa Lindi Sh. 1,831,204,400/=
Fungu 77 – Mkoa wa Mara... Shs. 3,288,398,000/=
Fungu 78 – Mkoa wa Mbeya Sh. 3,812,846,000/=
Fungu 79 – Mkoa wa Morogoro Sh. 2,775,501,000/=
Fungu 80 – Mkoa wa Mtwara Sh. 2,198,599,000/=
Fungu 81 – Mkoa wa Mwanza Sh. 2,057,210,000/=
Fungu 82 – Mkoa wa Ruvuma Sh. 1,680,001,000/=
Fungu 83 – Mkoa wa Shinyanga Sh. 1,152,671,000/=
Fungu 84 – Mkoa wa Singida...Sh. 1,228,100,000/=

*(Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Fungu 85 – Mkoa wa Tabora Shs. 1,135,701,000/=

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufahamu kama kiasi cha Sh. 100,030,000/= kinahusiana na ujenzi wa *Security Fence* ya Hospitali ya Kitete.

WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo inahusisha mambo yote mawili. (*Makofi*)

(*Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 86 – Mkoa wa Tanga Sh. 2,133,192,500/=

(*Fungu lililotajwa hapo Juu lilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo kwa wale mashabiki wa mpira. Kule Ujerumanini ambako inacheza timu ya Argentina na Ujerumanini, hadi *half time* hawajafungana. (*Makofi/Kicheko*)

Fungu 87 – Mkoa wa Kagera Sh. 4,230,125,900/=

Fungu 88 – Mkoa wa Dar es Salaam... Sh. 2,264,818,000/=

Fungu 89 – Mkoa wa Rukwa Sh.1,009,400,000/=

(*Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, taarifa sasa hivi ni kwamba *half* ya pili imeanza. Argentina wamefunga moja. (*Makofi/Kicheko*)

Fungu 95 – Mkoa wa Manyara Sh. 3,275,001,000/=

MHE. OMAR S. KWAANGW’: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante. Nilisimama kama ulivytaka, mapema kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa Mkoa wa Manyara, wakati nachangia hoja ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilisema ndio Mkoa ambao hauna Hospitali ya Mkoa. Sasa, ukiangalia pale kwenye *Subvote* 3001, Mwaka 2004/2005 zilitengwa Shilingi milioni 100. Mwaka uliofuata 2005/2006, hazikutengwa na sasa tena Shilingi milioni 100. Sasa, hebu nipate maelezo, fedha hizi zinaweza zikajenga Hospitali, au ni kwamba inalinda hii akaunti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata maelezo kidogo.

WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kueleza kwamba, Hospitali hii inajengwa kwa

awamu. Tunakwenda kidogo kidogo kulingana na uwezo wa fedha ya Serikali. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Kwaangw' avute subira. Hali ya uwezo wa kifedha nadhani ndiyo tatizo kubwa linalotukabili kwa sasa. Lakini, tunaamini maadam tumedhamiria kulifanya jambo hili, tutalifanya kwa uhakika kabisa.

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

(Bunge lilirudia)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi, baada ya kujadili taarifa ya mapato na mwelekeo wa kazi za Serikali, imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Asasi zilizo chini yake na yale ya Ofisi ya Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo basi, Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofii)*

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka 2006/2007
yalipitishwa na Bunge)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru kwa uvumilivu wenu, Kamati ya Matumizi ni wakati mgumu sana. Lakini, tutaendelea kuvumiliana. Nadhani kimsingi ni kwamba Makadirio haya yamepita.

*(Saa 01.21 usiku Bunge lilahirishwa Mpaka Siku ya Jumatatu,
tarehe 3 Julai, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*